Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 9 Julai, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZlLIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE.SAVELINA S. MWIJAGE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMATI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA NISHATI NA MADINI)**:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU BAKARI MAHIZA)**:

Randama za Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):**

Taarifa ya Majumuisho ya Mpango Mkakati wa Kujibu Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 191

**Kuhusu Barabara ya Makutupa Bumila Jimbo la Mpwapwa**

**MHE. GEOREGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Kijiji cha Makutupa hadi Kijiji cha Bumila inahitaji matengenezo makubwa ili kuweza kupitika wakati wote na kwa kuwa lipo korongo kubwa kariBu na shule ya msingi Bumila ambalo hufamya wananchi pamoja na wananfunzi kushindwa kwenda shule kutokana na maji kujaa wakati wa mvua.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hiyo inatengenezwa na kujenga daraja katika korongo hili kuondoa adha kwa wananchi wa Bumila?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Makutupa-Bumila ina urefu wa kilomita 4, aidha korongo hilo linalotenganisha sehemu kubwa ya Kijiji na shule ya msingi Bumila lina kina cha mita 7 na upana wa mita 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kijiji hiki kinahitaki barabara ili kurahisisha mawasiliano pamoja na huduma nyingine za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pia ni kweli kwamba korongo hilo ni hatari sana kwa wananfunzi na wananchi wa Bumila. Serikali ya awamu ya nne inatambua umuhimu wa barabara za Vijijini kama kiungo muhimu cha uchumi kwa wananchi, ikiwemo barabara ya Makutupa- Bumila.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuzifanyia matengenezo barabara za Wialya na za Vijijini kwa kutumia fedha za Mfuko a Barabara (*Road Fund*).

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa katika Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2010/2011 imetenga kiasi cha shilingi milioni 14 ili kuifanya matengenezo barabara. Pia, na pia Halmashauri iteaendelea kutafuta fedha ili kuweza kujenga daraja ambalo linaunganisha Kijiji na shule ambayo ni taasisi muhimu kwa maendeleo ya Kijiji cha Bumila na Taifa kwa ujumla na kuepusha usumbufu kwa wananchi wa eneo hilo.

**MHE. GEOREGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali ya nyongeza. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa kutenga milioni 14 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya Makutupa hadi Bumila na daraja na pia niishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mima, Mkanana mpaka Chibwegele. Sasa kwa kuwa fedha hizi ambazo zimetengwa hazitoshi.

Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba katika Bajeti ijayo tuongeze fedha ili tuweze kutengeneza barabara hizi kwa kiwango cha lami sehemu hiyo ya Mima na Buchibwegele ili kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nipokee hizo shukurani ambazo amezitoa na ningemshangaa sana Mheshimiwa Lubeleje kama asingemshukuru Waziri Mkuu kwa sababu Waziri Mkuu ameshakwenda kule kwake mara tatu mfululizo na hivi tunavyozungumza hapa juzi tumetoa tena hela nyingine. Lile daraja la Godegode tumepeleka shilingi milioni 500 na sasa tumemwongezea tena shilingi milioni 225, hii barabara nyingine anayoizungumzia hapa tumepeleka shilingi milioni 30 zimepelekwa pale. Unaweza kuona jinsi ambavyo tumefanya.

Lakini nataka nitambue jitihada za Mbunge huyu. Ni mtu mfuatiliaji sijapata kuona. Kila mahali anakubana kona hii na kona hii. Kwa hiyo, nataka nimthibitishie pia hata kwenye Bajeti ijayo atuombee kwa Mwenyezi Mungu kama mambo yataenda vizuri sisi tutakuwa hatuna tatizo kwenye jambo hilo tutafanya hivyo kama anavyoishauri Serikali. (*Makofi*)

Na. 192

**Serikali Kusaidia Ujenzi wa Zahanati**

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO (K.n.y. MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA)** aliuliza:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kusaidia ujenzi wa zahanati za Vijiji zinazojengwa kwa nguvu za wananchi zikiwemo zahanati za Vijiji vya Miegeo, Ngulwi, Kwemashai, Mazumbai, Mavului, Ungo Mbelei, Mdando, Bombo na Irente Wilayani Lushoto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassani Mshagana, Mbunge wa Lushoto, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa sasa ina Kata 32, Vijiji 217 na Vitongoji 1,672 ambapo ina hospitali 2, vituo vya afya 7 na zahanati 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza agizo la Serikali la kuwa na zahanati katika kila Kijiji,Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imekuwa ikizingatia Sera hii katika bajeti yake ya kila mwaka. Katiba bajeti ya mwaka 2007/2008 kupitia fedha za ruzuku ya maendeleo,Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilitenga jumla ya shilingi milioni 247.5 kujenga wodi 1 ya wagonjwa na jengo la huduma ya Mama na Watoto *(MCH),* zahanati mpya 12, na nyumba 5 za waganga.

Pia kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ilitenga jumla ya shilingi milioni 108.0 kwa ajili ya kujenga majengo ya OPD kwenye zahanati mpya 3, kukarabati zahanati,kujenga nyumba 2 za waganga na kumalizia nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassani Mshagana, Mbunge wa Lushoto napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wialaya ya Lushoto ilitenga jumla ya shilingi milioni 220.8 ili kumalizia ujenzi waa majengo ya OPD kwenye zahanati mpya 12. Aidha, , Halmashauri kupitia vyanzo vyake imetenga fungu la kumalizia zahanati mpya ikiwemo zahanati ya Irente ambayo imeuliziwa swali.

Pia kwa zahanati za Mazumbai na Mbelei zitanufaika kwa fedha za awamu ya kwanza za Mfuko wa kuchochea maendeleo ya Jimbo zilizokuja kwa Jimbo la Lushoto. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 207.0 kwa ajili ya kujenga zahanati mpya 4 ikiwemo zahanati ya Miego,kupanua zahanati 1 kuwa kituo cha Afya,Maabara, vyumba vya kupumzikia wagonjwa na nyumba 5 za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inatambua hitaji kubwa la ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za afya hivyo inajitahidi kushirikiana na wananchi katika kuendeleza na kuboresha huduma za afya. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali awamu kwa

awamu Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto itakamilisha zahanati zinazojengwa kwa nguvu za wananchi, hasa baada ta kupata mwamko kwa kuelimisha na kuhamasisha.

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kwa kuwa sasa Serikali inajua kwamba katika Jimbo la Lushoto kuna zahanati hizo 10 amabzo zinajengwa , vile vile katika Jimbo la Bumbuli kuna zahanati ya Msamaka, Mahezangulu, Kiviricha, Kwesine na Kisiwani ambazo zinajengwa. Je, Serikali imejiandaaje kuhusu hasa wafanyakazi wa zahanati hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikiliza Waziri wa Afya akizungumza hapa na sisi wenyewe TAMISEMI tumekuwa tunazungumza hapa. Moja ya mambo ambayo tumeyafanya sasa hivi ni kuruhusu kwamba hao wanafunzi wanaomaliza katika Vyuo vyetu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya waende moja kwa moja wapelekwe katika Halmashauri zinazohusika. Kwa hiyo, anasema jambo la maana kabisa kweli zahanati zitaongezeka pale nakubaliana na Mheshimiwa Shellukindo kwamba kuna haja ya kushirikiana ili kuhakikisha kwamba hivi vitu vinapata wataalamu wa aina mbalimbali ambao watasaidia. Liko katika mpango na tunakubaliana na mawazo yake. Kwa hiyo, linatunzwa hilo wala asiwe na wasiwasi kuhusu watumishi.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia masuala ya majengo na kwa kuwa katika kuboresha huduma za afya, mbali kuwa na majengo, lazima uwe na wahudumu,uwe na vifaa, uwe na Madakitari Bingwa. Je, Serikali inaisaidiaje zahanati iliyokuwepo Masaki Wilaya ya Kisarawe kwa kuongezewa huduma muhimu kama za Madakitari Bingwa, vifaa vya maabara na vifaa vya wodi ya wazazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huku Kisarawe anakozungumzia nimeshafika huko na nimeona na ninajua kwamba kuna matatizo haya. Sasa kwa vile limekuja hapa naomba nikitoka hapa tuwasiliane mimi nay eye kwa sababu anazungumzia Dakitari Bingwa na watu wengine ili niweze kumsaidia tuone jinsi tutakavyofanya kwa sababu anazungumzia maisha ya watu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa vile wananchi wote hapa Tanzania wameitikia wito wa Serikali kwa kujenga zahanati kila Kijiji na vituo vya afya kila Kata na kwa kuwa wananchi wa Msiu wamekamilisha upande wao wa kujenga Kituo cha Afya na zahanati za Ishinsi,Kinampundu na Lukomo.

Je, Serikali inasemaje sasa kuwaunga mkono ili wakamilishe zianze kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nako huko nimefika, nimefanya ziara kule nafahamu anachozungumza hapa. Sasa labda tuzungumze tu kwamba Sera yenyewe inasemaje. Pale popote ambapo jitihada za wananchi zimeonekana kama zipo kwa maana ya shule zimejengwa, kwa maana ya zahaanti kama anavyozungumza na vituo vya afya, kila wakati Serikali imehakikisha kwamba inaunga mkono jitihada za wananchi. Kwa hiyo, hata hili analolisema Mheshimiwa Mgana Msindai ambae anaonesha jitihada kubwa sana katika masuala haya, hatuna tatizo nalo asa long as wananchi wenyewe watakuwa wameonesha jitihada na sisi tutafanya hivyo kwa ajili ya kuunga mkono jitihada zao.

Na. 193

**Hitaji la huduma za kibenki – Mpanda**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa benki kama *NBC, STANBIC, Standard Chartered* na *CRDB* yana wateja wenye majina na vipato vikubwa na nyingine zilialianzishwa kwa lengo la kutoa huduma katika Miji mikubwa tu:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia juhudi za kushawishi Benki ambazo bado Watanzania wana kauli (mfano *CRDB* na Posta) kufungua matawi na kutoa huduma katika Mji wa Mpanda ambapo tawi la *NMB* pekee halikidhi mahitaji ya wananchi wakati huu wa ushindani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za kibenki hapa nchini. Hata hivyo, kwa kuwa benki nyingi ni za binafsi, baada ya Serikali kujitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughli za kibenki, utoaji wa huduma hizo za kibenki unaendana na upatikanaji wa faida kwa Wananchi na Benki zenyewe.

Kutokana na hali hiyo, uanzishwaji wa huduma za kibenki hutegemea zaidi matokeo ya upembuzi yakinifu, ambayo yanazingatia upatikanaji wa faida kwa pande zote mbili yaani benki na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuboresha miundombinu, Serikali itaendelea kuzishawishi benki za hapa nchini kupanua shughuli zake ili ziweze kuwafikia wananchi wengi hasa wale walio Vijijini ikiwa ni pamoja na Mji wa Mpanda.

Pamoja na juhudi za kuzishawishi Benki ya Posta na *CRDB* kufungua matawi katika Mji wa Mpanda pia kupitia Bunge lako Tukufu nawaomba wananchi wa Mpanda kujiunga pamoja na kuanzisha Benki ya Wananchi *(Community Bank)* ambayo itaweza kuwasaidia na hiyo itakuwa ni mali yao na faida itakayopatikana itawaongezea wanahisa kipato zaidi.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nichukue nafasi hii kwanza kwa niaba ya wananchi wa Mpanda Mjini niishukuru sana Benki ya *CRDB* ambayo tayari imeonesha nia ya kujenga Tawi lake pale Mpanda na jana rasmi wameanza kazi ya kujenga msingi, tunawashukuru sana kwa jitihada hizo.

Lakini bado nitaitaka Serikali iendelee kuishawishi Benki ya Posta na yenyewe ifungue Tawi Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa hivi mabenki haya yanafanya biashara zake kupitia katika mtandao. Nilikuwa naiomba Serikali initoe wasiwasi na wananchi pia wana usalama gani wa fedha zao ambazo zinapitia katika mtandao hasa kutokana na wizi mkubwa ambao unafanyika katika mitandao hii na pia uhakika wa uchumi wa Taifa na fedha haramu kupitia katika mtandao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilielezee Bunge lako Tukufu na wananchi kwamba utumiaji na usafirishaji wa fedha kupitia mitandao ni utalaam ambao Watanzania ni mpya kwetu.

Hivyo suala usalama ni lazima tushirikiane na wananchi wote na mabenki yote na pale itakapoonekana kwamba hapa matatizo ni vyema wananchi wakatuarifu wakaiarifu Serikali ili Serikali ikaweza kuchukua hatua mapema zaidi kabla uhalifu haujaendelea zaidi.

**MHE. SALIM KHAMIS HEMED:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mazingira ya Mpanda kibenki yanafaana fanana na hali ya Pemba.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kushawishi benki ya *CRDB* kufungua tawi lake kule ili kukidhi mahitaji ya wateja wake wengi walioko Bara lakini wanakaa Pemba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuzishawishi Benki hizi kuweza kufungua matawi yake pale ambapo kuna haja na kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya awali kwamba kama pahala popote pana mwenendo wa fedha ni nzuri, basi Serikali itashawishi benki hizi kuweza kufungua matawi yake.

Nataka nitoe takwimu fupi tu tokea mwaka 2006 hadi leo *CRDB* imeshafungua matawi 23 Tanzania nzima, matawi ya ziada 23. *NMB* wameshafungua matawi 29 toka

mwaka 2006. Hizi ni juhudi za Waheshimiwa Wabunge kila anayetaka benki hapa na pale na sisi tunawashawishi wanafungua na huko Pemba nao vile vile hasa Mkoa wa Kaskazini, tutashawishi zaidi wafungue. *(Makofi)*

**MHE. ELIATA N. SWITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa wakulima wa Mpanda wengi huvamiwa wakati wanakwenda kuweka fedha mjini Mpanda, na kwa kuwa *NMB* imekwishaweka *mobile manking* ya kutosha.

Je, Serikali inaweza kushawishi benki nyingine pia kuweka *Mobile Banking* ili wananchi waweze kufikiwa pale wasivamiwe mabenki mjini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, *Mobile Bank* ni utaratibu wa dharura tu. Lengo ni kujenga matawi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kuzishawishi benki nyingine kama walivyofanya wenzetu kuweza kuweka *Mobile Bank* ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Na. 194

**Mikopo ya Wajasiriamali**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na ugumu wa kuwakopesha wafugaji na wakusanya matunda chini ya mpango wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi, hali inaotokana na stahili yao ya maisha ikiwa ni pamoja na elimu duni ya darasani na uelewa wa jambo hilo hivyo kushindwa hata kubuni miradi ya biashara za kufanya baada ya kuchukua mikopo:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya makusudi ya kuisaidia jamii hizo ambao ndio hasa walengwa ili nao wafaidi mpango huo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi?

(b) Je, hadi sasa ni *SACCOS* ngapi zilizokopeshwa fedha hizo Basotu – Hanang, Orkesment huko Simanjiro na Yaeda Chini, huko Mbulu na ni watu wangapoi wamenufaika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge wa Viti maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Taifa wa uwezeshaji wananchi kiuchumi unalenga katika kuwawezesha wananchi kuchumi bila ya kubagua. Kutokana

na kuwa mpango huu unatekelezwa kupitia benki za biashara, hali hii imeonekana kuwaacha baadhi ya wananchi wakiwemo jamii ya wafugaji ambao kuhamashama ni staili yao ya maisha. *(Makofi)*

Kutokana na hali hii, Seriklai inaandaa utaratibu wa kuhakikisha kwamba jamii ya wafugaji wanapatiwa maeneo ambayo watatumia kwa ufugaji. Hali hii itasaidia sana kupunguza kuhamahama. Aidha, mpango mwingine wa Serikali ni kuzihamasisha jamii hizi vikundi vya *SACCOS* na VIKOBA, ili fedha ya uwezeshaji ipitie kwenye taasisi hizo na hatimaye kufaidika na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendeleza mpango wake wa kupeleka huduma muhimu katika maeneo ya wafugaji pamoja na kuwa na shule za Bweni. Njia hii itawasaidia sana jamii ya wafugaji kupata elimu ya kutosha na hatimaye kuwa na uwezo mzuri wa kujiendeleza kimaisha. Kwa upande wa wakusanya matunda, Serikali italiangalia zaidi tatizo lao kwani kimsingi ni tofauti na lile la wafugaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hakuna *SACCOS* zilizopata fedha katika maeneo ya Basotu – Hanang, Orkesment – Simanjiro na Yaeda Chini – Mbulu.

Hali hii imetokana na kwamba katika maeneo hayo *SACCOS* bado hazijafanyiwa tathmini kwa lengo la kutuwezesha kubaini kama zinaweza kukopesheka, vinginevyo ni kuzijengea uwezo ili hatimae ziweze kukopesheka. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba hakuna *SACCOS* hata moja iliyowakopesha wananchi huko Basotu – Hanang- Orkesment – Simanjiro na wala Yaeda Chini – Mbulu na kwamba mpango wa Serikali ni kujaribu kutenga maeneo ya wafugaji kufuga mifugo yao ili wasihamehame pamoja na kujenga shule za bweni mpango ambao mimi nauona ni wa muda mrefu.

Je, Serikali haioni kwamba kupitia mpango huu ambao sasa imepitisha awamu mbili imewanyima haki na fursa yao ya kukopa kwa muda huo wote na ina mpango gani wa kurekebisha jambo hilo? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa suala la uwezeshaji wananchi ni suala la kuwapa mitaji kwa maana ya fedha taslimu ili kufanya biashara suala ambalo linaweza kuwa ngumu kutokana na Mila na Desturi. Je, Serikali haioni kwamba mpango bado unatakiwa ili wafugaji hawa wanufaike kama wananchi wenzao Watanzania? Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatujawanyima haki wafugaji. Bado nafasi ipo na hivi

ninavyozungumza tayari benki yetu ya *CRDB* inazifanyia tathmini *SACCOS* zilizoko katika maeneo yale ili waweze kuanza kuwakopesha na hatimaye kuwakopesha wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni juu ya fursa ambazo wafugaji tungeweza kuwapatia. Nataka nimhakikishie kwamba bado nafasi ipo na wafugaji wana fursa vile vile kama wakulima na kama wengine kwa sababu na wao wanazalisha< wanapata mapato na bado kuna mipango muhimu sana ya kuwaendeleza wafugaji.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wafugaji hawajawahi kubahatika kupata mikopo na huu utaratibu unaendelea pole pole wa kusema kwamba tunaelimisha tunaelimisha. Je, Serikali ilipoandaa utaratibu wa kumsaidia mkulima kuwa na stakabadhi ghalani.

Je, Serikali haiwezi kutumia utaratibu huo huo kumsaidia mfugaji naye katika mifugo yake iwe ni kama sehemu ya mavuno yaliyoko ghalani naye apate mkopo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge nataka tukubaliane kwamba kuna tofauti kubwa baina ya mfugaji na mkulima. Mfugaji wa Tanzania ana ile hulka ya kuhamahama. Mfugaji mkulima unamwona kwamba ana *position* ambayo inaonekana. Nataka nilipokee suala lake kwa sababu ni jipya na tutalifanyia kazi ndani ya Serikali ili tuweze kuona ni kiasi gani tunaweza tukamkopesha mfugaji na vile vile ni kiasi gani huyu mkulima mfugaji ataweza kurudisha ile mikopo ambayo amekopeshwa na Serikali. Suala lake tutalifanyia kazi na tutampatia majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongezea tu baada ya majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. Kwanza kwa upande wa wafugaji Serikali imeshaanza kuchukua hatua nzuri sana za kuwasaidia wafugaji. Katika suala moja kubwa ambalo limewasaidia sana wafugaji ni kuhusu madawa ya kuogeshea mifugo.

Mpaka sasa hivi wafugaji wote katika nchi nzima ya Tanzania wakiwemo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge wanalipa asilimia 60 ya gharama zote za madawa ya majosho ambapo asilimia 40 wanalipiwa na Serikali. *(Makofi)*

Lakini pia katika mradi wa *DADPs* Serikali imekuwa ikichukua hatua za kuona ni kwa namna gani zinaweza zikawasaidia wafugaji. Kwa hiyo, Serikali imeshaanza kulifanyia kazi katika kuhakikisha kwamba wafugaji katika nchi hii wanasaidiwa kama ambavyo wanasaidiwa wenzao wakulima. *(Makofi)*

Na. 195

**Kuongezeka kwa Ajali za Barabarani**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Ajali za barabarani zinaendelea kuongezeka siku hadi siku na ajali nyingi kati ya hizo zinasababishwa na upasukaji wa mipira hasa ya mbele:-

(a) Je, kwa nini Serikali inaruhusu kuingizwa nchini tairi zisizo na viwango vya ubora ambazo zinachangia kuongezeka kwa ajali za barabarani hasa kwa mabasi na malori?

(b) Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* – Arusha kilikuwa kikizalisha matairi yenye viwango vya ubora. Je, ni sababu zipi zilifanya kiwanda hicho kufungwa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* hukagua ubora wa matairi yanayotoka nje ya nchi kabla ya kuruhusiwa kuingia katika soko la Tanzania. Matairi yanayokidhi matakwa ya viwango vya Tanzania ndiyo tu huruhusiwa kuingizwa nchini Tanzania na yale yanayobainika kutokuwa na ubora unaotakiwa hayaruhusiwi kuingizwa nchini. Aidha, *TBS* hufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maduka yanayouza matairi na kuchukua sampuli za matairi kwa nia ya kuendelea kuhakiki ubora wa matairi yaliyoko madukani.

Pamoja na kuendelea kuhakiki ubora wa matairi kabla ya kuingia nchini na wakati bidhaa hizo zikiwa madukani, *TBS* vile vile, itaendelea na utoaji wa elimu ya matumizi sahihi ya matairi ili kuepusha ajali za barabarani zinazoweza kutokea kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya matairi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Missanga kuwa Kiwanda cha *General Tyre* kilikuwa kinazalisha matairi yenye ubora wa hali ya juu na kilikuwa kinauza matairi yake nchini na katika nchi za jirani kama vile Kenya, Malawi, Msumbiji, Jamhuri ya Kongo, Burundi, Rwanda na kadhalika. Ubora wa matairi haya ndio ulikuwa matangazo ya kuuzia matairi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi wa kiwanda cha *General Tyre* ulianza kuporomoka miaka ya mwishoni mwa 1990 kutokana na uingizaji wa Matairi hasa ya mitumba kutoka nje. Pamoja na kwamba baadaye Serikali ilisimamisha uingizaji wa matairi ya mitumba, ufanisi haukuweza kuimarika.

Hii ilisababisha kiwanda kukopa kwenye mabenki yakiwepo ya nje kama benki za *HSBC* na *City Bank* madeni ambayo yalitishia kukifilisi kiwanda. Ili kukiokoa kiwanda kisifilisiwe na mabenki ya nje, Serikali ilitoa dhamana ya mkopo uliotolewa na

taasisi ya *NSSF*. Pamoja na mkopo huo uliotolewa mwaka 2005, ufanisi ulizidi kudidimia na fedha za uendeshaji nazo zikakosekana.

Hivyo ilipofika mwezi Septemba, 2007 uzalishaji ulisimama. Wakati huo ilitegemewa ufumbuzi ungepatikana katika kipindi kifupi lakini kwa vile kiwanda kilikuwa na deni kubwa la *NSSF,* haikuwa rahisi kupata mikopo.

Aidha, Serikali haikuwa tayari kutoa dhamana nyingine ili kuwezesha upatikanaji wa mkopo mwingine hasa kwa sababu mbia mwenza, kampuni ya *Continental AG* ya Ujerumani ambayo ndiyo ilikuwa imeshikilia usimamizi wa kiwanda haikuwa tayari kuwekeza katika kiwanda hiki ili kukifufua kwa madai kuwa shughuli za uzalishaji wa matairi sio za msingi kwao kwa sasa. Serikali inahitimisha majadiliano na mbia huyo na inafanya matayarisho ya kumpata mbia mwingine atakayesaidiana na Serikali kufufua kiwanda hiki.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Niulize maswali mawili yafuatayo:-

La kwanza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni kweli kabisa kwamba yapo matairi ambayo mpaka sasa yanaingia nchini ambayo ni *sub-standard*. Kwa kuwa kuna vyombo ambavyo vimeanzishwa hapa nchini vya kudhibiti uingiaji kwa bidhaa na vifaa ambavyo ni vibovu kama *TBS* kuna *fair compitition.* Sasa kama bidhaa mbovu bado zipo na vyombo hivi bado vipo hivi kuna sababu gani ya vyombo hivi kuendelea kuwepo badala ya kufutwa?

La pili, iko tetesi kwamba kiwanda cha Matairi cha Arusha *General Tyre* kimehujumiwa na kiwanda fulani nchi jirani. Sina sababu ya kuitaja na ndiyo maana kiwanda kile kimekuwa hakifanyi kazi sawa sawa, jitihada ambazo zimefanywa Mheshimiwa Waziri alizoeleza. Lakini kwa sababu kiwanda hicho cha nchi jirani kinataka kifanye biashara ya matairi na ndiyo wanafanya sasa hivi na ndiyo kimehujumu na kufikia hali hiyo. Je, Serikali inasemaje juu ya tetesi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba pamoja na jitihada za *TBS* na *Fair Compitition Commision* bado kuna wafanya biashara wachache ambao wanatumia mwanya mkubwa wa pwani yetu ilivyo kubwa na mipaka yetu ilivyo mipana kuingiza baadhi ya bidhaa zilizo mbovu. Lakini napenda nimshawishi akubaliane na mimi kwamba ukiondoa *TBS* leo au ukiondoa *Fair Compitition Commission* katika Tanzania basi nchi itajaa bidhaa mbovu pamoja na haya matairi yanayosemwa. Niseme tu kwamba jambo la msingi hapa ni kuendeleza jitihada za kuendelea kudhibiti uingizaji wa bidhaa hizo mbovu. Naomba ushirikiano wa wananchi na ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge pale unapoona kwamba bidhaa imeingia ambayo siyo nzuri toa taarifa mapema kama siyo kwa *Fair Compitition Commission* au siyo kwa *TBS* angalau kwa Polisi kwa sababu kuna

mashirikiano kati ya Jeshi la Polisi na *TBS*. Katika suala hilo na namna hiyo pole pole ndiyo tunaweza tukadhibiti kabisa suala hili la bidhaa feki ikiwa ni pamoja na matairi.

Swali lake la pili la kuhusu tetesi, kama alivyosema mwenyewe ni tetesi na hakuna uhakika kuhusu hilo.

Lakini kama kuna kiwanda cha nje cha Kenya au Uganda au mahali pengine pale ambacho labda kimefanya jitihada kuuza matairi yake kuliko Tanzania ili *General Tyre* isifanye kazi. Huo ndiyo ushindani wa biashara katika dunia. *(Makofi)*

Tunachofahamu sisi ni kwamba kiwanda kile kimekosa mitaji na mwekezaji mwenza hakupenda kuendelea kuwekeza na sisi tunafanya jitihada sasa hivi ili kumpata mwekezaji mwingine ambaye ana ushindani mzuri zaidi ili tuweze kutengeneza na kuuza bidhaa ambazo zinashindana katika soko hata kama kuna kiwanda cha nje *General Tyre* iweze kuuza bidhaa ambazo zina ubora zaidi ili tuweze kupata masoko katika eneo hili la Tanzania na vile vile katika eneo la Ukanda wa Afrika Mashariki na hata Kusini mwa Afrika.

**NAIBU SPIKA:** Umetumia maneno mengi katika suala hili. Sasa tunahama tunayo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 196

**Kituo cha Polisi cha Lupa Kupatiwa Usafiri**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Polisi cha Lupa kinahudumia Tarafa nzima ya Kipambwe yenye Kata saba na kwa kuwa kituo hicho hakina usafiri kabisa, hali inayohatarisha ulinzi na usalama.

Je, Serikali itapeleka lini usafiri wa gari kituoni hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango wa kuvipatia vituo vyote vya Polisi, kikiwemo kituo cha Lupa, vyombo vya usafiri hasa magari na pikipiki ili kuwawezesha askari wetu kutoa huduma kwa wananchi kwa urahisi zaidi. Mpango huu unatekelezwa kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni terehe 11 Juni, mwaka huu 2010 kituo hicho kilipatiwa pikipiki moja mpya. Ninachoweza kusema ni kwamba katika mwaka wa

fedha 2010/2011 kituo hicho kitaongezewa pikipiki nyingine moja kwa ajili ya kuimarisha ulinzi. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na nimeridhika sana, hasa hasa baada ya kuniambia kwamba Kituo cha Lupa cha Polisi wamekipatia pikipiki moja na katika mwaka huu wa fedha watakipatia pikipiki tena. *(Makofi)*

Pamoja na hayo Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza sana. Kutoka Lupa hadi Chunya mjini ambako kuna kituo cha polisi ni zaidi ya kilomita 50 na huko Lupa wakati wa msimu wa tumbaku wananchi wangu huwa wanakuwa na fedha nyingi sana na huwa wananunua pikipiki ambazo wanapelekewa na wafanyabiashara.

Kwa kuwa wao hawajui wananunua pikipiki wanaanza kuendesha. Sasa askari pale kwenye kituo huwa wanawakamata hasa wakati wa minada, wananchi wangu na kuwalipisha faini zaidi ya sh. 40,000/= au 50,000/= wakati mwingine bila risiti, kisa kwa kuwa wao hawana leseni.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuwaambia sasa askari wale kwamba kwanza wahamishe huduma za kutoa leseni kutoka Chunya Mjini kwenye Kituo cha Polisi kupeleka Lupa na pia waache kuwakamata ovyo wananchi wangu na kuwanyanyasa wakati wa mnada?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ya umbali kati ya Jimbo lake la Lupa na Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni Chunya, kwamba ni kilometa 50; nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tunalifahamu na tunazingatia na ndivyo nchi yetu ilivyo kubwa. Hii ni sehemu moja, lakini katika sehemu nyingi za Tanzania, hali iko namna hii. Lakini kwa kweli hilo tunalifahamu na bado tutaendelea kuimarisha ulinzi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili suala la pili kuhusu msimu wa tumbaku na hawa ndugu zetu ambao wanafanya hiyo biashara wakiwa na pikipiki. Nipende kusema kwamba Idara ya Polisi haihusiki na mambo ya kutoa leseni. Leseni za pikipiki zinatolewa na watu wa *TRA,* maana kule ndiko wanakolipa na kumalizana nao. Polisi inakuwa ni katika utekelezaji katika kukagua hivi vyombo kama vinakwenda na vinapokuwa barabarani viko sawasawa kwa maana ya kusema kwamba katika vitu vinginevyo leseni ziko sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niseme kwamba hili tumelizingatia. Kama kweli utakuwepo usumbufu kwa wananchi, maana hawa wananchi wa Lupa sio kwamba ni wakwako lakini ni Watanzania na haki zao ni lazima zitazamwe. Kwa hiyo, hili nilitaka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutalifanyia kazi na nitazungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha, ambao *TRA* iko chini yao ili tuone kwamba hawa wananchi hawasumbuliwi tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yanayotokea Lupa, yamefanana sana na pale kwangu Kilwa Kaskazini, pale Somanga. Japokuwa wananchi wamejitolea sana kujenga Kituo Cha Polisi pale Somanga kwa karibia 90%, lakini hatujui ni wapi kwa kuelekea ili tuweze kumalizia kituo kile na tuweze kufanikisha mambo yetu yafanikiwe vizuri pale.

**NAIBU SPIKA:** Hamfanani, wewe haulimi tumbaku. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, kuwasaidia kujenga Kituo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa kupitia kwake yeye ninaomba nimshukuru yeye mwenyewe binafsi, lakini pia niwashukuru wananchi wa Somanga kwa jitihada za kujenga Kituo, ambacho taarifa tunazo.

Lakini tatizo ambalo linatukabili sio la Somanga peke yake, linafanana na maeneo mengi katika nchi ya Tanzania, kwa sababu vituo hivi vinaendana na mambo mengine. Kujenga kituo ni kitu kimoja, lakini pia kuna kujenga Makazi ya Askari Polisi

na vitu vingine ambavyo vinaendana na miundombinu ya pale mahali. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, kwamba hilo suala tunalo katika Wizara na katika Idara ya Polisi na litatizamwa kwa kadiri tutakavyoweza.

Lakini nimwambie kwamba ninawapongeza wananchi na jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha za kutosha na ndivyo tutakavyokuwa tunakwenda awamu kwa awamu katika kukamilisha hivi vituo. Lakini nimhakikishie kwamba jitihada hizi tumezipokea na tunazifahamu na tunazifanyia kazi na kinachotubana ni ule uwezo tu ambao tunao kiserikali. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tatizo la Kituo cha Polisi cha Lupa, linafanana sana na tatizo la Kituo cha Polisi Kungumarwa, ambacho kinahudumia Tarafa mbili za Momashimba na Nyamilambo. Na kwa kuwa, Serikali imeahidi mara nyingi kukipatia chombo cha usafiri kituo cha Polisi Kungumarwa.

Je, katika utaratibu wa kutoa vyombo vya usafiri kwa vituo vya Polisi, Serikali itakuwa tayari kukiingiza Kituo cha Polisi Kungumarwa, katika awamu za mapema ili iweze kutekeleza ahadi yake mapema?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sakila Bujiku, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sakila atakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masha, aliposimama hapa wakati tunatoa hotuba yetu ya Bajeti alisema kwamba ingekuwa ni ndani ya uwezo wake, kila kituo katika Tanzania bila hata kuomba kingeweza kupata vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri.

Lakini azma hii inakuja inatuletea matatizo katika utekelezaji ni kwa sababu halisi inayoeleweka katika Tanzania; nimwambie tu kwamba, jitihada zitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Waheshimiwa Wabunge, niwaombe kitu kimoja; tunapozungumzia suala la ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika Taifa letu, tujue kwamba tunapoyatizama masuala haya, hata wahalifu wanayatizama pia, hata watu wenye nia mbaya katika Taifa letu wanayatizama pia.

Kwa hiyo, tunavyokwenda katika undani zaidi katika kuelezea baadhi ya mapungufu tuliyokuwa nayo, ni rai yangu kwamba haitusaidii sana isipokuwa turidhike tu kwamba Serikali inafanya kila jitihada kwa nia nzuri kabisa, lakini ndani ya uwezo ambao tunao.

Nimhakikishie Mheshimiwa Sakila, kwamba kilio chake kwa niaba ya wananchi wake tumekipokea na katika mtizamo mzima wa kutizama mambo yatakwendaje katika mgao, kwa kuwa tayari Bajeti imeshapita, tutatizama lile linalowezekana. Lakini ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada ambazo amekuwa anazifanya

hasa inapokuja katika masuala ya usalama wa raia na mali zao katika Jimbo lake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ukiona watu hawana pesa, maneno yanakuwa mengi. Sasa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, atauliza swali hilo kwa niaba, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya.

Na. 197

**Kuanzisha Miradi ya Umwagiliaji na Mabwawa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. PINDI H. CHANA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuboresha kilimo cha kisasa ambacho ndicho msingi wa Uchumi wa Kisasa:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanzisha Bwawa la Umwagiliaji na shughuli nyingine kama vile ufugaji wa samaki katika eneo la Ipogolo, Mkoani Iringa sehemu ambayo maji hutuama sana?

(b)Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha miradi ya umwagiliaji na mabwawa katika Wilaya ya Ludewa na Makete ambako kuna vyanzo vingi vya maji yanayofaa kwa umwagiliaji na ufugaji wa samaki?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, naomba nitoe maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 1960, wataalamu wa *FAO* walifanya uchunguzi na kubaini kuwepo kwa uwezekano wa kujengwa Bwawa kubwa kwenye eneo la Ipogolo kwa ajili ya uzalishaji wa umeme.

Hata hivyo uchunguzi huo ulibainisha maeneo mengine katika Bonde la Mto Ruaha la kujengwa mabwawa kwa kufuata vipaumbele.

Serikali ilitekeleza ujenzi wa bwawa la Mtera na hivyo ujenzi wa Bwawa katika eneo la Ipogolo haukufanyika. Pamoja na hayo, ujenzi wa miundombinu mbalimbali uliendelea katika eneo la Ipogolo. Miundombinu hiyo inajumuisha barabara kuu itokayo Mbeya – Dar-es-Salaam, kituo cha *transformer* cha umeme wa gridi ya Taifa, kituo cha kuchukulia maji ya kuhudumia manispaa ya Iringa, kituo cha kutoa mafunzo ya wakulima *(FDC),* stendi ya mabasi na barabara ya kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo na Mji wa Iringa na vile vile makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa serikali haina mpango wa kujenga Bwawa kwenye eneo la Ipogolo kwa ajili ya umwagiliaji na uvuvi. Eneo hilo limeendelezwa kwa miundombinu mbalimbali ambayo imeligharimu Taifa fedha nyingi. Serikali imeendelea na ujenzi wa mabwawa na miundombinu mingine kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mengine ya Mkoa wa Iringa, ambayo yameainishwa kuwa yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mipango ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika wilaya za Ludewa na Makete. Mipango hiyo inajumuisha uendelezaji wa *scheme* za Rifua, Mkiu, Mandan na Ibuma, wilayani Ludewa. Serikali pia imebainisha maeneo katika mto Ruhuhu, yanayofaa kwa ujenzi wa mabwawa na hasa uendelezaji wa eneo la Manda, wilaya ya Rudewa Mkoa wa Iringa na vile vile Lituhi Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Ruvuma.

Mhweshimiwa Naibu Spika, serikali imeanza utekelezaji wa *scheme* hizi kwa awamu. Katika *scheme* ya Rifua, ujenzi wa banio, mifereji miwili mikuu yenye urefu wa jumla ya kilometa mbili na maumbo mbali mbali ya kudhibiti na kugawa maji umekamilika. Uratatibu wa kumapata Mkandarrasi wa kujenga *scheme* ya Mkiu umekamilka na ujenzi wake utatekelezwa katika mwaka wa 2010/2011. Usanifu wa *scheme* ya Mandan a usanifu wa awali wa bwawa la mto Ruhuhu, umekamilika.

Hata hivyo, usanifu wa kina wa bwawa utakamilishwa kwa ushirikiano na Wizara ya Miundombinu ili tuta la Bwawa hilo litumike pia kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya za Ludewa na Mbinga. Wataalamu wa Wizara hizi mbili wameandaa hadidu za rejea kwa mtaalam mwelekezi atakayefanya kazi hiyo. *Scheme* ya Ibuma itafanya upembuzi yakinifu na usanifu katika mwaka wa 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wilaya ya Makete, wataalam wa umwagiliaji kutoka Ofisi yetu ya Kanda ya Mbeya, wakishirikiana na watumishi wa Halmashauri ya Makete, wameainisha maeneo yanayofaa kwa miradi ya kilimo cha umwagiliaji yanayojumuisha Luhumbu, Matenga na Mafumbi.

Mradi wa Luhumbu, utapata fedha za utekelezaji kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji katika Wilaya *(DIDF)* na ujenzi utafanyika mwaka 2010/2011.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa anafuatilia kwa karibu juu ya uharibifu wa mazingira jirani na maeneo ya mabwawa ya Mtera na Kidatu, jambo ambalo lilikuwa linaashiria na kuleta tatizo kubwa la upungufu wa maji katika mabwawa hayo.

Kwa hivi sasa nimeambiwa, kuna taarifa kwamba kuna watu ambao wanafanya shughuli za kilimo katika maeneo hayo.

(a) Je, Wizara yako ina taarifa hiyo ili kuweza kurekebisha hali hiyo kabla hatujapata tatizo?

(b) Kwa kuwa, Wizara yako ndio inahusika na utoaji wa vibali vya matumizi ya maji. Je, unapotoa vibali hivyo, unahusisha Wizara ya Nishati na Madini kwa Karibu zaidi ili kuhakikisha kwamba matatizo kama hayo hayajitokezi, kama ambavyo ilisikika pia katika Bwawa la Hai?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uharibifu wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji ni suala muhimu sana ambalo tayari Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, imeshaandaa mkakati karibu miaka takribani mitatu au minne iliyopita. Utekelezaji wake ni utekelezaji shirikishi kuanzia ngazi ya kitaifa mpaka ngazi ya kijiji. *(Makofi)*

Kuhusu maeneo ya mabwawa ya maji, wahusika pia vile vile ni sisi wenyewe katika Ofisi zetu za mabonde na vile vile wanaotumia maji hayo kama vile *TANESCO* na Halmashauri zinazohusika. Serikali inalifahamu na kila mtu anajua wajibu wake na tutaendelea kulisimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utoaji wa vibali vya maji; napenda kumhakikishia na kuthibitisha kwa Mheshimiwa Stella Martin Manyanya, kwamba utoaji wa vibali vya maji au Hati ya Haki ya Kutumia Maji, ni jambo shirikishi, halitolewi tu kwa mtu mmoja kukaa na kusema ninatoa kibali, hapana. Linashirikisha wadau wote katika eneo lile la Bonde ili kila mtu aweze kutoa ni vipi anaweza kuathirika namna gani na kile kibali au na eneo zima linaweza kufaidika namna gani. Kwa hiyo, ninaomba kuthibitisha kwamba hili ni jambo shirikishi kabisa. *(Makofi)*

Na. 198

**Upatikanaji wa Maji ya Bomba Vijiji vya Gwata, Gumba na Magindu**

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mradi wa Maji wa Wami – Chalinze, Serikali iliahidi kufikisha Maji kwa awamu katika Vijiji vya Gwata, Gumba na Magindu, katika Wilaya ya Kibaha lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

Je, ni lini wananchi wa vijiji hivyo wategemee kupata maji ya bomba?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, ninapenda kutoa maelezo ya awali kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Chalinze, ulibuniwa mwaka 1980 ili kutoa maji kutoka katika mto Wami kwa ajili ya huduma ya maji kwenye mji wa Chalinze na vijiji 61 vilivyo katika wilaya za Bagamoyo na Kibaha katika Mkoa wa Pwani. Mradi ulibuniwa na kutekelezwa katika awamu mbili.

Ujenzi wa awamu ya kwanza ulikamilika Disemba 2003, na unatoa huduma ya maji katika mji wa Chalinze na vijiji 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa awamu ya pili wa mradi wa maji, unajumuisha vijiji 47 na utahusisha makundi makuu matatu. Kundi la kwanza linahusu vijiji vya Mdaula, Msolwa, Ubena Zomozi, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Matuli na Tukamisasa, vilivyo katika Wilaya ya Bagamoyo. Kazi ya ujenzi ilianza mwezi Septemba, 2009 na itakamilika mwezi Machi, 2011.

Sehemu hii inagharimiwa na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu *(BADEA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la pili linahusu vijiji vya Kizuka, Ngerengere, Sangasanga, Kidugalo na Kinonko, vilivyo katika wilaya ya Morogoro. Kazi ya ujenzi ilianza mwezi Januari, 2010 na itakamilika mwezi Aprili, 2011. Sehemu hii inafadhiliwa na Serikali ya watu wa China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la tatu ni la vijiji vilivyobaki na viko katika Wilaya ya Bagamoyo na Kibaha. Utekelezaji wa sehemu hii ya mradi utaanza mwezi Agosti, 2010. Vijiji hivyo ni Kifuleta, Mihuga, Mkange, Kwekonje, Masimbani, Mandamazingara, Kiwangwamwavi, Fukayosi, Makurunge, Mkenge, Kidomole, Masunguru, Mwentemo, Msinune, Pongwe, Masungura, Madesi, Kisanga na Malivundo. Vijiji vingine ni Mindukeni, Kinzangu, Makombe, Talawanda, Msigi, Vigwaza, Chamakweza, Buyuni, Visezi, Magindu, Lukenge, Chahua, Bwata, Gumba, Kwaruhombo, Kwang'andu na Pongwe Kiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya, napenda kujibu swali Mheshimiwa Dr. Ibarahimu Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa maji katika vijiji vya Gwata, Gumba na Magindu, utafanywa katika awamu ya pili katika kundi la tatu. Taratibu za kuwapata Wakandarasi na Mtaalamu Mwelekezi atakayesimamia kazi za ujenzi ziko katika hatua za mwisho. Mikataba ya ujenzi itasainiwa mwezi Julai, 2010 na kazi ya ujenzi imepangwa kuanza mwezi Agosti 2010. Utekelezaji wa mradi utachukua miezi 18. Ujenzi wa sehemu ya awamu ya pili ambayo haimo katika mpango wa *BADEA* itagharimiwa na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, kufuatilia miradi ya maji katika Jimbo lake. *(Makofi)*

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa mradi huu mkubwa wa maji.

Kwa kuwa, utekelezaji wa mradi huu wa maji wa awamu ya pili utachukua karibu miezi 18; na kwa kuwa, wananchi wa Kata nzima ya Magindu wanategemea mabwawa ambayo hivi sasa yamepasuka na yanavuja maji.

Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kuchukua hatua za dharura za Serikali kutoa fedha ili ukarabati wa mabwawa haya ufanyike kama ambavyo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imeomba ili kunusuru matatizo ya upatikanaji wa maji kwa Kata nzima hii ya Magindu?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali na hasa ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama na kwa umbali ambao si mrefu kutoka katika maeneo wanayoishi.

Kuhusu suala mahususi la Magindu, naomba nimhakikishie kwa nia hiyo hiyo, nimhakikishie kwamba tutaliangalia kwa pamoja kati ya Wizara na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, tuone kama tunaweza tukaandaa mradi wa dharura wa kuwapatia maji wananchi wa Magindu.

Na. 199

**Serikali Kuzisaidia Hospitali za Mashirika ya Dini**

**MHE. WILSON M. MASILINGI (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, hospitali za kujitolea hasa zinazoendeshwa na Mashirika ya Dini zinatoa mchango mkubwa sana katika kutoa huduma nzuri tangu tupate uhuru; na kwa kuwa, bado zinahitajika katika baadhi ya maeneo kama vile jimbo la Muleba Kaskazini:-

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuzisaidia Hospitali hizo ili huduma hiyo isitetereke baada ya watumishi wengi kuhamia Serikalini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Hospitali za Mashirika ya Madini na hasa katika maeneo ambayo Serikali haijaweza kutoa huduma za afya. Kwa kutambua mchango huo Serikali inazisaidia Serikali hizi

katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa jamii. Maeneo hayo ni pamoja na ruzuku ya mishahara, ruzuku ya vitanda, dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya upungufu wa watumishi wa katika sekta hii ni tatizo kwa vituo vyote kutolea huduma. Aidha, katika hospitali za mashirika ya Dini upungufu ulikithiri hasa pale Serikali ilipoongeza mishahara kwa watumishi wa kada za afya. Hii iliwafanya watumishi wengi kurudi kufanya kazi Serikalini na kuacha pengo kubwa kwa vituo vya huduma za afya vinavyomilikiwa na Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango unaotolewa na hospitali za Mashirika ya dini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa utaratibu yaani *Service Agreement* ambapo hospitali, vituo vya afya na zahanati ambazo zinamilikiwa na Mashirika ya Dini au watu binafsi wataingia makubaliano na Halmashauri husika ili vituo hivyo vitoe huduma kwa niaba ya Halmashauri husika. Makubaliano hayo yatarahisisha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya afya ya msingi katika utaratibu huu. Halmashauri zimeshauriwa kwa ajili na kuwapanga watumishi kufanya kazi katika vituo hivyo pale pale wanaopatikana kwa lengo la kutoa huduma bora.

Aidha, vituo vya Mashirika ya Dini kwa kutumia vyanzo vya fedha vinashauriwa kulipa kulingana na taratibu za Serikali au zaidi ili kuwavutia watumishi wao waendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuu kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inatoa ruzuku ya Mishahara ya Watumishi na vitanda katika hospitali za Mashirika ya Dini kwa makubaliano maalum ili kutoa huduma zenye ubora. Naomba kutoa rai kwa wamiliki wa vituo vya huduma za afya vya Mashirika ya Dini kushirikiana na Halmashauri ili kuwa na makubaliano maalum na hasa katika maeneo ambayo hayana vituo vya afya vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utekelezaji wa makubaliano hayo mwaka 2009/2010 hospitali ya Peramiho, imeingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Hospitali ya Ilembula, imeingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Hospitali ya *Kilindi Lutheran* imeingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi na Hosptali ya *Baptist Kigoma* imeingia mkataba na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ni vizuri basi na hospitali ya Muleba ikafanya hivyo ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wilaya ya Muleba imekuwa inahudumiwa na hospitali ya shirika la dini Katoliki, Alubya na hospitali za Kagodo na Ndolage pia zimekuwa zinatusaidia kwa wilaya nzima pamoja na Muleba Kaskani na Kusini na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mtendaji mpya ambaye amekuta anajali afya zetu utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa kujenga hospitali ya Wilaya umeanza katika eneo la Marara. *(Makofi)*

Je, Serikali haiwezi ikatoa mtazamo wa kipekee wa kusaidia hizi hospitali za Mashirika ya Dini ambazo zimetusaidia kwa muda mrefu ili kusudi huduma za afya zinazotolewa ziboreke na hasa kama muuliza swali alivyouliza akisisitiza kuhudumia watumishi hawa, Madaktari na Wauguzi ambao sio tu kwamba mishahara yao ni midogo bali hata madai yao ya kupandishwa mishahara tumekuwa tunafuatilia Wizarani hayajalipwa kwa muda mrefu sasa?

**NAIBU SPIKA:** Naomba yawe maswali mafupi.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Kwa kuwa ushauri tuliopewa wa kuingia mikataba na hospitali hizi Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ni ushauri mzuri na sisi sasa tunajukumu la kujenga hospitali ya Wilaya Serikali haiwezi kutusaidia kwa sababu fedha mnazoleta ni kidogo huku kwenye Halmashauri ili kusudi mtoe pesa nyingi sasa hivi kusaidia hospitali zetu hizi tatu Rubia, Kagodo na Ndolage ili huduma iboreke zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama Mkurugenzi wa Maendeleo ya Wilaya ya Muleba na Halmashauri husika inataka kujenga hospitali ya wilaya lakini bado kama hospitali hizi tayari zinapata ruzuku Serikali itaendelea kutoa ruzuku. Kwa hiyo, kwa sababu sisi lengo ni kuwapatia huduma za karibu. Kwa hiyo, hili nafikiri halitakuwa tatizo lakini isipokuwa sasa wenyewe ni vizuri wakaweka katika Bajeti zetu za Halmashauri. Aidha vilevile madai ya wafanyakazi madai ya mishahara basi tuendelee kulifuatilia ili tuweze kuona tatizo ni nini. Kama madai hayo wamepeleka Wizarani basi ni suala la ufuatiliaji. Kwa hiyo, Mkurugenzi aweze kwenda pale Wizarani aendelee kufuatilia kwa taratibu zilizopo ili watumishi hawa madai yao yaweze kupewa kipaumbele na hatimaye kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala lake la pili masuala ya kwa vile wameshawekeana *Service Agreement* hata kama mtakuwa mnajenga hospitali yenu, inatakiwa vilevile na sisi tuwasaidie. *(Makofi)*

Labda tu niseme hivi kwamba Serikali kupitia Halmashauri labda niseme vipi kwamba Serikali kupitia Halmashauri inatoa fedha kwa hospitali hizo yaani hizo Hospitali za Mashirika ya Dini kutokana na fedha za mfuko wa pamoja wa Halmashauri *Council Health Basket Fund,* hospitali teule, yaani *DDH,* huwa zinapatiwa asilimia 25 hadi 35 zawadi na hospitali ambazo si teule zinapewa asilimia 10 hadi 15 ya fedha yote inayopelekwa katika Halmashauri.

Kwa hiyo, kwa kutumia fedha hii basi inavyotengwa ni halmashauri husika yenyewe ndiyo inapanga kuona kwamba watu wawape nini hata kama nimeandika hiyo

*Service Agreement.* Kwa hiyo, pesa tunayoileta pale inatosheleza kabisa kwa mipango tu mizuri. *(Makofi)*

Na. 200

**Huduma Zinazotolewa na MEWATA**

**MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE** aliuliza:-

Kwa kuwa, MEWATA wanatoa huduma nzuri sana ya kuwasaidia wanawake wenye saratani ya matiti na kwa huduma yao wameokoa mamilioni ya pesa na maisha ya wanawake wengi; na kwa kuwa madaktari hao inabidi wachangiwe kupitia kwenye televisheni kama omba omba:-

Je, kwa nini Serikali isitenge fungu maalum la fedha kwa kazi hiyo muhimu wanayofanya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa naiba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na MEWATA katika kupambana na ugonjwa wa saratani ya matiti, Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya kusaidia chama hiki kulingana na upatikanaji wa fedha. Mwaka 2008 Machi, Serikali ilitoa milioni 100 kugharamia kampeni za saratani ya matiti zilizofanyika katika mkoa wa Lindi na Mtwara. Mwezi Novemba, 2008 Serikali ititoa shilingi milioni 200 kupitia taasisi ya saratani ya *Ocean Road* kwa ajili ya kampeni zilizofanyika katika mikoa ya Dodoma na Manyara kwa kushirikiana na MEWATA.

Aidha, Julai, 2009 Serikali ilitoa shilingi milioni 100 kwa MEWATA kugharamia mkutano wa kimataifa Chama cha Madaktari Wanawake Duniani uliofanyika nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kulipia gharama za huduma za afya za jamii. Aidha, Serikali itaendelea kuthamini mchango wa huduma za afya zinazotolewa na vyama vya kitaalam pamoja na MEWATA, Taasisi na Asasi nyingine kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana MEWATA kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa katika suala zima la kutoa huduma kwa wagonjwa wa saratani za matiti lakini na saratani kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo; pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri nilikuwa naomba niulize swali la kwanza, kwanini Serikali isitenge Bajeti maalum kwa ajili ya kazi hii nzuri ambayo inafanywa na MEWATA badala ya mpaka waombe?

Akinamama wengi vijiji wana kawia kupata watoto na mwishowe huitwa wagumba. Lakini wale wa mijini huona *fertility Centre* au labda pengine mabingwa wa magonjwa ya kinamama.

Kwanini huduma kama hii pia isitolewa vijijini madaktari bingwa kwenda kuwasaidia akinamama kama hawa ambao labda matatizo yao pengine ni madogo madogo na baadaye wao pia kuweza kupata watoto wao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haiwezi ikatenga Bajeti maalum kwa sababu tu ya MEWATA, kama nilivyokuwa nasema nilivyojibu katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba huduma za afya zinatolewa na wadau mbalimbali na taasisi na asasi nyingine ikiwemo MEWATA.

Sisi Wizara ya Afya, tunapotenga Bajeti huwa tunatenga katika yale maeneo husika, kwa mfano tunapeleka pesa *Ocean Road,* ndiyo maana kwamba hawa MEWATA kama *pressure group* inapokuwa inafanya kampeni mbalimbali sisi tunachangia kama Serikali.

Kwa hiyo, itakuwa sio rahisi kama Serikali kuweza kuitengea MEWATA kwa sababu si MEWATA peke yake ambayo inashughulikia suala la saratani hapa nchini.

Kwa hiyo, kwa sababu sisi Wizara ya Afya kupitia kitengo cha *Ocean Road,* tunatoa kule. Kwa hiyo, watakuwa wanapata kule au katika pesa nyingine ambayo tutakuwa nayo sisi kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mheshimiwa kuhusu suala la Ugumba, nadhani hili tena limekuwa lingine ni jipya la kutaka tuweze kuwapatia akinamama *centres* au vituo ambavyo wanaweza wakapeleka matatizo yao ya ugumba.

Ninachotaka kusema tu ni kwamba ugumba kama mama yoyote anaona kwamba anashida ana tatizo la ugumba basi ni vizuri akaenda katika kituo cha kutolea huduma ambacho kiko karibu yake, mtaalam atamwona na ikibidi kama apate rufaa ya kwenda kwa daktari ambaye ni mtaalam zaidi au bingwa basi atapata hiyo rufaa.

Kwa sasa hivi hatutakuwa na uwezo wa kuweka wataalam ambao watashughulikia masuala ya uzazi hasa wale wenye matatizo ya ugumba katika maeneo ya ngazi ya vijiji. Kwa hiyo, tunaweza kulifanyia hivyo ili waweze kupata rufaa na huduma wataweza kuipata katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana maswali yamekwisha, na muda umeisha na naona nina orodha ndefu ya wageni. Kwa hiyo, ningependa muda mwingi utumike katika kujadili Wizara hii inayofuatia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madinia mbao ni Mke wake Bibi Blandina Ngeleja, naomba alipo asimame, ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu kuna Ndugu zake wengine yuko Bibi Kihigwa, Bibi Wejja, Ndugu Alex Balomi na mtoto wake Brian William. Kwa hiyo, naomba wasimame walipo, ahsanteni sana.

Halafu kutoka Wizarani na Taasisi zake kwanza kuna Katibu Mkuu Ndugu David Jairo, ahsante, Kamishna wa Madini Dr. Peter Kafumu, Kamishna wa Nishati, Ndugu Bashir Mrindoko, Mkurugenzi wa Mipango, Ndugu Inokavit Swai, Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi, Bibi Mhanga, Mhasibu Mkuu Bibi Waniha, Dr. Lutengano Mwakehesa, Mkurugenzi Mkuu wa *REA*, yeye ni mtu muhimu sana, wote karibuni sana. *(Makofi)*

Ndugu Haruna Masebu, Mkurugenzi Mkuu wa *EWURA,* Ndugu Ramadhani Khatibu - Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO,* Mkurugenzi Mkuu wa *STAMICO* Ndugu Gray Mwakalukwa, Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* Ndugu William Mhando, Mtendaji Mkuu wa *GST Dodoma,* Prof. Mruma, Mkuu wa chuo cha Madini Ndugu Stephano Ndambazi, Mkurugenzi mkuu *TPDS* Ndugu Yona Kiragane, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDS* General R. P. Mboma, wote kabisa ahsante na karibuni sana katika Ukumbi huu wa Bunge hapa Dodoma. *(Makofi)*

Tuna Mwakilishi kutoka wakala wa Nishati Vijijini, Ndugu Singi Madata, tuna Mtendaji M kuu wa *TMAA* Ndugu Paul Masanja. Pia wapo maafisa na Watumishi Waandamizi 147 wa Wizara na Taasisi zilipo chini ya Wizara hiyo ya Nishati na Madini, wote tunawakaribisha sana.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, ambao ni Mama yake Mzazi Ndugu Mariam Fivanu, mimi huyu ni dada yangu nimefurahi sana kukuona umefanya vizuri kumsindikiza Bwana mdogo hapa, yeye anafanya kazi yake vizuri.

Lakini yupo na mke wake Mheshimiwa Naibu Waziri huyu ni Ndugu Naima Mpwapwani, ahsante sana mama tumefurahi kukuona. Kuna mtoto wake Alia hakuja, amegoma. Kuna dada yake anakaa Boston Marekani, Regina, ama kwa umaarufu Mama Hawa, kuna wapwao zake Hawa na Hanifa watoto hawa nadhanai wa Mama Hawa, halafu kuna Shemeji yake Asna na Aisha. *(Makofi)*

Lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri ana wageni wengine viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya Mkuranga wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wilaya Mkuranga, Ndugu Ali Msikamo, Ndugu Msikamo ni maarufu sana kwa kazi aliyonayo mbele ya safari.

Kuna Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya, Ndugu Gilbert Kalima na Katibu mwenezi yuko Hassan Ndunda. Kwa hiyo timu nzima bado kuna Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Mkuranga Ndugu Ashura Mwago, ahsante sana. Kuna Diwani wa Kata ya Magawa, Mheshimiwa Juma Abeid, yupo na Mwenyekiti wa Wazazi mzee Khamis Mtutu ahsante sana, naona timu imekamilika kwa ajili ya ushindi katika Uchaguzi Mkuuu ujao wa mwaka huu Oktoba, 2010. (*Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Bujiku Sakila, ambao hakueleza uhusiano wake lakini yupo Ndugu Charles Yemba na Ndugu David Mulia na Ndugu Naftari Nongo, wengine ni wadogo sana basi karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Haroub Masoud ambao ni Bibi Asha Wakati, yeye anatoka Mjini Magharibi, yuko na mtoto wake sasa mtoto wake na Haroub nafikiri Abdi Salam Harou, yupo na mjukuu wake Ndugu Mtasim Subri na mjukuu mwingine Mkhari Sabri, Ramadhani Ali kutoka Wilaya ya Kati Unguja na yuko Ndugu Abdallah Khamis kutoka Wilaya ya Kati Unguja, karibuni sana tunashukuru kwa kuweza kufika hapa Bungeni hasa kutoka Upande wa pili, Zanzibar. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Janet Kahama, ambaye ni father Steven Gombera kutoka Visiga Seminary, Kanisa Katoliki Mkoa wa Pwani. Tuna wageni wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, hawa ni kada wa CCM Ndugu Abdullah Urembo, kuna Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Nyaso Musoma Mjini, Ndugu Paremo Peter, Mwenyekiti CCM, wewe ni mtu muhimu sana huko.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, ambao ni Mwenyekiti wa Kata, Mtimbira kiongozi Ndugu Yasin Mpira, Mwenyekiti wa Tawi

Lupilo, Ndugu Thabiti Ngong'ono, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Minepa, Ndugu Costatino Mbeya, Katibu Kata wa Yasofion, Ndugu Athony Matanda na Katibu Mwenezi Ndugu Peregreen Makambi.

Pia tuna Ndugu Selestine Makilika Katibu Mwenezi pia, tuna Ndugu Isaya Mugugulile Katibu Tawala Mkugira, tuna Ndugu Alfred Nyoka Katibu wa Tawi Biro Dar es Salaam, tuna Ndugu Amartus Ndangwe Katibu Tawi Biro Zambia, tuna Ndugu Expedito Lyangani Katibu Tawi Mkapa Kichangani.

Kuna Ndugu Wilson Kaweza Katibu Tawi Ikungua Kichangani, tuna Mjumbe na Mwanachana wa Mwembeni Ndugu Bakari Mwambungu, Mjumbe na mwanachama Ndugu Caritus Mlokota, Mjumbe na mwanachama Ndugu Haroub Kiharatu na Mwenyekiti wa Serikai ya Kijiji cha Malinyi Ndugu Kapanga Kiwanga. Wote karibuni sana mliofika hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tuna mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, ambaye amekuja kumwunga mkono katika kuwasilisha *Budget Speech* yake, ni mke wake mpendwa Bi. Fadhila, ahsante sana Mama. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 100 kutoka Martin Luther School, Dodoma na Walimu wao naomba wasimame, hii shule nadhani mnaifahamu iko hapa Dodoma, *Dar es Salaam Road* karibu na *St. Gasper.* Tumefurahi sana mmekuja. Pamoja nao yuko mtoto wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagana, ambaye anaitwa Joachim na rafiki yake Sunday bila shaka yupo. Nashukuru sana na ahsanteni sana walimu kwa kuwafunza watoto vizuri sana tunaona ni shule nzuri kupeleka watoto kwani ni *Boarding School.*

Kuna wanafunzi 22 na walimu 4 kutoka *World Vision* Simanjiro, ahsante sana kutoka Simanjiro ni mbali lakini karibuni sana na tunawatakia kukaa kwema hapa Dodoma nadhani mtajifunza mambo ya Bunge baada ya kukaa kikao hiki.Kuna mgeni wa Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Zeyuni Khamis, yeye ni Diwani Viti Maalum na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa CCM. Ahsante sana tutakutana huko kwenye mkutano Mkuu wa CCM kesho na keshokutwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Nishati na Madini wamewasilisha masahihisho kwenye kitabu cha hotuba, masahihisho hayo yameambatanishwa na dokezo hili nakala za kutosha kwa Wabunge wote zimeandaliwa. Kwa hiyo, kutakuwa na masahihisho kidogokidogo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Baada ya kusema hayo naomba tuendelee na shughuli zinazofuata. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa 2010/2011
### Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2009/2010.

Aidha, naliomba Bunge lako likubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, makadirio ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/2011. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwa pamoja leo.

Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Nishati na Madini kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, na kabla ya hapo aliniamini nitumikie Watanzania kupitia Wizara hii kwa nafasi ya Naibu Waziri kwa mwaka mmoja.

Aidha, nawapongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa uongozi wao madhubuti katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, pamoja na mipango na mikakati mingine ya kitaifa.

Vilevile, nawapongeza Mawaziri wote walionitangulia kwa kuwasilisha na kupitishwa bajeti zao. Aidha, nawaombea Waheshimiwa Mawaziri ambao hawajawasilisha bajeti zao tuwapitishie Bajeti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na wenyeviti wote wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa.

Nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa William Hezekiah Shellukindo na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, kwa michango, maoni na ushauri wao thabiti wakati wa uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/2011.

Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wanaonipa katika kusimamia na kuongoza Wizara, kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu ya sekta za nishati na madini, ili kuongeza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwa kuteuliwa kwao kuwa wabunge wa Bunge hili na Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema kwa kuteuliwa kwake kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Sengerema na viongozi wa Wilaya ya Sengerema kwa ushirikiano wanaonipa katika kuendeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo na Wilaya ya Sengerema na Taifa kwa ujumla. Naishukuru familia yangu, hususan mke wangu ambaye umemtambulisha Blandina na watoto wetu Brian na Brigette na wazazi wangu kwa kunitia nguvu na kunipa moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Lakini pia kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri namshukuru mgombea mwenza wake ambaye yuko hapa ambaye pia umeshamtambulisha kwa moyo na ushauri anaoumpa katika kusaidiana kuiongoza Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba, 2009 Taifa lilimpoteza kiongozi mahiri mzee wetu Rashid Mfaume Kawawa aliyekuwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu. Mwezi Novemba, 2009, Bunge lako lilimpoteza Mheshimiwa Siegfrid Seleman Ng'itu aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa. Aidha, kati ya mwezi Julai, 2009 na Juni, 2010, matukio ya ajali yalitokea katika machimbo ya wachimbaji wadogo katika sehemu mbalimbali nchini na katika mgodi mkubwa wa Bulyanhulu na kusababisha vifo vya jumla ya watu 32. *(Makofi)*

Natoa pole kwa familia za wafiwa, Bunge lako na wote walioguswa na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2009/2010, ulizingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; MKUKUTA; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Ahadi za Serikali Bungeni za Mwaka 2008/09; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2009/10 – 2011/12; Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2009/10, maeneo yafuatayo yalipewa kipaumbele: kukamilisha miradi ya kupeleka umeme kwenye makao makuu ya wilaya kulingana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005; kuimarisha Mfuko na Wakala wa Nishati Vijijini ikiwa ni pamoja na upelekaji wa umeme vijijini; kuboresha na kukarabati njia za umeme na vituo vya kupozea umeme katika gridi ya Taifa; kupanua mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili ya Songo Songo; kushiriki katika mikataba ya uzalishaji - *Production Sharing Agreements* (PSAs) kwa miradi ya Songo Songo na Mnazi Bay; kuwekeza katika mradi wa usambazaji wa gesi asili; kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta; uagizaji wa pamoja wa mafuta; kudhibiti bei na uchakachuaji wa mafuta ya petroli/dizeli; kuvutia utafutaji na uongezaji thamani madini; kutekeleza Mkakati wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini; kuendeleza ujenzi wa miundombinu muhimu ya ofisi za madini mikoani, Wakala wa Jiolojia na Chuo cha Madini Dodoma; kusimamia utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi; kuliboresha Shirika la Madini la Taifa - *STAMICO;* na kutunga sera na sheria mpya ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafanikio. Katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/10, Wizara ilipata mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuvuka lengo la ukusanyaji wa Maduhuli. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2010 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 65.2 ikilinganishwa na lengo la kukusanya Shilingi bilioni 48.5 kwa Mwaka 2009/2010 na hivyo kuvuka lengo la ukusanyaji kwa asilimia 34.4.

Hata hivyo, napenda kutumia nafasi hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 mapato hayo yalikuwa yameongezeka hadi shiling bilioni 70 na kwa maana hiyo kuvuka lengo kwa asilimia 44.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama ulivyosema hotuba yangu itasomwa na marekebisho yaliyogawiwa ambayo yanaendelea kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa upande wa sekta ya nishati mafanikio ni pamoja na kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya wilaya za Bahi, Kilolo, Kilindi na Uyui; kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa Serikali wenye uwezo wa kuzalisha MW 45 uliopo Tegeta, Dar es Salaam; kukamilika kwa mradi wa kupeleka umeme Ndanda - Nyangao – Masasi; kuanza ujenzi wa kuziunganisha wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi na eneo la Msimbati kwenye gridi inayotumia umeme wa gesi asili ya Mnazi bay; kukamilika kwa mchakato wa kuwapata wakandarasi wa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini; kukamilika kwa upelekaji umeme katika vituo sita (6) vya kusukuma maji Pangani, Mirerani na Orkesmet Wilayani Simanjiro; kuagizwa kwa mitambo 12 ya kufua umeme itakayofungwa katika Manispaa ya Sumbawanga (4) ambayo pia itafikisha umeme katika mji wa Namanyere ambao ni makao makuu ya Wilaya ya Nkasi, Kasulu (2), Kibondo (2) na Loliondo – Ngorongoro (4); na kukamilika kwa miradi ya kupeleka umeme Malya/Sumve, Mchinga A na B.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni pamoja na: kukamilika kwa mradi wa umeme wa nguvu za upepo wa kW 10 katika Shule ya Sekondari Wama Nakayama- Nyamisati Wilayani Rufiji; kupeleka umeme kwenye mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Mtakuja wilayani Moshi Vijijini; kukamilika kwa ufungaji wa mashine tano aina ya *ABC* zenye uwezo wa kufua umeme wa MW 1.25 kila moja hivyo kuzalisha jumla ya MW 6.25 katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Juni, 2010; kukamilika kwa ufungaji wa mitambo mitatu ya umeme yenye uwezo wa kufua MW 2.7 kila moja katika mji wa Somanga Fungu; kukamilika kwa mchakato wa kuwapata wakandarasi watakaoleta mitambo ya MW 100 (Dar es Salaam) na MW 60 (Mwanza); na kutangazwa kwa zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *MCC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika sekta ya nishati ni kukamilika kwa ujenzi wa mitambo 10 ya *bayogesi*, Songea vijijini*;*

kukamilika kwa ujenzi wa mashine za kutengeneza vitofali vya mkaa, wilayani Mpwapwa; kuzinduliwa kwa mradi mkubwa wa umeme wa jua *(Sustainable Solar Market Packages)* mkoani Rukwa; kusainiwa kwa Makubaliano ya Awali (MoU) ya kuandaa mkakati wa nishati ya tungamotaka kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya (EU); kukamilika kwa ujenzi wa vituo viwili, kimoja cha kushindilia gesi asili na kingine cha kujazia gesi asili kwenye magari jijini Dar es Salaam; kuongezeka kwa viwanda vinavyotumia gesi asili kutoka 26 hadi 32; kusainiwa kwa mkataba kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya Ophir wa utafutaji wa mafuta na gesi katika kina kirefu cha bahari mkoani Mtwara; na kusainiwa kwa mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya *Beach Petroleum* (Tanzania) Ltd wa utafutaji wa mafuta na gesi kusini mwa ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya madini, mafanikio ni pamoja na: kupitishwa kwa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010; kuanzishwa kwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA); kuanzishwa kwa ofisi ya Mpango wa Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (*Extractive Industries Transparency Initiative - EITI);* kutoa mafunzo kwa Wachimbaji Wadogo kuhusu usalama, utunzaji wa mazingira, biashara ya madini na masoko katika maeneo ya Wachimbaji Wadogo wa Ruangwa (Lindi), Mbinga (Ruvuma), Maganzo (Shinyanga), Igunga (Tabora), Makere (Kigoma), Sumbawanga na Mpanda (Rukwa), Songwe na Chunya (Mbeya); kukamilika kwa uchapishaji wa ramani za kijiolojia na kijiokemia za QDS 58, 74W, 74 - 77, na 94 - 95 katika wilaya za Kasulu, Kibondo na Urambo; kupiga marufuku uuzaji wa madini ghafi ya tanzanite yenye ukubwa wa zaidi ya gramu moja nje ya nchi; kukamilika kwa durusu ya mitaala ya Chuo cha Madini Dodoma ya jiolojia na utafutaji madini, uchimbaji na uhandisi wa uchenjuaji madini; kukamilika kwa ujenzi wa maktaba na nyumba mbili za watumishi wa Chuo cha Madini Dodoma; kutengwa kwa eneo la wachimbaji wadogo huko Winza, Mpwapwa; na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu nje ya nchi kutoka Dola za Marekani milioni 992.4 kwa mwaka ulioishia Desemba, 2008 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 1,036.46 mwaka, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto. Licha ya mafanikio yaliyopatikana, changamoto zifuatazo zilijitokeza katika utekelezaji: kuimarisha ukusanyaji zaidi wa maduhuli; kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini; kupata fedha za kutosha na kwa wakati; kuongeza uzalishaji wa umeme nchini; kukidhi ukuaji wa haraka wa mahitaji ya umeme; kupunguza gharama za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme nchini; kuhamasisha Watanzania kushiriki katika miradi ya ufuaji umeme; kupunguza upotevu wa umeme; kuondoa uchakachuaji na bei kubwa za mafuta; kuongeza kasi ya matumizi ya gesi asili na utafutaji wa mafuta na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni: kuongeza kiwango cha ukuaji wa mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa; kuongeza fungamanisho la sekta ya madini na sekta nyingine; kuboresha teknolojia na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wachimbaji wadogo; kutunza mazingira katika maeneo ya uchimbaji wa madini; kuondoa migogoro na kupunguza ajali katika maeneo ya uchimbaji wa madini; kuongeza wataalamu; na kuhamasisha ushiriki wa Watanzania katika miradi ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Nishati. Ukuaji wa Sekta na Mchango katika Pato la Taifa. Shughuli za umeme na gesi asili zilikua hadi kufikia asilimia 8.4 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2008. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutokana na gesi asili. Aidha, shughuli za umeme na gesi asili zilichangia asilimia 2.1 katika Pato la Taifa mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 2.0 katika mwaka 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Uzalishaji Umeme. Umeme uliozalishwa kwenye gridi ya Taifa uliongezeka hadi kufikia *Gigawatt-hour* (GWh) 3,290.25 mwaka 2009 ikilinganishwa na GWh 2,917.03 mwaka 2008, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme utokanao na gesi asili. Aidha, mahitaji ya juu (*Maximum Demand*) kwenye gridi ya Taifa yalifikia MW 755 Novemba, 2009 ikilinganishwa na MW 693.8 mwaka 2008 sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Hadi Mei, 2010 mahitaji ya juu yalifikia MW 791. Hata hivyo, uzalishaji haukidhi mahitaji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ongezeko la kasi ya mahitaji ya umeme, upungufu wa maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme, uchakavu wa mitambo na upotevu wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha Uzalishaji Umeme. Mwezi Desemba, 2009 Serikali ilikamilisha ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme unaotokana na gesi asili wa MW 45 uliopo Tegeta jijini Dar es Salaam. Kukamilika kwa mradi huu kumeongeza kiasi cha umeme unaozalishwa kutokana na gesi asili kutoka MW 291 mwaka 2008/09 mpaka MW 336 mwaka 2009/10. Uwezo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili umefikia MW 348, ikijumlishwa na MW 12 za kampuni ya Umoja Light ya Artumas.

Vilevile, mitambo mitatu yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 2.7 kila moja katika mji wa Somanga Fungu ambao ndani ya wiki hii majaribio yataanza kwa ajili ya kuwasha umeme katika eneo hilo, kwa kutumia gesi asili ya Songo Songo ulikamilika Juni, 2010. Aidha, mitambo ya IPTL ilitumika kuzalisha umeme wa dharura kuanzia Novemba, 2009 hadi Aprili, 2010. Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa kisheria ili kuwezesha mitambo hiyo kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili na mafuta mazito.

Umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 Ibara ya 43(b), Serikali imekamilisha upelekaji wa umeme katika Makao Makuu ya wilaya za Kilolo, Kilindi, Bahi na Uyui. Miradi hiyo ilitekelezwa na *TANESCO* kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini. Aidha, Serikali imekamilisha ufungaji wa mashine tano za aina ya *ABC* za *MW 1.25* kila moja katika mji wa Kigoma/Ujiji hivyo kuzalisha jumla ya *MW 6.25.* Mitambo hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Juni, 2010, ambacho kimefanya Manispaa ya Kigoma Ujiji kuwa na umeme wa ziada kuliko maeneo mengi sana nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Umeme Makao Makuu ya Wilaya na Vijijini. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 Ibara ya 43(b), Serikali imekamilisha upelekaji wa umeme katika Makao Makuu ya wilaya za Kilolo,

Kilindi, Bahi na Uyui. Miradi hiyo ilitekelezwa na *TANESCO* kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini. Aidha, Serikali imekamilisha ufungaji wa mashine tano za aina ya *ABC* za *MW 1.25* kila moja katika mji wa Kigoma/Ujiji hivyo kuzalisha jumla ya *MW 6.25.* Mitambo hiyo ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kupeleka umeme Mchinga A na B (Lindi) na Malya/Sumve (Mwanza), vijiji vya Mto wa Mbu (Arusha), Konga (Morogoro), mradi wa umwagiliaji Mtakuja (Moshi Vijijini) na mradi wa umeme wa nguvu za upepo na jua katika Shule ya Sekondari ya Wama Nakayama katika kijiji cha Nyamisati Wilayani Rufiji ilikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wakala wa Nishati Vijijini uliendelea kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme wa gridi vijijini, inayotekelezwa na *TANESCO* na wakandarasi binafsi. Mikataba imesainiwa kati ya *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini, kuwezesha wakandarasi kuanza utekelezaji wa miradi 41 kwenye mikoa 16 mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umeendelea kuhamasisha waendelezaji wa miradi iliyo nje ya Gridi ya Taifa ili waweze kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo husika. Katika kufanya hivyo, Wakala umeingia mkataba na mtaalamu wa kusaidia kuandaa Mpango wa Biashara (Business Plan) na upembuzi yakinifu wa mradi wa maporomoko ya maji yaliyopo kijiji cha Madege Wilayani Kilolo. Mradi huu unaomilikiwa na Dayosisi ya Iringa ya Kanisa la Roman una uwezo wa kuzalisha kiasi cha MW 2.4 za umeme. Mradi utakapokamilika jumla ya vijiji 24 vitaunganishwa. Aidha, Wakala unakamilisha zabuni ya kumpata mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa vyanzo 12 vilivyopo Mkoani Tanga na 22 katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Lengo ni kupata taarifa zitakazotolewa kwa wawekezaji walio tayari kuendeleza vyanzo hivyo. Vilevile, Wakala umetoa msaada wa kiufundi kwa ajili ya kukarabati mtambo wa kW 850 katika kijiji cha Mbingu na Mchombe Wilayani Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uzalishaji Umeme kwa Njia ya Maporomoko Madogo ya Maji. Wakala wa Nishati Vijijini ulipata ufadhili kutoka Sida kwa ajili ya kujenga uwezo wa kusimamia miradi, ununuzi na maandalizi ya uendelezaji wa vyanzo vidogo vya umeme. Upembuzi yakinifu wa maporomoko ya mito ya Mtambo na Nzovwe (Rukwa), Pinyinyi (Arusha) na Kwitanda (Ruvuma) ulifanyika chini ya ufadhili wa Serikali ya Norwe, kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuendeleza miradi hiyo. Serikali hiyo inagharimia upembuzi wa awali wa vyanzo vya umeme kwa kutumia nguvu za maji katika mikoa ya Iringa, Ruvuma na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njia za Kusafirisha Umeme. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuimarisha njia kuu ya usafirishaji umeme kutoka Iringa kupitia Dodoma, Singida hadi Shinyanga yenye urefu wa kilometa 650 kwa msongo wa kV 400 yamekalimika, baada ya mshauri kuwasilisha Serikalini taarifa ya upembuzi yakinifu wa Mradi. Kufuatia mkutano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo uliofanyika mwezi Aprili, 2010, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kufadhili sehemu ya Iringa – Dodoma yenye urefu wa kilometa 225 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 134.49, Benki

ya Maendeleo ya Afrika kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japani *(JICA)* itafadhili sehemu ya Dodoma – Singida yenye urefu wa kilometa 217, kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 129.71. Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB)* tafadhili sehemu ya Singida – Shinyanga yenye urefu wa kilometa 225, kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 134.49 na Shirika la Maendeleo la Korea *(EDFC),* litafadhili ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 36.06. Mradi huu utatekelezwa sambamba na usambazaji umeme katika vijiji vilivyopo kando kando ya njia hiyo. Utekelezaji utaanza baada ya Serikali kusaini mikataba na Washirika wa Maendeleo ifikapo Septemba, 2010 na Serikali kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea kusimamia ukarabati na kuimarisha mifumo ya umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro chini ya *Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP).* Mkandarasi ameteuliwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha umeme wa msongo wa kV 132/33, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro; kupanua vituo viwili vya umeme wa msongo kV 132 vya Ubungo na Ukanda wa Viwanda Na. III; vituo vipya vitatu vya umeme kV 132 vya maeneo ya viwanda, Mbagala na Kurasini; na njia kuu nne za umeme wa msongo kV 132 za Ubungo – Kurasini - Mbagala katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, Serikali ya Korea Kusini imeridhia ufadhili wa ujenzi wa njia kuu ya umeme kV 132 kutoka Kiyungi kwenda Njiro mkoani Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Kufua Umeme Dar es Salaam MW 100 na Mwanza MW 60. Katika kuongeza na kuimarisha uwezo wa uzalishaji umeme, *TANESCO* iliendelea na mchakato wa ununuzi wa mitambo ya MW 100 Ubungo II Jijini Dar es Salaam utakaotumia gesi asili na mtambo wa MW 60 Nyakato Jijini Mwanza utakaotumia mafuta mazito. Uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya mitambo hiyo umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kufua Umeme Kiwira MW 200. Katika jitihada za kuendeleza mradi wa Kiwira, Serikali ya China imeonesha nia ya kuwekeza katika mradi huo kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 400. Kulingana na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme wa Mwaka 2009 - 2033, Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira unatarajiwa kuzalisha MW 200 ifikapo mwaka 2012/13.

Mradi wa Kufua Umeme Kinyerezi MW 240. Makubaliano yamefikiwa kati ya *TANESCO* na Sumitomo Corporation ya Japani kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Mapendekezo ya kiufundi ya *Sumitomo Corporation* yamebainisha kuwa mtambo utakaojengwa utatumia teknolojia ya *combined cycle.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme wa Electricity V. Katika kutekeleza mradi wa *Electricity V. TANESCO* na Wizara ya Fedha na Uchumi walisaini makubaliano mwezi Februari, 2010 ili kuiwezesha Serikali kupokea Dola za Marekani milioni 50 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Mradi una lengo la kusambaza umeme katika vijiji, miji midogo na makao makuu ya wilaya katika mikoa ya Arusha, Shinyanga (Bukombe), Mwanza na Dar es Salaam. Mkandarasi kwa ajili ya kutathmini thamani ya mali za *TANESCO* alipatikana Mei, 2010 na atakamilisha kazi hiyo ndani ya

mwaka mmoja. Aidha, AfDB imeridhia tathmini ya zabuni ya kumpata Mshauri mwelekezi atakayesimamia Mpango Kabambe wa Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Mikoa Minne, ambaye ataanza kazi baada ya kusaini mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Makambako - Songea kV 132. Makubaliano kati Serikali ya Tanzania na Uswidi kwenye kipengele cha riba kilichokwamisha utekelezaji wa Mradi yalifikiwa mwezi Mei, 2010. Mradi utakapokamilika utafikisha umeme wa gridi ya Taifa katika miji ya Madaba, Songea, Namtumbo, Ludewa, Mbamba Bay na Mbinga. Mkandarasi atapatikana baada ya Serikali za Tanzania na Uswidi kusaini Mkataba wa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme. Serikali ya Japan kupitia shirika lake la maendeleo *(JICA)* inafadhili mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo ya Masaki, Mikocheni na *Oysterbay* kwa gharama ya shilingi bilioni 34. Uwekaji wa nguzo na uvutaji nyaya kuanzia Ubungo hadi Makumbusho umekamilika. Kazi ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme inaendelea. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa ruzuku kwa miradi miwili midogo ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika maeneo ya Mawengi (Ludewa) na Mapembasi (Njombe). Ujenzi wa miundombinu katika awamu ya kwanza ya mradi wa Mawengi (kW 150 kati ya kW 300) umekamilika. Hadi sasa nyaya zimetandazwa kwa wateja wapatao 300 zikiwemo taasisi za huduma za kijamii kama zahanati, vituo vya afya na shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *TEDAP* umeainisha vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme kwa kutumia maji na tungamotaka vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 80. Chanzo kimojawapo ni mabaki ya miwa (bagasse) inayozalishwa na Kiwanda cha Sukari cha *TPCL Moshi.* Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha *MW 20,* kati ya hizo MW 10 zitauzwa kwenye gridi ya Taifa ifikapo Agosti, 2010. Kwa sasa kiwanda kinazalisha MW10 ambazo zinatumika kwa mahitaji ya Kiwanda. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka kiwandani hadi sehemu ya kuunganisha na gridi ya Taifa unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Dunia ilitoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 25 mwezi Mei, 2010 ikiwa ni nyongeza ya fedha ya utekelezaji wa mradi wa *TEDAP,* kwa lengo la kuongeza kasi ya uwekezaji katika uzalishaji na uunganishwaji wa umeme. Kiasi hicho kitatumika kuwezesha benki za hapa nchini kutoa mikopo ya muda mrefu kwa waendelezaji wadogo wa miradi ya uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme Somanga Fungu. Mitambo mitatu ya kuzalisha umeme wa MW 2.7 kila mmoja ilikamilika mwezi Juni, 2010. Umeme utakaozalishwa na mitambo hiyo utasambazwa katika miji ya Somanga, Tingi, Nangurukuru, Kilwa Masoko na Kilwa Kivinje. Katika ufumbuzi wa muda mfupi miji ya Kibiti na Bungu itapata umeme kutoka mitambo ya Ikwiriri. Aidha, makubaliano yalifikiwa kati ya *TANESCO* na *TANROADS* juu ya uvushaji nyaya za msongo wa kV 33 katika Daraja la Mkapa lililopo mto Rufiji, ambapo Mkandarasi anaandaa michoro ili kazi hiyo ianze katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya *MCC:* Kufua Umeme wa Nguvu ya Maji ya Mto Malagarasi MW 8. Upembuzi yakinifu wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya mto Malagarasi ulikamilika mwezi Machi, 2010 na kuainisha kuwepo kwa konokono adimu *(rare specie).* Kulingana na taratibu za masuala ya kimazingira, utekelezaji wa mradi ulisimama. Hata hivyo, wafadhili wa mradi *(MCC)* wamekubali kufadhili upembuzi yakinifu mpya katika eneo la Igamba III kwenye mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha na Kupanua Usambazaji Umeme katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya. Upimaji wa njia za umeme katika maeneo hayo umekamilika. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa njia hizo itafunguliwa Julai, 2010.

Aidha, zabuni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme zilifunguliwa mwezi Mei, 2010 na uchambuzi unaendelea. Mkataba na mkandarasi unatarajiwa kusainiwa mwezi Julai, 2010. Maandalizi ya malipo ya fidia ya mali za wananchi watakaoathiriwa na mradi yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kujenga *Submarine Cable* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja. Mkataba wa ujenzi wa submarine cable kutoka Dar es Salaam hadi unguja ulisainiwa mwezi Mei, 2010 kati ya *MCA-T* na Kampuni ya *VISCAS* ya Japan. Uchambuzi wa zabuni za ujenzi wa vituo vya kupozea umeme unaendelea. Zabuni za ujenzi wa njia ya juu ya ardhi ya umeme wa msongo wa kilovoti 132 kutoka Ubungo hadi Ras Kilomoni kupitia Tegeta na Ras Fumba hadi Mtoni kwa upande wa Zanzíbar inafanyiwa mapitio ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuunganisha Gridi ya Taifa na Nchi Jirani. Serikali iliendelea na mpango wa kuunganisha gridi ya Taifa na gridi za nchi za Zambia na Kenya kupitia mradi wa *Zambia - Tanzania - Kenya Power Interconnector (ZTK).* Mradi huu ni muhimu kwa vile Tanzania ni mwanachama wa *Southern Africa Power Pool (SAPP)* na *Eastern Africa Power Pool (EAPP).* Uanachama wa Tanzania unatoa fursa ya kununua na kuuza umeme wa ziada. Mawaziri wa Nishati wa nchi wanachama wanatarajia kusaini mkataba wa makubaliano mwaka 2010/2011 utakaonadi Mradi huo kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Ibara ya 43(a) (iii), Serikali iliendelea na kazi ya upembuzi yakinifu wa Mradi wa Umeme wa Rusumo (MW 60), chini ya Nile Basin Initiative. Mradi utajenga kituo cha kuzalisha umeme na njia za usafirishaji (kV 220) kwenda kwenye gridi za Tanzania, Rwanda na Burundi. Aidha, Benki ya Dunia imeridhia kutoa msaada wa Dola za Marekani milioni tatu kwa ajili ya kuandaa mpango wa kulipa fidia *(Resettlement Action Plan).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ruhudji *MW 358.* Serikali iliendelea kufanya majadiliano na mwekezaji binafsi wa mradi *(Nordic-Group)* baada ya kuajiri mwelekezi wa kisheria *(Legal Advisor).* Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuajiri washauri wawili waliobaki *(Financial na Technical Advisors).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme wa *Stiegler's Gorge MW 2,100.* Mkakati wa Serikali ni kuendeleza mradi wa *Stiegler's Gorge* katika sehemu kuu tatu: kilimo cha umwagiliaji, kupeleka maji Dar es Salaam na kuzalisha umeme chini ya *RUBADA* iliyopewa mamlaka ya kuendeleza Bonde la Mto Rufiji. *RUBADA* inaendelea kufanya majadiliano na mwekezaji ili kuingia mikataba ya uendelezaji wa Mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma wa MW 400. Katika mwaka 2009/10 wawekezaji sita (6) kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kuzalisha umeme wa MW 400 kwa kutumia Makaa ya Mawe ya Mchuchuma walipatikana baada ya kutangaza zabuni ya kimataifa. Wawekezaji hao wametakiwa kuwasilisha mapendekezo ya mradi *(Request For Proposal).* Utafutaji Mafuta na Gesi Asili

Mheshimiwa Naibu Spika, majadiliano na Kampuni ya Beach Petroleum iliyoshinda zabuni ya kutafuta mafuta eneo la Ziwa Tanganyika Kusini, yamekamilika na mkataba ulisainiwa mwezi Juni, 2010. Mkandarasi anaandaa mpango wa ukusanyaji takwimu utakaowasilishwa Baraza la Mazingira. Pia, majadiliano yaliendelea na Kampuni za *Tullow Oil* (eneo la Ziwa Tanganyika Kaskazini), *Tower Resources* (eneo la Wembere) na Motherland (eneo la Malagarasi). Vilevile, takwimu zaidi za mitetemo ya 3D zilikusanywa katika kitalu Na. 2 cha Statoil na vitalu Na. 5 na 6 vya Petrobras. Takwimu hizi zitatumika kubainisha maeneo ya kuchimba visima mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima vinne vya utafutaji mafuta na gesi vilichimbwa katika maeneo ya Kilwa na Kampuni ya Dominion; Rufiji na kampuni ya *Maurel & Prom;* na Mikindani Kampuni ya *Tullow Oil.* Kisima cha Mafia kilianza kuchimbwa mwezi Agosti, 2008 na Kampuni ya *Maurel & Prom* na kilifikia tamati yake kwenye mita 5,600 chini ya usawa wa bahari. Kisima hiki kilionesha dalili za kuwepo kwa gesi asili na utafiti zaidi unaendelea kuthibitisha kuwepo kwa gesi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikamilisha majadiliano na kuingia mikataba na Kampuni ya *Ophir* mwezi Mei, 2010. Mikataba hiyo inahusu uendelezaji wa gesi asili ili kuzalisha *Liquified Natural Gas (LNG)* kwa ajili ya kuuza nje ya nchi, iwapo gesi nyingi itagundulika. Ukamilishaji wa mikataba hii utawezesha wawekezaji kuendelea kupanga uchimbaji wa visima vya utafutaji kwenye vitalu vya maji ya kina kirefu.

Aidha, *TPDC* ilichimba visima vifupi sita (6) vya utafiti katika mkoa wa Lindi ili kupata takwimu za miamba katika mabonde, kwa ajili ya kuboresha taarifa za kutangaza maeneo ya utafutaji mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchakachuaji na Bei za Mafuta. Hatua zilizochukuliwa na *EWURA* katika kupambana na tatizo la uchakachuaji wa mafuta na ukwepaji wa kodi, ni pamoja na: kutoza faini; kufuta leseni na au kufunga vituo

vinavyouza mafuta yasiyokidhi viwango; na kuhakikisha kuwa wahusika wanarekebisha miundombinu mibovu inayosababisha mafuta kuchanganyika na vimiminika vingine (mfano maji). Aidha, *EWURA i*mekamilisha taratibu za kuanzisha mfumo wa kuweka vinasaba (fuel marking) kwenye mafuta. Mwezi Juni, 2010, *EWURA* iliingia mkataba wa miaka miwili na Kampuni itakayofanya kazi hiyo. Sambamba na hilo, mfumo huu pia utahusisha maabara zinazohamishika *(mobile laboratories)* ambazo zitatumika katika kupima ubora wa mafuta na kutoa majibu ya papo kwa hapo. Kazi hii inatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *EWURA* imekamilisha maandalizi ya Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja. Mtaalamu Mshauri alikamilisha na kuwasilisha mapendekezo ya mfumo huo. Kanuni za Kusimamia Mfumo huo zinatarajiwa kukamilishwa ili ziweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji na Uwekezaji katika Miradi ya Songo Songo na *Mnazi Bay*. Ili kuiwezesha kampuni ya Artumas kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme katika maeneo mengine ya mikoa ya Lindi na Mtwara, Serikali imeingia mikataba na kampuni hiyo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu husika. Hadi kufikia mwezi Juni, 2010, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 13.7 kama sehemu ya mfuko wa kufidia bei za umeme *(National Tariff Equalization Facility (NTEF)* kwa sehemu hiyo. Aidha, Serikali kupitia *EWURA* ilitoa Msamaha wa Leseni *(Licence Exemption)* kwa *Artumas* pamoja na Kanuni za kukokotoa Bei za jumla na rejareja za umeme zitakazotumika katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Pia, kupitia mradi huo, miji ya Ndanda, Nyangao na Masasi imepatiwa huduma ya umeme. Makabidhiano kati ya *TANESCO* na *Artumas* yalitarajiwa kufanyika mwezi Mei, 2010. Hata hivyo, Artumas iliomba muda wa miezi miwili hadi Julai, 2010 kukamilisha taratibu zao kabla ya makabidhiano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* kwa kushirikiana na *Pan African Energy* imeanza kutekeleza mradi hamasishi wa kusambaza gesi asili iliyoshindiliwa *(CNG).* Mtambo wa kushindilia gesi ulizinduliwa Julai, 2009 na kituo cha kujazia gesi kwenye magari kilianza kutumika Februari, 2010. Magari 14 ya petroli yamewekewa mfumo wa kutumia gesi asili, nyumba 13 kwenye eneo la Mikocheni zimeunganishwa kwenye mfumo wa kutumia gesi asili na hoteli ya Movenpick imeanza kutumia gesi asili iliyoshindiliwa. Katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi 2010, matumizi ya gesi asili ya Songo Songo na *Mnazi Bay* yamewezesha Taifa kuokoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 2.27 na Dola za Marekani milioni 11 sawia, ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya mitambo ya umeme na viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nishati Mbadala. Uendelezaji wa Nishati Jadidifu na Mbadala. na mwezi Desemba, 2009, Serikali ilisaini mkataba na Mkandarasi *M/s Communication and Accessories* International wa Ujerumani kwa lengo la kutekeleza mradi mkubwa wa umeme wa jua *(Sustainable Solar Market Packages (SSMP).* Mradi huu ulizinduliwa rasmi mwezi Aprili, 2010 na utatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza imeanza kutekelezwa wilayani Sumbawanga. Umeme huo ambao unakadiriwa

kufikia *MW 1* utatumika majumbani, katika zahanati na vituo vya afya; shule za sekondari, vituo vya polisi, taa za barabarani na sehemu nyingine ambazo jamii hujumuika *(Community Centres).* Maandalizi ya awamu ya pili ya mradi yanaendelea kwa kufanya tathmini katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Ruvuma, Shinyanga na Tabora chini ya Kampuni ya *M/s Data Vision International (T) Limited* ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa kuendeleza matumizi ya umeme wa jua hadi sasa umefika katika mikoa 14, ambapo mikoa ya Tabora, Manyara na Singida imejumuishwa katika mwaka 2009/2010. Mradi unatekelezwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Uswidi na Tanzania. Jumla ya mafundi mchundo 156 na wafanyabiashara 167 walifundishwa namna ya kufunga na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme wa jua majumbani na kuboresha uendeshaji biashara. Mradi mwingine wa kuendeleza matumizi ya umeme wa jua unaofadhiliwa na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na *Global Environment Facility (GEF)* uliendelea kutekelezwa katika mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera na Shinyanga. Jumla ya mifumo 132 ilifungwa katika shule za sekondari, zahanati, vituo vya afya na polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika; Serikali, kupitia Wakala wa Nishati Vijijini chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia, iliendesha *Lighting Rural Tanzania Competition 2010* mjini Arusha, mwezi Aprili, 2010. Lengo la shindano hilo ni kuhamasisha matumizi ya taa za umeme wa jua ili kupunguza na hatimaye kuondoa matumizi ya taa za chemli, mishumaa na vibatari. Shindano hilo lilihusisha waendelezaji wa miradi ya nishati bora wapatao 81 kutoka ndani na nje ya nchi, ambapo washindi 10 walipewa takriban shilingi milioni 130 kila mmoja kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na utafiti wa rasilimali ya jotoardhi katika eneo la Songwe – Mbeya. Utafiti uliofanyika katika awamu ya kwanza ulibainisha kuwepo kwa rasilimali ya jotoardhi. Makubaliano ya Awali (MoU) ya utafiti wa awamu ya pili yalisainiwa mwezi Januari, 2010 kati ya Serikali na Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia ya Ujerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza maelekezo ya Ibara ya 43a (iv) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, kuhusu uendelezaji wa nishati ya upepo, Kampuni za Wind EA na Power Pool Limited zinaendelea na maandalizi ya kujenga vituo vya uzalishaji umeme wa *MW 50* katika mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji wa Bayofueli Nchini. Kikosi kazi cha kuratibu uendelezaji wa bayofueli nchini kimeundwa. Kikosi hicho kinajumuisha wajumbe kutoka: Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; *TPDC;* na TIC. Aidha, Hadidu za Rejea zilikamilishwa kwa ajili ya kuwapata wataalamu washauri wa kuandaa sera, sheria na muundo wa kitaasisi katika uendelezaji wa bayofueli. Washauri hao pia watabainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali kufuatana na tabianchi na ikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi Bora ya Nishati.Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa *SADC-ProBEC* iliendelea kuhamasisha matumizi bora ya nishati ya tungamotaka, hususan, kuni na mkaa kwa kutumia majiko sanifu. Jumla ya mafundi 147 walifundishwa juu ya matumizi bora ya nishati. Aidha, takriban majiko sanifu 17,000 ya kuni na mkaa yalisambazwa majumbani na katika taasisi mbalimbali. Pia, Mradi uliwawezesha wakulima wa tumbaku kujenga makaushio matano zaidi, hivyo kufanya idadi ya makaushio ya aina hiyo kufikia 18 mkoani Tabora.

Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu kuhusu uzalishaji umeme kutokana na mionzi ya jua, upepo pamoja na kuandaa Mpango wa Biashara (Business Plan). Katika mafunzo hayo wajasiriamali 150 walishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha ufanisi katika matumizi ya nishati *(energy efficiency and conservation)*, hususan matumizi ya vifaa na teknolojia zinazotumia nishati kwa ufanisi; na matumizi mbadala ya kuni na mkaa vikiwemo motopoa, gesi ya kupikia ya petroli *(Liquified Petroleum Gas - LPG)* na gesi asili kwa ajili ya kupikia na kwenye magari. Aidha, *TPDC* kwa kushirikiana na *Oryx* ilifanya utafiti juu ya namna bora ya kuhamasisha matumizi ya *LPG* maeneo ya vijijini, katika miji ya Mtwara, Kahama, Bariadi, Kigoma, Kasulu, Kibondo, Singida, Mpwapwa na Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini: Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kilikuwa asilimia 1.2 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2008. Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa kwa mwaka 2009 ulikuwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2008. Upungufu katika kiwango cha ukuaji na kushuka kwa mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kulitokana na mdororo wa uchumi duniani mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,075.94 mwaka 2008 hadi kufikia Dola milioni 1,103.41 mwaka 2009, sawa na ongezeko la takriban asilimia 2.6. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya dhahabu kwa asilimia 94. Thamani ya mauzo ya dhahabu iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 992.8 mwaka 2008, hadi Dola za Marekani milioni 1,039.46 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 4.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera na Sheria ya Madini. Serikali ilipitisha Sera Mpya ya Madini ya Mwaka 2009 mwezi Julai, 2009, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Madini ya mwaka 1997. Lengo kuu la Sera mpya ni kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa na kufungamanisha sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi ili kuchangia kupunguza umaskini.

Utekelezaji wa Sera hiyo unaambatana na kuandaliwa kwa mikakati ya Sera ya Madini, kutungwa kwa Sheria mpya ya Madini na kufanya marekebisho ya sheria nyingine zinazohusiana na usimamizi wa sekta ya madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kufikia malengo yake, Serikali ilitunga Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010 ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika sekta ya madini. Muswada wa Sheria hiyo ulipitishwa na Bunge mwezi Aprili, 2010. Sheria hiyo ilisainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Mei, 2010. Majadiliano na Kampuni ya Willcroft kuhusu Uendeshaji wa Mgodi wa Mwadui

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mabadiliko ya umiliki wa Kampuni ya *Wiliamson Diamonds Limited (WDL)* inayoendesha mgodi wa almasi wa Mwadui kutoka Kampuni ya Willcroft Limited, kwenda Kampuni ya *Petra Diamonds,* Serikali iliendeleza majadiliano na Petra Diamonds kuhusu namna bora ya kuendesha mgodi huo kwa faida. Masuala mengine yanayojadiliwa ni kuweka utaratibu wa kudumu wa uuzaji wa almasi zitakazozalishwa katika mgodi wa Mwadui. Kutokana na makubaliano ya awali, wataalamu wa Wizara hufanya tathmini ya awali ya almasi zinazozalishwa kabla ya kupelekwa kwenye mnada *Antwerp* – Ubelgiji kwa ajili ya kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko hayo ya umiliki na uendeshaji wa mgodi huo yanalazimu kurekebisha majukumu ya *TANSORT*. Katika majadiliano yanayoendelea kati ya Serikali na Petra, Mkataba mpya utabainisha utaratibu wa kuchambua na kuthamini almasi zinazozalishwa kwenye Mgodi wa Mwadui. Wakati huo huo, Serikali imehamisha kitengo cha *TANSORT* kilichokuwa London, Uingereza kuja nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendelezaji Wachimbaji Wadogo. Katika juhudi za kuwaendeleza wachimbaji wadogo, kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 38(d) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Serikali iliendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika sehemu mbalimbali nchini. Maeneo hayo ni Chakonko wilayani Same na Malagarasi-Ilagala mkoani Kigoma. Taratibu za kisheria kwa ajili ya kutenga na kugawa rasmi maeneo hayo kwa wachimbaji wadogo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza uchimbaji mdogo, Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kusaidia miradi ya uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani na utengenezaji wa zana na nyenzo za uchimbaji wa madini. Wizara ilitoa matangazo ya kukaribisha michanganuo kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya wachimbaji wadogo wa madini kutoka kwa taasisi, wajasiriamali, wachimbaji wadogo binafsi na vikundi vya wanawake wachimbaji, itakayogharimiwa na fedha zilizotengwa na Serikali. Miradi hiyo ni ya ukopeshaji wa vifaa vya uchimbaji, usanifu na uongezaji thamani madini. Washindi wamepatikana kwa ajili ya uanzishaji wa vituo vya ukodishaji wa vifaa vya uchimbaji mdogo katika maeneo ya Rwamgasa - Geita, Londoni - Manyoni na Pongwe - Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuwaelimisha wachimbaji wadogo, Wizara iliwapeleka wazalishaji watano wa chumvi nchini India kwenye mafunzo ya muda mfupi ya teknolojia bora ya uzalishaji chumvi. Vilevile, mwezi Mei, 2010 Wizara

iligharimia mafunzo ya ujasiriamali ya wachimbaji wadogo 34 yaliyofanyika Jijini Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasimu za miongozo ya kusaidia wachimbaji wadogo ziliandaliwa katika nyanja za: teknolojia ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini, usalama na afya migodini; utambuzi wa madini ya vito; utunzaji wa mazingira; na ujasiriamali katika masuala ya madini. Katika kutoa huduma za ushauri kwa wachimbaji wadogo, utambuzi wa sampuli za miamba zilizowasilishwa katika maabara uliendelea. Aidha, rasimu ya mwongozo wa "Namna ya Kutambua na Kuthamanisha Madini ya Vito kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini" iliandaliwa. Lengo ni kuwasaidia wachimbaji wadogo kutambua na kujua thamani ya madini ya vito.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uimarishaji wa Usalama, Afya na Utunzaji wa Mazingira Migodini. Ukaguzi wa migodi mikubwa ulifanyika ili kudhibiti matumizi ya kemikali na baruti na kuhakikisha usalama na afya ya wafanyakazi migodini.

Aidha, upitiaji wa rasimu za mipango ya ufungaji wa migodi (mine closure plans) ulifanyika kwa migodi ya Tulawaka, Golden Pride na Mwadui ili kuhakikisha usalama na utunzaji wa mazingira unazingatiwa katika mchakato wa ufungaji wa migodi hiyo. Wizara iliendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa maelekezo kwa wachimbaji wadogo juu ya uchimbaji unaohakikisha usalama na afya ya wachimbaji na jamii inayowazunguka.

Aidha, Wizara ilitoa maelekezo kwa kampuni za madini kuweka fedha kwa ajili ya kuwezesha ukarabati wa migodi ya madini *(rehabilitation bond)* kwenye ama *escrow account, insurance guarentee bond au bank guarantee bond.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika mgodi wa North Mara, ukaguzi wa mara kwa mara ulifanyika ili kuona maendeleo ya hatua zilizochukuliwa na Mgodi katika kukabiliana na hali ya mtiririko wa maji yenye tindikali katika mgodi huo. Kwa sasa tatizo hilo limedhibitiwa na ukaguzi wa kawaida unaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufuatilia malalamiko ya wafanyakazi wa mgodi wa *Tanzanite One,* Serikali iliunda Kamati ya Wataalamu kwa ajili ya kuchunguza malalamiko yao kuhusu madhara wanayodai kupata kutokana na kupitishwa kwenye mashine za mionzi *(x-ray body scanners),* ambazo zimefungwa mgodini hapo. Uchunguzi wa kitaalamu umethibitisha kuwa hakuna madhara yanayotokana na mionzi ya mashine hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi na Udhibiti wa Shughuli za Biashara ya Madini. Katika kuhakikisha kuwa madini yote yakiwemo madini ya vito yanaongezwa thamani hapa nchini kabla ya kusafirishwa nje, Serikali kupitia Tamko lake *(GN)* Na. 146 la mwezi Aprili, 2010 imepiga marufuku usafirishaji nje ya nchi madini ghafi ya tanzanite yenye uzito wa gramu moja na zaidi. Madini ya tanzanite yenye uzito chini ya gramu moja na madini mengine ya vito yataendelea kuruhusiwa kusafirishwa nje yakiwa

ghafi hadi hapo uwezo wa kuyaongezea thamani utakapoimarishwa hapa nchini. Hatua hii inalenga kuongeza ajira kwa Watanzania na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini *(SMMRP).* Mwezi Septemba, 2009 Serikali ilianza kutekeleza Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini *(Sustainable Management of Mineral Resources Project (SMMRP)* unaotekelezwa kwa miaka mitano. Chini ya Mradi huo, Wizara imefanya kazi za ukusanyaji wa takwimu kuhusu uchimbaji mdogo; ukusanyaji wa takwimu za kupima manufaa yatokanayo na uwekezaji mkubwa katika migodi ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi na Mwadui; kufanya tathmini ya kimazingira, kijamii na kisekta; na kuandaa utaratibu wa kusaidia wachimbaji wadogo kimitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini. Mafanikio yaliyopatikana mwaka 2009/10, katika kutumia mtandao wa *flexicadastre,* ni pamoja na kuongeza uwazi zaidi katika shughuli za utoaji na usimamizi wa leseni na kuongeza kasi ya utoaji wa leseni.

Katika kipindi hicho, jumla ya maombi 6,897 ya leseni za madini yalipokelewa, kati ya hayo, maombi 5,665 yalikuwa kwa ajili ya leseni ndogo za uchimbaji madini, yaani, *Primary Mining Licences (PML),* maombi 30 ya uchimbaji mkubwa na wa kati yaani, *Mining Licences (ML)* na maombi 1,202 kwa ajili ya leseni za utafutaji mkubwa wa madini yaani, *Prospecting licences (PLR* na *PL).* Jumla ya leseni 3,787 zilitolewa, kati ya hizo leseni 3,185 za uchimbaji mdogo, leseni 11 za uchimbaji madini wa kati na mkubwa, na leseni 591 za utafutaji madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yaliyojitokeza katika kutumia mfumo wa flexicadastre ni pamoja na kukosekana kwa mawasiliano ya mara kwa mara ya mtandao kati ya Makao Makuu ya Wizara na ofisi za madini zilizopo mikoani. Wizara inaendelea kulifanyia kazi tatizo hilo kwa lengo la kuboresha na kuimarisha zaidi utendaji kazi wa mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafutaji wa Madini ya Urani. Shughuli za utafutaji wa madini ya urani zinaendelea. Kutokana na kuwepo uwezekano wa kufunguliwa migodi ya urani katika maeneo ya Mkuju wilayani Namtumbo na Manyoni wilayani Manyoni, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuboresha usimamizi wa shughuli hizo katika utafutaji, uchimbaji, utunzaji, utumiaji na usafirishaji wa madini hayo. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kuandaliwa kwa rasimu ya "Kanuni za Madini ya Mionzi" ikiwemo madini ya urani.

Aidha, Wizara imepeleka watumishi wawili kwenye mafunzo ya muda mfupi juu ya taaluma ya mionzi. Pia, Serikali ya Marekani imejitolea kutoa mafunzo kwa Watanzania kuhusu taaluma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Asasi ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji *(Extractive Industries Transparency Initiative (EITI).* Kufuatia Tanzania kupewa uanachama wa awali mwezi Februari, 2009, Mheshimiwa Rais alimteua Jaji mstaafu Mark Bomani mwezi Desemba, 2009 kuwa Mwenyekiti wa Kamati Tekelezi ya *EITI* nchini.

Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2009/10, ni pamoja na kusainiwa kwa Makubaliano ya Awali kati ya Serikali na Kamati Tekelezi kwa lengo la kuonesha dhamira ya Serikali kushirikiana na Asasi za kijamii na kampuni za uziduaji, ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa uvunaji wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asili. Makubaliano hayo yataendelea kutumika wakati sheria ya kusimamia shughuli za *EITI* ikiandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za *EITI* zimejikita katika kuchanganua malipo yanayofanywa na kampuni za uziduaji kwa Serikali na taarifa kutolewa kwa umma kuhusu mapato yaliyopokelewa Serikalini kutoka kwenye kampuni hizo. Migogoro katika Shughuli za Madini

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kufanya tathmini ya maeneo yaliyo chini ya leseni za kampuni kubwa za madini, ambayo yanaweza kuachiwa kwa uchimbaji mdogo. Kazi hii ililenga kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 38(e) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Wizara imechukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro hiyo ikiwa ni pamoja na kuendeleza majadiliano ambapo wawekezaji wakubwa walikubali kuachia baadhi ya maeneo ya leseni katika maeneo ya Rwabasi, Tagota na Itandula wilayani Tarime, Mgusu wilayani Geita, Matabe wilayani Chato na Mkoro wilayani Mbinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya *Mining Inter-State Holders Forum (MISF)* imefanikiwa kutatua migogoro ya mipaka kati ya kampuni ya *Kazakh Mining Africa Ltd.* na wakazi wa kijiji cha Mwanangwa – Mabuki mkoani Mwanza. Aidha, usuluhishi wa mgogoro kati ya mgodi wa *North Mara* na wenyeji wa vijiji vinavyozunguka mgodi huo umefikia hatua ya kutiliana saini makubaliano ya amani ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uimarishaji wa Ofisi za Madini. Katika mwaka 2009/2010, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya ofisi za madini za mikoani, ambapo ujenzi wa ofisi ya Singida umeanza. Michoro kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Mwanza na Mbeya imekamilika. Tathmini ya gharama za ujenzi kwa ofisi za Mbeya na Mwanza inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(Tanzania Minerals Audit Agency (TMAA)* ulianzishwa mwezi Novemba, 2009 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245. Wakala umerithi kazi na majukumu yaliyokuwa yakifanywa na Sehemu ya Ukaguzi wa Dhahabu *(Gold Audit Program (GAP)* chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Majukumu ya Wakala ni pamoja na: kusimamia na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa na kuuzwa nje ya nchi na wachimbaji

wakubwa, wa kati na wadogo kwa lengo la kutathmini mapato stahili ya madini hayo na kuwezesha ukusanyaji wa mrabaha stahiki.

Majukumu mengine ni kukagua gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa na ya kati, kwa lengo la kukusanya taarifa sahihi za kodi na kuziwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na vyombo vingine husika vya Serikali; kufuatilia na kukagua shughuli za utunzaji wa mazingira katika maeneo ya migodi, bajeti iliyotengwa na matumizi ya fedha kwa ajili ya ukarabati endelevu wa mazingira na ufungaji wa migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Mei, 2010, jumla ya wakia 1,187,835 za dhahabu, wakia 357,237 za fedha na ratili 8,339,893 za shaba zenye thamani ya jumla ya Dola za Marekani 1,305,398,859 zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na migodi mikubwa ya *Golden Pride,* Geita, Bulyanhulu, *North Mara,* Tulawaka na Buzwagi. Jumla ya mrabaha wa awali *(provisional royalty)* uliolipwa na migodi hiyo kwa madini yaliyozalishwa na kuuzwa ni Dola za Marekani 34,841,134.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kukagua na kuhakiki hesabu za fedha za migodi mikubwa ya *Golden Pride* (kwa miaka ya 2003 hadi 2007), Buzwagi (kwa miaka ya 2006 hadi 2008), Geita (kwa mwaka 2007 na 2008) na *Tanzanite One* (kwa miaka ya 2004 hadi 2008) ilikamilika. Taarifa za uhakiki zimeandaliwa na zinaendelea kufanyiwa kazi na Wakala kwa kushirikiana na TRA na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kusimamia na kukagua shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira katika migodi ya Geita, *Tanzanite One,* Tulawaka na Buzwagi ilikamilika. Tathmini ya kiasi cha fedha zinazohitajika kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa mazingira na kufunga mgodi wa Buhemba ilikamilika. Taarifa za ukaguzi wa shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira kwenye migodi zinaendelea kufanyiwa kazi na Wakala kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na *NEMC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST.* Wakala wa Jiolojia Tanzania ilipima ramani mpya nane za kijiolojia na kijiokemia katika mkoa wa Kigoma katika *QDS 58, 74 – 77, 74W,* 75, 94 na 95. Uchoraji wa ramani hizo unaendelea. Aidha, ramani 11 za maeneo yaliyoko Kusini Magharibi ya Tanzania za *QDS 205 –* 211 na *QDS 224 - 227* zilichorwa katika mfumo wa elektroniki kutoka katika mfumo wa karatasi ili kurahisisha matumizi yake. Vilevile, ramani maalumu tano zilichorwa zinazoonesha vyanzo vya maji mkoani Dodoma, eneo la makaa ya mawe la Ngaka, eneo la madini ya chuma la Liganga, maeneo yenye vyanzo vya jotoardhi na eneo la kijiolojia la Rungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za matukio ya matetemeko ya ardhi ziliendelea kukusanywa katika vituo vya Dodoma, Kibaya, Kondoa, Babati, Mbeya,

Singida na Manyoni. Aidha, vituo 27 vya muda viliwekwa katika ukanda wa Pwani, maeneo ya Kusini na Kusini Magharibi mwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ramani maalumu ya Mlima Oldonyo Lengai inaendelea kutayarishwa kwa kushirikiana na Wakala wa Jiolojia wa Marekani *(United States Geological Survey).* Ramani hiyo itaonesha maeneo yaliyoathirika kwa uchafuzi wa mazingira na mpangilio wa miamba ya *volkano* katika eneo hilo. Lengo ni kusaidia kuelekeza wadau kuhusu matumizi ya eneo linalozunguka mlima huo kwa kuwa majivu yanayotoka katika volkano la mlima huo yana kemikali zenye sumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa matumizi ya madini ya viwanda kwa ajili ya kutengeneza matofali yanayohimili joto kali *(refractory bricks) na lining materials* ulikamilika. Wakala unaendelea na utafiti wa madini hayo kwa lengo la kupunguza matumizi ya nishati katika sehemu mbalimbali, hususan, kwenye shule, Magereza na hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umetoa mafunzo kwa wazalishaji wa chumvi wa maeneo ya Bonde la Ufa *(foot-hill salt producers)* katika mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara. Kutokana na mafunzo hayo, uzalishaji wa chumvi yenye madini joto uliongezeka kutoka asilimia 39 kabla ya mafunzo hadi asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati wa kuwezesha viwango vya maabara ya Wakala wa Jiolojia kutambuliwa Kimataifa, Wakala umejiunga na *Southern Africa Development Community Accreditation Certification (SADCAC).* Suala hili kitaifa linaratibiwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).* Chuo cha Madini katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Chuo cha Madini – Dodoma kilifanya kazi za kutoa mafunzo ya ngazi ya cheti na stashahada kwa jumla ya wanafunzi 210 katika fani za jiolojia na utafutaji madini; uhandisi katika uchimbaji madini; uhandisi katika uchenjuaji madini; kuendelea kukamilisha mtaala wa fani za mafuta na gesi *(Petroleum Engineering)* kwa kushirikiana na wadau; na kujenga uwezo wa kitaaluma na kitaalam ambapo jumla ya watumishi 15 walihudhuria mafunzo mbalimbali. Aidha, Chuo kilikamilisha ujenzi wa maktaba na nyumba mbili za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kukiunganisha Chuo cha Madini na Chuo Kikuu cha Dodoma ili kiwe sehemu ya Shule ya Uhandisi Migodi na Petroli *(School of Mines and Petroleum)* uliendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO.* Serikali ilianza mchakato wa kuiboresha na kuiimarisha *STAMICO,* ambapo taratibu za kurudisha mali za Shirika zilizokuwa zimehamishiwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania zimeanza. Aidha, Shirika lilianzisha na kusajili kampuni inayoitwa *Strategic Engineering Services Agency Limited* ambayo inamilikiwa kwa ubia kati yake na kampuni za *Elgin Group na Channel Construction (Pty) Limited* za Afrika Kusini. Lengo ni kuanzisha Kituo cha uhandisi mjini Dodoma cha kusanifu, kutengeneza na kukarabati vifaa na mitambo ya uchimbaji na viwanda vingine nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC.* Kituo kiliendelea kutoa huduma za kitaalamu kwa taasisi za madini za nchi wanachama pamoja na sekta binafsi inayowekeza katika sekta ya madini. Pia, kilishiriki katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya taaluma ya madini kwa kushirikiana na nchi wafadhili, hususan, Jumuia ya Ulaya na nchi mbali mbali za Afrika katika kutoa mafunzo kwa wataalamu kutoka nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Madini wa nchi wanachama wa Kituo cha Utafiti na Uendelezaji wa Sekta ya Madini *(SEAMIC)* kilichopo Kunduchi, Dar es Salaam ulifanyika mjini Dar es Salaam mwishoni mwa mwezi Mei, 2010. Nchi za Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* zilikaribishwa kushiriki kama watazamaji na kutoa ahadi ya kuanza mchakato wa kujiunga na Kituo hicho. Inatarajiwa kuwa nchi hizo zitakuwa zimejiunga ifikapo mwaka, 2011.

Mkutano ulitathmini utekelezaji wa majukumu ya kituo kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, ikiwa ni pamoja na kupitisha Mpango kazi na Bajeti ya Kituo kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira na Maendeleo ya Watumishi. Mwaka 2009/2010, Wizara iliajiri watumishi 98 wa kada mbalimbali pamoja na kuwapatia Mafunzo elekezi. Pia, iliendelea kujenga uwezo wa utendaji kazi kwa kuwapeleka mafunzoni watumishi 144. Kati ya hao, watumishi 13 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 131 ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara ilitoa huduma ya chakula na dawa kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wanaougua magonjwa nyemelezi yanayosababishwa na UKIMWI. Vilevile, Wizara kupitia Programu ya Kuboresha Utendaji Katika Utumishi wa Umma *(PSRP II),* imeanza kutayarisha Mfumo wa kupokea, kuhifadhi na kutumia kumbukumbu za watumishi kwa njia ya elektroniki. Ili kuboresha mfumo wa utoaji huduma kwa wadau, Wizara ilizindua rasmi Mkakati wa Huduma kwa Mteja *(Client Service Charter)* mwezi Agosti, 2009. Aidha, Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano pia uliandaliwa kwa lengo la kuimarisha mawasiliano na kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2010/2011. Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2010/2011, yamezingatia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2000 – 2015); Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya MKUKUTA; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Ahadi za Serikali Bungeni za Mwaka 2009/2010; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2010/2011 – 2012/2013; Maagizo ya viongozi wakuu wa Serikali; Kauli mbiu ya Serikali kuhusu KILIMO KWANZA na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Nishati. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika sekta ya nishati kwa mwaka 2010/2011 ni: kuendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye makao makuu ya wilaya na miradi ya umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini; kujenga mitambo ya kufua umeme ya *MW 100* Ubungo, Dar es Salaam na *MW 60* Nyakato, Mwanza; kuimarisha na kuboresha mifumo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuendeleza na kuhamasisha utafutaji wa mafuta na

gesi asili; kuimarisha na kupanua miundombinu ya gesi asili, kuendeleza taratibu za kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta na uagizaji wa mafuta kwa pamoja; kuhamasisha uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala; na matumizi bora ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya. Katika Mwaka 2010/11, Serikali, kupitia Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini pamoja na *TANESCO*, itaendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme makao makuu ya wilaya zilizobaki za Namtumbo (Ruvuma), Nkasi (Rukwa), Loliondo (Ngorongoro), Longido (Arusha), Bukombe na Kishapu (Shinyanga), Kasulu na Kibondo (Kigoma). Aidha, Wilaya ya Nanyumbu (Mtwara) itapatiwa umeme chini ya miradi ya Artumas.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji Umeme Vijijini. Kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, miradi 41 ya kusambaza umeme wa gridi vijijini katika mikoa 16 ya Tanzania bara itatekelezwa. Mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mbeya, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara na Shinyanga. Miradi hiyo itakapokamilika, jumla ya wateja wapya wa awali 20,000 wataunganishiwa umeme. Utekelezaji wa miradi hii umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, jumla ya wateja wapatao 5,000 katika Wilaya za Sumbawanga, Rungwe, Tandahimba, Newala, Songea Vijijini, Njombe na Ludewa wataunganishiwa umeme utokanao na maporomoko ya maji na umeme wa jua kupitia Vyama vyao vya Ushirika. Kazi hii itafanyika kupitia mradi wa *TEDAP (off grid)* ambao lengo lake ni pamoja na kuongeza uunganishwaji umeme kwa wateja vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa *Millenium Challenge Corporation (MCC)* ambao unaimarisha na kupanua usambazaji wa umeme katika mikoa sita (6), jumla ya vijiji 289 vitapatiwa umeme kama ifuatavyo: Mwanza (42), Tanga (129), Dodoma (45), Mbeya (18), Iringa (17) na Morogoro (38). Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika mikoa hiyo sita (6) zitafunguliwa mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa *submarine cable* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja ulisainiwa mwezi Mei, 2010 kati ya *MCA-T* na Kampuni ya *VISCAS* ya Japan. Aidha, uchambuzi wa zabuni za ujenzi wa vituo vya kupozea umeme unaendelea. Zabuni za ujenzi wa njia ya juu ya ardhi *(over head line)* ya umeme wa msongo wa *kV* 132 kutoka Ubungo hadi *Ras* Kilomoni inaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo ya kufua umeme Dar es Salaam *MW* 100 na Mwanza *MW* 60. Serikali itaiwezesha *TANESCO* kununua na kufunga mitambo ya kufua umeme wa *MW* 100 na *MW* 60 itakayofungwa Ubungo Dar es Salaam na Nyakato Mwanza sawia. Mitambo hiyo itaunganishwa kwenye gridi ya Taifa ili kuboresha upatikanaji wa umeme katika Jiji la Dar es Salaam na kwenye gridi ya Mikoa ya Kaskazini Magharibi mwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kufua umeme Kinyerezi *MW* 240. Serikali itaendelea na majadiliano na *Sumitomo Corporation* ya Japan iliyoonesha nia ya

kuendeleza mradi wa Kinyerezi wa *MW* 240 kwa utaratibu wa *turnkey*. Baada ya ujenzi, mitambo hiyo itamilikiwa na *TANESCO*. Sambamba na jitihada hizo, Serikali itasimamia upanuzi wa mitambo ya kusafisha na kusafirisha gesi asili ya Songo Songo ili kuhakikisha upatikanaji wa gesi katika kituo hicho na kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mnazi Bay *MW* 300. Serikali imesaini Makubaliano ya Awali na mwekezaji binafsi, Kampuni ya China *Machinery* ili kuendeleza mradi wa Mnazi Bay *MW* 300, pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Mtwara hadi kituo cha Singida kwa msongo wa *kV* 400. Majadiliano kati ya Serikali na mwekezaji yanatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2010 na utekelezaji wa miradi yote miwili ya ujenzi wa kituo cha kufua na njia ya kusafirisha umeme utaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Ruhudji *MW* 358. Serikali itaendelea kufanya majadiliano na mwekezaji binafsi wa mradi baada ya kuajiri washauri wawili waliobaki katika maeneo ya fedha na ufundi, ili mradi uanze kutekelezwa. Majadiliano yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2011 baada ya makubaliano ya ufadhili wa mradi kukamilika *(financial closure)* na mradi unategemewa kukamilika mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Stiegler's Gorge MW 2,100. Serikali kupitia *RUBADA* na wadau muhimu itaendelea kufanya majadiliano na mwekezaji wa mradi (*IDF*) ili kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa *Stigler's Gorge*. Serikali inaendelea kutafuta wawekezaji wengine kushiriki katika Mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Kufua Umeme Kiwira *MW* 200. Baada ya umiliki wa mgodi wa Kiwira kurudishwa Serikalini na kuwekwa chini ya *STAMICO* na *TANESCO*, Serikali itakamilisha majadiliano na Serikali ya China ambayo imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa mradi wa umeme wa Kiwira wenye uwezo wa kuzalisha *MW* 200 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ngaka wa *MW* 400. Katika mwaka 2010/2011 upembuzi yakinifu utakamilishwa ili kuwezesha uendelezaji wa mgodi wa makaa ya mawe na mradi wa kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme wa Makaa ya Mawe Mchuchuma wa *MW* 400. Katika mwaka 2010/2011, wawekezaji sita (6) walioshinda zabuni ya awali ya kuendeleza mradi wa umeme wa makaa ya mawe wa Mchuchuma wanatarajiwa kuwasilisha mapendekezo ya mradi huo, na mshindi anatarajiwa kupatikana ifikapo mwezi Septemba, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Kufua Umeme wa *IPTL MW* 100. Mitambo ya *IPTL* itaendelea kutumika wakati wa dharura, ili kuziba pengo la uzalishaji umeme pale inapotokea haja na dharura. Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa umeme wa ziada *(reserve margin)* kwenye mfumo wa uzalishaji umeme. Aidha, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na wataalamu wa Kampuni ya Wartsila juu ya kubadili mitambo ya *IPTL*, ili iweze kutumia mafuta na gesi kwa nyakati tofauti kwa kutumia teknolojia ya *dual fuel system* baada ya kumalizika kwa mashauri yaliyopo Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi na uboreshaji wa njia za kusafirisha umeme. Serikali itaendelea na upanuzi wa gridi ya Taifa kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida kwa msongo wa *kV* 400 na Makambako hadi Songea kwa msongo wa *kV* 132; upanuzi wa gridi ya Kaskazini - Magharibi yenye msongo wa *kV* 220 kutoka mkoa wa Mwanza hadi Mbeya kupitia mkoa wa Kigoma na Rukwa; kusimamia utekelezaji wa mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa *kV* 132 kutoka Ubungo hadi Makumbusho sambamba na kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Ubungo na Makumbusho. Aidha, kupitia mradi wa *TEDAP (on grid)* unaotekelezwa na *TANESCO*, ukarabati na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha utaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa sekta binafsi katika kuzalisha umeme. Serikali itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika miradi midogo ya uzalishaji umeme kati ya *kW* 10 na *MW* 10 kwa ajili ya kuuza kwenye gridi na nje ya gridi ya Taifa. Mikataba mahsusi ya kuuzia umeme *(Standardised Power Purchase Agreements – SPPA)* na inayotoa mwongozo wa bei za umeme *(Standardised Power Purchase Tariffs – SPPT)* imeanza kutumika. Lengo la utaratibu huu ni kupunguza muda wa majadiliano ya mikataba ili kuvutia sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza miradi midogo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji mafuta na gesi asili. Serikali inatarajia kukamilisha majadiliano ya mikataba miwili ya utafutaji na uzalishaji mafuta *(PSA)* na kampuni za *Tullow Oil* ya Ireland katika eneo la Ziwa Tanganyika Kaskazini na *Motherland Homes* ya India, katika eneo la Malagarasi. Kampuni ya *Ophir* itaanza kuchimba visima vya utafutaji wa mafuta katika Vitalu Na. 1, 3, 4 na *Petrobras* katika Vitalu Na. 5 na 6, kwenye kina kirefu baharini eneo la Mtwara. Aidha, kipaumbele kitawekwa katika kuvutia wawekezaji katika miradi ya kutumia gesi asili ya Msimbati kuzalisha mbolea, umeme na *methanol*. Matarajio ni kuongeza kiasi cha gesi kwa kuchimba visima viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika Miradi ya Songo Songo na Mnazi Bay. Serikali itatimiza azma yake ya kuipatia *TPDC* asilimia 50 ya fedha zinazotokana na mauzo ya gesi asili (*retention*), ili kuliwezesha Shirika kuchangia asilimia 20 ya gharama za uwekezaji katika uendelezaji wa uzalishaji wa gesi kwenye miradi ya Songo Songo na Mnazi *Bay*. Lengo ni kuiwezesha Serikali kufaidika kwa kupata mapato makubwa yanayotokana na rasilimali yake ya gesi asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Songas na *Pan-African Energy* zitaanza utekelezaji wa mradi wa kupanua miundombinu ya kusafisha gesi asili Kisiwani Songo Songo kutoka kiwango cha sasa cha futi za ujazo milioni 90 kwa siku na kufikia futi za ujazo milioni 200 kwa siku. Aidha, *EWURA* imeridhia utekelezaji wa mradi huo ambao unategemewa kukamilika ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* kwa kushirikiana na *Pan-African Energy* wataendelea na mradi wa uunganishaji gesi asili *(compressed natural gas - CNG)* kwa ajili ya matumizi ya majumbani na hotelini. Lengo ni kuunganisha nyumba zote za *TPDC* zilizopo Mikocheni, Dar es Salaam na hoteli kubwa za Kilimanjaro *Kempinsky*, *Southern Sun, Holiday Inn, Paradise* na *New Africa*. Pia, taasisi za Magereza Keko na Kambi ya Jeshi Mgulani, Jijini Dar es Salaam zitaunganishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(Bulk Procurement)*. Mfumo wa uagizaji wa mafuta wa pamoja utaanza kutumika mwaka 2010/2011, baada ya kukamilisha taratibu husika ikiwemo kutangaza kanuni za mfumo huo katika Gazeti la Serikali. Utaratibu huu utasaidia kupunguza gharama za uagizaji mafuta, msongamano wa meli bandarini, ukwepaji kodi, kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi na udhibiti wa ubora wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Udhibiti wa Bei na Uchakachuaji wa Mafuta. *EWURA* itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upandaji wa bei za mafuta katika soko la dunia na kutoa bei elekezi na kikomo zitakazotumika hapa nchini. Aidha, kama ilivyoelezwa na Waziri wa Fedha na Uchumi hapa Bungeni mwezi Juni, 2010, uwianishaji wa kodi za mafuta ni suala la msingi litakalofanyiwa kazi. Katika kipindi cha mpito, utaratibu wa kuweka vinasaba katika mafuta utaanza kutumika ili kukabiliana na tatizo la uchakachuaji mafuta. Pia, ukaguzi wa mara kwa mara utaendelea katika maghala, vituo vya mafuta na magari ya kusafirishia mafuta kwa lengo la kubaini na kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wasio waaminifu. Vile vile, mafuta yanayosafirishwa nchi jirani yatawekewa alama ili kudhibiti uchakachuaji na ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala. Katika kupanua wigo wa vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji umeme utokanao na maporomoko madogo ya maji, mionzi ya jua, upepo na tungamotaka. Wizara itaendeleza utafiti wa jotoardhi kwenye maeneo ya Songwe mkoani Mbeya ili kubaini ukubwa wa rasilimali hiyo, sambamba na kufanya tathmini ya kasi ya upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme mkoani Rukwa na kisiwani Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi bora ya nishati. Wizara kupitia mradi wa *SADC-ProBEC*, itaendelea kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya matumizi bora ya majiko sanifu majumbani na kwenye taasisi na uendelezaji wa teknolojia za kupunguza matumizi ya kuni katika makaushio ya tumbaku. Wizara kwa kushirikiana na mafundi waliofundishwa nchini inatarajia kusambaza majiko bora 26,000. Aidha, makaushio bora 100 ya tumbaku yanatarajiwa kujengwa na wakulima wa tumbaku Mkoani Tabora. Vile vile, chini ya Wakala wa Nishati Vijijini, miradi 10 ya kuhamasisha matumizi ya nishati bora vijijini ili kuondokana na vibatari, mishumaa, chemli na kandili itatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na wadau wengine, itaendelea kuandaa viwango vya ubora katika vifaa vinavyotumia nishati ya umeme. Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya

nishati ili kupunguza upotevu wa umeme majumbani, majengo ya taasisi, maeneo ya biashara na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini. Serikali katika kipindi cha mwaka 2010/11, itakamilisha mkakati wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kuandaa Kanuni za Sheria ya Madini. Katika kipindi hicho, Sera ya Madini ya Mwaka 2009 itatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kusambazwa kwa wadau. Aidha, utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 utalazimu kufanyia marekebisho baadhi ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali. Sheria zitakazofanyiwa marekebisho ni pamoja na Sheria ya Fedha za Kigeni Sura ya 271; Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332; Sheria ya Ardhi Sura ya 113; Sheria ya Utwaaji wa Ardhi Sura ya 118; Sheria ya Mazingira Sura ya 191 na Sheria ya Ushuru na Forodha Sura ya 403.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa uchimbaji mdogo. Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuendelea kutenga fedha za kuimarisha uchimbaji mdogo na kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Mfuko wa Kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Aidha, Wizara itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kwa uchimbaji mdogo na kuangalia uwezekano wa kuyatenga kwa ajili ya kuyagawa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini *(SMMRP),* Wizara itaendelea kuboresha huduma za ugani na kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo yakiwemo ya ujasiriamali kwa ushirikiano na wachimbaji wakubwa, *VETA, SIDO, SEAMIC* na Chuo cha Madini. Wizara pia itaendesha mafunzo kwa viongozi wa Halmashauri za Wilaya za Geita, Kahama, Biharamulo na Tarime kuhusu sekta ya madini, ili kuwezesha Halmashauri hizo kuandaa mipango ya maendeleo kwa kuhusisha kampuni za madini na jamii zinazozunguka migodi mikubwa. Mipango hiyo itahamasisha uwianishaji wa sekta ya madini na shughuli nyingine za kiuchumi Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongezaji thamani wa madini nchini. Kituo cha ukataji madini ya vito - Arusha *Gemstone Carving Centre* kitaboreshwa kwa kukipatia mashine zaidi za ukataji, usanifu na utengenezaji wa mapambo ya vito; madarasa yatakarabatiwa na kuajiri wakufunzi wenye fani hizo ili kituo hicho kiweze kutoa mafunzo ya elimu ya jemolojia, ukataji, usanifu vito na usonara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusimamia vizuri shughuli za uongezaji thamani madini na usonara nchini, sheria ya uongezaji thamani madini itaandaliwa. Sheria hii inalenga kuhamasisha uwekezaji, uendelezaji na usimamizi wa shughuli hizo ili ziweze kuleta manufaa zaidi kwa Taifa. Kuwepo kwa Sheria hiyo kutafanikisha utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ya kuwataka wachimbaji wakubwa kutenga sehemu ya madini yanayozalishwa kuongezewa thamani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini. Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa maelekezo kwa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji na

matumizi ya baruti, haviathiri usalama na afya kwa wafanyakazi na wananchi wanaoishi maeneo yaliyopo karibu na migodi hiyo. Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa migodi inatunza na kurudisha mazingira kwa kiwango kilichokubaliwa kupitia tathmini ya athari za mazingira na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira *(Environmental Management Plans- EMP)* za migodi hiyo. Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine kama vile *NEMC* na *OSHA* kufanikisha ukaguzi katika baadhi ya migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha upitiaji wa mipango ya kufunga migodi *(mine closure plans)* ya *Tanzanite One, Resolute,* Tulawaka na *North* Mara. Serikali pia itaendelea kujadili mipango ya ufungaji migodi ya Mwadui, Bulyanhulu, Geita na Buzwagi. Mipango hiyo husaidia Serikali kupanga viwango na aina ya dhamana ya ukarabati wa mazingira *(rehabilitation bond)* itakayowekwa na wawekezaji wa migodi husika. Lengo ni kuwa na dhamana ya ukarabati wa mazingira itakayotumiwa na Serikali kugharimia ufungaji na kurudisha mazingira ya mgodi husika katika hali stahiki inapotokea ulazima wa kufunga mgodi kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutoa mafunzo ya uchimbaji salama ili kupunguza ajali zinazotokea katika migodi mikubwa, ya kati na midogo. Ni matarajio ya Serikali kuwa wawekezaji katika migodi watatekeleza kwa vitendo kaulimbiu yao ya "Usalama Kwanza".

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mazingira na malalamiko ya fidia. Wizara kwa kushirikiana na taasisi zingine za Serikali, itaendelea kusimamia taratibu za hifadhi na udhibiti wa uchafuzi na uharibifu wa mazingira migodini, kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kufuatilia maendeleo ya hatua zinazochukuliwa na migodi katika kukabiliana na changamoto za utunzaji wa mazingira migodini. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine, itaendelea kusimamia malipo ya fidia kwa wananchi wanaoishi maeneo karibu na mgodi wa *North* Mara kwa kufuata sheria za fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji na uchimbaji wa madini ya urani nchini. Serikali itakamilisha kanuni za sheria kwa ajili ya kusimamia shughuli za utafutaji, uchimbaji, utunzaji, usafirishaji na biashara ya madini ya urani. Wizara itaendelea kukusanya taarifa muhimu kutoka nchi zinazochimba madini ya urani na taasisi zinazosimamia masuala ya mionzi na kuendeleza mawasiliano na wadau wakiwemo: Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomu na kampuni zinazojihusisha na utafutaji wa urani nchini, ili kukamilisha utungaji wa kanuni hizo. Aidha, Serikali itawapeleka watumishi nchi zenye uzoefu wa uchimbaji na usimamizi wa madini ya mionzi kama Marekani, Namibia na Australia kupata mafunzo ili waweze kusimamia vyema shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya urani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA).* Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania *(TMAA)* kwa lengo la

kuongeza mapato ya Serikali. Ukaguzi utakaofanyika utahusisha migodi mikubwa, ya kati na midogo kwa madini yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)*. Wakala wa Jiolojia Tanzania utafanya upimaji na utengenezaji wa ramani nne mpya za kijiolojia *(QDS* 159, 176, 194 na 212*)* katika Mikoa ya Singida na Mbeya; kufanya uchunguzi wa awali wa kijiolojia na madini katika maeneo mawili teule ambayo hayajafanyiwa uchunguzi; kuchapisha kijarida cha madini yanayopatikana katika wilaya za Tanzania Bara; kuendeleza uchunguzi wa vyanzo vya nishati ya jotoardhi kwa ushirikiano na wadau wengine hapa nchini; kuanzisha maabara ya utafiti wa mazingira na maabara ya jioteknolojia na uhandisi ili kukidhi mahitaji ya wateja wa Wakala wanaohitaji huduma hizo; kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchakataji, utunzaji na usambazaji wa taarifa za kijiosayansi hapa nchini; kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa Wakala kwa lengo la kuwapatia huduma bora wateja wa Wakala; na kuendelea kuimarisha miundombinu ya Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Madini. Kazi zilizopangwa kutekelezwa na Chuo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya maabara, karakana na zahanati na kuanza ujenzi wa viwanja vinne vya michezo; kuendelea kutoa mafunzo ya ufundi sanifu madini na kukamilisha mtaala wa kozi ya mafuta na gesi; kufanya marekebisho ya mitaala ili kukidhi matakwa ya wadau; kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wachimbaji wadogo na wadau wengine katika sekta ya madini na kuimarisha utendaji wa wakufunzi kwa kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* Sheria iliyounda *STAMICO* itarekebishwa ili iwiane na majukumu mapya ya Shirika hilo na Mpango wa Biashara *(Business Plan)* wa Shirika utaandaliwa. Kwa upande wa uwekezaji, *STAMICO* itakamilisha taratibu za kumpata mbia mpya wa Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef*. Aidha, kampuni ya *Strategic Engineering Services Agency Limited (SESA)* ambayo inamilikiwa kwa ubia kati ya *STAMICO* na kampuni za *Elgin Group* na *Channel Construction (Pty) Limited* za Afrika Kusini, itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Uhandisi katika eneo la viwanda Kizota - Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira na Maendeleo ya Utumishi. Wizara itaendelea kutekeleza mpango wake wa mafunzo kwa kuwapeleka mafunzoni watumishi 139. Kati ya hao, watumishi 42 watahudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 97 mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza na kutoa mafunzo zaidi kuhusu Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi *(OPRAS)*. Aidha, Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa kada zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini utaboreshwa ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na taasisi au mashirika yaliyopo chini yake, itaandaa Mpango Kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti na Kupambana na Rushwa. Kuhusu watumishi wenye virusi vya UKIMWI na wanaougua magonjwa nyemelezi yanayosababishwa na UKIMWI, Wizara itaendelea

kuwahudumia kadiri wanavyojitokeza. Tathmini ya hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika Wizara itafanyika ili kuweka mipango itakayosaidia kupunguza maambukizi hayo mahali pa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa Kimataifa. Katika mwaka 2009/2010, Wizara ya Nishati na Madini ilinufaika kwa misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za nchi za Jamhuri ya watu wa China, Japani, Kanada, Korea ya Kusini, Marekani, Uswisi na Ujerumani.

Vile vile, natoa shukurani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Umoja wa Ulaya, pamoja na mashirika ya *FMO, GEF, GTZ, IAEA, JICA, MCC, NDF, NORAD, ORIO, Sida, SAEDF, IFC, IDF, UNDP, UNIDO* na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. Katika Mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wengine katika kuendeleza sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wake mkubwa na thabiti anaonipa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, nawashukuru: Bw. David Kitundu Jairo, Katibu Mkuu, wakuu wote wa idara na vitengo, viongozi na watendaji wakuu wa taasisi na mashirika yaliyopo chini ya Wizara, wakiwemo wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Kamati zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini na taasisi zake kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa katika kipindi cha uongozi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 249,915,404,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2010/2011. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 184,001,395,000, kati ya fedha hizo shilingi 124,927,391,000 ni fedha za ndani na shilingi 59,074,004,000 ni fedha za nje; na

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 65,914,009,000, ambapo shilingi 11,768,071,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na taasisi au mashirika yaliyopo chini yake na shilingi 54,145,938,000 ni matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii, ninalo tangazo hapa. Mtu mwenye gari *Toyota Land Cruiser* Namba *T 991 BDZ* akutane na askari pale kwenye *gate*, aende sasa hivi.

Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii au Makamu wake. Eeh, Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu uekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa Fedha 2009/2010, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilikutana tarehe 3 Juni 2010, Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam katika Kikao ambacho Mheshimiwa William M. Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini aliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2009/2010 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Katika vikao hivyo, Kamati yangu ilipata fursa ya kufahamishwa mambo mbalimbali kuhusu Wizara kama ifuatavyo:-

(i) Dira na Madhumuni ya Wizara;

(ii) Uongozi na Muundo wa Wizara;

(iii) Majukumu ya Idara na Vitengo vya Wizara;

(iv) Maelezo kuhusu Taasisi zilizo chini ya Wizara; na
(v) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilijulishwa mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Wizara katika kipindi cha mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mwaka 2009/2010. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Wakati ikipitia Taarifa ya Wizara, Kamati iliridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa baadhi ya ushauri uliotolewa na kuzingatia kuwa baadhi ya ushauri unaendelea kutekelezwa. Aidha, kwa maeneo ambayo utekelezaji wake haukufanyika kabisa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa utekelezaji katika maeneo hayo ufanywe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009, maeneo yafuatayo yaliyopangwa kupewa kipaumbele:-

(i) Kukamilisha miradi ya upelekaji umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwa Wilaya zilizobaki kulingana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005;

(ii) Kuimarisha Mfuko wa Nishati Vijijini na Wakala wa Nishati Vijijini ikiwa ni pamoja na upelekaji wa umeme Vijijini;\

(iii) Kupanua mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili ya Songosongo;

(iv) Kuboresha na kukarabati njia za umeme na vituo vya kupozea umeme katika Gridi ya Taifa;

(v) Kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa mafuta, kushiriki katika mikataba ya uzalishaji – *(Production Sharing Agreements (PSAs)* kwa miradi ya Songosongo na Mnazi Bay; na uwekezaji katika mradi wa usambazaji wa gesi asili;

(vi) Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta.

(vii) Kuvutia utafutaji na uongezaji thamani Madini;

(viii) Kuimarisha Ofisi za Madini za Kanda zilizopo Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Mpanda, Mwanza, Arusha, Mtwara, Shinyanga, Singida na Mbeya kwa kuzijengea uwezo wa kukagua utafutaji, uchimbaji, biashara ya Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli;

(ix) Kutekeleza Mkakati wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini ili kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa;

(x) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu muhimu ya Wizara, hususan, Ofisi za Madini za Mbeya, Singida, Mwanza, Ludewa pamoja na Chuo cha Madini na Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)*;

(xi) Kuhakikisha mazingira ya maeneo ya Migodini yanatunzwa kwa usalama wa Wananchi;

(xii) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano kwa lengo la kueleimisha umma juu ya sekta za nishati na madini;

(xiii) Kuwezesha Wakala wa Jiolojia Tanzania kukusanya, kuchambua na kutunza takwimu na kujenga sehemu ya kuhifadhi sampuli za miamba *(core shades);*

(xiv) Kuwezesha uendeshaji na uendelezaji wa Chuo cha Madini Dodoma; na

(xv) Kuliwezesha Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* katika kutekeleza majukumu yake baada ya kuhuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010, Wizara ya Nishati na Madini ilipata mafanikio katika maeneo mbalimbali kama vile umeme, nishati mbadala, mafuta na gesi asili, madini pamoja na uendelezaji wa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa mafanikio yaliyopatikana, changamoto zifuatazo zilijitokeza katika utekelezaji:-

(i) Kutopata fedha za maendeleo zilizotengwa katika Bajeti za kutosha na kwa wakati;

(ii) Kuhitajika kupeleka umeme kwa kasi kwa Wananchi wengi Vijijini;
(iii) Kuhitajika kubuni mbinu nyingi katika ukusanyaji wa Maduhuli;

(iv) Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme Vijijini kutokana na kutopata fedha za kutosha;

(v) Kuwepo kwa mahitaji makubwa ya Umeme na uwezo mdogo wa uzalishaji wa Umeme nchini; na

(vi) Kuhitajika kwa ukarabati wa miundombinu ya umeme ili Kupunguza upotevu wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 86,926,200,000. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya shilingi 70,961,400,000 zitakusanywa na Idara ya Madini, shilingi 15,912,800,000 zitakusanywa na Idara ya Nishati na Petroli na shilingi 54,000,000 zitakusanywa na Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na Wizara ya Nishati na Madini katika kusimamia rasilimali za Nishati na Madini nchini. Kwa kutambua umuhimu wa rasilimali hizo katika kukuza Pato la Taifa, bado mapato yatokanayo na Rasilimali za Nishati na Madini hayaridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa changamoto hiyo, Kamati inapenda kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa hatua ilizochukua katika kuongeza ukusanyaji wa maduhuli katika Kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 ambapo jumla ya kiasi cha shilingi 59,450,920,919 sawa na asilimia 122.54 kimekusanywa.

Kamati imefarijika na makusanyo hayo na inashauri Wizara na Taasisi nyingine za uzalishaji ziige mfano wa Wizara hii. Kwa msingi huo, Kamati inatoa maoni na ushauri zilizo chini ya taasisi hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la makusanyo ya maduhuli nadhani ndilo ambalo tungelitilia mkazo zaidi tukusanye ili tuweze kupata na kupanga matumizi yake, kwa hiyo mkazo zaidi utiliwe katika makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (*Tanzania Minerals Audit Agency – TMAA)* ni Chombo kipya cha Serikali kilichoanzishwa mwezi Novemba, 2009 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa GN. 362 la tarehe 06 Novemba, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi aliochukua wa kuanzisha Wakala wa Ukaguzi wa Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala umeridhi kazi na majukumu yaliyokuwa yakifanywa na Kitengo cha Ukaguzi wa Madini *(Gold Audit Program – GAP)* kilichokuwa chini ya Idara ya Madini katika Wizara ya Nishati na Madini. Wakala huu ulianzishwa kwa ajili ya uimarishaji, ufuatiliaji na ukaguzi wa shughuli za uchimbaji madini ili kuongeza maduhuli ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miezi kumi sasa imepita tangu kuanzishwa kwa Wakala huu na katika kipindi hicho Wakala umeweza kufanya kazi kwa gharama nafuu za Shilingi Bilioni 3.4 kwa Mwaka 2007/2008 ikilinganishwa na gharama zilizokuwa zikitozwa na Kampuni ya *ASAGBC* za Shilingi Bilioni 16.4 kabla ya Wakala hawajaanzishwa ikiwa na maana kwamba kiasi cha Shilingi Bilioni 13 bakaa baada ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuupongeza Wakala huu kwa kazi nzuri zinazofanywa katika kusimamia na kukagua shughuli za uzalishaji na biashara ya Madini, kukagua hesabu za fedha za Migodi, shughuli za utunzaji wa mazingira na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa na kuuzwa na wachimbaji kwa lengo la kuongeza manufaa kwa Serikali kutokana na shughuli za uchimbaji kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala huu, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo Wakala unakumbana nazo katika kutekeleza majukumu yake. Kwa mfano, Wakala umekuwa ukilaumiwa kwamba unafanya kazi za Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Mtazamo na maoni ya Kamati ni kwamba Wakala huu umeanzishwa mahsusi kwa ajili ya kusimamia masuala ya ukaguzi wa Madini na mambo yote yanayohusiana na Madini.

Katika hili, Kamati inashauri kuwa ili Wakala huu uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa kujitegemea ubadilishwe na kuwa Mamlaka ya Ukaguzi wa Madini (*Tanzania Minerals Auditing Authority*) ili kuipa nguvu zaidi kiutendaji kama Mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inashauri kwamba Wakala uongeze juhudi katika kutoa elimu kuhusiana na majukumu yake ili uweze kufahamika kwa wananchi. Hii itasaidia pia kutoa uelewa kwa Wananchi wa namna Serikali inavyosimamia rasilimali za madini kwa sababu kwa muda mrefu Serikali imeonekana haisimamii eneo hilo. Sasa kiko chombo mahususi ambacho tunasema kipewe nguvu zaidi za kisheria na kuwa *authority* badala ya Wakala

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kasoro mbalimbali ambazo Wakala umezibaini katika ukaguzi iliofanya, Kamati inashauri kwamba kasoro hizo ziainishwe vizuri ili waweze kubaini zile ambazo wataweza kuzifanyia kazi na kwa zile zilizo nje ya uwezo wao waziwasilishe katika vyombo husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* unajukumu la kuwezesha, kuratibu na kuhamasisha uendelezaji wa miradi ya Nishati bora Vijijini ili ichangie ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na hivyo kuboresha hali ya maisha ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wakala umeweza kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Mkinga, Bahi, Uyui, Kilindi na Kilolo;

(ii) Kupeleka umeme katika Shule ya Sekondari ya Chief Oswald Mang'ombe Mkoani Mara;

(iii) Kupeleka umeme Matema *Beach* Wilayani Kyela;

(iv) Kupeleka Umeme katika Kijiji cha Ngage B, Wilayani Simanjiro;

(v) Kupeleka umeme katika Vijiji vya Mto wa Mbu Wilaya ya Monduli;

(vi) Kutoa fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa mali zilizoathiriwa na miundombinu ya bomba la gesi litokalo Songosongo Wilayani Kilwa hadi Jijini Dar-es-Salaam na kwenye maeneo ya wadau pamoja na miundombnu ya njia za umeme;

(vii) Kupeleka umeme kwenye pampu za maji katika maeneo ya Mererani Wilayani Simanjiro, Pangani na Orkesmet (Simanjiro);

(viii) Kuharakisha mpango wa usambazaji umeme wa Gridi Vijijini;

(ix) Uendelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kutokana na maporomoko ya maji;

(x) Kuhamasisha uendelezaji na matumizi bora ya Nishati;

(xi) Kugharamia ufungaji wa vifaa vya kupimia kasi ya upepo;

(xii) Kuwajengea uwezo waendelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini;

(xiii) Uanzishaji wa Mfuko wa Wawekezaji *(Credit Line);* na

(xiv) Kuendesha Shindano la Kueneza Matumizi ya Mwanga Bora Vijijini *(Lighting Rural Tanzania Competition).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uanzishaji wa Vyama Vya Ushirika vya Waendelezaji Nishati, hili ni mojawapo ya mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza bajeti ya 2009/2010. Kamati inapenda kuupongeza Wakala huu kwa hatua hiyo ambayo itasaidia waendelezaji hao katika vyama hivyo kubuni na kuendeleza vyanzo mbalimbali vya Nishati ambavyo vitasaidia kuondokana na tatizo la upungufu wa Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuuwezesha Wakala huu uweze kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi yake, Kamati inashauri kwamba, ni vema Serikali ikabuni vyanzo vingine vya fedha, mfano makato kutoka kwa watumiaji wa huduma za simu ambapo asilimia fulani ingepelekwa katika Mfuko wa Nishati Vijijini. Aidha, tozo linaloendelea kukatwa hivi sasa la asilimia 0.3 limesaidia sana katika upatikanaji wa fedha za kuendeleza miradi. Lakini pamoja na tozo hilo bado fedha imeonekana kutokukidhi mahitaji, ni vema kiwango cha tozo sasa kiwe asilimia 0.5 (0.5 %).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na miradi mingi kuchelewa kutekelezwa kwa wakati, Kamati inapenda kuisisitiza kwamba Serikali itoe fedha za kutosha na kwa wakati ili miradi husika iweze kutekelezwa na kuwapatia wawekezaji umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miradi ya umeme inahitaji vifaa vingi ambavyo huagizwa kutoka nje ya nchi, Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu wa kutoa ruzuku kwa vifaa vinavyoingizwa nchini kwa ajili ya shughuli za Umeme. Aidha, ili kuongeza matumizi ya Umeme wa Nishati ya Jua *(Solar Energy),* Serikali ione sasa umuhimu wa kuhimiza Wafanyabiashara kuagiza vipuri vingi kwa ajili ya matengenezo ya mitambo ya nishati ya jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu pia inashauri kwamba kwa miradi mbalimbali ya Umeme inayotumia Gesi, *REA* iendelee kushirikiana kikamilifu na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* katika kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu ya Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* katika Kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 Shirika limepata mafanikio yafuatayo:-

(i) Ukarabati wa vituo vya kuzalisha Umeme vya Kidatu, Kihansi, Mtera, Pangani *Falls* na baadhi ya Vituo vidogo vya Mafuta;

(ii) Upanuzi wa Umeme wa msongo wa Kilovolti 132 DSM kwa kujengwa kwa njia ya Ubungo hadi Kituo cha Oysterbay *(Oysterbay Substation);*

(iii) Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato kwa asilimia 19 kati ya Mwaka 2008 na 2009;

(iv) Kuanzishwa kwa matumizi ya teknolojia za kisasa katika mauzo ya umeme kwa njia ya *M-Pesa, Zap, NMB ATMs, CRDB na PoS.*

(v) Kuanzishwa kwa matumizi ya teknolojia za kisasa za transfoma zisizotumia mafuta, udhibiti wa Mita za umeme *(smart metering system)* kwa wateja wakubwa na mfumo mpya wa usambazaji Umeme (*High Voltage Distribution System).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado Shirika linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uwezo mdogo wa uzalishaji wa umeme unaofanya kuwepo na mgao wa umeme mara kwa mara;

(ii) Uchakavu wa miundombinu ya umeme unaosababisha upotevu wa umeme ufikiao asilimia 23 (23%) na kupelekea ubora wa umeme kuwa wa kiwango cha chini;

(iii) Uwezo mdogo wa Shirika kimtaji na hivyo kushindwa kuwekeza kikamilifu kwenye sekta ya umeme;

(iv) Wateja kutolipa bili zao kwa wakati;

(v) Upatikanaji mdogo wa fedha za utekelezaji wa miradi ya Kitaifa inayotekelezwa na Shirika;

(vi) Kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa wadau kuhusu gharama kubwa za kuunganisha umeme kwa wateja wapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo na ili kuhakikisha kwamba Shirika linatekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inapenda kuishauri Serikali ifuatavyo:-

(i) Serikali iliwezeshe Shirika kifedha na kuliongezea kasi ya utekelezaji wa Mpango Maalum wa kurekebisha hali ya kifedha ya Shirika *(Financial Recovery Plan).* Hatua hii ihusishe pia kuzihimiza Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na watu binafsi kulipa bili zao kwa wakati. Kwa vile Idara za Serikali zenye madeni ya zaidi ya Miezi Sita, basi kuwekwe utaratibu wa kukata fedha hizo kwenye bajeti zao kabla ya kuzipeleka kwenye Idara hizo.

(ii) Serikali ibuni vyanzo mbalimbali vya mapato vitakavyosaidia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya umeme ili kuzuia uharibifu na upotevu wa umeme;

(iii) Suala la Sheria ya upanuzi wa barabara ili kuruhusu miundombinu ya *TANESCO* iweze kupita vizuri, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ili iweze kukidhi mahitaji ya watoa huduma wengine kama Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka na *TANESCO*;

(iv) Kamati inashauri kuwa Mchakato wa kukamilisha mradi wa Umeme wa *MCC* katika Mkoa wa Kigoma uharakishwe ili maeneo husika yaweze kupatiwa umeme kama ilivyopangwa.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* una majukumu ya kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za kjiosayansi (jiolojia, Jiokemia na jiofizikia), kutengeneza na kusambaza ramani mbalimbali, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina ya mbalimbali za Miamba. Pia Wakala hufanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimali nchini na kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, maporomoka ya ardhi, mionzi asili na kadhalika. Vilevile Wakala husaidia Wachimbaji Wadogo hasa katika kubaini maumbile na aina ya mishapo yao, kutambua aina na ubora wa madini pamoja na namna bora ya kuchenjua madini yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majukumu yaliyoainishwa hapo juu, Kamati inapenda kuishauri Serikali kuendelea kuuwezesha Wakala kifedha ili uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo hususan katika kuwasaidia wachimbaji wadogo katika utambuzi wa madini na aina za mashapo pamoja na kutoa mafunzo endelevu kwa Watumishi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uboreshaji wa miundombinu na vifaa vya Wakala kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, changamoto iliyopo ni upatikanaji wa fedha. Kamati inashauri Serikali kuuwezesha Wakala kwa kuwapatia fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili lilianzishwa kwa madhumuni ya kujihusisha na shughuli zote zinazohusu Madini ambazo ni pamoja na utafuataji, uchunguzi, uchimbaji, uchenjuaji, utunzaji, usafirishaji, biashara na uongezaji thamani.

Shirika limeweza kutekeleza majukumu hayo, pamoja na mengine kwa kuingia Ubia na Kampuni nyingi au kwa kununua hisa, kutafuta Ufadhili katika Kampuni mbalimbali na vilevile kufanya kazi hizo lenyewe kwa kutumia mapato yake ya ndani yatokanayo na shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupitishwa kwa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Bunge lako Tukufu, Kamati inasisitiza Serikali kuwa, kutokana na sheria kuipa majukumu *STAMICO* kama msimamizi Mkuu kwa niaba ya Serikali wa Raslimali za Madini nchini, Kamati inashauri Serikali ikamilishe mchatako wa Marekebisho ya Sheria ya *STAMICO* ili iweze kukidhi matakwa ya Sheria mpya ya Madini ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mali za *STAMICO* ambazo ni Nyumba zilizouzwa, Kamati inashauri kwamba fedha zilizopatikana kutokana na kuuzwa kwa nyumba hizo, zikabidhiwe kwa *STAMICO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Migodi ya Kiwira na *Backree*f ambayo Kamati ilishauri kwamba iwekwe chini ya usimamizi wa *STAMICO,* Kamati inashauri kwamba Serikali iharakishe kutafuta fedha kwa ajili ya kuiwezesha *STAMICO* kuendeleza Migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC)* mwaka 1969, Shirika limeendelea na shughuli za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asili pamoja na ufuatiliaji wa maslahi ya Taifa kwenye soko la Petroli. Utafutaji wa mafuta nchini umekuwa ukifanywa chini ya Sheria ya Utafutaji Mafuta ya Mwaka 1980 na Mfumo wa Mikataba ni wa Mikataba ya Kugawana Mapato ya Uzalishaji *(Production Sharing Agreements (PSAs)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyogundulika kuwa na gesi asili, kwa mfano Songosongo, kwa sasa inazalisha Gesi katika mtambo wa umeme Ubungo (Dar-es-Salaam), Mnazi Bay (Mtwara) inayozalisha gesi asili na kutoa umeme kwa ajili ya maeneo ya Mikoa ya Mtwara na Lindi. Maeneo ya Mkuranga Mkoa wa Pwani na Nyuni karibu na Songo Songo yamegundulika kuwa na gesi asili mnamo mwaka 2007 na 2008 na tathmini zake zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, *TPDC* imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kunadi maeneo ya Utafutaji Gesi na Mafuta;

(ii) Ukamilishaji wa Mikataba ya (*PSA);*

(iii) Ukusanyaji wa Takwimu za mitetemo;
(iv) Visima vinne vya utafutaji vilichorongwa ambavyo ni Mihamba -1;

(v) Muhoro-1, Likonde-1 na Mafia Deep-1;

(vi) Urudishaji maeneo ya utafutaji *(Acreage Relinguishment)* kwa mikataba ya *PSA* iliyomaliza muda wake wa kipindi cha awali;

(vii) Uzalishaji Gesi Asili;

(viii) Mradi wa ukusanyaji wa takwimu za mitetemo ndani ya bahari *(Continental Shelf);*

(ix) Mauzo ya Gesi Asili;

(x) Mradi wa usambazaji wa Gesi Asili, Dar es Salaam; Mradi hamasishi *(Pilot Project)* wa matumizi ya Gesi Asili Majumbani na kwenye Magari na Taasisi;

(xi) Ushiriki katika mradi wa Mafuta ya biofueli; Utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kulitaka Shirika kushiriki ubia katika kampuni ya *SEKAB* na kuwasilisha Mkataba wa Hisa na Ubia kwenye Wizara ya Nishati na Madini;

(xii) Utekelezaji wa Agizo la Serikali la ufufuaji wa Kampuni ya Mafuta ya Kitaifa (*COPEC);*

(xiii) Kutayarisha Mpango wa Biashara *(Business Plan);*

(xiv) Mchakato wa kuanzisha Hifadhi ya Mafuta ya Akiba na Dharura;

(xv) Ufuatiliaji wa mwelekeo wa bei za mafuta duniani;

(xvi) Maandalizi ya Mradi wa kuzalisha mbolea itokanayo na Gesi Asili ya Mnazi Bay; na

(xvii) Maandalizi ya Utaratibu wa Kununua Mafuta kwa Wingi (*Bulk Procurement).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Kamati yangu iliishauri Serikali kupitia Hazina kuhakikisha kuwa katika kipindi hiki cha Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, *TPDC* inapewa asilimia hamsini *(Retention)* ya mauzo ya Gesi ili miradi husika iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Hazina imekubali utekelezaji wa azma hii na kwamba utaratibu huu utaanza katika mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua hii kwa kuwa itasaidia Shirika kujiimarisha kifedha ili liweze kuwekeza katika Miradi ya Ubia *(Joint Venture Arrangements)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Nchi inaondokana na tatizo la upungufu wa mafuta, kama ilivyokwisha kutoa katika miaka ya hivi karibuni, Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 iliipa *TPDC* jukumu la kuanzisha na kusimamia

Hifadhi ya Mafuta ya Akiba na Dharura nchini. Katika kutekeleza azma hii *TPDC*, imeanza mchakato wa kuifufua Kampuni ya Kitaifa ya Biashara ya Mafuta – *(Commercial Petroleum Company of Tanzania (COPEC)* ambayo itafanya kazi chini ya mfumo wa Kushirikiana na Sekta ya Umma (*Public Private Partnership)* kwa ubia na Kampuni itakayoshinda zabuni. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa juhudi hizo na kuishauri ihakikishe kwamba utaratibu huu unaanza kutumika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ulianzishwa mwaka 2006 ili kudhibiti Sekta za Nishati na Maji ikiwemo na sekta ya mafuta ya Petroli. Sekta ya Petroli hapa nchini imekuwa na ushindani mkubwa kuanzia Mwaka 2000 ambapo uagizaji wa Mafuta ya Petroli unafanywa na Kampuni mbalimbali ambazo sasa zimefikia takribani 20. Kuongezeka kwa Kampuni hizo kumepelekea pia kuwepo kwa ongezeko la Vituo zaidi vya uuzaji wa Mafuta ya Petroli ambavyo kwa sasa vimefikia takribani Vituo 700 ambavyo vimesambaa sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la uagizaji wa mafuta ya petroli nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inasimamia shughuli zifuatazo:-

(a) Kupokea maombi na kutoa leseni ya kufanya biashara ya Mafuta ya Petroli;

(b) Kupokea na kutoa vibali vya ujenzi wa Miundombinu; Kudhibiti ubora wa mafuta na miundombinu *(Quality and Standards);*

(c) Kuhamasisha ushindani wa haki katika biashara ya Sekta ya Mafuta na Petroli;

(d) Kutoa maagizo kwa wenye leseni, sambamba na Sheria ya Petroli au ya *EWURA*;

(e) Kutoza tozo mbalimbali kutoka kwa Wafanyabiashara kwenye Sekta kwa Mujibu wa Sheria; na

(f) Kuhakikisha kuwa shughuli za biashara ya mafuta haziharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2006 baada ya Mamlaka hii kuundwa, Mamlaka imefanya mabadiliko makubwa hasa katika kuhakikisha kuwa biashara ya uagizaji na uuzaji wa mafuta ya Petroli inafanyika kwa kuzingatia Sheria za nchi na kuweka uwanja wa ushindani ulio sawa wa biashara hiyo na unaozingatia matakwa ya watumiaji na kupunguza mazingira hatarishi ya ajali za moto na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazohusiana na biashara ya Uagizaji na Uuzaji wa Mafuta ya Petroli Nchini.

Changamoto hizo ziko kwa upande wa wafanyabiashara ambao hushindwa kutimiza masharti ya leseni na kubwa zaidi ni lile la uchanganyaji au uchakachuaji wa Mafuta ya Taa au ya Ndege kwenye Mafuta ya Petroli na Dizeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matukio mbalimbali ya uchakachuaji yaliyogundulika ni pamoja na lile linalohusisha magari ya Mheshimiwa Rais kuwekewa mafuta yaliyochakachuliwa huko Moshi hivi karibuni na urejeshwaji wa malori kumi na nane (18) nchini Tanzania kutoka Rwanda ambayo yaligundulika kubeba mafuta ya petroli yaliyokuwa chini ya kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa wakichanganya Mafuta ya Taa au ya ndege na hata hutumia vitu kama *ethanol, hexane, condensate* na kemikali zenye sifa zinazorahisisha uchakachuaji huo. Tatizo hili linasababisha athari nyingi zikiwemo za kiafya, ukwepaji wa kodi, uharibifu wa magari na mitambo mbalimbali na pia kusababisha ushindani katika biashara hiyo kwa upande wa nchi yetu kuwa mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya vituo vya mafuta vilivyopo njiani hasa sehemu za Mlandizi hadi Mdaula, Mkoa wa Pwani hutumika kwa ajili ya kufanya uchakachuaji huo kwa kutumia matenki makubwa na pampu za kusukuma mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kupambana na kutokomeza tatizo la uchakachuaji, Mamlaka imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye vituo mbalambali vya mafuta na maghala ya petroli. Katika Mwaka 2009 Mamlaka imeweza kukagua vituo na maghala 454 ya mafuta na magari ya usafirishaji wa mafuta yapatayo 35 na kuchukua sampuli 1,289. Kati ya sampuli hizo, sampuli 368 (30%) hazikukidhi ubora wa mafuta uliotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maghala hayo ni pamoja na lile la *British Petroluem Tanzania Ltd (BP) na Oryx Oil Tanzania Ltd* ambayo yote yalikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango na kupewa adhabu ya faini ya shilingi milioni kumi (10,000,000/=) za Tanzania na kufungiwa biashara kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) kila mmoja. Hata hivyo adhabu hiyo ilitenguliwa na Mahakama ya Ushindani wa Biashara (*Fair Competition Tribunal)* baada ya Kampuni hizo mbili kukata rufaa na kushinda na hivyo maghala hayo yalifunguliwa na kuendelea na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la uchakachuaji wa mafuta nchini limekuwa sugu, Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati maalum ikishirikisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ili kuondoa tatizo hili mara moja kwani linatuletea sifa mbaya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuishauri Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuwabana wafanyabiashara wa mafuta kwa kutumia vipengele vya Sheria zilizopo ili kuhakikisha wanafanya biashara kwa kuzingatia Sheria na kuwa na ubora wa mafuta unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, kuwekwe utaratibu maalumu wa kukabidhiana mafuta kati ya waagizaji na wanunuzi na kuweka kumbukumbu za viwango vya mafuta kabla na baada ya kupakuliwa. Aidha, adhabu za kosa la uchakachuaji ziongezwe maradufu ili ziwe fundisho kwa wakaosaji na wanaofikiria kuendeleza uchakachuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kwa mara nyingine kuipongeza Serikali kwa kuurejesha Mgodi wa Makaa ya Mawe, Kiwira Serikalini. Pamoja na kuchukuliwa hatua hiyo, Kamati imebaini kwamba miundombinu ya Mgodi huo hivi sasa imeendelea kuchakaa, wafanyakazi ambao wanaendelea kulinda mgodi huo kutolipwa mishahara yao kwa takribani miezi saba sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Bajeti ya 2010/2011, Mgodi wa Kiwira umetengewa fedha, Kamati inapenda kusisitiza kwamba kipaumbele cha fedha hizo kitumike katika kuwalipa Wafanyakazi wa Mgodi huu mishahara haraka iwezekanavyo ili waweze kuendelea kutunza miundombinu ya Mgodi huo. Aidha, Serikali iharakishe zoezi la ufufuaji wa mgodi huo ili uweze kuanza kuzalisha makaa kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua ilizochukuliwa za kutangaza rasmi Madini ya *Tanzanite* kuwa Kito maalum *(Specified Gemstone)* kwa mujibu wa kifungu cha 14A cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na kusitisha usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi nje ya nchi. Kwa kutambua kuwa Serikali na Watanzania kwa ujumla hawanufaiki na Madini ya Tanzanite kutokana na Madini hayo kuuzwa kwa bei ndogo yakiwa ghafi, zuio hili litasaidia Madini hayo kusanifiwa hapa hapa nchini na hivyo kuongeza dhamani yake na hatimaye nchi kunufaika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi April, 2009, Kamati yangu ilipokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi wa Mgodi wa *Tanzanite One* huko Mererani kuhusu athari wanazopata kutokana na Mashine za Mionzi *(X-Ray Body Scanners)* zinazotumiwa kwa ajili ya upekuzi. Uliunda Kamati Maalum ya kushughulikia suala hili na Kamati hiyo ilifanya kazi tangu tarehe 21/7/2009 na 3- 4/9/2009. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa uchunguzi huo umekamilika na Taarifa iliwasilishwa kwako tarehe 2 Julai, 2010 na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya mafanikio ambayo Serikali imeyapata katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010 ni kuanzishwa kwa Tasnia ya Uziduaji *(Extractive Industry Transparency Initiative - EITI).* Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Tasnia hii. *EITI* ni muhimu kwa sababu itaisaidia Serikali na Wawekezaji katika kuweka uwazi kwenye mapato yatokanayo na rasilimali za Madini na Gesi ambapo pande mbili yaani Mlipaji Kodi na Mpokeaji Kodi zitatakiwa kuweka wazi mapato na malipo ya Kodi. Hatua hii itawawezesha wananchi kujua mapato halisi ya Wawekezaji na kiasi halisi cha malipo kilichopokelewa na Serikali na hatimaye mapato hayo yalivyogawiwa au kutumika na Mwananchi wa kawaida alivyonufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuanzishwa kwa chombo hiki ambacho kitahusisha wadau mbalimbali, Kamati inaishauri Serikali kukitumia chombo hiki ipasavyo ili kuleta uhuru na uwazi katika mapato ya Rasilimali za Madini. Aidha, mikakati mahsusi iwekwe katika kuhakisha kwamba chombo hiki muhimu kinakuwepo kisheria, badala ya kutumia utaratibu wa makubaliano tu *(Memorandum of Understanding).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango ambayo Wizara ya Nishati na Madini imelenga kuitekeleza katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mambo yafuatayo ambayo Kamati imeyaona ni ya muhimu sana:-

Serikali itenge fedha zakutosha kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa kuweka kipaumbele kwenye uzalishaji wa umeme wa Makaa ya Mawe Kiwira na ule wa kutumia maji wa Kihansi na Ruhudji. Aidha, Serikali ifuatilie kwa karibu Mradi wa kuzalisha umeme chini ya Shirika la *RUBADA* huko Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mafuta kuwa la Muungano au la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanyie kazi kwa pamoja na kulitolea maelezo endelevu nao dumisha Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitishwa kwa Sheria mpya ya Madini ya Mwaka 2010, Serikali sasa iharakishe utungaji wa Kanuni zitakazosaidia utekelezaji wa sheria hiyo pamoja na kuanzisha wa Mfuko wa Madini kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. Hapa, Kamati inatoa Angalizo kuwa baada ya Sheria kutangazwa kutumika, inachukua muda mrefu kutumika bila Kanuni, hivyo Kamati inashauri kuwa Kanuni ziwekewe muda wa Kutungwa pengine miezi miwili (2) au mitatu (3) baada ya Sheria kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa miundombinu ya pamoja ya usambazaji wa Mafuta ya Petroli (*SBM)* lifuatiliwe kwa karibu na Serikali kwani kumekuwa na mvutano ambao unachelewesha utekelezaji wa Sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 kati ya Mamlaka ya Bandari *(TPA)* ambao ni Wamiliki wa Miondombinu hiyo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) ambao wamepewa jukumu kubwa la kuanzisha na kusimamia Hifadhi ya Mafuta ya Akiba na Dharura nchini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* ambao wamepewa jukumu la kupokea na kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu hiyo na Kampuni ya kuhifadhi Mafuta ya Petroli *(TIPPER).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshangazwa kwa kuwepo mvutano kati ya Taasisi hizi ambazo zote ni za Serikali. Kamati inashauri Serikali kuingilia kati na kumaliza mvutano huu kwa maslahi ya Taifa letu. Kamati yangu imekwishawasilisha suala hili kwako kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu gharama wanazotozwa Wananchi na Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kabla ya kuunganishiwa huduma za Umeme liangaliwe kwa undani kwani vifaa vyote vya usambazaji umeme toka kwenye nguzo hadi ndani ya nyumba za wananchi ni mali ya Shirika hilo. Hivyo hali halisi kwa mwananchi binafsi kutozwa gharama za miundombinu hiyo. Vinginevyo itaeleweka kuwa mwananchi yeyote baada ya kulipia vifaa hivyo vitakuwa mali yake binafsi na ana uwezo wa kuving'oa au kuvifanyia matumizi mengine. Vifaa hivyo ni Nguzo, Waya na Mita. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza na kuishauri Serikali kuondoa kabisa gharama za kulipia nguzo, wanya na mita kwa sababu ni mali ya *TANESCO* au Kampuni ingine yeyote itakayosambaza Umeme. Hili likifanyika mwananchi atabaki na jukumu moja tu la kulipia umeme aliounganishiwa na Shirika. Hata hivyo, kwa Kampuni za Biashara na uzalishaji ziingie Mikataba ya kuchangia gharama kwa sababu gharama hizo zinaingizwa kwenye gharama za jumla za mradi au Kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke utaratibu bora wa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili fedha hizo ziweze kutumika katika kutekeleza miradi hiyo kwa wakati. Kamati inasema hivi, kwa sababu Miradi muhimu na yenye mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa kama umeme wakati mwingine inachelewa kutekelezwa na kufanya gharama ziongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya ya Nishati na Madini chini ya Fungu 58 inaomba jumla ya Shilingi 249,915,404,000/= zinazoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha hizo Shilingi 65,914,009,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi 11,768,071,000/= kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Mashirika yaliyo chini yake, Shilingi 54,145,938,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(Other Charges)* na Shilingi 184,001,395,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo Shilingi 124,927,391,000/= ni Fedha za Ndani na Shilingi 59,074,004,000/= ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2010/2011. Pia nimshukuru Mheshimiwa William M. Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake Mheshimiwa Adam K. Malima, kwa ushirikiano wa dhati walioutoa wakati wa kujadili Bajeti hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu David Jairo, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii pamoja na Wataalam wote kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao walioonyesha wakati wa kuchambua Bajeti hii na kuridhia sasa iwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mjumbe; Mheshimiwa Lolesia J. M Bukwimba, Mjumbe; Mheshimiwa Asha M. Jecha Mjumbe; Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mjumbe; Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mjumbe; Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mjumbe; Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mjumbe; Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa, Mjumbe; Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mjumbe; Mheshimiwa Dk. James A. Msekela, Mjumbe; Mheshimiwa Omar Shekha Mussa, Mjumbe; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mjumbe; Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mjumbe; Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mjumbe; Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mjumbe; Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka, Mjumbe na Mheshimiwa Mohammed S. Sinani, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, amani na utulivu kama ilivyoainishwa katika dhima ya Bunge. Aidha, Kauli Mbiu yako ya kuliongoza Bunge hili kwa kasi na viwango *(Speed and Standards)* ilidhihirika waziwazi na sote ni mashahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakupongeza kwa dhati na kukutakia mafanikio mema kwenye kipindi kingine kinachokuja cha uchaguzi wa Mwezi Oktoba, 2010. Tuna imani kuwa Wapiga Kura wako wa Jimbo la Urambo Mashariki ni waelewa, waungwana na wenye upendo kwako na Taifa letu na kwamba hawatakosea katika uamuzi wao na kwamba watakuchagua kwa kura za kishindo. Nyie Wanyamwezi ni Watani wangu kwa hiyo, nawakumbusha kuwa hamchagui Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki tu, bali hata sisi ni Mbunge wetu Kitaifa. Fanyeni lililo jema kwenu na kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Bumbuli kwa imani kubwa waliyonipa ya kunichagua na kwa ushirikiano wao walionipa katika vipindi vitatu mfululizo ambavyo nimewawakilisha hapa Bungeni. Naamini wanakumbuka tulikotoka, tulipo sasa na mwelekeo wetu wa kutaka kwenda mbele zaidi. Watapima na kuamua nani awaongoze katika kipindi kijacho cha Uchaguzi tunaouelekea. Sifa za Mbunge ziko wazi katika Ibara ya Sitini na Saba (67) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msikubali kuchomekewa sifa za unyanyasaji wa kundi lolote la wananchi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashillilah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuwezesha Kamati hii mpya katika kipindi chote kufanya kazi zake kwa ufanisi bila matatizo yoyote.

Naomba pia niwashukuru kwa dhati Makatibu wa Kamati hii Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Stella Bwimbo kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuihudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mola wetu Mtukufu kwa kutujaalia sote hapa uzima na kuwajibika kwa kulitumikia Taifa letu. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni na ushauri kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu Na 99(7), Toleo la 2007 kuhusu mapato na matumizi ya Wizara nyeti ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa kuwa nimewasilisha mezani, naomba inukuliwe kama ilivyo katika *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Jimbo la Mkanyageni kwa upendo na ushirikiano wanaonipa kufanikisha kazi ya kulitumikia Jimbo, pia nawashukuru kwa kunipa kura nyingi za maoni lakini katika hili hakuna mshindi kwa sababu sote tulikuwa wa chama kimoja kwa hivyo ushindi ni wa chama chetu si vinginevyo.

Nikipongeze pia Chama changu cha *CUF* (Chama cha Wananchi) kwa kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni kwa kipindi cha miaka mitano inayokaribia kumalizika. Kwa maana hiyo nawaomba tena wananchi wa Mkanyageni pamoja na *CUF* wanirejeshe tena Bungeni katika Uchaguzi Mkuu ujao ili nitumie uzoefu wangu nilioupata kwa kuleta maendeleo zaidi Jimboni na kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijisikii faraja moyoni bila ya kukutaja wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Spika kwa uongozi wenu makini na mahiri uliosababisha Bunge hili la tisa kupata heshima kubwa ndani na nnje ya mipaka yetu. Halikadhalika Kiongozi wetu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Naibu wake Dr. Willibrod Slaa kwa ushupavu na ujasiri wao wa kuikosoa na kuishauri Serikali katika nyanja zote za Kisiasa, Kiuchumi na Kimaendeleo. Hakika busara na uzoefu wao ni hazina kubwa kwa Taifa hili na kwa maana hiyo niwaombe wananchi wa Jimbo la Wawi na Karatu wawarejeshe hapa Bungeni na chonde chonde wasije kufanya makosa katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio kwa umuhimu napenda pia nimpongeze Naibu wangu Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa msaada wake mkubwa katika matayarisho ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2009/2010. Napenda kulikumbusha Bunge lako kwamba, bajeti ya mwaka 2008/2009, Bunge hili liliidhinisha matumizi ya Wizara hii ya Shilingi bilioni 362.9(Sh. 362.922.265.600/=) lakini kiwango hicho kiliongezeka baada ya kufanyika uhamisho *(reallocation)* na kufikia Shilingi bilioni 368.8(Sh. 368.800.298.884/=) kwa maana ya ongezeko la Shilingi bilioni 5.87(Sh. 5.878.033.200/=).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Bunge likaidhinisha matumizi ya Shilingi bilioni 226.9 (Sh. 226.926.047.000/=) kwa mara nyingine kiwango hiki

kiliongezeka baada ya uhamisho *(reallocation)* na kufikia Shilingi bilioni 254.6 (Sh. 254.606.047.000/=) kutokana na kuongezeka matumizi ya kawaida kutoka Shilingi bilioni 55.279 (Sh. 55.279.578.000/=) hadi Shilingi bilioni 82.9(Sh. 82.959.578.000/=) kwa maana ya ongezeko la Shilingi bilioni 27.68. Sababu za uhamisho ni ununuzi wa mafuta ya mitambo ya kuzalisha umeme wa *IPTL* na malipo ya mishahara ya mgodi wa Kiwira na kuimarisha ukaguzi wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni kuwa mara ngapi bajeti za Wizara hii zitakuwa hazina uhakika na kila mwaka lijitokeze suala la uhamisho *(reallocation)*? Ni kiasi gani hasa kwa mwaka gharama zilizotumika kwa *IPTL* wakati Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilitoa hesabu ya Shilingi 20.038.410.493/= ($ 180.796.690) *(exchange rate* 1330) na Serikali hiyo hiyo kupitia Wizara hii ikatoa hesabu hizo kuwa ni Shilingi 24.917.379.000/= ($ 190.524.110). Jee ni ipi ya uhakika? Kiasi gani kililipwa mishahara ya Kiwira na ngapi kwa *TMAA*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya 2008/2009, mnamo Aprili 2009 Wizara hii ilikuwa imepokea asilimia 80.4 ya fedha iliyotegwa kwa matumizi ya kawaida yaani bilioni 39.179 kati ya bilioni 48.73. Kwa miradi ya maendeleo Wizara ilipokea asilimia 5.5 ya fedha zilizotengwa bilioni 17.57 kati ya bilioni 320.067.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Serikali itoe sababu na maana ya kufanya uhamisho ikiwa hata hiyo fedha iliyoidhinishwa na Bunge haikufikiwa ? Kwa hadithi kama hiyo tena mwaka jana 2009/2010, Bunge lako liliidhinisha shilingi bilioni 226.926, kiwango hiki kiliongezeka hadi shilingi bilioni 254.606 kwa sababu ya kuongezeka matumizi ya kawaida kutoka shilingi bilioni 55.279 mpaka shilingi bilioni 82.959 kufuatia uhamisho wa fedha *(re-allocation)* kwa ajili ya gharama za mafuta ya mitambo ya *IPTL*, malipo ya mishahara ya Mgodi wa Kiwira na kuimarisha ukaguzi wa madini *(TMAA)* ambao sina shaka nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 26 Mei 2010, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 40.95 tu. Kati ya kiwango hicho kilichopatikana asilimia 88.75 kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaani bilioni 73.632 kati ya bilioni 82.959 na ambapo kwa miradi ya maendeleo ni asilimia 17.91 kwa maana ya shilingi bilioni 30.744 kati ya bilioni 171.646 zilizoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo langu hapa nataka Bunge lako lijue kwamba katika kipindi cha miaka miwili mfululizo iliyopita (2008/2009 na 2009/2010) Wizara hii imekuwa ikifanya uhamisho (*reallocation*) na hasa katika bajeti ya mwaka jana ya shilingi bilioni 27.68 bila hata kutimiza kwanza fedha iliyoidhinishwa na Bunge kufikia kutolewa kiwango chake halafu ya ziada ikaombwa. Je, hii maana yake nini? Pili, mbona fedha ya maendeleo ni asilimia ndogo sana (5.5% - 2008/2009 na 17.9% - 2009/2010) lakini matumizi ya kawaida inapatikana tena kwa asilimia kubwa? (80.4% - 2008/2009 na 73.6% -2009/2010). Kulikoni hapa? Au ndio kusema tunapenda kutanuwa zaidi kuliko miradi ya maendeleo? Au ndio faida/hasara ya kutegemea wafadhili? Naitaka Serikali itoe ufafanuzi wa suala hili.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ya usambazaji umeme vijijini. Katika bajeti ya mwaka jana (2009/2010) miradi ya kusambaza umeme vijijini (kasma 3001 -3112 na kasma 3001 – 3113) ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 82.388 kati ya fedha hizi ni shilingi bilioni 7.832 tu ndio fedha za nje. Katika fedha hiyo miradi iliyopangwa kutekelezwa ni kupeleka umeme Magindu, Mbwewe, Malya/Sumve, Ihanja, Mvumi-Mlowa, Mchinga A&B, Mgwashi, Itiryo-Tarime, Bukene na Berega. Pia kwa ajili ya ununuzi wa majenereta ya Wilaya za Kasulu, Kibondo, Loliondo na Sumbawanga. Fedha hiyo pia inajumuisha matumizi kwa Wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wa nishati Vijijini ambao wana mkataba na *TANESCO* kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya za Kilolo, Kilindi, Uyui, Mkinga na Bahi pamoja na maeneo ya kiuchumi na huduma za kijamii ya Matema *Beach*, Sekondari ya *Chief* Oswald na Ngage B.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi hiyo ya usambazaji umeme vijijini, Serikali ilitoa shilingi bilioni 2.2 tu kati ya shilingi bilioni 10.6 ambayo ni asilimia 20.75 kwa miradi ya kusambaza umeme.Hiki ni kiwango kidogo sana na kwa mipango ya namna hii upatikanaji wa umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zilizobakia itachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa miradi iliyopewa kipaumbele katika mpango wa bajeti ya mwaka 2010/2011. Kwa mujibu wa taarifa ya *TANESCO* iliyotolewa kwa kamati ya Nishati na Madini ya mwezi Mei 2010 ibara ya 2.2.5(Umeme Vijijini), Wilaya 13 bado hazijapatiwa umeme ambazo ni:-

Kilolo, Rufiji, Namtumbo, Bukombe, Kasulu, Kibondo, Ngorongoro, Longido, Bahi, Nanyumbu, Nkasi, Kilindi na Uyui. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka huu Wilaya ambazo zimetajwa hazijapata umeme ni:-

Namtumbo(Ruvuma),Nanyumbu(Mtwara), Loliondo(Ngorongoro), Longido(Arusha), Nkasi (Rukwa), Bukombe na Kishapu (Shinyanga), Kasulu na Kibondo(Kigoma) na ambazo hazikutajwa katika bajeti ya mwaka huu ni Kilolo, Rufiji, Bahi, Kilindi na Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ni moja tafauti hizi zinatia mashaka ya kiutendaji na kwa kuwa Kamati husika haijapata kutembelea miradi hii hata siku moja ni vyema Mheshimiwa Waziri atufafanulie tatizo hili ,ili kupata ukweli halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hii imekuwa ikipangiwa fedha nyingi za ndani lakini utekelezaji wake umekuwa ni mgumu kutokana na upatikanaji wa fedha. Sote tumeshuhudia katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, fedha iliyopatikana kwa miradi ya maendeleo ni asilimia 5.5 na 17.91 kwa miradi yote ya maendeleo kwa ujumla wake.

Mhashimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kutoa Kauli ya Serikali hapa Bungeni siku ya terehe 2 Julai 2010

iliyofafanua miradi yote ya usambazaji umeme vijijini ambayo aliitengenezea jedwali linaloonyesha ukubwa wa mradi, muda wa utekelezaji ,gharama husika kwa kila mradi, kiwango cha umeme *(tension in KV)* na kampuni husika ya ujenzi wa mradi huo. Kwa mpangilio huo aliotuletea Mheshimiwa Waziri amezima kiu yangu kwa kutekeleza maombi ya kufanya hivyo katika bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana na kwa hivyo sasa itakuwa rahisi kwa Bunge lako hili kufuatilia utekelezaji halisi wa miradi ya kupeleka umeme vijijini. Taarifa hizo zilizopatikana zitaliwezesha Bunge lako kupitia Kamati husika kuelewa kwa kina mafanikio na mapungufu, ucheleweshaji mradi, matumizi ya fedha na ufuatiliaji wa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge, Nishati na Madini katika kipindi hiki cha miaka mitano inayomalizika haijapata hata siku moja kutembelea na kufuatilia angalau mradi mmoja wa kusambaza umeme vijijini na kujionea hali halisi ingawaje imeshatembelea baadhi ya vyanzo vya kuzalisha umeme pamoja na migodi/vituo vinavyozalisha gesi asilia. Huu ni udhaifu na fedha nyingi ya Serikali zinatumika katika miradi ya namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hii ya kupeleka umeme vijijini kwa bajeti ya mwaka huu pekee kasma 3001 – 3112 na kasma 3001 – 3113 imepangiwa shillingi bilioni 57.23 ambapo fedha za nje ni shilingi bilioni 5.848 tu. Hivyo itakuwa ni rahisi Bunge lako kufuatilia ikiwa pamoja na mambo mengine ikiwa mpango unaopendekezwa hapo juu utatekelezwa. Ni imani yetu kwamba hayo yakifanikiwa tutaweza kuwapunguzia mzigo wa lawama wanazobebeshwa *TANESCO*, Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* na Mfuko wa Nishati vijijini *(REF).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mitambo ya kuzalisha umeme ya dharura *(Emergency Power Plants).* Miradi hii ya dharura ilikuwemo katika bajeti ya mwaka jana kwa hivyo ni endelevu, ambayo ni *100MW* kwa kutumia gesi asilia utakaofungwa pale Ubungo kuziba pengo la *Dowans* na ule wa *60MW* wa kutumia mafuta mazito *(HFO)* utakaofungwa Nyakato Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka jana tulielezwa hapa Bungeni kwamba gharama za miradi hii ni Dola za Marekani milioni 120 sawa na Shilingi bilioni 168 na Dola za marekani milioni 80 sawa na shilingi bilioni 112 kwa mpangilio (*exch rate -1400)* na kwa bajeti hiyo ya 2009/2010 ilipangiwa shilingi bilioni moja milioni 750 kwa Ubungo na milioni 250 kwa Nyakato.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza la kushangaza ni kupewa kasma(*code*) tofauti katika ukurasa wa muhtasari ambayo ni 3001-3147 ukilinganisha na maelezo kamili katika randama ambayo ni 3001- 3137, katika bajeti hiyo ya mwaka jana. Lakini pia katika bajeti ya mwaka huu kasma ni tofauti pia katika muhtasari na katika maelezo kamili kama ilivyokuwa 2009/2010. Katika bajeti ya mwaka 2008/2009, kifungu 3001 – 3137 kilitumika kwa ajili ya Ubungo/*Emergency gas fired Power plant* kama ilivyoonekana katika muhtasari wa bajeti ya maendeleo na pia katika maelezo kamili. Mradi huo ulikamilika hivyo sioni sababu ya kutumika kwa kifungu hicho hicho kwa mradi mwingine mpya. Namwomba Waziri atupatie ufafanuzi wa kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili la kushangaza katika bajeti ya mwaka huu miradi hii inaombewa shilingi bilioni 49.543.391.000/= fedha za ndani na hakuna fedha za nje, ambapo katika maelezo ya kina mradi wa Ubungo unaombewa shilingi bilioni 26.543.391.000 na wa Nyakato unaombewa shilingi bilioni 20 kamili. Je. hii ziada ya bilioni 3 ambayo haikupangiwa popote inakwenda wapi? Ikiwa ni kosa la uchapishaji kwa nini litokee katika vitabu vyote? Kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi, jambo hili linatia wasiwasi mkubwa sana. Naomba Serikali irekebishe kosa hili haraka iwezekanavyo kuondoa tafsiri mbalimbali za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu la kushangaza ni kuwa hii mitambo ni ya dharura, lakini katika maendeleo ya utekelezaji tuliyoelezwa mwaka jana katika miradi yote miwili ni kuwa ununuzi wa zabuni umekamilika, wazabuni wanaendelea na matayarisho ya urejeshwaji wa zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu maendeleo ya utekelezaji hadi sasa ni kuwa zabuni zilifunguliwa tarehe 1 Aprili, 2010 uchambuzi wa zabuni ulikamilika na ripoti iliwasilishwa kwa Bodi ya Manunuzi tarehe 11 Aprili, 2010 kwa zabuni ya Ubungo na kwa upande wa Nyakato ripoti ilipelekwa tarehe 09 April, 2010. Swali la kujiuliza utekelezaji wa aina hii ndio kasi mpya? Miradi ya dharura zabuni zimechukua mwaka mmoja fedha iliyotengwa kwa miaka miwili ni bilioni 50.543, fedha inayohitajika kwa miradi yote miwili ni bilioni 280, je, kwa mwendo huu, dharura hii itakamilishwa kwa miaka mingapi kuziba hilo pengo la *Dowans* na ukosefu wa maji? Naomba ufafanuzi kwa Serikali ili Watanzania waelewe aina ya Ari na Kasi Mpya ya namna hii. Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa ujumla ni Shilingi 270 bilioni. Mradi huu wa Mwanza na Ubungo wa *160MW* peke yake thamani yake ni 280 bilioni! Hii maana yake ni kuwa Serikali haijapanga fedha za kutekeleza mradi huu, je, utatekelezwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii imechelewa sana wakati hali ya umeme nchini ni mbaya sana. Mahitaji ya umeme nchini yanakuwa kwa kiwango cha 15% kwa mwaka *(suppressed demand)* ambacho ni sawa na mara mbili ya ukuaji wa pato la Taifa. Nakisi ya umeme nchini ni 300 *MW*, lakini serikali inafanya mambo kana kwamba umeme umejaa nchini bwelele. Izingatiwe kuwa ni asilimia 14 tu ya Watanzania wenye kupata umeme. Kwa kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, imekubali kuanza kuwekeza katika uzalishaji wa umeme, tunashauri kuwa Mchakato huu wa zabuni ambao sasa umekwishakamilishwa uhamishiwe kwa mifuko hii kwa kuundwa kwa kampuni yenye Ubia wa *TANESCO* na mifuko hii ili mradi uanze mara moja na nchi iondoke mashakani katika suala la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kinyerezi *(gas fired power plant)* Mradi huu unahusu ujenzi wa Mtambo wa *240MW* katika eneo la Kinyerezi Dar es Salaam utakaofua umeme kutokana na gesi asilia. Matarajio ni kujengwa na kampuni ya *SUMITOMO* kutoka Japan na unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 560(*USD* milioni 400).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu wa Kinyerezi sio mpya kimaneno, labda nikumbushe kauli ya Waziri wa Nishati na Madini iliyotolewa tarehe 14 Februari 2006 hapa Bungeni Dodoma. Nanukuu: "Kwa kuwa nchi yetu imekuwa ikikumbwa na ukame na matatizo ya uzalishaji umeme mara kwa mara na ili kuondokana na hali hili kabisa siku za usoni, Serikali imeamua yafuatayo hapa yalitajwa mambo sita, nitaendelea kunukuu moja tu, nalo ni:-

Kufanya maandalizi ya kujenga kituo cha umeme wa gesi hapo Kinyerezi cha *300MW* kwa kushirikisha taasisi za umma za hapa nchini. Kituo hiki kinaweza kukamilika miezi 12 – 18." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni hizi kauli na mipango ya Serikali ambazo hazina utafiti wa kutosha na mwendelezo wa ufuatiliaji ulio makini. Mradi huu katika *PSMP* iliyotengenezwa kwa kutumia gharama kubwa ya *USD* milioni 2, ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili, Kinyerezi 1,*100MW* mwaka 2009 na Kinyerezi 2,*100MW* mwaka 2010. Baadaye katika mpango ulioitwa Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme 2009 – 2033 (2009 *PSMP UPDATE)* katika semina iliyotolewa mwezi July 2009, ukumbi wa Pius Msekwa tukaelezwa kwamba utekelezaji wa mradi huu wa Kinyerezi *240MW* na kuanza uzalishaji hapo ifikapo mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hii kauli ya mwisho bado haitekelezeki hasa ukitilia maanani muda uliotumika kwa mradi wa Tegeta wa *45MW* na kubwa zaidi gesi ya kuendesha Mtambo huo haipo kutokana na miundombinu. Kwa taarifa na ukweli wa mambo ni kwamba hivi sasa umeme unaozalishwa kutokana na gesi ni wastani wa wa *336MW* (Songas 191*MW, TANESCO Ubungo100MW*, *TANESCO* Tegeta *45MW*). Mitambo hiyo kwa jumla inatumia gesi futi za ujazo milioni 83 *(mmscfd)* kwa siku. Ongezeko la Mtambo mwingine mpya wa gesi unaotaka kufungwa Ubungo wa *100MW* kuziba pengo la *Dowans* kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, maana yake tutafikia uzalishaji wa umeme wa gesi wa kiwango cha *436MW* na kupelekea ongezeko la matumizi ya gesi kufikia futi za ujazo milioni 108 *(mmscfd)* kwa siku kwa mitambo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo uliopo hivi sasa wa mitambo ya kusafisha gesi ya Songo Songo *(Processing Plant)* ni futi za ujazo milioni 70 *(mmscfd)* ambao unaweza kuongezwa kwa mbinu maalum hadi futi za ujazo milioni 90 *(mmscfd)* bila ya kujenga Mtambo mwingine. Sio hilo tu,uwezo wa juu wa kusafirisha gesi hiyo (*maximum pipeline capacity)* ni 105 *mmscfd* tu.Hii ni kutokana na kikwazo cha bomba la inchi 12 lilioko baharini (Songo Songo - Somanga Fungu 25 Kilomita) pamoja na bomba la nchi kavu la Somanga – Dar es Salaam la inchi 16(207Km).

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miujiza gani Mheshimiwa Waziri atakayofanya ya kujenga Mtambo wa Kinyerezi wa *240MW* na kukamilika 2013 bila kwanza ya kuwepo mtambo mwingine wa kusafisha gesi na bila ya kupanua miundombinu ya usafirishaji? Ni vyema Bunge lako na Watanzania tuelezwe ukweli sio kuburuzana namna hii. Shirika la *TPDC* kwa mkopo kutoka *NSSF* wana mradi wa kupanua uwezo wa kuzalisha Gesi Songosongo. Serikali imechukua hatua gani kuiwezesha *TPDC* kukamilisha

mazungumzo na *NSSF* ili mradi huu uanze? Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, kuna ndoa gani kati ya Songas na Wizara ya Nishati na Madini kiasi cha kushindwa kuiruhusu *TPDC* kukopa humu ndani na kuwekeza katika mradi muhimu kama huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayasema hayo huku tukijua pia kuwa viko Viwanda 26 vilivyounganishwa kwa matumizi ya gesi, matarajio ya kuunganisha au kusambaza gesi hotelini ambayo hivi sasa yanatumia futi za ujazo milioni 10 na ongezeko hadi 20 *mmscfd* ili kupunguza matumizi ya mkaa pamoja na ndoto ya *IPTL* ya kubadilisha kutoka mafuta mazito (*HFO*) na kutumia gesi. Je, Serikali imeliona hilo? Tafadhali Waziri tupatie ufafanuzi wa mipango yako ya kuaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha suala hili la umeme na gesi, pamoja na yote hayo niliyoyasema, lipo suala nyeti la makubaliano la mkataba wa Songo Songo na Serikali. Wawekezaji (Songas) wamepewa haki ya kwanza ya kukataa *(the right of first refusal)* kuwekeza katika upanuzi wa Mitambo hiyo ya kusafisha gesi. Mazungumzo yamekwama kwa muda mrefu kutokana na *EWURA* hawajakubaliana na gharama za uwekezaji huo na ughali watakaobebeshwa watumiaji wa gesi hiyo huku Songas waking'ang'ania kurejesha haraka fedha yao ya uwekezaji. Ikumbukwe tu kwamba ujenzi wa upanuzi wa mitambo ulikuwa uchukue muda wa mwaka mmoja na ukamilike mwezi wa Juni 2010 lakini wapi mambo ndiyo hivyo. Watanzania tutumie vyema bongo zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kifungu cha sheria ya umeme *(Electricity Act 2008)* ambapo kutokana na uzoefu wa mkataba wa kitapeli wa *Richmond*, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilishawishi kuwekwa kwa mazingira ambayo Kampuni zilizokuwa na Mikataba na Serikali kutopewa leseni kwa miaka mitano baada ya sheria hii kuanza kazi. Mwathirika wa kwanza wa kifungu hiki cha sheria (kifungu namba 41 (6) na (7)) alikuwa ni Kampuni ya *ARTUMAS* ambayo ina mradi wa kusambaza umeme Mkoani Mtwara. Ilibidi kampuni hii kupewa *exemption* na *EWURA* ili kuweza kupata leseni. Kwa kuwa kifungu hiki tayari kimetimiza lengo lake la kukomesha mikataba mibovu na yenye kuinyonya nchi, tunashauri kuwa kifungu hiki kifutwe ili kuwezesha watu wa Mikoa ya Kusini kusambaziwa umeme mbele ya haja ya kupata *exemption* kila wakati.

Kufutwa kwa kifungu hiki pia kutawezesha kampuni zilizopo nchini zilizokuwa na mikataba na Serikali kujipanua katika kuzalisha na kusambaza umeme na hata kupata mikopo katika taasisi za fedha bila vikwazo vya kisheria. Kupitia mabadiliko ya sheria mbalimbali, Serikali ifute kifungu hiki cha 41 cha Sheria ya Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* Mikataba ya *Production Sharing Agreement* huiwezesha Serikali kupitia *TPDC* kupata mgao bila kuwekeza na endapo mwekezaji akagundua mafuta au gesi inayoweza kuzalishwa kibiashara basi *TPDC* hupewa fursa ya kuwekeza kwa kiwango cha asilimia tano hadi asilimia 20 ili kuongeza mgawo wake na mgawo wa Serikali. Katika hotuba yangu ya mwaka 2007/2008, nilieleza kwa kirefu umuhimu wa *TPDC* kutengewa fedha

za kuwekeza katika miradi ya gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay au kupatiwa *retention* ya mauzo ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya 2009/2010, wakati Serikali inajibu hoja za Kamati za mwaka 2008/2009, (Muhtasari Fungu 58, Juni 2009, ukurasa wa 10) naomba kunukuu: "Serikali ihakikishe kuwa Waraka ulioandaliwa kwa lengo la kuiwezesha *TPDC* kuwekeza kwenye shughuli za mafuta na gesi kwa kupewa asilimia 50 ya mauzo ya gesi asili ufanyiwe kazi haraka, ili Shirika liweze kushiriki kikamilifu katika miradi ya utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi. Majibu ya Serikali- Mwaka 2008/2009, Serikali iliruhusu *TPDC* kupatiwa sehemu ya mapato yatokanayo na mauzo ya gesi kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli za mafuta na gesi. Utekelezaji unatarajiwa kuanza mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka mitatu imeshapita TPDC bado haijapewa hiyo hiyo *retention,* je, Serikali inasema nini au ndio kusema haihitaji kuwekeza? Kama wameruhusiwa mwaka huu kulikuwa na sababu gani za kucheleweshwa uamuzi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa linahusu uharakishwaji wa mradi wa gati la kupakulia mafuta la *SBM (SINGLE BUOY MOORING)* Serikali imeamua kuifanya hifadhi ya *TIPER* kuwa eneo huru la kusafirisha bidhaa nje ya nchi *(an export processing zone)* na kuipatia hadhi kuwa kituo kisichokuwa na kodi. *TIPER* sasa maana yake ni *Tanzania International Petroleum Reserves Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa gati la *SBM* ni mkubwa na unatoa fursa kwa meli kubwa za mafuta yaliyosafishwa hadi 120,000Mt huweza kupakuliwa kwa muda mfupi sana, pia kuwepo kwa *SBM* kutatoa fursa za kibiashara kwenye Bandari ya Dar es Salaam ukilinganisha na bandari nyingine katika Ukanda wa Afrika Mashariki na utekelezaji wa Sheria ya mafuta na uwezekano wa *Bulk Procurement* kutekelezeka kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Mpango wa kuagiza mafuta kwa wingi *(Bulky procurement),* Bunge lilifanya mabadiliko ya Sheria ili kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta kwa wingi ili kupunguza ujanja wa wafanyabiashara kuuza mafuta kwa bei kubwa. Kuna taarifa kuwa Serikali imeamua kutoa kazi hiyo kwa kampuni ya Kizalendo ambayo ni kampuni binafsi ya watu binafsi iitwayo *LIVE TECH* na sio kampuni ya Umma kama ilivyokuwa imeamuliwa. Namtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, kampuni hiyo ilipatikana namna gani, kwa taratibu zipi na kwa Waziri alipata wapi Mamlaka ya kupata kampuni tofauti na *TPDC* katika kazi hii? Tunapenda kujua ni nini chanzo cha Serikali kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuiandikia *TPDC* kuwa Shirika hilo halitashughulika na Biashara ya Mafuta isipokuwa utafutaji wa mafuta pekee. Tunamtaka Waziri afafanue hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Gesi za majumbani *LPG*. Shirika la *TPDC* lina miradi miwili muhimu sana. Mmoja ni ule wa kuchuja Gesi ya *Binzantine* ili kutengeneza *LPG* kwa ajili ya gesi ya kupikia majumbani. Gesi yote inayotumika hivi sasa nchini inaagizwa kutoka nje ya nchi (*imported*) na hivyo Taifa kutumia pesa nyingi

za kigeni. Wakati huo huo kupitia gesi ya songosongo na kwa kuwa hatuna uwezo wa kuchuja (*extract*), kila mwaka tunachoma gesi nyingi sana ambayo ingeweza kutumika katika mitungi ya gesi na kutumia majumbani. Gharama ya mradi huu ni dola za Kimarekani 35 milioni. *TPDC* imefikia wapi katika kupata fedha za mradi huu wenye mafanikio makubwa kwa Taifa na utakaookoa fedha za kigeni za kuagiza gesi toka nje ilhali tunayo hapa hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme Zanzibar. Napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa niaba ya watu wa Unguja na Pemba kwa kufanikisha kwa pamoja mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga uliozinduliwa rasmi tarehe 9 Mei 2010 na kufanya Zanzibar yote kuunganishwa na *Grid* ya Taifa. Ushirikiano mkubwa uliooneshwa na *TANESCO* kwa upande wa Tanzania Bara na *ZECO* kwa upande wa Zanzibar ni wa kupongezwa na ni mfano bora wa kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo baadhi ya mambo ambayo yanaleta kero za Muungano kama vile ankara kubwa ya umeme inayopelekwa *ZECO* iliyoongezeka kutoka asilimia 21 hadi asilimia 168 na hivi karibuni kuongezeka tena hadi asilimia 202 ni mambo ambayo yatawafanya Wazanzibari kushindwa kulipia gharama za umeme huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tozo ya asilimia 0.3 kwa kufidia Wakala wa Nishati Vijijini Tanzania Bara inayoingizwa katika ankara hiyo si halali kwa Zanzibar na naomba itolewe. Inasikitisha kuona agizo la Waziri Mkuu kuhusiana na suala hilo bado halijatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hadi juzi nilipokamilisha hotuba hii bado haijapata barua yoyote. Mheshimiwa Waziri Ngeleja suala hili unalijua na bado hujatoa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *submarine cable* mradi unaofadhiliwa na mfuko wa *MCC* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja tumearifiwa katika kauli ya Waziri hapa bungeni kwamba mkataba ulisainiwa tarehe 30 April 2010 na matarajio ni kukamilika kwa mradi Agosti 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kuelewa ni sababu gani za mradi huo kuchukua muda mrefu wa namna hiyo? Wakati inaeleweka kwamba kwa teknolojia ya siku hizi ya kuzika waya baharini ni jambo la muda mfupi sana kazi kubwa ni kutengeneza *cable* husika? Tunaomba maelezo kwa sababu *cable* iliyopo hivi sasa imeshazidiwa sana na Wazanzibari wanahofu ya kutokujirudia giza zito lililowahi kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini. Muundo na shughuli za *TANSORT*. Serikali ilitoa maelezo mafupi kwa Kamati ya Nishati na Madini mwezi Januari 2010, kuhusiana na *Tanzania Diamond Sorting Organization (TANSORT)* iliyosajiliwa nchini Uingereza mwaka 1966 kwa lengo la kulinda maslahi ya Serikali ya Tanzania katika uuzaji wa almasi zinazozalishwa Tanzania. Lengo kuu ni kuona Serikali inapata bei nzuri

ya almasi zinapouzwa kwa kampuni ya *Central Selling Organization (CSO)* iliyoko London, ambayo sasa inaitwa *Diamond Trading Company (DTC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Tansort kulilenga kuzuia *transfer pricing* ili Serikali isipunjwe kwa kuwa mbia wa Serikali ambaye ni *Willcroft Company Limited* kwenye mgodi wa *WDL* alikuwa na uhusiano na mnunuzi *CSO/DTC*. Kitengo hiki cha *Tansort* hakikuwa katika muundo wa Serikali na baada ya kupigiwa kelele na kujulikana mapungufu hayo Serikali ilifanya marekebisho na kuingizwa katika muundo wa Serikali mwezi April 2001. Lakini Serikali ilichukuwa miaka mitatu hadi Julai 2004 kutenga gharama za uendeshaji wa kitengo kuingizwa katika bajeti ya Serikali na kufanya Ada za uchambuzi na utathmini wa almasi unaofanywa na Tansort kuingia kwenye mfuko wa Serikali, Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Taarifa ya Kamati Ndogo ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* inayohusu uchunguzi wa *Tansort* na *London Trade Centre* ya Agosti 2004 pamoja na ushauri wa Kamati ya Nishati na Madini hatimaye Rais wa Jamhuri ya Muungano akatoa agizo mwaka 2006 la kuhamisha kitengo hicho kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhia hii ya *Tansort* na Almasi za Mwadui bado inaleta utata na Serikali bado haijaweka wazi na Watanzania bado tunabakia na maswali mengi ya kujiuliza yakiwemo yafuatayo:-

(i) Serikali inatuambia kuanzia Novemba 2009 *Tansort* iliacha kufanya uchambuzi wa Almasi za mgodi wa *WDL* kutokana na umiliki wa HISA asilimia 75 za *WDL* kwenda kwa kampuni ya *Petra Diamond Limited* ambayo iliinunuwa kampuni ya *Willcroft Limited* kutoka kampuni ya *DeBeer* kwa asilimia 100. *Petra* ilianza kuuza almasi zake moja kwa moja kwenye soko na mahitaji ya kisheria ya *Tansort* kuchambua almasi yalikoma.

(ii) Wakati huo huo Serikali inatueleza kwamba hivi sasa yapo makubaliano ya mpito *(Interim Sales Arrangement)* kati yake na kampuni ya *Petra Diamonds* ambapo uchambuzi wa almasi unafanywa kwenye mgodi wa *WDL* na almasi kuuzwa kwa njia ya zabuni huko Antwerp, Belgium. Wataalam wa *Petra Diamonds, Tansort* na Wizara wanachambua almasi mgodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea Serikali kutoa taarifa za utatanishi za namna hii, Bunge lako na Watanzania kwa jumla tueleweje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa jedwali linaloonyesha matokeo ya uchambuzi na mauzo ya almasi za *WDL* kwenye soko la dunia huko Antwerp mwaka 2009, lakini ukilinganisha na takwimu nyingine za uchambuzi zilizofanyika na kutathminiwa na *Tansort* katika soko la London mwaka 2008, utaona tofauti kubwa ya wastani wa bei wa *USD* 136.7 kwa karati moja wakati katika soko la Antwerp ni wastani wa bei ya *USD* 126.5 kwa karati moja. Je, kitendo cha *Petra Diamonds* kuhamisha soko kutoka London ambako wateja wengi ndiko wanakotokea na kuuza kwa zabuni huko

Antwerp tena chini yao, kuchambua almasi mgodini chini yao, mwanya waliopewa *Petra* wa kurudishiwa *royalty* ni matokeo mabovu ya makubaliano ya mpito *(Interim Sales Arrangement)* hivyo ni dhahiri kuwa *Petra Diamonds* wameboresha ujanja wa *DeBeers* na kuiingiza nchi katika hasara zaidi na kuthibitisha kwamba utathmini wa Mwadui ni bure kwa sababu kama bei ya Mwadui ni *USD* 160 kwa karati moja lakini bei ya Antwerp ikawa ni *UDS* 110, kwa karati, Serikali inalazimika kurejesha baadhi mrahaba(*royalty*) iliyokusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano haya ya mpito hayalindi kabisa maslahi ya nchi isipokuwa yale ya *Petra Diamonds* tu. Naomba Serikali itoe ufafanuzi wa kina na ulio wazi na pia kurekebisha tatizo hili. Katika hotuba ya bajeti ya mwaka jana (ukurasa wa 39 na 40) Waziri alikiri mabadiliko hayo ya umiliki wa *Willcroft* yamesababisha kutofuatwa kwa utaratibu wa kupeleka almasi za *WDL* huko London kwa ajili ya kuchambuliwa na *Tansort*, pia alisema Serikali inaendelea na majadiliano na *Willcroft* ili kupata mkataba mpya wa ubia utakaozingatia maslahi ya pande zote mbili mkataba ambao pia utahusisha majukumu mapya ya *Tansort*.

Maswali ya kujiuliza hapa ni kwa nini Serikali iliridhia uhamisho huo tokea Februari 2009 ambapo ni kipindi cha mwaka mmoja na nusu sasa na majadiliano hayo bado hayajakamilika na huku tunaendelea kupoteza mapato mengi ? Hivi sasa katikati ya *interim sales arrangement* tayari *PETRA* wamekwishapoteza *carat* 14000 ya almasi zetu zenye thamani isiyopungua shilingi bilioni 4.9(*USD* 3.500.000,-) au *insurance* italipa? Ambapo pia kupanda Kwa gharama za bima kutazidisha za *Petra* ambapo kuna uwezekano wa kuzipitishia Serikalini kama hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania ilikubaliwa kujiunga rasmi tarehe 16 Februari 2009 na Asasi ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji *(Extractve Industries Transparency Initiatives - EITI)* ni vyema basi Serikali ikamilishe mchakato wake kwa kuhusisha wajumbe kutoka Asasi zilizo huru pamoja na watetezi wa wananchi ambao ni Wabunge na tunaomba kazi yake ya mwanzo ni kufutilia mapato na matumizi ya Almasi zinazozalishwa Tanzania kwa jumla na mwenendo wa makampuni yote husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo. Mgusu Geita. Kwa masikitiko makubwa naomba kufikisha kilio kikubwa cha wachimbaji wadogo wa eneo la Mgusu, Wilaya ya Geita ambao tayari walikwishapata kibali cha kumilikishwa eneo hilo toka kwa Kamishina wa Madini kwa barua yenye Kumb. Na. DA. 88/171/01/50 ya tarehe 30 Oktoba 2009. Bahati mbaya maafa yalitokea katika machimbo hayo na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa amri ya kufunga machimbo hayo kwa muda wa miezi mitatu toka April 2009, lakini hadi sasa machimbo hayo yamefungwa na askari Polisi wanalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe tamko rasmi kwa wakazi wote wa Mgusu kuhusiana na hatma ya maisha yao, kwani wao sio wafugaji, wakulima wala wavuvi bali wanaendesha maisha yao na familia kwa kutegemea machimbo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya kutoa tathmini hiyo kuhusiana na mwenendo mzima wa utendaji kazi wa Wizara hii, Kambi ya Upinzani inarudia tena kuwa Wizara hii inahitaji kiongozi ambaye atafanya maamuzi magumu ambayo wachache wanaonufaika na ukubwa wa Wizara hii wataumia na wengi tutanufaika na maamuzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia tena kuwa kwa takwimu ambazo tunapatiwa na Serikali kuhusiana na miradi mbalimbali ya kumaliza tatizo la umeme, ni wazi kuwa Serikali imeshindwa. Hivyo basi, tunawaomba Watanzania walione hilo na watupe ridhaa sisi watu makini ili tutumie rasilimali hizi kuondoa kabisa tatizo la umeme katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ama kweli wewe ndiye unayeitwa Eng. Mnyaa. Umeacha kufundisha siku nyingi sana lakini leo unatufundisha sisi. Ahsante sana kwa kuwasilisha. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeshawaambia mnakataa kujadili hotuba zingine sasa hapa mpo 47. 47 wote hawa hata iweje hamtafikiwa. Sana sana kwa hesabu zetu tunaweza kufika watu 18. Kwa hiyo wale wasiochangia hata mara moja wako saba, waliochangia mara moja wako kumi, basi ni kama hao. Kwa hiyo watakaoanza atakuwa Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, ambaye hajachangia hata mara moja, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Bukwimba, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Khalifa Sulemani Khalifa, Mheshimiwa Lyamba na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na nafikiri wanaweza wakafika mchana, halafu baadaye Mwenyekiti atakuja kutangaza wengine.

Waheshimiwa Wabunge, nitamwomba Mwenyekiti Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid aweze kushika kiti. Nawatakia siku njema.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na moja kwa moja namwita mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, natoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, umeme umefika Mchinga. Mungu akubariki sana. Lakini umeme huu ni mtihani kwangu. Nguzo zimekomea nyumbani kwangu pale kwenye Kitongoji cha Nachikoyo. Kuanzia pale kwenda Vitongoji vya barabara ya Pwani, Mchangani mpaka Namkuya, umeme haujafika na mafundi wamemaliza kazi yao. Huu ni mtihani kwangu haswa katika kipindi hiki kwamba Mbunge amepeleka umeme nyumbani kwake. Sasa

ninamwomba Waziri asijitie lawama bure ya kuua wakati wanaonikorogea sumu ni wengine, yeye anakuja kuhamisha *glass. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mwaka 2008 Bunge hili lilipitisha Sheria ya kupanua wigo wa huduma za umeme ili kuondoa ukiritimba wa *TANESCO*. Sheria hii ilikaribisha sekta binafsi katika kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme kwa ujumla, Sheria hii ilisaidia sana kuondoa tatizo la umeme lakini kukajitokeza mambo ya mkataba huu ambao haikueleweka vizuri na ikaleta msukosuko mkubwa ndani ya Bunge letu ndipo Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge hili ikapendekeza kuwepo Sheria ya kusimamisha kwanza uhuru huu wa kuinyima *TANESCO* ukiritimba, kukaundwa kifungu cha 46 kifungu kidogo cha 6 na cha 7 ambacho kilipiga marufuku kampuni yoyote ile kupewa leseni ya kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano ilikuwa Sheria yenye manufaa kwa wakati ule kwa sababu kifungu hiki kilitaka kuzuia kampuni zenye mikataba mibovu na Serikali kupata leseni. Kwa sisi tunaoishi vijijini anapoingia Mbweha katika nyumba yako au mtaa wako huanzi kufungia kuku kwanza zizini unamfukuza yule mbweha halafu ndiyo unakamata kuku unawaweka zizini, suala la mbweha likiisha kuku wanaachiwa wale, sasa suala hili lilishakwisha makampuni hayo yalishazuiwa, tunabakia kuishi kwa maisha yale yale ya kifungu cha 46 vifungu vidogo vya 6 na 7, madhara ya Sheria hii kwa sasa ni makubwa sana tunafikiri tulitengeneza dawa lakini kwa kweli tumekuwa kama watu wanaozidiwa na panya katika chumba halafu anachukua mikate iliyopakwa siagi na jibini halafu anakwenda kuziba kwenye matundu ya panya, panya hawatakimbia watakuja kwa wingi tu kuja kukudhuru zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Sheria hii tunapozungumza imetengeneza Kimungu mtu anayeitwa *EWURA*. *ARTIMUS* alinyimwa leseni na leseni anayoendelea nayo sasa ilibidi atoe kitu kinachoitwa *exemption* na hivi leo ndugu zetu wa Tunduru na Namtumbo wakitaka umeme *ARTUMAS* hawezi kwenda kupeleka umeme mpaka turudi kwa *EWURA*, Kimungu mtu tukapate *Exemption.* Hali hii ni ya hatari na Kampuni yoyote inayotaka kuja kuzalisha umeme sasa iwe ya upepo sijui wa kitu gani lazima ikapate *exemptio*n *EWURA,* sasa *EWURA* ndiyo inakuwa Sheria, ndiyo inakuwa *Alpha* na *Omega* katika biashara ya umeme hapa nchini, katika utawala wa Sheria jambo hili haliwezekani, kuna ushindani katika sekta zingine za mawasiliano simu zinapungua bei, mahoteli, vyombo vya habari lakini ikifika kwenye umeme mawasiliano haya yamepigwa LUKU, jambo hili hatuwezi kuliachia liendelee hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushughulikie tatizo kama tatizo, kuna maofisa ambao wanaingia mikataba feki tuhangaike nao wao. Lakini siyo kututoa watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kafara maana Sheria hii inatuumiza zaidi sisi. Sasa *EWURA* kwa mfano, tunaingia mkataba sisi na Serikali tulikubaliana umeme uuzwe *cent* 26 za Kimarekani kwa *kilowatt* lakini leo *EWURA* wametoa idhini, umeme Mikoa ya Lindi na Mtwara umepanda mpaka kufikia *cent* za Kimarekani 40 kwa *kilowatt* hivyo sisi watu wa Lindi na Mtwara kwa ufuta tu na korosho mnataka tukae kwenye umeme au tukae gizani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangaa na tunashangazwa sana *EWURA* kuendelea kuwapandishia hawa bei ya gharama za umeme wakati Serikali imetoa kwanza mkopo wa dola milioni saba kusaidia kupunguza gharama za uendeshaji. Ikatoa shilingi bilioni 6.8, ikatoa bilioni tano, pesa zote zimekwisha na bado hawa watu wamepewa tena idhini ya kumleta mtu anaitwa *MULTBOLT* kuja kuendesha, wenyewe wamemaliza pesa hawajiwezi bado tuko na *EWURA* tu sisi wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Wizara imeshatufahamu, tukawaambia Sheria hii ifutwe ya 46(6) na (7) maana kazi yake imekwisha, lakini wenzetu wa *AG* wanasema wao hawawezi kuleta kwenye *Miscellaneous Amendment*s wiki ijayo sisi tunasema iletwe hiyo Sheria wiki ijayo na ningewaombeni Wabunge wenzangu kama tuliwaunga Mkono wenzetu wa Tabora wiki iliyopita mtuunge mkono na sisi kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupeana ni kikoa, ukila nyama ya mwenzako na wewe yako iliwe. Hili tushirikiane Wabunge tunaumia Serikali ilete katika *Amendments* zake wiki ijayo, Wizara walishapeleka *Attorney General* ana matatizo gani na hii? Serikali ina matatizo gani na hii? Sheria hii haikuletwa na Serikali ililetwa na kati ya Nishati na Madini, sisi Wabunge ndiyo tunasema sasa iondoke, nyie bado mmeng'ag'ania kuna nini kati ya EWURA Kimungu mtu na kati ya *EWURA* na Serikali na *EWURA* na *ARTUMAS*. Nasema tutasimama jioni hapa na tusingependa tufike huko, tunakwenda kwenye Uchaguzi Serikali yetu ni sikivu, tunataka hii Sheria ijumuishwe na nitoe tamko leo hapa namna nyingine patachimbika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ni sikivu suala hili la *EWURA* lilikuja kwa muda tatizo limetoka hakuna sasa habari ya *RICHMOND* au *DOWANS* wala kitu gani vyote vimekwisha kwa nini tunashindwa kurudisha…..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Ya kwanza au ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya mwisho.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawasalimia wale wanaojua mbio Jimboni kwangu, najua njia. Watanikuta nimefika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nichukue nafasi hii kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu, lakini la pili niwapongeze Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii pamoja na watendaji wote. Nawafahamu hawa Mawaziri nimekuwa nikicheza nao mpira katika timu ya Bunge, Mheshimiwa Ngeleja *center back* na Mheshimiwa Malima ni kiungo, mkabaji, mimi mwenyewe ni kiungo, ni mzuiaji wa nyuma katika timu ya Bunge, nasema hongereni sana kwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia umuhimu wa umeme ambao kila mtu hapa anaujua. Umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya mtu binafsi lakini pia ni

muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Sisi wananchi wa Kisiwa cha Pemba takriban miaka 46 baada ya mapinduzi kisiwa kile kiko katika kiza totoro kwa muda mrefu sana, kwa muda mrefu sana wananchi wamekuwa wakikwazika katika kujiendeleza kiuchumi lakini na nchi pia ilikwama katika kuleta maendeleo ya kiuchumi katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Pemba kina fursa nyingi za kiuchumi lakini kutokana na sababu ya kwamba sasa Kisiwa cha Pemba kimepata umeme wa uhakika unaotoka Tanzania Bara kupitia Tanga sasa naona mambo yatakuwa mazuri. Kwa muda mrefu kisiwa hiki kilikuwa kinategemea majenereta manne ambayo yalifungwa katika Kisiwa cha Pemba mwaka 1976, majenereta haya takriban yote manne ni mabovu yaliyokuwa yanatembea kwa kipindi kilichopita, yalikuwa ni mawili tena kwa kusuasua na kutokana na hilo Pemba wakati wote ilikuwa katika giza totoro kutokana na ukosefu wa mafuta ya kuendeshea mitambo hiyo lakini kadhalika kutokana na uchakavu wa mitambo hiyo ya umeme ambayo ilikuwepo. Kwa hiyo, tunashukuru sana ni naipongeza Serikali na *TANESCO* pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba imechukua juhudi za kutosha kuhakikisha kuwa mmechukua juhudi za kutosha kuhakikisha kuwa umeme Pemba unapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo pia nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Amani Abeid Karume kwa kuzindua rasmi umeme huu wa gridi ya Taifa kule Pemba. Ni matumaini yangu kwamba sasa wananchi wa Pemba tutumie fursa hii kujiendeleza kiuchumi lakini kadhalika nitoe wito hapa Bungeni kwamba sasa tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuja kuwekeza katika shughuli za kiuchumi kule katika Kisiwa cha Pemba. Tunashukuru sana na tunawapongeza sana, kwa sababu tunategemea kwamba watakapoingia wawekezaji tutaweza kuzalisha zaidi ajira na kuweza kuthamanisha zaidi mazao ya mkulima na kuweza kupata bei iliyo nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali na *TANESCO* ningependa pia kutoa angalizo ambalo pia Mheshimiwa Mnyaa aliligusia, ni lazima Serikali ijue kwamba wananchi wa Pemba walikuwa maskini kwa muda mrefu kutokana na kukosa fursa za kiuchumi. Ni lazima bei za umeme zilingane na hali halisi za wananchi wa Pemba au wananchi wa Zanzibar kwa ujumla kusiwe tena na suala la kukomoana baina ya watumiaji wa umeme wa sehemu mbili za Muungano, lakini kadhalika Shirika la Umeme la Zanzibar lisibweteke likaona kuwa limepata umeme wa gridi ya Taifa kutoka Tanzania Bara zile jenereta zilizobaki pale wasije wakaziacha au zikaharibika au wakazifungua na kuzitoa ngawira, tujifunze yaliyotokea Zanzibar Kisiwa cha Unguja baada ya kutokea hitilafu katika Kituo cha Fumba ni jinsi gani wananchi wa Unguja walivyohangaika na kuathirika kwa ukosefu wa umeme katika kipindi cha miezi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii ulisimama, uchumi uliathirika, malaria yaliathiri kwa sababu watu walikuwa hawawezi kufunga vyandarua na matatizo mengi yalitokea kutokana na uhaba wa umeme, kipindi kile ambacho Unguja ilikosa umeme. Lakini pia labda nitoe angalizo lingine kwamba ni lazima *TANESCO* na *ZECO* waheshimu mikataba waliyofungiana katika suala zima la utoaji au ugawaji wa umeme lakini pia katika suala

zima la ku-*charge* gharama za kutoa umeme huo. Kwa kuweza kuheshimu mikataba hiyo bila shaka tutakuwa tumewaheshimu wananchi wetu na kuweza kuwapatia wananchi wetu umeme wa uhakika wakafaidika na kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshaeleza umuhimu wa umeme kwa maendeleo ya mtu binafsi na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Ni dhahiri haipendezi kabisa kuona kwamba sehemu moja katika nchi hii wanapata umeme wa uhakika, sehemu nyingine wanapata umeme wa kusuasua lakini sehemu nyingine hawapati umeme kabisa siyo jambo zuri na ni dhahiri kabisa kusema kwamba wala haipendezi kuona kwamba kuna tofauti baina ya sehemu katika nchi hii katika ugawaji wa huduma ya umeme, Serikali yetu imekuwa ikichukua hatua kubwa sana kuona kuwa inazalisha umeme kwa ajili ya matumizi ya raia wake lakini pia niseme kwamba kutokana na takwimu za Serikali ni kwamba sasa hivi nchi ina pungufu wa umeme karibu *megawatt* 300 na hata umeme unaozalishwa katika nchi hii takriban 23% unapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni dhahiri kabisa kuwa bado nchi hii ina mahitaji makubwa ya umeme. Sasa ili kutatua tatizo hili nadhani tumekuwa tukipitisha Sheria hapa za umeme kuona ni namna gani Serikali ianaweza kutatua tatizo hili kwa manufaa ya wananchi wake. Mheshimiwa Mudhihir amezungumza na nilitaka kusema kwamba tumepitisha Sheria moja hapa mwaka 2008 *Electricity Act 2008,* ambayo pia ilikuwa inaruhusu kama alivyozungumza Mheshimiwa Mwenzangu kwamba makampuni binafsi yaingie katika suala zima la kuwekeza katika kuzalisha na kuuza umeme sasa. Aidha, katika kutambua umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa umeme nchini hata Kamati yetu ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma POAC ilifanya juhudi ya kuitisha pamoja viongozi wakuu wa Mifuko ya Jamii *NSSF, PSPF* pamoja na Mifuko mingine pamoja na *TANESCO, TPDC* Serikali yenyewe kuona ni jinsi gani mifuko hii inaweza kujiingiza katika uwekezaji katika suala zima la kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Kamati hii ya *POAC* chini ya Uenyekiti wake Mheshimiwa Zitto Kabwe na Estherina Kilasi kwa hatua walizochukua zimeanza kuzaa matunda na kwamba viongozi wa Mifuko hii wameshakaa na kuona ni namna gani wanaweza kusaidia nchi kuwekeza katika kuzalisha umeme katika nchi hii. Sasa pamoja na kuipongeza Kamati na Serikali kwa ujumla hii Sheria ambayo imetungwa na ambayo pia Mheshimiwa Mudhihir ameizungumza, imekuwa ni kikwazo kwa wazalishaji binafsi wa sekta hii ya umeme, naunga mkono sana, naunga mkono maneno ya Mheshimiwa Mudhihir kwamba umefika wakati sasa hivi *stumbling blocks* zifutwe…..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote, niishukuru sana Wizara, nimshukuru sana Waziri wa Nishati na Madini

kaka yangu Mheshimiwa Ngeleja, Naibu Waziri pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii. Kweli wamenionyesha ushirikiano mkubwa hasa nilipokuwa nikifuatilia kero za wananchi katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii ya kipekee kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kutupa Mkoa wa Geita. Mimi binafsi nimefarijika pamoja na wananchi kwa ujumla wa Jimbo la Busanda tumefarijika sana kupata Mkoa wa Geita na kwa kuwa Mkoa huu Makao Makuu yake bado hayajajulikana ni wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kusema kwamba Katoro panafaa sana kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Geita, Katoro ni mji mzuri sana kwa wale ambao wamefika pale kwa kweli unapendeza pamoja na kwamba hakuna umeme kwa sasa hivi lakini kwa kweli mji ni mzuri na unapendeza, una watu wengi katika sensa ya mwaka 2002 kulikuwa na idadi ya watu 150,000 ukiunganisha Buseresere na Katoro. Kwa hiyo, hii inaonyesha shamrashamra zilizopo pale katika mji Mkuu wa Busanda ambao ni Katoro na ukiwa Makao Makuu ya Mkuu ya Mkoa kwa kweli itakuwa ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja ambayo iko pale ni kutokuwa na umeme. Nichukue nafasi hii kusema kwamba Mheshimiwa Ngeleja tunaomba umeme kwa haraka zaidi ili mji wetu uweze kujiendeleza na hata Makao Makuu yatakapokuja tuweze kunufaika na mambo mazuri kwa sababu tunapokuwa Mkoa sasa Makao Makuu ya Mkoa kuna mambo mazuri ambayo tunapata na tunamshukuru Rais kwa kuleta huduma karibu na sisi wenyewe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme nasema kwamba, ni muhimu sana kwa wakati huu kwa sababu bila ya umeme hatuwezi kufanya kitu chochote. Kupitia umeme tutaweza kusindika mazao yetu kwa sababu Mkoa wa Geita au Jimbo la Busanda ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo, pia tuna suala la uvuvi, sasa tunapovua samaki kwa wingi bila ya umeme hatuwezi kutunza vizuri mazao yetu ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa Mheshimiwa Waziri, kweli suala la umeme tulipe kipaumbele kwa haraka sana hasa katika mji wa Katoro, Rwamgasa, Bukoli na Nyarugusu kwa sababu miji hii ni miji mikubwa ambayo inaendelea katika Jimbo hili. Tukiweka umeme tutakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kuongeza pia ajira kwa vijana wetu, kwa sababu kwa kupitia umeme tutaweza kuwa na biashara ndogondogo za uzalishaji mali na viwanda vidogo vidogo. Kwa hiyo, ili kuweza kuboresha hali ya maisha naomba tupatiwe umeme ili tuweze kunufaika sisi wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na suala hilo hata hospitali zetu zahanati ambazo Serikali imejenga tunahitaji umeme, akinamama wengi wanapokwenda kutibiwa wanaambiwa watoe shilingi 1500/- ya mafuta ya taa, suala hili linanisikitisha sana na tukipata umeme tutakuwa katika nafasi nzuri ya kuwahudumia wananchi vizuri bila mashaka yoyote. Kwa hiyo naomba sana suala la umeme tulizingatie kweli ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo pia wanahitaji umeme, wakati huu wanatumia majenereta ambayo ni gharama, mafuta yanakuwa ni ghali sana, kwa hiyo mapato yao yanakuwa ni kidogo kwa sababu wanatumia fedha nyingi kuweza kutumia kama mtaji katika uchimbaji wa madini. Lakini tutakapopata umeme katika sehemu za uchimbaji madini kama Rwamgasa, Katoro na sehemu zote zile nilizozitaja za Nyarugusu nina imani kubwa hatutabaki kama tulivyo, tutabadilika, kutakuwa na maendeleo ya kutisha sana katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni suala la kipaumbele na kwa sababu mara kwa mara Waziri mmekuwa mkiniahidi mkisema umeme unakuja, kwa hiyo, naomba basi wakati wa majumuisho mnieleze wazi ili na wananchi waweze kusikia kwamba suala la umeme ni lini hasa tutapata, lakini ningependa kwa kweli mwezi huu usipite bila kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu wachimbaji wadogo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Wizara ya Nishati na Madini kwa kunisikiliza kero zangu hata sehemu ambayo ilikuwa imefungwa sasa imefunguliwa pale Sabora Kaseme lakini pamoja na hayo Jimbo la Busanda lina wachimbaji wengi sana ambao mgodi huo tu peke yake hautoshi, naomba hata katika maeneo ya Rwamgasa kule Bingwa *leaf* pamoja na Tembo *Mine*, wapewe wananchi wachimbe. Kwa sababu wananchi pale wanategemea uchimbaji, wanasomesha watoto wao kupitia uchimbaji. Kwa hiyo, naomba sana Serikali inisikilize na pia Nyarugusu katika sehemu ambayo wanahitaji kwa ajili ya kuchimba sehemu ya Buziba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri na Naibu Waziri msikilize kero yangu hii, watu ni wengi ukilinganisha na sehemu zingine tupo wengi sana katika eneo hilo na tunategemea uchimbaji wa madini. Naomba sana suala la uchimbaji lizingatiwe sana na tukizingatia sheria mpya ambayo inaangalia kuboresha maisha ya wachimbaji wadogo. Nashukuru katika bajeti hii ni matarajio yangu kwamba tutaweza kuwasaidia hawa wachimbaji kuwapa mitaji, kuwapa teknolojia mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya tele kwa kipindi chote cha miaka mitano nikaweza kuwepo na kufanya shughuli zangu toka mwaka 2005/2010 na hadi leo hii niko mbele yako nikichangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Nishati na Madini hasa Waziri Ngeleja pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri iliyoletwa mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze mchango wangu kwa kuishukuru na kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo imetekeleza majukumu ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010 kwa kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo fursa ya kuweza kuchimba madini yao wenyewe hasa madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepiga marufuku uuzwaji nje madini ya vito kama vile *Tanzanite*, ikiwa ghafi. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa jinsi gani haya madini yatakavyoweza kudhibitiwa kutoka kwenye machimbo hadi kupelekwa kwenye mashine za ukataji. Ningeomba kwa wakati huu Serikali ilipoamua kwamba eneo la Mji mdogo wa Mererani kuwa maalum kwa uwekezaji wa viwanda, ningeomba Serikali ihamasishe wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali, waje waweke viwanda vyao katika Mji mdogo wa Mererani kwa sababu tayari eneo lilishatengwa kwa ajili ya viwanda. Hivyo basi, tunawakaribisha wawekezaji waweze kuja kuweka viwanda vyao kwa ajili ya kukata na kuyasanifu madini ndipo yaweze kupelekwa nje yakiwa yamekwishasanifiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogo wadogo kuhusu kuwezeshwa, wachimbaji wadogowadogo wanatakiwa wapatiwe mfuko wao maalum kwa ajili ya kuwapa elimu ya uchimbaji bora, wapatiwe elimu ya masoko ili waweze kujua hata wanapozalisha madini wanaweza kuyauza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingelikuwa ni vema wapewe elimu, vile vile hawa wachimbaji wadogo wadogo, si wengi wanaojua kuandika mikataba au wanaojua kuandika michanganuo kwa maana ya *proposal*. Hapa inaonekana kwamba wameambiwa waandike *proposal* ili waweze kupatiwa mikopo. Ni vema wapate elimu kwanza kabla ya kuwaachia wenyewe kujitafutia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye eneo la *Tanzanite*, migogoro iliyopo kati ya *Tanzanite one* na wachimbaji wadogo wadogo kuhusu zile *scanning machine*. Wachimbaji wadogowadogo wenyewe wanaolalamika kwamba mashine hizi zina madhara kwa sababu madhara ni wao wenyewe wanayapata siyo mtu mwingine aliyepo nje ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakilalamika kwamba hata kama kuna Kamati maalum iliundwa mashine ile ambayo inawaumiza, inafichwa wanaoneshwa zingine ambazo sizo. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie sana kwa sababu wanaoumia ni wachimbaji wadogowadogo siyo Wawekezaji wakubwa, hivyo ningeomba Serikali ipige marufuku kabisa mashine hizi kwa sababu kuna namna nyingi za kuweza kuwadhibiti siyo lazima kumpiga mtu *X-Ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kibali maalum kinachotolewa na kampuni ya Tanzanite One, kibali kinachoitwa *Tanzanite foundation* ina maana kwamba wachimbaji wadogowadogo na watu wengine wafanyabiashara wazawa wa nchi hii

hawawezi kuuza bila kupata kibali maalum kinachotoka kwa hawa Wa-South Africa. Hivyo, nimeona kwamba hiki kibali hakina maana kwa sababu kinamnyima mchimbaji mzawa haki yake ya kuuza madini yake mahali popote. Hiki kibali maalum kinachotolewa na kampuni ya *Tanzanite One* hakina maana kwa sababu madini ni ya Watanzania na hatuoni sababu ya kwenda *South Africa* kutafuta kibali cha kuuza madini yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia Serikali kwa jinsi ambavyo imefanya vema kutafuta uwakala, huyu Wakala ameonesha uaminifu mkubwa katika kufanya shughuli zake hata kuweza kutetea rasilimali hii ya Tanzania. Inaonesha amefanya kazi hii kwa shilingi bilioni tatu, hivyo, ameliokolea Taifa letu shilingi bilioni kumi na tatu. Tunaona kwamba ni vema watu hawa wakapewa ushirikiano na Serikali ili wasije wakakwama mahali popote kwa sababu tunaona kwamba hawa watu watatuletea faida na uchumi wetu utapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia pia namna ya kudhibiti madini hasa upande wa *Tanzanite* Mererani. Kumekuwa na watu ambao siyo waaminifu wanaotengeneza madini yanayofanana na *Tanzanite* na kuyauza kwa bei kubwa na yanafanana kabisa na *Tanzanite*. Naomba kuwepo na kibali maalum kutoka kwa yule mchimbaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Dorah ni kengele ya mwisho hiyo.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami nichangie katika hotuba hii ya Nishati na Madini. Kama walivyosema wenzangu nianze nami kuwashukuru sana Waziri na watendaji wote wa Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa nchi yetu. Pia nimepewa salamu maalum na wananchi wa eneo la Madaniwa kule Jimbo na Gando kuwa nimshukuru Waziri pamoja na Waziri Mkuu na *ZECO* kwa kuwapatia transfoma ingawa wanasema kuwa transfoma tupu bila kukamilisha yale waliyoyaomba awamu ya pili haijawasaidia sana lakini wanashukuru katika ile hatua ya kwanza na kuwaomba sana katika kipindi hiki kilichobakia kidogo wamalizie ili lile lengo la kuwaondoa katika dhiki liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi sana yamesemwa na Kambi ya Upinzani katika suala zima la upande wa Nishati na Madini. Mimi ninayo machache sana ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la Kiwira, katika siku za nyuma tumeona hoja nyingi kuhusu Kiwira. Napenda kuuliza hivi kinachokwaza ni nini mpaka pale, miundombinu ipo, wafanyakazi wapo lakini hawalipwi, maamuzi hayachukuliwi, ni

kitu gani hasa kinachopelekea hali hii. Hatuoni kuwa watu wanaanza kupata wasiwasi wa kutochukuliwa kwa maamuzi sahihi labda kuna lengo la kuwarudishia walewale walionyang'anywa na kama hivyo ndivyo ni kwa maslahi ya nani? Kama lengo ni zuri basi ni vizuri Serikali ikafanya maamuzi haraka ili katika mradi ule tukaweza kufaidika kwa sababu tukiacha mitambo haizalishi, wafanyakazi hawalipwi au kama wanalipwa wanapokea pesa za bure, hiyo ni kupoteza kodi za Watanzania isivyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunganisha na mradi wa Mchuchuma, toka nimeingia hapa Bungeni hapa Awamu ya Tatu ile mwaka 1995 mpaka leo suala hili la Mchuchuma linasemwa na tunasikia juu ya mradi mkubwa wa Mtwara *Corridor*, hivi tunaunganishaje mradi huu wa Mchuchuma na Mtwara *Corridor* lakini kwa maana ya kuutekeleza siyo kwa kusema. Kwa sababu tumesema toka Awamu ya Tatu mpaka leo hatujafanya chochote, watu wanakuja wanataka kuwekeza lakini utasikia kuna mtu hapa hapa anataka kupewa, hapewi huyu wa hapa wala yule wa pale, waliokuwa wana lengo la kuwekeza hawapewi. Kwa nini hatufanyi maamuzi ambayo yataweza kuwasaidia Watanzania kuondokana na dhiki hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naomba nizungumzie suala la madini. Suala hili kwa nafsi yangu naona limekuwa na utata mkubwa. Katika bajeti ya Waziri wa Fedha alitaja suala la *fencing* ambalo nilidhani sasa tunataka kutekeleza kwa dhati yale mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Tume ya Bomani katika suala la kuangalia upya mikataba hii ya wachimba madini. Lakini mwisho sentensi tatu tu mbele inasema wale walioingia mikataba na Serikali hawataguswa. Sasa kama huwagusi kwa nini huwagusi wakati matatizo makubwa yapo katika makampuni yale ambayo yalishaingia mikataba na Serikali na ndiyo yanayochimba na yanayochukua mali nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ombi maalum kwa Serikali, hii ni bajeti ya mwisho itueleze yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika kipindi hiki cha miaka kumi kuanzia mwaka 2000 mpaka leo 2010, wachimba madini wamechimba madini kiasi gani katika nchi yetu na katika uchimbaji huo sisi tumefaidika nini? Maana yake ukija hapa tunaambiwa tunapata mrabaha wa asilimia tatu. Lakini ukitazama asilimia tatu, asilimia mbili kuna kauli kuwa wanachukua *Alex Stewart* ndiyo wanaokusanya hiyo kodi sisi tunapata asilimia moja, hivi ni nchi gani katika dunia ambayo mali yake inagawiwa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tujue maana yake huwezi kusema mtu ananigawia naridhika mpaka ujue hicho chako wewe ni kiasi gani, wanachimba kiasi gani na mpaka leo jambo hili Serikalini limekuwa ni utata. Hatupati maelezo hapa Bungeni kwamba wachimba madini wa dhahabu kwa mfano, katika nchi nzima wanachimba kiasi gani kwa mwezi, au wanachimba kiasi gani kwa mwaka na katika hiyo sisi tunapata kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ningependa tuelezwe vinginevyo tutakuwa tunawaambia watu wanapata, unakuja unataja asilimia, dola milioni mia saba lakini kumbe zinazochukuliwa ni dola bilioni kumi. Sasa hii ni vizuri tukapata maelezo ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala pili ni kuhusu wachimbaji wa madini wadogo wadogo. Kuna barua nimewahi kuisoma hapa inatoka kwa Kamishna wa Madini akiwaelekeza wachimbaji fulani sehemu za Mpwapwa. Lakini ile barua anavyolalamika Kamishna wa Madini na alivyodharauliwa inasikitisha sana. Kwa sababu inaonekana ametoa maelekezo ya kufanya na amewaingiza viongozi katika jambo hili, lakini sijui kuna maslahi binafsi. Maagizo ya Kamishana wa Madini yamepuuzwa. Si hilo sehemu nyingi tu utasikia watu wanalalamika mara wachimbaji wadogo wananyang'anywa hapa mara pale, inaonekana kuna upuuzwaji wa maagizo yanayotoka kwenye Wizara yako, naomba hili uwe mkali. Kwa sababu haiwezekani watu wanaangalia maslahi binafsi tu, tena ikawa ni viongozi bila kuangalia maslahi ya watu walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watu wanaishi kwa kutegemea madini. Sasa unapowadhulumu au unapowafanya watu wachache wachimbe lakini wale uliowapa haki ya kuchimba wanazuiliwa kuchimba hii ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la almasi. Toka uhuru sisi tunachimba almasi lakini uwazi wa usafishaji wake haupo. Kwanza, tuliambiwa inasafishwa London, nchi ndogo tu Botswana, Namibia wameanza juzi tu uchimbaji, lakini huwezi kutoka hata na gramu moja kwa sababu kila kitu kinafanywa ndani ya nchi yao. Hivi sisi ni kwa sababu hatuwezi kusafisha haya madini mpaka tupeleke Uingereza au mpaka tuwape watu wengine kwa nini na katika hilo tunafaidika nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nizungumzie suala la mafuta. Suala hili limekuwa utata mkubwa, naomba Wizara itueleze kupitia *TBC* hivi katika nchi yetu mafuta yapo, yameonekana? Kwa sababu utafiti wa mafuta umefanywa muda mrefu, ni wakati muafaka kuambiwa kama yapo au hapana. Inawezekana yapo lakini hayafai kuchimbwa au yanafaa kuchimbwa. Hili tungependa tuelezwe ili ile habari ya kuwa mafuta sijui ni suala la Muungano au si suala la Muungano, inaweza likawa ni suala la Muungano lakini likawa halipo, ningeomba tupewe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa kuokoa muda nakushukuru kwa kunipa nafasi na nawatakia kila la kheri waliowasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na nikupongeze kwa kuweza kuokoa muda, sasa namwita Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na Mheshimiwa Paschal Degera ajiandae.

**MHE. CLEMANCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu mdogo mchana wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza sana Waziri William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Mbunge wa Mkuranga na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kuwasilisha hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mkutano huu ni wa mwisho katika Serikali ya Awamu ya Nne, sina budi kwanza kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza Serikali hii kwa umakini na mafanikio makubwa katika kuinua uchumi na kujenga amani, upendo na utulivu katika nchi yetu, bila yeye kusimama kidete kuyasimamia haya kwa umakini tusingekuwa hapa tulipofika mpaka hivi sasa.

Nichukue fursa hii pia kuwapongeza wasaidizi wake wote, waaminifu waliotimiza wajibu wao katika kutekeleza majukumu kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila nisipowashukuru wapigakura na wananchi wote wa Jimbo la Mikumi, kwa imani na heshima kubwa walionifadhili kwa kunichagua kuwa Mbunge wao mwaka 2005. Ninaamini nimewatumikia ilivyostahili. Kwa ushirikiano, tumefanya mambo mengi ambayo yanastahili kuendelea kuyatekeleza mpaka pale panapoweza kufikiwa. Kwa maana hiyo, naomba waniunge mkono kwa nia ninayoitangaza kwamba natarajia kutetea Jimbo la Mikumi katika Uchaguzi Mkuu ujao na Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani za pekee tena kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutugawia Jimbo la Kilosa kuwa Majimbo mawili, Jimbo la Gairo na Jimbo la Kilosa. Hiki ni kilio cha miaka mingi, zaidi ya kumi na tano lakini hatimaye tumefanikiwa kupata Majimbo ambayo yatasaidia kusogeza huduma za ustawi wa jamii na kiuchumi pamoja na kusogeza utawala karibu sana na wananchi ili kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ila sio kwa umuhimu, nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kuhangaika sana pamoja na Wanajeshi wa JWTZ, Watanzania wenye mapenzi mema, taasisi mbalimbali kwa namna walivyotufadhili katika mafuriko yaliyotupata katika Wilaya ya Kilosa. Tunasema Mungu awarejeshe nguvu na yote ambayo wanastahili kutokana na kujitoa kwao huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niingie moja moja katika kusema kwamba naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Nishati na Madini. Nianze kwa kushukuru sana kwa kusikia kilio cha wananchi wa Kata ya Mabwerebwere, Masanze na Kilangali kwa kupeleka umeme katika Kijiji cha Kondoa, sehemu ya Mamoyo, Changarawe na Kivungu. Cha kusikitisha ni kwamba baada ya mafanikio haya yaliyotekelezwa mwisho wa mwaka uliopita, miradi hiyo pamoja na mingine ambayo ilikwishafanyiwa *survey* imesimama kwa kisingizio kwamba nguzo hazitoshi na fedha zimekuwa finyu. Naiomba Wizara ya Nishati na Madini kwa vile maeneo yaliyosalia ni muhimu sana kwa kutekeleza dhana ya Kilimo Kwanza katika Vijiji vya Kilangali,

Zombo, Ulaya, Kisanga ambako pia kuna sekondari maarufu ya Msolwa, vina msimu wa kulima mpunga na mahindi na mbogamboga mara mbili kwa mwaka. Kwa maana hiyo, vina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu kwa upande wa kilimo. Ni vema sana Serikali ikalijua hili kama ambavyo tulivyokwishawafahamisha na kama walivyokwishafanya *survey* kwa kukubali kupanga mipango inayohusika watekeleze azma hii, la sivyo itakuwa tunachezea ardhi yenye rutuba, yenye kuweza kutoa mazao ambayo tunaweza tukaanza kuyasindika kwa kukoboa na kusaga mpunga, mahindi na mazao mengine kama mazao ya mbegu za mafuta yanastawi sana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na madini, nafurahi kutoa taarifa ambayo bila shaka mtakuwa mnaifahamu kwamba Kampuni ya *Kastan Minning Limited* ambayo ilikuwa imedhamiria kuchimba shaba katika Kata ya Uleling'ombe, hatimaye imeweza kupewa leseni na ninaipongeza sana Wizara kwa kuwapa leseni tarehe 21, mwezi wa Juni, 2010. Kwa sababu wanatarajia kujenga Kiwanda kikubwa cha Shaba kule, Vijiji ambavyo ni jirani ambapo moto utapita kama Malolo na Kisanaga vingeweza kunufaika moja kwa moja na umeme ambao utapelekwa kwenye kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba kwa sababu Watanzania tunajulikana kwa kuchelewesha maamuzi na kwa sababu kampuni ilikuwa imeshaanza kukata tamaa, kwa sababu kibali kimechukua muda mrefu kupatikana, niiombe Serikali ifanye kila jitihada kufanikisha mahitaji yao yote yatakayowezesha kujenga kiwanda kile mapema kwa manufaa ya Taifa letu kwa sababu itakuwa ni Kiwanda pekee cha Shaba nchini na shaba yenye ubora kwa kiwango kinachokaribiana na au kuzidi shaba inayotoka Zambia na Congo. Kwa naiomba sana Serikali izingatie kilio hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda nitaje Vijiji vingine ambavyo viko jirani na mtambo wa kuzalisha umeme wa Kidatu, Kijiji cha Kidogobasi na Msowero, viko jirani kabisa na Kijiji cha Kidatu ambako umeme unafuliwa. Haya ni maeneo ambayo yanazalisha miwa na Vijiji jirani ambavyo tayari vina umeme. Kwa hiyo, ni suala la kuunganisha katika maeneo hayo. Lakini miradi hii ilikuwa imeanza kutekelezwa ikahairishwa kwa sababu ya matatizo yanayosemekana ni ukosefu wa nguzo. Ingekuwa ni bora na ni muhimu kama utekelezaji huu ungefanyika haraka itakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kuhusu bei za umeme na kuunganisha umeme katika nyumba za wananchi hususani Vijijini. Mwaka 2008, Wizara ilitoa tamko kwamba wana lengo la kufanya mikakati yoyote inayowezekana ili wapunguze gharama za kuunganisha umeme, naomba watekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba hii iliyo mbele yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri lakini imejaa mambo ya baadaye kuliko hali halisi ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko hapa nina masikitiko makubwa sana kuona Awamu ya Nne imezima umeme Liwale wakati kuna uchaguzi uko mbele yetu. Liwale sasa hivi kuna shida ya maji, tuna shida ya umeme wenyewe, wananchi sasa hivi hawajui watasaga wapi kwa kuwa umeme hamna. Nimepewa ahadi nyingi sana, nimefuatilia tangu wakati wa ARTUMAS na nimeuliza maswali yasiyopungua saba katika awamu hii yanayohusu umeme na ahadi nilizokuwa nimepewa ni nzuri na nzito. Mwisho nikawaambia basi jawabu kwa Liwale mtupatie majenereta angalau mapya, ili tuweze kuendelea kupata umeme mpaka hapo mtakapoamua kwamba ARTUMAS itakuja au kutakuwa na mpango mwingine. Lakini na hilo mkalikataa, mkasema kutakuwa na majenereta mawili ya kutoka Ikwiriri, Ikwiriri mpaka leo hii tunavyozungumza hawajapata umeme. Baadaye likaja wazo kwamba jenereta iliyoko Kilwa karibu watapata umeme wa Songas, kwa hiyo, jenereta lile litahamishiwa Liwale hivi karibuni. Hali halisi ni kwamba lile jenereta lililoko Kilwa nalo halipo katika hali nazuri, linahitaji *maintenance*, linahitaji kuwa *overhaul* na hayo mnayajua, lakini bado mkatupa ahadi kwamba hilo litakuja kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumepata umeme kwa kutumia jenereta aina ya *Rolls Royce* zikawa zinahitaji vipuli, jamani mnashindwa hata kununua vipuli? Sisi tuko tayari kujikongoja na hayo mpaka hapo utaratibu mwingine utakapotufikia, lakini hadi leo hii ninavyozungumza Liwale ipo gizani. Wakati Wilaya nyingine wanapelekewa umeme, sisi tunazimiwa umeme ambao Wilaya ilikuwa imefungiwa mwaka 1975, sasa niielewe vipi Awamu hii ya Nne? Jambo hili nikalizungumzie wapi? Wananchi wa Liwale niwaambie nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba ni kwamba tafadhali fanyeni mambo ya kiutendaji, kama mtatuletea umeme basi uje umeme au jenereta haraka iwezekanavyo. Kwa hivi sasa wananchi wanahangaika, wanatembea kilomita saba kwenda mtoni, kwenda kuchukua maji wakati miundombinu yote ya maji ilikuwa imeshakamilika na umeme ulikuwa unafanya kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiihada ya kwenda kuonana na Mawaziri husika nimeifanya sana, mpaka sasa hivi sielewi nimlilie nani. Sijui wakati wa kampeni safari hii, kama Rais atakavyokuja kufanya kukampeni, naye atakuwa kwenye giza au vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa, sikuwa na jambo lingine lolote na sina haja ya kushukuru au kuwapongeza, kwa hili, mmeniharibia na sitaunga mkono kwa lolote mpaka mnipe jibu umeme utapatikana vipi Liwale ambayo sasa hivi iko gizani. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake, kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, pia nitumie nafasi hii kutoa shukurani. Napenda nimshukuru sana, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kusikiliza kiu cha wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini cha muda mrefu sana cha kupata Wilaya. Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake, ametupa Wilaya mpya ya Chemba ambayo itakuwa katika Jimbo la Kondoa Kusini. Kwa niaba ya wananchi hao, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo wa busara. Tunaamini kabisa kwamba sasa wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini, watapata huduma karibu na wanakoishi. Aidha, tunajua kabisa kwamba mwaka huu hatukutengewa bajeti, lakini miaka ijayo tutatengewa bajeti yetu ya Wilaya, hivyo tunaweza kufanya mambo makubwa ya maendeleo katika Wilaya hiyo mpya, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukurani hizo, naomba sasa nichangie na mimi maeneo machache tu ya hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini na nijielekeze katika usambazaji wa umeme Vijijini. Mwaka jana nilichangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini na nilimueleza kwamba Jimbo la Kondoa Kusini ambayo sasa hivi itakuwa Wilaya ya Chemba, ilikwishafikishiwa umeme wa gridi kutoka Babati hadi Kondoa na wakati wa kutekeleza mradi wa kupeleka umeme Kibaya – Kiteto, njia kubwa ya umeme huu unaopelekwa Kiteto unapitia katika Jimbo la Kondoa Kusini. Bahati mbaya sana ni kwamba wakati wa utekelezaji wa mradi huu, Vijiji vilivyokuwa jirani na njia hii ya umeme inayokwenda Kibaya, havikupatiwa umeme. Kwa hiyo, kwa muda mrefu, Vijiji hivi 32 vilikuwa vinasubiri vipatiwe umeme na kwa muda mrefu kwa kweli kilio chao hakijasikilizwa maana havijapatiwa umeme, hadi leo ni miaka kumi bado wanaendelea kusota kusubiri umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kumbukumbu ya Mheshimiwa Waziri, naomba nivitaje hivyo Vijiji ambavyo havijapatiwa umeme kwa muda wa miaka kumi iliyopita ni pamoja na Kidoka, Kambi ya Nyasa, Chemba, Paranga, Kelemaku, Isni, Kelema Balai, Sori, Cheku, Waida, Pongai, Pio, Dalai, Tandala, Mtakuja, Makamaka, Mirambo, Igunga, Madaha, Churuku, Kinkima, Jinjo, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mapango, Mwailanje, Mwaikisabe, Magasi, Igulali, Isusume na Songambele. Hivi Vijiji viko jirani sana na njia ya umeme na havina gharama ya kuvipelekea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tukumbuke kwamba wakati wa kutekeleza mradi huu, Vijiji hivi viliombwa vitoe idhini ya umeme kupita katika maeneo yao bila kulipwa fidia. Kwa hiyo, Vijiji vilitoa maeneo yao, mashamba yao, miti yao na sehemu nyingine hata kubomoa nyumba zao bila fidia yoyote na mategemeo ya Vijiji hivi ni kupata hiyo huduma ya umeme. Lakini shukrani ya Serikali ni kutokuwapa umeme kwa miaka kumi. Kwa kweli inanipa tabu sana kujieleza kwa wananchi wangu, inaleta aibu

kwa Serikali yenyewe ambayo kwa kawaida ni sikivu, lakini kwa hili kwa kweli Serikali haijafanya la busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia sana katika Kitabu cha Waziri hapa, miradi ya umeme wa gridi ambayo inafikishwa kwenye Vijiji, sijaona hata Kijiji kimoja kati ya hivi Vijiji 32 ambavyo viko jirani sana na umeme ama njia ya umeme vilivyopangwa katika utekelezaji wa miradi iliyotengwa na Serikali. Napenda niseme kwamba wananchi kwa kweli wamekatishwa tamaa sana na hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea kuzungumza, naomba niseme hili, kama hivi Vijiji nilivyovitaja vimesahauliwa, naomba katika hatua ile ya kujibu hoja za wachangiaji, waniambie ama Waziri aniambie katika Vijiji hivi 32, ni vipi ambavyo vitapatiwa umeme katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hilo, naomba sasa nichangie kidogo kuhusu gharama za umeme. Wakati tulipokuwa tunatunga Sheria ya Nishati, mimi nilikuwa mmoja ya wachangiaji katika Muswada ule ambao sasa hivi ni Sheria kuhusu Gharama za Kuunganisha Umeme kwa Wateja. Tulisema kwamba, ile Sheria iliyotungwa ilikuwa imelimbikiza gharama nyingi kwa wateja, ukiangalia kuna *deposit* ya kulipa kabla hujaunganisha umeme, kuna nguzo ya kuchangia kabla hujaunganishiwa umeme, naambiwa hata mita unatakiwa uchangie, pia naambiwa kwamba kuna gharama pia ya kuunganisha umeme. Sasa unaambiwa kwamba utachangia nguzo na gharama nyingine lakini nguzo inabaki kuwa ya *TANESCO*, mantiki hii mimi bado sijaielewa, kwa nini wateja wanachangishwa vifaa vingine ambavyo ni vya Shirika la *TANESCO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, napenda niwashukuru Waziri Ngeleja na Naibu wake, kwa kazi nzuri, ripoti ni nzuri. Pia tunampongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Mashirika ya *TANESCO, REA*, kwa kazi nzuri waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kuwapongeza wapigakura wangu wa Jimbo la Kilombero ambapo ni Wilaya nzima ya Kilombero, kwa ushirikiano walionipa katika miaka hii mitano. Kazi kubwa tumeifanya na kuna mambo makubwa ambayo nitayataja hapa na hata huyu anayefikiria kuja, awaze kwanza aende au asiende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa miwa ambao walikuwa wanatozwa kodi katika uzalishaji, tumeondoa kodi zote kwa miaka hii mitano. Uwekezaji, tumeshaanza kuwekeza, mashamba makubwa ya KPL, tayari wameshaanza kulima pale. Tuna mashamba mengine ya Ruipa Merera yatakuja chini ya Kampuni ya *Syngen Fuel and Agri-Products,* kuna kule Ngalimira, nako kutakuwa na mashamba. Barabara ya Kidatu – Ifakara, Serikali imeshasema katika majumuisho ya Waziri wa Miundombinu, imekubali kujenga kwa kiwango cha lami kwa ushirikiano na Serikali ya Uswisi. Vilevile barabara ya Ifakara hadi Mlimba mwaka huu tumetengewa fedha ya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro ambao umedumu kwa muda wa miaka 14, katika Vijiji vya Chita kule, tumeutatua. Kwa hiyo, wananchi wa Vijiji vile viwili pamoja na matumizi bora ya ardhi, wanaishi vizuri na Jeshi la Kujenga Taifa katika maeneo yale. Mawasiliano ya simu, Wilaya nzima tunaongea. Shule za Sekondari tulizikuta saba sasa ziko 43. Changamoto tuliyonayo ni pamoja na afya, juzi juzi tumefungua Kituo cha Afya cha kufanya upasuaji mdogo kwa akina mama wajawazito pale Mlimba. Kwa hiyo, hayo ni matatizo makubwa tuliyoyatatua kwa uchache mengi yako kwenye Kitabu cha Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala ambalo lipo mbele yetu. Tupo hapa kujadili hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Napenda niishukuru Wizara hii mwaka huu tumebahatika na sisi kupata mradi wa *MCC* wa kutoa umeme pale Kihansi unaokwenda Malinyi unapita katika Vijiji vyangu. Kwa hiyo, wananchi wa Chisano, Kalengakelo, Ngwasi, Mpanga, Utengule, Ngalimira, mkae mkao wa kula kusubiri umeme huo kwa ajili ya maendeleo ya sehemu zetu. Ninachoomba, umeme ukifika Mpanga, mimi napendekeza umeme ule upite Utengule halafu uvuke Mto Mnyera uende Ngalimira, ndiyo uvuke kwenda Biro hadi Malinyi. Tukiupitishia Mpanga moja kwa moja hadi Ngalimira kuna shule ya sekondari pale katikati ya Mpanga na Utengule, watakosa umeme na kile Kijiji cha Utengule hakipo mbali, ni kilomita tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda vilevile niwapongeze Wakala wa Umeme Vijijini (*REA),* kwa kutusaidia Kituo chetu cha *Convent* ya Masista pale Mbingu, wao wanafua umeme wa kilowati 850. Leo katika kumsaidia yule *Sister* Mkuu, *Sister* Seki katika kurekebisha mitambo ile nao hatimaye wamekubali kuuzia wananchi umeme ule. Kilowati 850 ni karibu *megawatt* moja, unatosha vijiji vyote vile vya Mbingu, Namwawala hata Mofu utafika hadi Mchombe katika kituo chetu cha Afya cha Lukolongo. Kwa hiyo, wananchi wa hapa nao tunapenda kuishukuru *REA* na ninapenda Serikali tuipe uwezo mkubwa sana chini ya Dr. Mwakahesya ili waweze kufanya vitu vidogo vidogo, *TANESCO* tuiachie mambo makubwa, Stigler's Gorge, Mpanga, Ruhuji lakini hivi vidogo vidogo vya megawati 10, vya megawati moja, kilowati 800, 700, tuwaachie *REA* na tuwape nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Tunaingia kwenye ushindani wa soko, bila umeme, bila *electrification* vijijini, Kilimo Kwanza hakitawezekana. Bila *electrification* vijijini, hivi viwanda tunavyovizungumzia kwamba viwanda ni sekta mama katika uzalishaji, hatutaweza kuwa na viwanda bila kuwa na umeme. Hatuwezi kuwa na *agro-processing industries* za mazao yanayozalishwa Kilombero kisha tukapeleka Tandale, ndiyo tufanye pale ukoboaji halafu tu-*pack,* tufanye kule kule tunakozalisha. Ili kufanya hivyo, lazima *rural electrification* ipewe msukumo mkubwa. Pamoja na kwamba *REA* tunawachangia asilimia tatu, wangepewa zaidi, Serikali *intentionally* iweke *fund* pale ili waweze kupata fedha nyingi kwa ajili ya kufanya *rural electrification.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wakati mwingine huwa nawaza kwamba inawezekana fursa hizi tumezipoteza tangu mwanzo. Sisi tumepata uhuru mwaka 1961, Ghana wamepata uhuru mwaka 1957, tofauti ya miaka minne tu lakini wenzetu Ghana walipopata uhuru tu, walipokwenda kwenye mambo ya *villagization* kitu kilichofuata ni *rural electrification* na kuanzisha ile *the famous Akosambo Dam.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi nilikwenda Ghana, nikauliza *electrification* vijijini ikoje? Wakasema 75% ya watu wao wanapata umeme. Sisi miaka hamsini ya uhuru watu wetu ni asilimia 10 tu ndiyo wana-*access* umeme. Lakini Ghana walipoingia kwenye *rural electrification* katika mipango mikubwa kama ile ya Stigler's Gorge kama tungekuwa nayo tangu siku nyingi na sisi labda tungekuwa na asilimia 75% ya watu wetu wana umeme. Kwa hiyo, tukienda kwa hali hii ya kutegemea *TANESCO* tutafika tena miaka 50 labda watu asilimia 30 ndio wana umeme. Kwa mawazo yangu, nafikiri kama tutaitumia *REA,* tutakwenda haraka zaidi na *TANESCO* tukamwachia hii miradi mikubwa ya Stigler's au mradi wa Mchuchuma na mradi wa Ngaka sasa hivi na mito mikubwa mikubwa hii lakini hii midogo midogo kwa mfano katika Wilaya yangu mimi, nina vyanzo kama sita hivi vya mito ambayo unaweza kupata umeme bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika ujenzi wa miundombinu, niiombe sasa *REA,* kuanzia pale Kihansi kwenda Malinyi ya upande wa kulia, upande wa kushoto unaenda upande wa Ifakara, hapa katikati tumefungua uwekezaji mkubwa sana. Yako mashamba makubwa ambayo yanaweza kuchochea uzalishaji wa chakula katika nchi yetu. Kwa mfano, ukitoka Kihansi tu pale Chita JKT, wale wamepewa jukumu ya kuzalisha mbegu na *Tanzania Seed Agency*. Ukichepuka Chita unakwenda Kijiji cha Merera, kuna kampuni ambayo inasubiri, si muda mrefu wataanza kilimo cha mpunga, inaitwa *Syngen Fuels and Agro-Products* kutoka India, wanapewa pale hekta karibu 15,000. Tukiteremka kidogo ndiyo unakuta hiyo *Kilombero Plantations Limited* ambayo tayari wana-*operate*. Ukienda mbele kidogo, tunategemea kuweka Kiwanda cha Sukari cha Ruipa. Kwa hiyo, maeneo haya yamefunguka lakini hayana umeme. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali kupitia Wizara hii, iangalie eneo hili ambalo limefunguka kiuchumi ili waweze kupata umeme tusije tukampa kazi mwekezaji akaja akasita kuwekeza pale kwa sababu umeme hamna. Chanzo cha umeme kiko karibu, ni kuvuta tu, unapita pale JKT, unakwenda kwenye mashamba hayo. Kwa hali hiyo, tutakuwa tumewezesha nchi yetu kufunguka vizuri kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ligallama. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Omari Shaaban Kwaangw', lakini namwomba radhi kwa vile Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella ameingia. Sasa nampa nafasi ili awe mchangiaji wetu wa mwisho mchana wa leo.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nichukue muda mfupi kutoa shukrani zangu za dhati ambazo nimetumwa na wananchi wa Wilaya ya Ukerewe kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na hasa Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Ukerewe hivi karibuni akizindua umeme wa vijijini. Ninadhani sisi na watu wa Simanjiro, tunapaswa kutoa shukrani za dhati kwa sababu ni kati ya Wilaya ambazo tuko pembezoni lakini nchi hii isivyokuwa na ubaguzi, tumepewa umeme katika mazingira magumu. Umeme umevuka maji, umeme umesambaa vijijini, pamoja na kwamba bado kuna maeneo ambayo hayajapata lakini Mheshimiwa Rais alipokuja alitupa matumaini ya kuwa kazi hii bado inaendelea na wale ambao hawajafikiwa nao kuna siku watafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Mawaziri wanaohusika, Waziri Ngeleja na Waziri Malima, kwa jitihada wanazozifanya. Mimi mtu anapowakosoa hawa vijana, nasema hatuwatakii mema. Vijana wetu hawa tunawalea, ndiyo watakaokuwa viongozi wa kesho na kazi hii ya kuendesha Wizara, unaweza kumwona mwenzako hafai, ni kama kusonga ugali wa muhogo. Ukiona mwenzako unausonga ule mwiko unaenda haraka unafikiria ni mwepesi lakini ukiweka mwiko wewe unaanza kunyanyuka na sufuria. Kwa hiyo, ni vizuri pale panapofanywa kazi vizuri, tukawapa moyo vijana hawa, wamefanya kazi ngumu katika mazingira magumu, katika nchi ambayo haina uchumi wa kutosheleza mahitaji ya kila mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa pia mfano wa pili, haya mambo ya siasa tusiyafanye kama ya uke wenza. Akiolewa mwanamke mwingine, anakuambia kwamba, mke wako huyu alikuwa hajui kupika, mke wako huyu alikuwa hajui kukufulia nguo, yeye akifua nguo za bwana mkubwa ndiyo zinachanganyika rangi, huoni nyeupe ni ipi, nyekundu ni ipi na atasema aah, samahani sana nimepitiwa. Kwa hiyo, katika siasa tusifanye kama mambo ya uke wenza. CCM itakuwepo na itaendelea kuwahudumia walio wana CCM na wasio wana CCM ili mradi tu tuwe na subira na tusiwadanganye wananchi ya kwamba akija mtu mwingine ataweza kuliko CCM, CCM ni nambari *one*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tu niseme kwamba katika mradi huu wa Ukerewe, tumejifunza mengi. Tumejifunza jinsi maisha ya wananchi yanavyobadilika kwa dakika moja. Hivi sasa ukienda Ukerewe, tunauliza unakunywa bia, bia ipi, baridi au moto, hilo tulikuwa hatuna kabisa. Sisi kule tulikuwa tunaomba bia tu, tulikuwa hatuangalii. Mimi nilipolelewa ningali mtoto mdogo, tulikuwa na kitu kinaitwa senti mpaka ulaya, umeme umebadilisha badala ya kutazama kale sijui kabajeti kamoja hivi unaweka *slide*, unaweka *slide* inaitwa senti kumi, sasa hivi Ukerewe wameangalia Kombe la Dunia yaani walivyokuwa wanaangalia London, walivyokuwa wanaangalia Marekani na Ukerewe tulikuwa tunaangalia na kushangilia. Ni mabadiliko makubwa sana tena sana na siku hizi mimi napiga kampeni nyumba bora, maana watu wanabadilisha nyumba haraka sana kwa sababu huwezi kuweka umeme katika nyumba ambazo wanaziita kushoto kulia, kushoto kulia, kushoto kulia huku kachumba, huku kachumba katikati una kasebule kadogo lakini wamejitahidi, sasa unakuta nyumba zinabadilika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ndoa siku hizi, sisi tuna mila ya kuangalia mji kama kweli unafaa kumwozesha binti yako. Watu wameanza kuangalia, kule ule mti mkavu mrefu karibu na ile nyumba anakoolewa? Kwa hiyo, ndiyo maana safari moja niliwaambia hawa vijana, Waziri Malima pamoja na mwenzake, waweke umeme, wake zao wasiwe wanajigongagonga kwenye mawe na visiki usiku. Natumaini watakuwa wamelitekeleza. Watanijibu kama wameweka umeme vijijini kwao, kama hawajaweka kwa kweli mimi nitatoa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nataka niseme haya yafuatayo, mawili tu ya kutoa ushauri. Watu wote hapa tunahitaji umeme, kwa hiyo, tubuni namna ya kupata pesa ili mradi wa umeme nchini usiwe wa mahali hapa na pale. Ifike mahali uwe ni jambo la kawaida, hawa tunaowawakilisha, wananchi wanahitaji umeme. Kwa hiyo, kama mimi nimefurahia umeme, ningependa kwa kweli kila Mbunge aliyeko hapa, nyumbani kwake umeme ufike. Lakini hatuwezi kuufikisha kwa bajeti ndogo ndogo hizi lazima kuwepo na namna ya kubuni rasilimali za uhakika zitakazoelekezwa kwenye umeme ili tuweze kufanya *industrialization,* tuweze kufanya na mambo mengine na kupunguza shuruba kwa akina mama kwa sababu ukishapata umeme, unakuwa na nishati hata ya kuweza kutumia kwa mambo mengine ambayo yanamchukulia mwanamke muda mrefu na kwa hiyo mwanamke wa Tanzania atakuwa ameendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa pendekezo katika usambazaji wa umeme, jambo lingine ambalo nimeliona ni *maximization,* yaani kuhakikisha kwamba unapofikisha umeme basi sambaza kwa kiasi kikubwa ili uwe na wateja wengi kuliko kuwa na wateja wachache lakini jibu limekuwa ni nguzo. Basi nitoe pendekezo kwamba, hatuwezi kuwa na njia mbadala? Mimi nimetembea huku duniani, huwa sioni nguzo, wanatumia mabomba, yanapita ardhini na nyaya zako zinapita humo, ikifika pale unapohitaji, umeme unaibuliwa. Kwa sababu kama tutaendelea kutumia nguzo, nguzo, nguzo tutachukua muda mrefu kuliko kutumia mabomba ambayo yanakwenda chini kwa chini kama tunavyotandika mabomba ya maji halafu ikifika mahali ule waya unaibuliwa. Mimi ni pendekezo ambalo ningependa nilitoe ya kwamba tutumie na njia mbadala badala ya kutegemea nguzo na ninadhani watu wa Mazingira nao wataacha kutupigia kelele. Kwa hiyo, tubadilike kidogo na twende kwa kasi ili kila Mtanzania afurahi, achekelee kama sisi Ukerewe tulivyofurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeona umati uliokuja kumpokea Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri na Naibu Waziri wetu wa Nishati na Madini, mngefikiria labda wengine tumewaazima kutoka Kenya na Uganda kwa sababu tuko majirani. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana hao wawili hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikae chini, kwa kweli nimesimama kuonyesha furahi yangu, kuwashukuru, hawa vijana msiwaponde, wapeni moyo na nyie muwahi kupata umeme, uke wenza acheni, mkipewa mtanyanyuka na sufuria la ugali. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante. Hoja imeungwa mkono na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella.

Waheshimiwa Wabunge, huyo alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo. Labda sasa nianze kuwataja wanne ambao wataanza jioni ya leo. Kwanza, atakuwa Mheshimiwa Omari Shabani Kwaangw', atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na wa nne atakuwa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda uliobakia hautoshelezi mchangiaji mwingine yeyote kuja kuchangia na hatuwezi kuendelea na hizi shughuli, naomba sasa nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na michango na kama nilivyozungumza hapo awali kabla hatujasitisha shughuli za Bunge, ni kwamba tukirudi, tutaanza na Mheshimiwa Omari Kwaangw', kwa hiyo, tutaanza na huyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, ajiandae.

**MHE. OMARI SHABANI KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo juu ya hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuhakikisha kwamba hii silaha kubwa ya maendeleo tunaitumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo kama manne, lakini kwa sababu ya muda, nitajitahidi kusema kwa haraka zaidi. La kwanza, niseme, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli hapa Bungeni, kauli ya kwanza ilikuwa inahusu uchakachuaji wa mafuta. Jambo hili la kuchakachua mafuta, limeshusha sana heshima ya nchi, limeshusha sana sifa ya nchi, limeshusha sana uchumi wa nchi, lakini vilevile jambo hili linauwa viwanda vyetu, mitambo yetu, magari, mashine na mambo chungu nzima. Sasa tatizo hili naliona kama hujuma kubwa kwa Taifa na kwa kweli ushauri wangu ni kwamba ni lazima watu hawa wanaofanya vitendo hivi washikishwe adabu kwa sababu jambo hili ni kubwa na zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri kwamba badala ya kuhangaika kuwaadhibu watu hawa kwa kutumia Sheria iliyounda *EWURA* na kanuni zake, hawa watu walitakiwa washikishwe adabu chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi, ndio inatakiwa

twende huko, hili ndio jambo zito kabisa. Kwa hiyo, ninaishuri kabisa Serikali waachane na adhabu hizi za shilingi milioni tano sijui shilingi milioni kumi, hawa ni watu wenye uwezo, hawa ni watu wanaouwa kabisa uchumi wa nchi. Kwa hiyo, ni vizuri tuwapeleke kwenye ile Sheria ya Uhujumu Uchumi, halafu muone, hebu jaribuni kidogo tu, kama jambo hili halijakoma chini ya Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vizuri Serikali ijiulize, hivi ni kwa nini vituo vingi vya mafuta vinajengwa kati ya Mlandizi, Kibaha, kote kule, kila kilometa moja, kituo cha mafuta, kwa nini? Ndio maghala yenyewe hayo. Kwa hiyo, chukueni hatua za kutosha kuhakikisha kwamba vituo vile vinavyotakiwa tu ndio vinabakia, mbona huku kwingine hakuna vituo na unasafiri hapa mpaka Babati, hakuna kituo hapa mpaka uingie Kondoa? Ni kwa nini pale kila kilometa moja unakuta kituo cha mafuta? Ni kwa nini Serikali haishtuki? Nilitaka kusema hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri alitoa kauli hapa ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ambao kwa kweli utatumia shilingi bilioni 98.4. Nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa ujumla katika kuhakikisha kwamba kweli fedha hizi zitakwenda kwenye miradi ile ya umeme vijijini. Sasa kwa Jimbo la Babati Mjini, kwa kweli nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kukubali ombi la wananchi tangu tulipokuwa tunanadi Sera na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2005, wananchi wa Kata mbili waliomba sana wapelekewe umeme na Kata hizo ni Kata ya Singe na Bonga, Kata hizi mbili ndizo zinazolisha mji wa Babati. Mambo yote ya uzalishaji yanatoka kwenye Kata hizi. Kwa hiyo, kupeleka umeme kwenye kijiji cha Managa, Himiti, Bonga na Haraa, ni jambo la msingi sana. Kule tumejenga taasisi, shule zipo nyingi, vilevile kuna Kituo cha Afya na taasisi nyingine na kuna shughuli nyingi sana za kiuchumi. Kwa hiyo, hili ni jambo la faida sana na kwa kweli tunataka kutumia nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali kukubali ombi hilo.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, lakini naomba niweke angalizo kidogo katika kauli ambayo aliitoa Mheshimiwa Waziri. Angalizo lenyewe ni kwamba nimeona kampuni ya *Namis Corporate Services Tanzania,* imepewa kazi kwenye Mikoa mine na vilevile nimeona kuna kampuni nyingine, kwa mfano *Symbion Power, USA,* nayo imepewa Mikoa kama mine. Sasa nilikuwa ninajiuliza kwa sababu ya utekelezaji, mara nyingi Wakandarasi hawa wanatupa tabu sana, anaanza kazi kidogo hapa, anakimbilia kwingine, anaanza kidogo, anaacha, anakimbilia kwingine. Sasa ningeomba Wizara ituhakikishie kwamba Kampuni hii ya *Namis Corporate Services Tanzania,* inao uwezo wa kujenga miradi iliyotajwa kwenye Mkoa wa Manyara ambayo itagharimu shilingi bilioni 2.9, Mkoa wa Tabora shilingi bilioni 8.7, Mkoa wa Kigoma shilingi bilioni 8.7 na Mara shilingi bilioni 4.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwa kweli, wakati mwingine makampuni haya yanaweza kuwa na *tendency* ya kuona kuwa mradi huu ni mdogo na kwa hiyo yanakimbilia ule mkubwa na huu mwingine wanauacha. Mimi ninashukuru kwamba kampuni hii imeanza mradi huo ambao nimeutaja wa Managa, Himiti, Bonga na Haraa, wameshafanya *survey* ikiwa ni pamoja na *pegging* kuonesha kwamba nguzo zitapita wapi na kila kitu. Lakini kwa sababu Mkoa mzima wa Manyara, miradi hii ya

umeme inagharimu shilingi bilioni 2.9. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kampuni hii ianze huu mradi mdogo halafu iende kwenye hii miradi mikubwa ya shilingi bilioni 8, 7, ili tuone kwamba hii kazi inaweza kuisha kwa mara moja tu na kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo lingine ni kwenye Kitabu cha Hotuba, nikilinganisha na kauli aliyoitoa, muda wa utekelezaji wa mradi kwenye kauli umeonesha ni miezi 12, lakini kwenye kitabu wakati leo ninajaribu kuangalia ni miezi sita. Hebu jambo hilo waliangalie na mimi ninadhani mradi kama huu ulioko Manyara wa shilingi bilioni 2.9 ni mradi ambao sio mkubwa sana, kampuni hii inaweza kutekeleza hata chini ya miezi sita. Lakini ningeomba *clarification* kwa sababu huku kwenye kauli imeonesha miezi 12 na hapa ni miezi sita, itatusaidia sana kuona tunakwenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye jambo la tatu. Ni changamoto kwa Serikali katika suala la ucheleweshaji wa fedha. Makampuni haya yakianza kazi, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba wanapewa fedha. Hii itatusaidia sana kuhakikisha kwamba kwa kweli miradi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mipango ya Babati Mjini, *TANESCO* katika jambo hili la tatu, wameonesha kupeleka umeme katika sehemu mbalimbali katika Mji wa Babati, hii ni pamoja na mtaa wa Mruki, Urara Juu, Waang'warai kule *VETA,* Sawe, Komoto na Gendi Mnadani na kijiji cha Sigino. *TANESCO* wana uwezo, wanachokosa kwa kweli ni mtaji. Pale Babati tuna *Sub-Station* ambayo kwa kweli ni kubwa na ina umeme wa kutosha. Nadhani ni *megawatt 32* na ninadhani hatujatumia hata robo ya uwezo wa ile *Sub-Station,* tatizo kubwa ni usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme moja kwa mfano, pale kwenye mtaa unaoitwa Maweni na Ari, kuna *transformer* iliyokuwa iwekwe chini ya mradi wa *Electricity IV,* haikuwekwa pale mpaka leo *TANESCO* wanasema wamepeleka maombi Wizarani, sasa jamani hata *transformer* tu mpaka Wizarani? Kwa hiyo, *TANESCO* muiwezeshe vya kutosha mambo madogo madogo kama haya ya kuweka *transformer* na nini, kwa kweli yangeweza kutekelezwa katika eneo husika ingeweza kutusaidia sana. Pamoja na kwamba *transformer* hiyo wanasema ni *underline transformer,* kwa hiyo, inabidi iombwe kule Wizarani, lakini nadhani pia haya ni mambo ambayo yangeweza kufanyika bila kuwa na urasimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme vilevile Serikali iijengee uwezo *TANESCO* kama nilivyosema, *TANESCO* wanao ujuzi wa kutosha, wanakosa tu mtaji. Hii itaweza kusaidia sana kutekeleza miradi hii midogo midogo kwa haraka zaidi wakisaidiana na *REA,* mimi ninadhani mambo yatakwenda vizuri. Ni vizuri *TANESCO* katika mipango yao inayokuja kwa Mji wa Babati, sasa wapeleke umeme vilevile kijiji cha Kiongozi, Hala na Mtuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Shabani Omari Kwaangw'.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii, kuwatambulisha wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge) ambao ni wageni kutoka Ubalozi wa China, *Mr. Liu* ambaye ni *Consular* na *Miss Wang Hoo, Diplomat Attachee.* Wageni hawa wako Dodoma kwa mwaliko wa Mkutano Mkuu wa CCM. *You are most welcome to the National Assembly of Tanzania and to the CCM General Assembly. Welcome to Dodoma. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya utambulisho huo, sasa tutaendelea na michango. Sasa atafuata Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ajiandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza sana mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu, nawapongeza sana kwa dhamana kubwa mliyoibeba katika kuliletea maendeleo Taifa letu, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Wizara hii ya mwaka uliopita, Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* wametenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kupeleka umeme Wilayani kwangu na Jimboni kwangu, kupeleka umeme katika kijiji cha Lupa Tingatinga, Mlima Njiwa na Sangambi. Walitenga fedha, kampuni ikapatikana, imeanza kazi mwezi huu, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ukiwa na harusi ambayo imefana, halafu ikawa imenoga kweli kweli, Bwana Harusi amepambwa vizuri, wale wasindikizaji wanakuwa na nyimbo nyingi sana nzuri za kumsifia Bwana Harusi. Sasa mimi Jimboni kwangu, wasindikizaji wangu hoja na wimbo wao mkubwa kwenye hii harusi yangu, ilikuwa ni kwamba umeme hauwezi kuja Lupa mpaka mimi niwe Mbunge, umeme hauwezi kuja Sangambi mpaka mimi niwe Mbunge, umeme hauwezi kuja Mlima Njiwa mpaka mimi niwe Mbunge, wewe rafiki yangu wewe, umeme haleti Mbunge, umeme unaletwa na serikali. Kazi ya Mbunge, ni kujenga hoja, kuishauri Serikali, kuiomba na kuishinikiza, inayoleta umeme ni Serikali, sio Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana ninachukua nafasi hii kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu, nawashukuru sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, rafiki yangu, ahsante sana. Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, mdogo wangu Naibu Waziri, ahsante sana, nawashukuru sana. Mheshimiwa David Jairo, rafiki yangu, ahsante sana. Mheshimiwa Dokta Humphrey Lutengano

Undule Makahesya, Mkurugenzi wa *REA,* ahsanteni sana. Ninawaambia wasindikizaji wimbo wa umeme Lupa Tingatinga, wimbo wa umeme Sangambi, wimbo wa umeme Mlima Njiwa, Serikali imetekeleza, anzeni nyimbo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizo kwa rafiki zangu hawa, hii ndio raha, starehe ya kuwa na marafiki, ninaomba niongelee Wakala wa Jiolojia Tanzania. Wakala wa Jiolojia Tanzania, kazi yake kubwa ni kufanya utafiti na kutambua maeneo ambayo yana madini. Sasa Wilayani kwangu Chunya, Wakala huu walifanya utafiti mwaka juzi na mwaka jana wakachora na ramani, maeneo mapya ambayo yana madini. Maeneo ya Ngwala, maeneo ya Kambi Katoto, ya Mafyeko, walipofanya kazi hiyo ya kuchora ramani, wamepeleka Wizarani, tatizo linaanzia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Wizarani viongozi wa Wizara, sio hao niliowasema, Dokta Kafumu, vijana wake, Kamishna wa Madini, sijui wanafanyaje mchakato wa kuwapatia watu leseni ya sehemu ambazo kuna madini? Mimi ninadhani kungekuwa na *transparency* kwamba Wilaya inayohusika ijue kwamba kuna maeneo ambayo yana madini, Halmashauri ijue, wachimbaji wadogo wadogo wa sehemu zile wajue. Sasa nilijua kwamba mmefanya utafiti huo, nimeenda Wizarani, jamani tuone ramani hizi, ayaa, zote zimejaa leseni, mmegawaje? Hapa hakuna *transparency.* Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, pale Wizarani kwenye Kitengo cha Madini iongezeke *transparency.* Sio kwamba ninakupiga madongo Dokta Kafumu, najua wewe ni Mbunge mtarajiwa, lakini naomba iongezeke *transparency* kwenye sehemu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee Wakala wa Ukaguzi wa Madini. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Nishati na Madini, hawa Wakala wamefanya kazi nzuri sana kwa gharama nafuu kukagua hesabu za migodi ya madini, kusimamia na kukagua shughuli za mazingira, wamefanya kazi nzuri sana kwa gharama nafuu. Naiomba sana Serikali, namwomba Mheshimiwa Waziri, imefika wakati sasa Wakala huu iwe Mamlaka kamili ili iongezewe nguvu za kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba niongelee bomba la kupakulia na kusambaza mafuta kwa pamoja. Pale Bandarini kuna mchakato wa kutaka kujenga bomba jipya kubwa kuanzia mwaka juzi lakini kuna mgongano kati ya *TPA* ambaye ndiye mwenye Bandari na *TPDC* ambao ndio wana dhamana ya mafuta na *EWURA,* wanachelewesha kufanya bomba hili lijengwe. Nchi kama Zambia zinategemea sana mafuta kupita kwetu kwenda kwao. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ulisimamie suala hili ili bomba lijengwe haraka na liweze kuchangia maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Mheshimiwa Waziri, aweze kusimamia kwa haraka Mgodi wa Kiwira uanze kuzalisha umeme. Serikali imeshauchukua mgodi huu na inasema inampa *STAMICO* na *TANESCO*, sasa ni nini kinachosubiriwa? Tuna *Megawatt* 200 pale ambazo zingesaidia sana kupunguza makali

ya ukosefu wa umeme nchini kwetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri alisimamie suala hili haraka sana yaani umeme wa kutoka Kiwira, unahitajika juzi na wala sio jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba niongelee suala ambalo ameliongelea mwenzangu Mheshimiwa Kwaangw', la uchakachuaji wa mafuta. Aibu tuliyoipata Tanzania ni kubwa sana, ni aibu kweli kweli na watakaopoteza katika hili ni wafanyabiashara, wao walidhani ni wajanja, lakini wao ndio wapotezaji. Nchi ya Rwanda imegundua kwamba tunapeleka mafuta ambayo yamechakachuliwa, sisi hatujagundua! Hii ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nimesema mara nyingi sana hapa, jamani kutoka Kibaha mpaka Mlandizi kilometa 20, *Petrol Stations,* zipo karibu 30, zinafanya nini? Nimesema sana mimi, jamani hizi *Petrol Stations,* zina maukuta huku nyuma, marefu zaidi ya *Fort Jesus,* ni ya nini haya? Juzi Mheshimiwa Waziri, ametoa kauli anasema Viongozi wa Mkoa wa Pwani pamoja na *EWURA* walisema kwamba waliviagiza hivi vituo vya mafuta kwamba wabomoe maukuta kama *Fort Jesus* ambayo yako nyuma yao huku, wachache ndio wamebomoa, mengine bado yapo. Kwa hiyo, hata kama tukisema kwamba kuanzia mwezi ujao *EWURA* watadhibiti zaidi kwa kufanya *marking* kwenye mafuta, lakini bado wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba rafiki yangu Bwana Haruni Masebwe, Mkurugenzi Mtendaji wa *EWURA* kaangalie tena, yale maukuta huku nyuma bado yapo, wanafanya nini? Sio hapo tu, sehemu zote hata ukija njia ya kuja Dodoma kutoka Morogoro, vipo vituo vya petroli ambavyo vina maukuta nyuma, yanafanya nini? Uwe mfano kwetu, tumepata aibu kubwa sana na hii itafanya biashara ya mafuta na biashara nyingine, nchi jirani zihamishe kutoka Bandari ya Dar-es-Salaam, ziende kwenye Bandari nyingine. Hapa tu nchi ya Malawi na nchi nyingine, wanahamisha huduma kutoka Bandari ya Dar-es-Salaam kupeleka Beira Msumbiji kwa sababu *efficiency* ya kule ni kubwa, *seriousness* ya kule ni kubwa, huku kwetu *seriousness* na *efficiency* ni ndogo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, ulishughulikie suala hili kwa karibu sana na kwa umakini sana, ili aibu ambayo tumeipata nchi yetu tusiipate tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hotuba yangu ilikuwa ni kushukuru tu hasa kwa kupelekewa umeme kwetu Chunya. Naomba kuishia hapa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii na niwapongeze Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne inayoendeshwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, hususan Wizara ya Madini na Nishati pamoja na Viwanda na Masoko, kwa kufanya kazi ambayo haikutegemewa. Kwa karne nzima imezungumzwa bila mafanikio lakini leo

tunazungumza habari ya maendeleo ya chuma liganga na makaa ya mawe kule Mchuchuma. Hongera sana CCM na wananchi wa Ludewa na Mkoa mpya wa Njombe. Sasa tukae mkao wa kula kutarajia kupaa kwa maendeleo katika Mkoa huo mpya na Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea katika mradi wa kwanza wa chuma ghafi, ni uandaaji wa miundombinu ya barabara katika maeneo ya migodi, uchorongaji ili kutambua kuna madini kiasi gani kwenye eneo la kampuni ya Maganga Matitu walilopewa kwa ajili ya mradi huo pamoja na maeneo ya makaa ya mawe Mchuchuma au Ketawaka. Lakini vilevile kuna kuchukua sampuli za chuma, pamoja na sampuli za makaa kwa ajili ya uzalishaji wa majaribio ili kuona *product* zitakazozalishwa kule zitakuwaje na kisha kuanza kujenga kiwanda na kuanza machimbo yenyewe rasmi kwa ajili ya uzalishaji wa chuma ghafi. Changamoto iliyopo ni kwamba wananchi wanaozunguka maeneo hayo hususan Vijiji vya Mundindi, Amani, Shaurimoyo na Mkomang'ombe, hawajapewa fidia zao stahili kwa sababu tayari miradi hii imeanza lakini fidia zao hazionekani, tunaomba zishughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nataka nipongeze mkataba mzuri uliowekwa kati ya mwekezaji na Serikali katika Mradi wa Maganga Matitu, kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi wa Ludewa kushiriki kikamilifu katika mradi wa kasi mpya wa chuma ghafi. Fedha zimetengwa kwa ajili ya *capacity building* au *empowerment* kuwawezesha wananchi kubuni miradi yao na shughuli zao zingine za maendeleo ambazo ni endelevu zinazoweza kuendana na mradi huu wa kasi mpya. Programu ambayo ni ya pekee katika Tanzania kwani hakuna mwekezaji kufikia leo aliyekuwa ameweka au kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi ili na wao waweze kushiriki kikamilifu katika miradi mikubwa ya maendeleo kama huu. Ninaomba mradi huu/programu hii ya kuwawezesha au kuwa-*empower* wananchi, ianze mara moja kwa sababu tunazidi kuchelewa, fursa zinapotea kwani wakati mradi umeshaanza, programu ya kuwawezesha wananchi hao wa Ludewa imechelewa na haijaanza mpaka leo. Ninaomba ianze mara moja ili wananchi hawa nao wajipange vizuri waweze kufaidi matunda ya kuanzisha mradi wa kasi mpya wa chuma ghafi kule Liganga na Ketawaka/Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naishukuru vilevile Serikali kwa ruzuku iliyotolewa katika mradi wa umeme mdogo wa maporomoko ya maji katika kata ya Mawengi ambapo umeme tayari unazalishwa na wananchi wameanza kufaidika kutokana na umeme katika Kata hiyo. Najua kwamba umeme unaozalishwa pale ni *kilowatt 150* ambayo ni pungufu kwa asilimia 50. Hapa tunaomba Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano, ihakikishe kwamba fedha inatengwa na ikiwezekana katika bajeti hii kuhakikisha kwamba uzalishaji wa *kilowatt* nyingine 150 unawezeshwa ili wananchi wa Kata yote ya Mawengi waweze kufaidi umeme na kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, nataka niipongeze Serikali kwa hatua iliyofikiwa kwa Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe kule Mchuchuma. Kati ya vitu ambavyo

vimekuwa ni ndoto, imekuwa ni kuzalisha umeme Mchuchuma. Leo tunazungumzia makampuni matano au sita ambayo tayari yapo na yameelekezwa kuleta mapendekezo (*proposal)* kwa ajili ya kuonyesha jinsi watakavyoweza kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme *megawatt* 400. Wananchi wamekuwa na wasiwasi kwamba miradi haiwezekani. Nataka niwathibitishie kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Nne, ilijipanga vizuri, imefanya kazi nzuri na tayari tunategemea mwekezaji wa mradi huo mkubwa wa *megawatt* 400 apatikane ifikapo Desemba au Septemba mwaka huu. Tunaomba Serikali ituambie wazi baada ya hapo utekelezaji wa mradi huo utaanza lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, nizungumzie Mradi wa Umeme Ludewa Mjini kwani sijaona kwenye kitabu hiki kama kuna kupanua mradi huo ili uweze kwenda kwenye kijiji jirani ambacho ni sehemu ya Kata ya Ludewa. Umeme wanafaidi watu wachache sana pale Makao Makuu wakati Vijiji vinavyozunguka hasa Ludewa Vijijini, havipati umeme. Hivyo tunaomba mradi huu upanuliwe ili wananchi wale waweze kufaidi umeme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Mheshimiwa Waziri, mambo yote mazuri nimeyasema lakini suala la ofisi ya Afisa Madini Ludewa, kila mwaka wa bajeti ananiambia tutajenga na kila mwaka naamini inatengwa bajeti kwa ajili ya kujenga afisi ile, lakini kila mwaka sioni ujenzi huo. Nataka Mheshimiwa aniambie safari hii kwa mara ya mwisho wakati tunaagana hapa, nithibitishiwe kamba safari hii fedha zimetengwa kwa ajili ya kujenga ofisi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, nashukuru Serikali kwa kuwezesha wananchi wavuvi wa Mwambao wa Ziwa Nyasa kupewa teknolojia mpya na ya kisasa ya uvuvi kwa kupewa boti na *engine kt* vijiji kumi na moja Mwambao wa Ziwa Nyasa. Uvuvi huu utawawezesha kwenda kuvua samaki Kilindini lakini samaki watakuwa wengi na wataendelea kukausha samaki kwa kutumia kuni na kukata miti kwenye miteremko ya milima Livingstone. Naomba Serikali au Wizara hii, mueleze mtawasaidiaje wananchi wa Mwambao katika Wilaya yangu ili waweze kupata teknolojia mbadala ya kukausha samaki ili tuhifadhi maeneo ya Mwambao wa Ziwa Nyasa ambayo yanaendelea kuathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashukuru sana Serikali kwa hatua iliyochukua katika sekta ya umeme na madini katika Wilaya ya Ludewa na ninaamini katika kipindi cha miaka mitano tunayoianza, Wilaya ya Ludewa itapata mafanikio sana katika eneo hilo na kujiletea maendeleo ambayo yalikuwa hayajapatikana kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri pamoja na wataalam wote

wa Wizara na taasisi zote ambazo zipo chini ya Wizara hii. Nafahamu kuna wataalam wa kutosha wa kuelewa haya mambo lakini sisi lazima tuendelee kuishauri Serikali na matumaini yetu ni kwamba siku moja labda mtaweza kukubaliana na sisi mia kwa mia kwa yale tunayowashauri kwa sababu tunayaona ni ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la uchakachuaji. Nilizungumza hili katika *Finance Bill* lakini leo narudia na najaribu kutoa *option* au njia mbadala ni jinsi gani tuepukana na tatizo hili. Suala zima alilolizungumza Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake juzi, mimi bado nasema kwamba Serikali inapoteza muda, hawa watu wanaofanya kazi hii ya kuchakachua, ni majangili, hawataacha, wataendelea kufanya, hivi sasa wanatafakari wafanye mbinu gani ili waendelee kufanya uchakachuaji bila Serikali kuweza kuwabana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba ni vyema Serikali ikapandisha Kodi ya Mafuta ya Taa, ikapunguza Kodi ya *Diesel, Petrol*. Katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba mafuta ya *petrol* kodi inayotozwa ni mia tano thelathini na tisa, kodi ya *diesel* ni mia tano kumi na nne, lakini ukija kwenye mafuta ni shilingi 52 na bei za mafuta ya *diesel* pamoja na *petrol* haziko mbalimbali ni 1500, 1600 zina-*range* hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitazama bei ya mafuta ya taa na kodi inayotozwa ya shilingi 52, wakati bei ya mafuta ya taa ni shilingi elfu moja na kidogo mpaka shilingi elfu moja na arobaini, hakuna uwiano kwa sababu huku kwenye *diesel* karibu theluthi moja ni kodi, kwenye *petrol* theluthi moja ni kodi lakini kwenye mafuta ya taa hakuna uwiano, shilingi 52 na bei iwe shilingi elfu moja na mia moja uwiano upo wapi wa theluthi moja kwenda huko, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi *TRA* inapopanga hizi kodi katika mafuta ya taa kwa nini haiweki bayana kuna tatizo gani lakini hakuna uwiano wa kodi na bei ya mafuta ya taa inayouzwa! Kwa hiyo, bado mwananchi anaumia pamoja na kusema kwamba tunatoza kodi ndogo au kodi inayotozwa ni ndogo, shilingi 52 na mafuta ya ndege ni bure, sasa uwiano huu haupo kabisa. Wangepunguza shilingi 150 kwenye *petrol*, shilingi 150 kwenye *diesel* wakaongeza shilingi mia tatu kwenye mafuta ya taa sasa uwiano wa kodi hapa na bei ya mafuta ya *petrol, diesel* na *kerosine* hazina tofauti kubwa sana. Hapo ndiyo itakuwa *permanent solution* ya uchakachuaji, vinginevyo tunahangaika bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ni binadamu, wanauza mafuta ya kuchakachua, ni binadamu, watakaa pembeni, watazungumza, wote sio sawa, wote hawako katika uzalendo sawa. Sasa tutapoteza muda, kwa kweli tutapiga kelele hapa na hatimaye Serikali itatuona kama wendawazimu, tunapiga kelele wakati ninyi wenyewe mna uhakika au tuambieni ukweli kuna vigogo gani basi wana maslahi katika hili ili na sisi tupate kujua basi tusianze kupiga kelele na hatimaye tunyamaze kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nalotaka kuzungumza ni hili la mafuta ya taa, leo tuna gesi kwa nini msi-*compansate* kwenye gesi mnakwenda kwenye mafuta ya taa, pandisheni bei hiyo ya mafuta lakini huku kwenye gesi mpunguze basi kodi iwe bure au iwe shilingi hiyo 52 angalau yule mwananchi apate ile gesi kwa wingi kule vijijini ili aondokane na kutumia mafuta ya taa ama sivyo kutakuwa hakuna faida kwa sababu gesi iliyopo hapa inaweza ikatosheleza wananchi. Mpeni *TPDC* afanye kazi hiyo na wafanyabiashara kule vijijini watamudu kuuza gesi na wananchi wetu wa Tanzania sio mbumbumbu, wanaweza wakaitumia gesi majumbani. Leo mwananchi wa kijiji anaweza akatumia *mobile phone,* akatuma *message*, akapokea *message*, itamshinda kutumia gesi katika nyumba yake? Haiwezekani, msiwadharau, hawa wananchi wanaelewa kila kitu, hebu fanyeni haya mambo tuweze kumalizana na hili tatizo la uchakachuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *TANESCO* irekebishe tatizo la kuuza nguzo, waya na mita kwa mwananchi halafu yeye akiashaanza kutumia umeme ile nguzo inakuwa sio yake, waya sio zake na mita sio yake, imeshazungumzwa hapa sitaki kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la uingizaji wa mafuta, meli zinazotumiwa kuingiza mafuta nchini ni meli ndogo, gharama ya mafuta inakuwa kubwa. Tumezungumza hapa na Serikali inalifahamu hili kwamba sasa hivi tunatakiwa tulete mafuta kwa wingi katika *bulk* kwa kutumia meli kubwa lakini kunatakiwa kuwe na *SBM* ambayo itajengwa kwa ajili ya meli kubwa. Sasa sijui tatizo liko wapi? Nasikia kuna mvutano kati ya *EWURA*, *TPDC* na *TPA.* Sasa hebu jamani kama kuna mvutano, tuyasawazishe, tumalize hili tatizo la kujengwa *SBM* kwa ajili ya kupokea meli ambazo ni kubwa ili tupunguze tatizo la kuingiza mafuta nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kusema kwamba Mheshimiwa Waziri, tafadhili, mimi miaka mitano iliyopita umeniletea transfoma moja tu Pangani ya Kipumbwi lakini safari hii tunapokuja na Mungu atujalie turudi, nina Vijiji vyangu vitano havijapata umeme mpaka leo, naomba unisaidie na nitatuma kwa maandishi Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu hadi leo kuweza kuwatumikia wananchi wa Temeke na nawaambia nawapenda sana na bado nina nguvu ya kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa dhati kabisa, kwa hotuba nzuri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wote na wafanyakazi wote wa Wizara. Nitakuwa mchoyo nisipompongeza Eng. Muhando, kwa kuchaguliwa kuwa kiongozi kwenye Shirika la Umeme Tanzania, napongeza Bodi, nampongeza Waziri na Naibu Waziri na nampongeza sana Rais kwa uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri imefika wakati tunatakiwa tujifunze, eneo kama la *TANESCO* linahitaji kiongozi mwenye sifa kama za Eng. Muhando. Mara nyingine unaweza ukamchukua Mtaalam wa mambo ya Fedha, ukampeleka kwenye Shirika ambalo kazi yake haihusiani na mambo hayo. Nasema hivyo kwa sababu Muhando namjua, nimekuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO,* nilichaguliwa na Mheshimiwa Msabaha, namshukuru sana, Mwenyezi Mungu atamzidishia, Muhando ni msikivu, Muhando anaheshima wadogo na wakubwa. Nasema hivi nina maana ya kwamba kama Serikali tutaipa uwezo *TANESCO* na wafanyakazi watampa ushirikiano wa dhati Muhando, basi nina uhakika, tutavuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi na hali yenyewe leo si nzuri sana lakini nilikuwa nataka kuzungumzia ukurasa wa 15, kifungu cha 25, Serikali iliendelea kusimamia ukarabati na kuimarisha mifumo ya umeme katika Mkoa wa Dar es Salaam, nawashukuru sana lakini tunalo tatizo la fidia. Tulilipa fidia shilingi bilioni saba, kwenye maeneo yale ya Kurasini, Mbagala, Ubungo, tulifanya mikutano miwili pale na uongozi uliopita wa *TANESCO*, tukakubaliana kuna nyongeza ya vifaa asilimia 18, sasa wananchi wale mpaka leo hawajapata malipo, tunakwenda kwenye uchaguzi, tutahukumiwa bila sababu na kilichokuwa cha mtu ni haki yake. Mimi niombe sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nishukuru sana, mwaka jana hapa nililalamika juu ya wananchi wa Temeke kutaka kuuziwa nyumba zao kwa ajili ya bili kubwa ya umeme lakini Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na huyo huyo Muhando akiwa *General Manager* walitusaidia sasa hivi wananchi wote wanafungiwa Luku na wanalipa kidogo kidogo. Kwa hiyo, nawaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Temeke tatizo letu ni umeme kukatikakatika na tunapata umeme mdogo yaani *low voltage,* lakini naamini kwa uongozi wa *Engineer* Muhando, sina nongwa, najua mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kuhusu suala la kuchakachua lakini kwa Kiswahili kizuri ni kuchanganya mafuta. Mimi nasema hili suala linaniuma kwa sababu makampuni mengi na makubwa ya mafuta yako kwangu Temeke, makampuni hayo ni *BP, Oilcom, Camel Oil, GBP* na kadhalika. Sasa tatizo ninalolipata ni kwamba zile kampuni zina sifa nzuri lakini matokeo yake wanaochukua mafuta, wakipeleka mbele, wanayachakachua na kuyauza, matokeo yake kampuni zile za Temeke zinapata lawama. Kwa hiyo, naomba Kaka yangu Haruna Masebe, mimi nakupongeza kwa sababu mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya, Kibaha, wakati ule lilikuwa linafanyika tena kwa kiasi kikubwa na tulikuwa hatusemi lakini sasa hivi umelisimamia kwa kweli unalipunguza, Serikali mpeni nyenzo, nina uhakika litawezekana kumalizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mzee Maulid ambaye yuko London, ana miaka 40 katika Ofisi ya Almasi, tokea tumefungua ile ofisi mpaka juzi imefungwa, yule Mzee anadai kalipwa pesa siyo stahili yake. Wizara mtazameni yule Mzee mumlipe kwani Mzee analalamika na si vema watu kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na sasa namwita Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu na Mheshimiwa Mgana I. Msindai sasa ajiandae. Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa naona hayupo kwa hiyo nafasi hiyo sasa nampa Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu atafuatiwa na Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Halima J. Mdee ajiandae.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri ya bajeti waliyoiwasilisha leo. Ninawapongeza vilevile kwa mambo mazuri na mafanikio makubwa waliyoyapata katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba umeme ni kichocheo muhimu katika kuleta maendeleo lakini hadi sasa ni asilimia ndogo tu ya Watanzania wanaopata umeme na nina uhakika kwamba watu wanaopata umeme katika Mkoa wa Kagera wastani ni ndogo zaidi kuliko hata ule wastani wa Kitaifa. Kwa mfano, sehemu kama Bukoba Vijijini pale Katoma, Lukindo, kinachohitajika ni *substation* kusudi maeneo kama ya Lukindo, Kyambeo, Mauguru mpaka kwenye shule ya Msingi ya Kilaini yaweze kupata umeme. Gharama zake nilishaziwasilisha kwenye ofisi ya Waziri, lakini ni karibu miaka miwili waliniahidi kwamba kwa kupitia Mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini wataweza kuhakikisha kwamba hiyo *substation* inapatikana na wakati huo gharama zake zilikuwa chini ya shilingi milioni mia moja. Sasa ninapenda Waziri anieleze katika bajeti hii, je, kuna *provision* hiyo kwamba sehemu hiyo basi itafungwa hiyo *substation* kusudi wakazi wa pale waweze kupata umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba Bukoba kuna mvua za kutosha, hali ya hewa nzuri na kwa sababu hiyo basi kilimo cha ndizi, matunda, maua, mboga za majani na kadhalika kinashamiri na vilevile kinaweza kupanuliwa. Hata sasa ukienda utakuta ndizi, nanasi na kadhalika ni nyingi. Ili kumuinua mkulima huyu wa Mkoa wa Kagera hususani wa Bukoba Vijijini, ni kuweka viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda, tukatengeneza *juice, biscuits, jams* na kadhalika ili akishauza basi aweze kupata fedha na aondokane na umaskini. Lakini bila umeme, wakulima hawa wataendelea kuuza matunda yakiwa hivyo hivyo, hawataweza kuongeza thamani kwenye mazao yao na matokeo yake ni kwamba watendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiambia Serikali kuwa wakazi wa Mkoa wa Kagera na hususani wa Bukoba, wako tayari kulima zaidi lakini wanachohitaji ni umeme ili kusudi waweze kusindika mazao yao. Ninaomba Waziri anieleze katika Mpango wa Usambazaji wa Umeme Vijijini, ni vijiji vingapi na ni vipi ambavyo vitapatiwa umeme katika bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una Wilaya mbalimbali mojawapo ni Ngara. Wilaya ya Ngara, ina fursa kubwa ya kuweza kuendelea na ikiendelea itaweza kuchochea maendeleo katika Mkoa wa Kagera kwa sababu iko *strategically positioned*, iko mpakani mwa Rwanda na Burundi. Tukiweza kuipatia Ngara umeme, ina maana kwamba itakuwa imeendelea na Mkoa mzima utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Ngara tuna Maporomoko ya Rusumo ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu lakini hadi sasa tumeshindwa kuyatumia ila tungeweza kuyatumia. Kufuatana na *statistics* zilizotolewa na *Nile Basin Initiative,* Watalaamu wanasema unaweza ukafungwa mtambo pale na tukazalisha mpaka *megawatt 60* za umeme, sisi tukatumia 20, Burundi tukawapa 20 na Rwanda tukawapa 20. Kinachonishangaza ni kwamba maporomoko yako pale lakini sioni *initiative.* Walianza kusemasema lakini ni kitu gani sasa kinaendelea? Ninaomba Waziri anieleze kwamba ni kitu gani kinaendelea kusudi tuweze kufua umeme kutoka Rusumo ili watu wa Mrusagamba na maeneo mengine waweze kupata umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo Ngara wao wanategemea kwamba kama Serikali itaweza kuwapatia fedha katika bajeti hii ili waweze kufunga mitambo mikubwa miwili na kwa kupitia mitambo hii basi upatikanaji wa umeme unaweza ukaongezeka kutoka *megawatt* 1-3.5 na kunahitajitaka kufungwa *substation* moja ili sasa umeme uweze kusambaa kuelekea Lulenge, Mabawe na Mrusagamba. Sasa naiuliza Serikali, je, imetenga fedha kwa ajili ya Wilaya hiyo ili kusudi waweze kusambaza umeme katika hizo sehemu nilizozitaja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kagera hatuna maeneo mengi yenye madini, lakini yaligundulika madini ya *Nickel* pale Kabanga na mradi huu mwanzoni watu walionekana kuuchangamkia sana hata *Environmental Impact Assessment* ikafanyika baada ya hapo tunaona kimya. Lakini tunajua kwamba kwa kupitia mradi huu, Halmashauri kama wangeweza ku-*take off* wakaanza kuchimba hayo madini na Halmashauri ingeweza kupata mapato kama mrahaba na kwa hiyo ingekuwa ni *source* ya mapato kwa ajili ya Halmashauri lakini vilevile wakazi wa pale wangeweza kupata ajira za kutosha, lakini siyo hilo tu na wakazi wapale wangeweza kupata soko la ndani la kuuza bidhaa zao. Sasa tunauliza mko katika *stage* gani maana tunaona ni kimya na mradi huu ni lini utaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa sababu tangu muingie kwenye Wizara hii mambo yamechangamka na tunaona mambo yanakwenda kwa kasi sana. Pia ni mategemeo yangu kwamba kwenye Majimbo yenu

wanaona kazi mnazofanya, watawapima kwa kazi mnazofanya ili waweze kuwarudisha kwenye Bunge lijalo ili kusudi muendelee kuchochea maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na sasa namwita Mheshimiwa Mgana I. Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima J. Mdee na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara ya Nishati na Madini. Mimi nitajikita zaidi kwenye umeme na muda ukiniruhusu, nitachangia pia kwenye mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba kwa kweli Jimbo la Iramba Mashariki katika kipindi hiki cha miaka mitano, tumepata kutoka kwa Mungu, Wilaya, Halmashauri, daraja na umeme kwenye maeneo mengi ambayo nitayazungumzia. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii moja kwa moja kuunga mkono hoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dr. Jakaya M. Kikwete, kwa uongozi wake bora na kwa kuwezesha Iramba Mashariki ambapo tumeomba Wilaya kwa miaka 37 safari hii tumepata. Kwa hiyo, wale mavuvuzela wanaozungukazunguka huko walie tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeze sana Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wote wa Mashirika yanayofanya kazi na Wizara hii pamoja na Watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninavyozungumza *transformer* ya umeme katika Kijiji cha Singa, wanamalizia kuifunga na nguzo ambazo zilikuwa zinaleta matatizo, zimeshakwenda Singa na Tumuri, kwa hiyo, kwa kweli kazi ya uhakika imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wananchi wa maeneo ya Msingi na Gumanga watapata umeme kutoka njia kuu iliyoko Kinampanda na hivi juzi tuliamua kwa kauli moja kuwa Makao Makuu ya Wilaya yawe Nduguti na Mheshimiwa Rais amesema umeme uende kwenye Wilaya mpya 18 haraka iwezekanavyo. Kwa kweli nampongeza sana na ninampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi za uhakika wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameniahidi kwamba umeme utakwenda katika Shule ya Sekondari ya Iguguno ambayo ni kilomita mbili, Shule ya Tumuli robo kilomita na umeme ukienda Gumanga utakwenda Gumanga Sekondari kwa wakati muafaka. Vilevile naipongeza sana Serikali kwa sababu imeahidi kupeleka umeme Ibaga na maeneo mengine ya Iramba Mashariki. Mimi sina la kulaumu ni kuwapongeza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishaahidi kuleta kampuni za kutafuta umeme wa upepo Iramba Mashariki kwenye Vijiji vya Kikonda, Singa, Nkalakala, Mwanga, Mwangeza, Kinyambuli, Matongo, Milade, Tumuli na vijiji vinginevyo. Tunaomba kazi hii kwa kweli iharakishwe kwa sababu sisi tuna upepo wa uhakika ambao unaweza kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mradi wa umeme kutoka Mtinko kwenda Nkungi na hatimaye Ilunda na Iyambi na ufike hadi Nduguti. Mimi nina uhakika kabisa kwamba baada ya kupata Wilaya na Rais kuagiza kwamba Vijiji hivi vipate umeme, vilevile Shirika la Umeme lilishapima Kijiji cha Kinyangiri, kwa hiyo, tunaomba umeme uende kama ulivyopangwa. Kwa kweli wananchi wa Wilaya mpya ya Mkalama wamejiandaa kupokea umeme kwa sababu wameshaanza kujenga nyumba nyingi za kisasa, kwa sababu umeme unaogopa kuingia kwenye nyumba za tembe. Lakini pia ukija Wilaya ya Mkalama tumejiandaa ipasavyo na vijana wako tayari kuupokea umeme kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Kwa kasi hii mnayokwenda nayo, mimi nina uhakika mtarudi. Kwa kasi hii mnayokwenda nayo na Mashirika kwa mfano Shirika la Umeme na Shirika linalosambaza Umeme Vijijini, nina uhakika wataendeleza kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya. Wilaya ya Mkalama tukipata umeme na kwa sababu sisi ni wakulima na wafanyabiashara wazuri, tutaanza kusindika mafuta ya Alizeti, Katamu na mazao mengi hukohuko kwenye Vijiji vyetu. Nalishukuru sana Shirika hili kwa sababu wanajituma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nimpongeze sana *Regional Manager,* Ndugu Mbonela, *Engineer* Katula na Watumishi wote wa Ofisi ya Mkoa na Wilaya ya Iramba, kwa kweli wanafanya kazi nzuri pale ambapo wanashindwa wanasema ukweli. Tatizo kubwa tulilonalo, ni la nguzo na gharama ya kuingiza umeme kwenye nyumba zetu. Sisi tunaomba Serikali itafute njia nyingine kwani wananchi wetu hawawezi kulipia nguzo kwa mara moja, ni afadhali hizo gharama za kuingiza umeme ziwe zinakatwa kidogo kidogo kwenye bili ya kila mwezi mpaka hapo mwananchi atakapomaliza kulipia hizo nguzo. Nina imani Serikali yetu ni sikivu na nina imani huu mpango utaingizwa kwenye mipango yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kwamba sasa hivi umefika wakati hizi Luku ziende mpaka Vijijini ili wananchi wetu watumie umeme ule ambao wanaweza kuulipia. Kwa kweli hii itaondoa adha ya wananchi kuichukia Serikali yao na hasa Shirika la Umeme. Kwa hiyo, mimi ninashauri hayo yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuchanganya mafuta, wajumbe wenzangu wameshazungumza hapa Bungeni, kwamba itafutwe njia ya kutatua tatizo hili kwa sababu kuweka rangi haitasaidia, Watanzania ni wajanja, watachukua hata rangi za mikeka, watachanganya na mambo yatajipa. Kwa hiyo, itafutwe njia ambayo italeta suluhu ambayo haitaumiza mwananchi wala mitambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgana I. Msindai, sasa namwita Mheshimiwa Halima J. Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka na muda ukituruhusu Mheshimiwa Godfrey W. Zambi ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Vilevile nawapongeza Mawaziri hawa ambao ni vijana kwa kazi wanayoifanya, ni rafiki zangu na kwa kweli wameonyesha utendaji kazi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijaanza kuchangia, nianze kwa kutoa ombi ambalo nilishalitoa, la umeme katika Kijiji cha Chasimba ambacho kiko katika Kata ya Bunju, Jimbo la Kawe. Kijiji hiki licha ya kwamba kiko mjini na kwenye Jimbo la vigogo lakini ni aibu mpaka sasa hivi hakina umeme. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri katika Fungu lake hilo, kile Kijiji chenye watu 7,000 ambao wanaweza wakawa wateja wazuri sana wa *TANESCO*, akififikirie kwa kuwapelekea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Mchango wa kwanza, Waheshimiwa wamekuwa wakipongeza sana mafanikio na mimi kama nilivyosema, ninawapongeza kwa sababu ni vijana, mmefanya kazi katika mazingira magumu sana lakini kwa mtazamo wangu, mafanikio yote lazima yaendane na fedha. Ninasema hivyo kwa sababu kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo hazitolewi, ama ziko kiduchu sana, sidhani kama haya mafanikio tunayozungumza hapa ni ya kweli, inawezekana tukawa tunazungumza mafanikio ya kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninalisema hilo? Nina Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, ya mwaka 2009 na ninalizungumza hili kwa madhumuni ya kuwasaidia Ngeleja na Malima hapa, kwa sababu Wizara ya Fedha inawaonea. Wanatengewa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo, fedha hazitolewi, tunakuja tunaambiwa hapa kwamba kuna mafanikio. Sasa kama kuna vyanzo vingine vya fedha ambavyo sisi hatuvijui inabidi mtueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 58, Mkaguzi Mkuu wa Serikali, anasema kabisa kuanzia mwaka 2006 mpaka 2009, Wizara ya Nishati na Madini, imeonesha utekelezaji usioridhisha kutokana na ufinyu wa bajeti ya maendeleo. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumza vyema kabisa kuhusiana na bajeti ya matumizi ya kawaida. Mnatumia mnachopata, mnaongeza na zaidi lakini ukija kwenye bajeti ya maendeleo mwaka 2006/2007, Bunge letu liliidhinisha shilingi bilioni 229, kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 33. Tunazungumzia miradi ya maendeleo, hatuzungumzii pesa za semina, mishahara na mambo mengine ambayo hayamhusu Mtanzania maskini na wa kawaida ambaye miradi ya maendeleo kwake ndiyo *issue*, hivi vitu vingine kwake siyo *issue*, mwaka 2006/2007 ni asilimia 14 ya fedha tulizoidhisha hapa ndio zimetoka. Ukija mwaka 2008, kwa makeke kabisa bajeti imeongezeka na kujigamba kwamba umeme utakwenda kwa wingi vijijini, tulitenga shilingi bilioni 312, kiasi

kilichoidhinishwa kilikuwa shilingi bilioni 28 asilimia tisa tu ya fedha ya maendeleo. Sasa huu umeme mnaotuambia umeenda vijijini umekwenda kwa fedha ipi na kwa mipango ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 kiasi tulichoidhinishwa kilipungua kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita, shilingi bilioni 243, Wizara ya Fedha ikawapatia Fungu lenu la shilingi bilioni 45, asilimia 19 ya bajeti nzima ya maendeleo. Leo tunasema haya mambo, akina mama Mongella wanatutukana matusi ya nguoni tu hapa. Lazima tuseme ukweli tuwasaidie vijana wetu waweze kufanya kazi vizuri. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, shughuli za kupeleka umeme vijijini lazima ziende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mkaguzi hapa ameanisha miradi. Kuna miradi mikubwa zaidi ya 20 ambayo haijatekelezwa, tukisema tunaitwa wake wenza, tutakuwa wake wenza kweli kweli hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi imeshindwa kuendelea zaidi ya 20. Miradi mikubwa na mingine mnairudia kila siku kwenye hotuba zenu hapa, kumbe inashindwa kutekelezeka kwa sababu hamna fedha, sasa na nyie sijui kwa sababu ya uoga wenu hamsemi, mnabakia kusifiasifia tu hapa. Hilo la kwanza nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kutokana na ile Sheria ya Madini, Sura Na. 123, ambapo kuna leseni ziligawiwa kwa wachimbaji wadogo wadogo katika eneo la Winza, Mpwapwa kwa Mzee Lubeleje pale. Tunaomba hili ulifuatilie. Inasemekana hawa vijana wetu maskini ambao wamepewa hizi leseni wanashindwa kuanza kuchimba kwa sababu kuna wavamiaji haramu na inasemekana kati ya hawa wavamiaji haramu ni uongozi wa Wilaya. Viongozi wa Serikali ambao tunatarajia watakuwa watetezi wa wale wachimbaji wadogo wadogo maskini, ndiyo wanaowaua. Tuna barua hapa kwenda kwa Mkuu wa Mkoa, sitaki kusema imetoka wapi, nitakupatia, lakini ujue inatoka Wizarani kwako. Kwa hiyo, Sheria tumepitisha ikiwa na dhamira njema, lakini kuna wapuuzipuuzi huko Wilayani wanawanyima haki Watanzania maskini. Mheshimiwa Waziri, nitampatia hili. Mheshimiwa Lubeleje analijua hili kwa kina kwa sababu yeye alikuwa ni sehemu ya ile Kamati ya watu ambao walitengeneza leseni. Sasa ninaamini kwamba Mheshimiwa Lubeleje akiwa yeye ni mdau kule atakusaidia ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata leseni zao na waweze kuanza kuchimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa, ninaamini muda utaniruhusu, kuna wafanyakazi 700 walipunguzwa kutoka kwenye Kampuni ya Williamson Diamonds mwaka 1993. Mheshimiwa Waziri, hawa wafanyakazi wanadai mafao yao. Kuna siasa zinapigwapigwa hapa katikati, wakakutanishwa na Kamati ya Madini, wakakutanishwa na Waziri wa Kazi, wakasikilizwa, wakatolewa nje, wakaambiwa nyie mmelipwa kila kitu wakati mtu aliyefanyakazi miaka 32 amelipwa shilingi 900,000/=. Mheshimiwa Waziri, suala hili naomba ulifuatilie. Mimi siamini kama watu wazima na akili zao watakuwa kila siku wanarudia kulalamika kwamba wameonewa na wameibiwa. Naomba ulifuatilie, ndugu zetu hawa maskini 700 zaidi ya miaka 15 wamekuwa wakitafuta haki

yao. Sasa ninaamini wakati huu utawala wenu ukimalizika kabla ile awamu nyingine haijaingia ambayo haijulikani ni ya nani, mtekeleze huu wajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru. Naomba Kijiji cha Chasimba, Kata ya Bunju, Jimbo la Kawe kipatiwe umeme. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mwongozo wa Spika. Kanuni ya 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati msemaji aliyemaliza kuzungumza sasa hivi akichangia hoja hii, amesema humu ndani kuna wake wenza wenzake. Nilitaka tu labda afafanue ni nani ambaye ni mke mwenzake humu ndani, ili tuweze kujua. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hilo wala sitalipa Mwongozo. Tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii, kuchangia Wizara ya vijana wenzangu, inayoongozwa na Mheshimiwa Ngeleja na mdogo wangu Adam Malima. Ninawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya na mimi nasema kwa sehemu kubwa kwa kweli ninaungana nao isipokuwa sehemu moja ambayo baadaye nitawaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninakutakia kila la kheri katika uchaguzi unaokuja ili urudi tena na uendelee kubaki kwenye Kiti chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sipo kidogo, nilikuwa Jimboni na nitamke hili kwa dakika moja tu kwa kutoa ushauri wa bure kwa Wabunge wenzangu na hasa wa Chama changu kutokana na mchezo mchafu wa kadi feki zilizoanza kutengenezwa na kuelekezwa katika baadhi ya Majimbo likiwemo Jimbo langu. Mnione tu kwa wakati wenu ili niweze kuwaonesha kadi hizi zinazofanana na za CCM, zilizoanza kugawanywa na kuingizwa kwenye daftari la wapigakura kwa nia ya kuhujumu demokrasia ndani ya Chama chetu na bahati mbaya sana baada ya kuuliza naambiwa hata wale wenzangu wanaopiga kelele dhidi ya ufisadi, nao huko wanashughulikiwa na kadi hizo feki. Lakini nasema Mbuyu, Mgunga, hauangushwi kwa kisu cha kukatia nyanya jikoni, kwa hiyo, wanapoteza muda wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kushukuru Serikali ya Chama changu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuwasha umeme Makao Makuu ya Wilaya Simanjiro, Orkesumet**.** Hii tena si hadithi, kazi imekamilika, tumewasha umeme Orkesumet, tumewasha umeme Gange B, bado Gange A, tumewasha Umeme Loiborsoit,

nimefarijika kabisa kuona kwamba kwenye kauli ya Waziri sasa tuna uhakika wa kuwasha umeme katika vijiji vya Msitu wa Tembo kupitia Kijiji cha Kiruani kuelekea Magadini na hatua ya pili imani yangu tunaelekea Ngorika A na C na baadaye Elimkuna. Imani yangu pia ni kwamba ombi la siku nyingi la wananchi wa Kata ya Oljoro na Kata ya Terrat na Kata Komolo na kuvuta umeme kutoka Oljoro JKT nalo sasa lifikiriwe katika bajeti ijayo na kupangiwa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kama faraja kwa wananchi wa Jimbo langu na hata wale wanaotumwatumwa pale, wanaokuja na kadi feki, hata wao baadhi ya nyumba zao zimewekewa umeme. Wale ambao hawana nyumba, natarajia wakimalizia nao tutawavutia hapo hapo maana viwanja viko Orkesumet.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuzungumzia nafasi ya madini, nikianza tena kushukuru Serikali na Bunge kwa kubadilisha Sheria iliyokuwa Sheria ya Madini, ambayo imeweka kifungu kinachohakikisha kwamba madini ya vito yanabaki kwa ajili ya Watanzania. Nimesomasoma kwenye baadhi ya magazeti, kwenye mitandao, kuna baadhi ya watu wanajifariji na kujidanganya kwamba wao sheria hii haiwahusu, sijui kiburi hiki wanakipata wapi, lakini nadhani hapa wanajidanya na pengine kuwadanganya wabia wao, wanalazimika kufuata sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria tunazozitunga hatutungi kwa ajili ya weusi peke yao, tunatunga hata kwa ajili ya weupe na hata wangekuwa wa kijani sheria hii bado inawahusu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafarijika pia na suala la kuzuia uuzwaji wa Tanzanite ghafi nje, lakini bado nasema kuna haja ya kwenda mbele zaidi kuhakikisha kwamba madini yote ya vito yanaongezewa thamani hapa nchini ili kuweza kutoa ajira kwa Watanzania na kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu ambayo sitaki nipoteze muda mrefu bila kutofautiana na rafiki yangu na mdogo wangu Waziri wa Nishati na Madini, kwenye ukurasa wa 38 wa hotuba. Mheshimiwa Waziri anasema naomba kunukuu:-

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia malalamiko ya wafanyakazi wa mgodi wa Tanzanite One, Serikali iliunda Kamati ya Wataalam kwa ajili ya kuchunguza malalamiko yao, kuhusu madhara wanayodai kupata kutokana na kupitishwa kwenye mashine ya mionzi ya X-Ray Body Scanners ambazo zimefungwa katika migodi. Uchunguzi wa kitaalam umethibitisha kuwa hakuna madhara yanayotokana na mionzi ya mashine hiyo”*. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri ajipe muda wa kusoma taarifa zote mbili, taarifa ile ya Kamati nyingine ya Wataalam wa Wizara na taarifa ile ya watu wa mionzi, maana angeendelea mbele zaidi, angefika mahali pa kueleza kwamba, wataalam wake wamefika hatua ya kushauri kwamba sasa *X-Ray Body Scanners* zinazotumika na *Tanzanite One* kuwa-*scan* Watanzania wanaofanya kazi katika mgodi huo, zinafanana kwa mujibu wa ripoti na zile zinazotumika ku-*scan* mizigo katika viwanja vya ndege kama *Kilimanjaro International Airport.* Wataalam walioweka mahali

pa kupitisha mizigo na mahali pa kupitisha binadamu, hawakukosea lakini leo *scanner* inayotumika kuwa-*scan* Watanzania kwa kile kinachoonekana kama ni udhibiti wa madini katika kiwanda na katika machimbo ya *Tanzanite One*, ni *X-Ray Body Scanner* inayofanana na ile ya kukagua mizigo. Nataka niwaambie, wana Simanjiro sio mizigo, hawastahili kuonewa kwa kiasi hicho na bado naliomba Bunge lako Tukufu liendelee kumshauri Waziri asichukulie mstari mmoja ulioko kwenye ripoti hiyo na kuwa mwanya wa kurudisha *scanners* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Waziri ni Mwanasheria, anaelewa, hivi unapokuwa wewe ni mtuhumiwa halafu inaundwa Tume wewe unakuwa ni sehemu ya wanaokwenda kujichunguza kwa sababu Mamlaka iliyotoa leseni ya *scanners* hizo, miongoni mwa watumishi wa Taasisi hiyo ndiyo ambao wako kwenye Tume kwa sehemu kubwa inayokwenda kujichunguza. Wafanyakazi wa *Tanzanite One,* nao ni sehemu ya Kamati iliyoundwa eti kwenda kuichunguza *Tanzanite One,* matokeo yake hatimaye ripoti ile badala ya kuja kwenye Kamati yako ya Nishati na Madini iliyokuja kulalamikiwa, badala ya kwenda kwa Waziri na ikaendelea kuwa siri mpaka itakapowasilishwa Bungeni, inapelekwa kwa Mkurugenzi wa *Tanzanite One,* kana kwamba Watanzania na Tume iliyoundwa na Serikali ni vibarua na vibaraka wa kampuni ya *Tanzanite One.* Ninataka Serikali iitupilie mbali ripoti hiyo ambayo waliokwenda kuiandaa ni watu wenye maslahi, maana watu wa Tume ya Mionzi wana maslahi maana wao ni watuhumiwa na wafanyakazi wa *Tanzanite One,* wao wana maslahi na kwa kweli mnajua anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua wimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa wanakwenda huko, ni haki gani wanyonge hawa wanapata? Ninaitaka Serikali itoe kauli juu ya mionzi hiyo wanayopigwa Watanzania, ripoti ya Kamati yetu bado haijawasilishwa Bungeni, lakini nenda ZAIN ambaye ni Mkurugenzi wa *Tanzanite One* anayo ripoti na ndiyo imetawanywa pale na ameanza kuitekeleza hadi wafanyakazi wa *Tanzanite One* wakagoma na hatimaye akawatukana na akafunguliwa kesi iliyoko Mahakamani Babati. Sitaki kuingia kwenye habari ya kesi, ninachotaka kusema ni kwamba, hatuwezi kuandaliwa ripoti na watuhumiwa. *Tanzanite One* ni watuhumiwa, watu wa mionzi ndiyo wanaotoa leseni ni watuhumiwa, Waziri ambaye ni Mwanasheria, tupilia mbali ripoti hiyo na hata wao wenyewe wamefika mahali pa kuona haya wakasema, *Tanzanite One* watafute njia mbadala kwa ajili ya kudhibiti madini yao. Wamedanganya kwamba Afrika Kusini kuna migodi inafanya hivyo, Australia, Canada, wameambiwa wathibitishe wameshindwa. Hakuna sehemu nyingine duniani mpaka sasa. Tume zako zimeshindwa kuthibitisha ambako binadamu wanakuwa *scanned na X-Ray Body Scanners*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema siungi mkono hoja mpaka nipate maelezo hayo. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya bajeti kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wao wote, kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara yao. Lakini pamoja na pongezi na kazi nzuri wanazofanya, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umeingia Mbozi mwaka 1994, lakini Wilaya ya Mbozi yenye karibu Vijiji 200, ni vijiji si zaidi ya 20 ambavyo vina umeme. Kwa hiyo, unaweza ukaona pamoja na kwamba, ni muda mrefu kidogo tumepata umeme lakini kasi ya usambazaji ya umeme katika Wilaya yote ya Mbozi ni ndogo sana. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, kuna vijiji ambavyo vimepitiwa na *line* au gridi ya Taifa tangu mwaka 1994 mpaka leo havina umeme na wananchi hawa wameendelea kunisumbua mpaka leo. Leo naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Dr. Mwakahesya, Mkurugenzi Mkuu wa *REA*, amekuja Mbozi, tumezungumza juu ya vijiji hivi, wanasema kuna mpango lakini naomba Mheshimiwa Waziri, anihakikishie. Kuna vijiji vya Nanyala, Senjele, Ivwanga, ambavyo viko Mlowo na Kijiji cha Songwe, viko karibu na hiyo *line* ya umeme. Pia shule za Sekondari za Myovizi, Isangu, Ihanda, Mlowo, Nalyelye, Igamba na Idimi. Hizi shule ziko jirani sana si zaidi ya kilomita moja kutoka kwenye *line* ya umeme, lakini umeme unapita juu, wanafunzi wanapata tabu, hakuna umeme, kuna tatizo gani maana nasikia wenzangu hapa kuna maeneo mengi tu ambayo transfoma zinawekwa kwa ajili ya kushusha umeme kulikoni kwenye vijiji hivi ambavyo tumekuwa kila mwaka, nadhani karibu miaka mitatu sasa, tunatenga pesa ya kununua transfoma mpaka leo hakuna kilichofanyika? Hebu naomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu natamka hapa wananchi wa Vijiji hivi wananisikia, nilipokuwa Jimboni kabla sijaja Bungeni wamenifuata na mimi nikasema Serikali ina mpango, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze mipango hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna miradi ya umeme ya zamani sana katika Wilaya ya Mbozi, Mheshimiwa Waziri anaijua na bahati nzuri alipokuwa anatoa taarifa ya Serikali hapa aliitaja.

Lakini napenda nimshukuru Dr. Mwakahesya alikuja Mbozi tukazunguka baadhi ya maeneo ya miradi hiyo, lakini kuna sehemu ya mradi wa Vwava/Hasamba siioni kwenye taarifa yoyote. Nimezungumza nao wanasema kwamba wataangalia namna ya mradi huu utakavyotekelezwa, kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri *seriously,* mradi huu wa Vwawa/Hasamba uwepo kwenye orodha ya ardhi ile mitatu vinginevyo Mheshimiwa Waziri labda tuombe tusirudi hapa Bungeni, maana tukirudi hatutaweza kuelewena tena kipindi kingine na mimi nina hakika wananchi wa Mbozi watanirudisha kwa sababu wanajua kazi ninayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie umeme unaokwenda Itaka. Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini ni shahidi alikuja na Mheshimiwa Rais mwaka jana Wilayani Mbozi na Mheshimiwa Rais alimsimamisha yeye mwenyewe akasema zungumza kuhusu umeme wa hapa, waliahidi kwamba tunaleta umeme Mbozi lakini kwenye Bajeti hii naona iko kimya. Sasa wananchi wa vijiji vya

Itepula, Shasya, Msanyila, Lwati, Halungu, Itewe, Itaka yenyewe na Nambinzo wanasubiri umeme huu unakwenda lini. Maana hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na mimi sidhani kama Rais, anasimama mbele ya watu anawaeleza kitu ambacho hakiwezi kutekelezwa. Lakini inapokuwa na Waziri mwenyewe yupo na Mheshimiwa Waziri amenisimamisha mimi tena akanisifu sana Mheshimiwa Waziri kwamba Zambi ni mchezaji mzuri, ni beki mwenzangu, sasa kama tunasifiana hivyo halafu mambo haya hayaendi vizuri hatuwezi kwenda namna hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hili la umeme ulifanyie kazi (umeme wa Itaka na Nambinzo na maeneo mengine) kwenda mpaka kule Kamsamba. Ni vizuri tukasikia kauli vinginevyo tutaanza kusimama kwenye vifungu tukaanza kuulizana, haitapendeza sana hasa pale jambo ambalo mlikuwa mmeahidi ninyi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la makaa ya mawe kule Magamba, Mbozi kumegunduliwa makaa ya mawe, kijiji cha Magamba kata ya Isansa katika tarafa ya Igamba. Tangu mradi wa makaa ya mawe ule umegunduliwa nadhani ni zaidi ya miaka saba sasa. Wapo watu ambao wanasema wanafanya utafiti pale, wanachukua tani na tani za makaa ya mawe wanasema kwamba wanakwenda kuyafanyia utafiti. Miaka karibu saba sasa na wale wachimbaji pale bahati mbaya ni wabaguzi kweli kweli, wananchi wa Kijiji cha Magamba na maeneo jirani wanalalamika hawaoni faida ya kuwa na watu ambao wanatafiti halafu wenyewe ni wabaguzi sana.

Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie *status* au hali halisi ya makaa ya mawe ya Magamba ikoje? Maana wananchi walinituma kwamba nije niwaulizie *status* ikoje. Kingine naomba pia Mheshimiwa Waziri atueleze kuna mkanganyiko, mradi ule upo Chunya au Mbozi? Pamoja na kwamba eneo ambalo wameanza kuchimba ni eneo la Mbozi, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la wenzangu wamezungumzia mafuta. Kuna mawazo hapa kwamba ili kuzuia uchakachuaji wa mafuta, kwa sababu kengele imelia basi niseme naunga mkono hoja lakini bei ya mafuta ya taa isipande. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tuna dakika tano tu kwa ajili ya mchangiaji anayefuata na nisingependa nimpe muda mfupi tu Mheshimiwa huyu ambaye angechangia lakini kuna Mheshimiwa yeye amesisitiza atazitumia hizo hizo tano, sasa nitampa huyo ili amalizie kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri na mtoa hoja waweze kuhitimisha hoja yao. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ili atumie dakika tano tu. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja hii kwanza na baada ya kuunga mkono, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili, hoja ya kwanza ni namna ya kutekeleza miradi ya umeme vijijini ambayo imechukua muda mrefu sana. Ninachoomba

na nakuomba Mheshimiwa Waziri unapohitimisha hapa utoe matamko yanayoeleweka kwa sababu miradi hii imekuwa ni ya siku nyingi sana na sasa inaanza kuwa ni kero kwa wananchi. Kwa mfano, umeme wa kutoka Lamadi, Kalemela, Nyamikoma, Nyakaboja mpaka Nyashimo nina miaka mitano humu Bungeni kila siku nauzungumzia na Serikali inaahidi na nauliza maswali kila wakati lakini sijapata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naambiwa makaratasi na kwenye mpango imo, sasa nataka kuthibitisha anayosema Waziri kwenye hotuba yake humu ndani kweli inatekelezwa? Lakini pili kuna umeme kwenda *ginnery* ya Ngasamo, hiki ni kinu cha kuchambua pamba ni rasilimali kubwa sana kwa uchumi wa eneo husika na kwa nchi hii, hivyo hatuoni kwamba kuchelewa kupeleka umeme haraka Ngasamo ni kuwanyima wananchi huduma hii lakini pili ni kurudisha nyuma uchumi wa nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima na hasa msukuma analima pamba, anashindwa kusindika pamba yake kwa urahisi zaidi inabidi apeleke mbali. Naomba sana hili Mheshimiwa Waziri aliangalie na alizungumze hapa, naomba kupata jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa sababu muda wangu ni dakika tano tu ni suala la uchakachuaji wa mafuta. Hii tabia ni mbaya na kama hatutaamua hatua za makusudi ni tatizo kwa nchi, tusiangalia pointi ya watu kupandisha bei ya mafuta ya taa peke yake, tuangalie athari kiuchumi. Leo hii magari yanaharibika, *spare* nyingi zinahitajika na fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya marekebisho yake, lakini kibaya zaidi hawa watu wanakwepa kodi. Leo shilingi bilioni 200 zingekwenda kwenye huduma ya jamii tusingekuwa na shida kwenye Bajeti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachosema naomba Mheshimiwa Waziri awe mkali, *EWURA* fanyeni kazi. Unajua kadri unavyoweka hatua kama hizi unavyobana *EWURA* wenyewe dau lenu linapanda kwa wachakachuaji wa mafuta. Kama mlitaka mpewe shilingi milioni tano mtapewa shilingi milioni 20 kama ganji. Tunaomba hii tabia ife na naomba Serikali mchukue hatua bila ya kumwonea mtu haya. Watanzania tufike mahali sasa tuchukue hatua ambazo hatuhitaji kuoneana haya, kwa kweli naomba Wizara hii wachukue hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba tuache kupangapanga, tutekeleze sasa. Wakati wa kupangapanga, wa kusema tuko mbioni, tunaweka mikakati, tunachakachua, tunafanyaje, imeshapitwa na wakati. Sasa Serikali mjipange kufanya kazi kwa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Kilolo, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri – Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu na

Wakurugenzi kwa hotuba nzuri sana na yenye malengo sahihi hasa kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo hadi Kidabaga bila kushusha kwenye vijiji ambapo umeme huo umepita. Je, ni lini umeme huo utashushwa kwenye Shule ya Sekondari Udzungwa, Vijiji vya Ilamba, Lulanzi, Utengule, Lukanina na Ihimbo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Wizara ilipima njia ya umeme kwenda Vijiji vya Irole na Imalutwa na pia kutoka Ihila, Masukanzi, Kitonga, Mahenge, Mtandika na Ruaha – Mbuyuni. Je, upelekaji wa umeme huo utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara kila kheri katika utekelezaji wa majukumu yake.

**MHE. FATMA A. FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la bei ya umeme – Zanzibar, tunashukuru kwa jitihada za Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya *Norway* kwa kuweza kuhakikisha mradi wa kupeleka umeme Pemba kutoka Tanga umekamilika. Hatua hii ni ya kutia moyo sana, lakini kuna masikitiko makubwa kuhusiana na bei hiyo ya umeme, ambapo *TANESCO* inaipelekea ankara kubwa *ZECO*, ambayo huzidi kuongezeka kila kukicha kutoka asilimia 21, kwenda asilimia 168 na hivi karibuni imeongezeka tena hadi kufikia asilimia 202. Hali hiyo inaleta ugumu sana kwa watumiaji umeme huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi ilifanya safari kwa makusudi kwenda Dar es Salaam kwa madhumuni ya kuonana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, lakini la kusikitisha, Waziri huyo hakuweza kuonana na Kamati hiyo kwa sababu ambazo Wizara hiyo inazijua yenyewe. Je, hiyo haikuwa ni kukidhalau chombo cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambacho ndicho chenye jukumu la kusimamia maslahi na kero za Wazanzibari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri alieleze Bunge hili ni kwa nini hakuweza kuonana na Kamati hiyo? Kama wakati huo hakuwa na nafasi, kwa nini asiiandikie Kamati hiyo kueleza wakati muafaka wa kuonana nao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo la 0.3% ambayo inaingizwa kwenye ankara zinazopellekwa *ZECO* inayohusiana na kufidia Wakala wa Nishati Vijijini Tanzania Bara, haikubaliki kabisa na tunaomba itolewe.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam A. Kighoma Malima, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara hii na taasisi zake kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa mafanikio makubwa katika kuendeleza na kutekeleza miradi ya umeme, gesi na madini. Ninatoa pongezi na shukrani, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mkinga kwa kuwekewa umeme Makao Makuu ya Wilaya – Kasera pamoja na Vijiji vya karibu vya Mkinga Leo, Mwakiponda, Menjamwenye, Golasingo na Karozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tuna masikitiko makubwa sana kwa kuwa ahadi za siku nyingi za kuviwekea umeme Vijiji vya Kwale, Daluni, Gombero, Unga na Boma imekuwa ikisuasua. Awali uwekaji umeme kwa vijiji hivi ulikuwa chini ya MCC. Miaka miwili iliyopita miradi hii imehamishiwa *REA* na *REA* pamoja na Wizara zimekuwa zikionesha vijiji hivyo kuwa katika mpango wa umeme vijijini. Ni jambo la ajabu sana kwamba katika hotuba ya Waziri, Vijiji vitakavyowekewa umeme Mkoani Tanga ni vile vya Wilaya ya Handeni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mheshimiwa Waziri kutoa kauli kwamba Wizara bado itajielekeza kwenye uwekaji umeme wa vijiji hata vile ambavyo havikutajwa, naona kauli hiyo haina uzito kwani hata ahadi ambazo zilikuwa zimeandikwa kwenye vitabu na kutengewa mafungu hazikutekelezwa, sembuse hii ahadi ya mdomo tu! Naunga mkono hoja kwa matumaini kwamba ahadi aliyotoa Mheshimiwa Waziri kuhusu umeme vijijini itatekelezwa na kwamba Vijiji vya Kwale, Gombero, Daluni na Vuga na Boma vitawekewa umeme, kama ambavyo Serikali imeahidi zaidi ya miaka minane sasa.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa sana zinachukuliwa na Wizara hii ya Nishati na Madini kuona kwamba umeme unapatikana katika kila kona ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria iliyopitishwa na *Bunge Electricity Act, 2008* inatoa fursa kwa sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini. Lakini Kifungu cha 41(7) cha Sheria hiyo imekuwa ni kikwazo kwa wazalishaji binafsi wa umeme. Kikwazo hicho pia kimeathiri sana kwa Kampuni ya Atumas kupata leseni ya kuzalisha na kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, hali inayopelekea wasiwasi kwa mikoa hiyo kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuangalia vifungu vya Sheria ambavyo vinaonekana ni kikwazo kwa sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji na usambazaji wa umeme nchini. Kadhalika kila kifungu cha sheria kinachozuia *EWURA* kutoa leseni kwa ajili ya shughuli ya uzalishaji umeme nchini kwa kipindi cha miaka miatano kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vyote hivi ni lazima vifutwe kabisa na kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kabla ya Bunge hili kumalizika ilete sheria hizo hapa Bungeni tuzifanyie marekebisho ili Serikali itoe ruhusa kwa *EWURA* kutoa leseni kwa sekta binafsi kuzalisha na kusambaza umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atupe ufafanuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nchi imekumbwa na aibu ya uuzaji wa mafuta yaliyochakachuliwa. Aibu hii imeonekana kuwa nzito zaidi pale yalipohusika magari ya Ikulu. Ni dhahiri kwamba biashara hii imekuwepo kwa muda mrefu hapa nchini. Utashangaa sana katika kipindi kifupi cha hivi karibuni kumejitokeza ujenzi uliokithiri wa vituo vya kuuzia mafuta na hasa katika barabara ya Dar es Salaam – Morogoro. La ajabu zaidi vituo vya nje ya miji vinauza mafuta kwa bei ndogo zaidi ukilinganisha na vituo vilivyoko mjini. Hali hii inatia wasi wasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ifanye utafiti wa kina kuona kwamba ujenzi wa vituo vya mafuta uliokithiri na kushuka kwa bei za mafuta isivyo kawaida kwa vituo vya pembenii mwa miji iwapo una-*direct relationship* na biashara ya uchakachuaji mafuta na kuwauzia wananchi mafuta hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatimaye hatua madhubuti zaidi zichukuliwe kuhakikisha kwamba aibu hii inaondoka hapa nchini. Kwani hakuna asiyejua hapa nchini athari ya mafuta yaliyochakachuliwa kwa uchumi wa nchi, kwa mazingira na afya za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote kwa juhudi ambazo wanachukua katika Wizara hii.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yao yaliyoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, nina mchango mdogo ambao ningependa nipatiwe maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza na ya muhimu ni tatizo kubwa la ukosefu wa umeme katika Kijiji cha Chasimba Kata ya Bunju – Boko katika Jimbo la Kawe. Kijiji hiki kinatambulika kisheria na kilipata usajili mwaka 1975, kimepakana na Kiwanda cha Saruji cha *Twiga Cement* ambacho kina umeme wa kutosha. Hali kadhalika maeneo mengine ya pembezoni mwa kijiji hicho (chenye wakazi zaidi ya 7,000) yanapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakipeleka maombi *TANESCO*, Kinondoni *North Branch* pasipo mafanikio kupitia kampuni yenye dhamana ya kusimamia upatikanaji wa umeme eneo hilo *(Electrical Contrator) RED FAM GEN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya nini kikwazo katika kupeleka umeme eneo ambalo liko mjini karibu kabisa na vyanzo mbalimbali vya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni la madai ya wafanyakazi 700 waliopunguzwa kutoka Kampuni ya *Wiliamson Diamond* mwaka 1993. Tatizo hili limekuwa la muda mrefu sana. Ni muhimu Wizara ikalifuatilia kwa karibu sana hasa ukizingatia kwamba kulikuwa na ukiukwaji mkubwa sana wa Sheria na uonevu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa ni mafungu yanayotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali zinaonesha kwamba ni kiasi kikubwa sana kinachotolewa dhidi ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwailisha.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi. Katika mradi wa usambazaji umeme Vijijini, ni vijiji vipi vimenufaika na vipi vipo kwenye bajeti hii? Vijiji vya Mkoa wa Kagera vitapatiwa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipeleka ombi langu Wizara, ya Nishati na Madini, nikiomba umeme katika Kijiji cha Lukinde, Kata ya Katoma Bukoba Vijijini. Niliomba *sub-station* ifungwe ili sehemu za Kyambeo, Mahuguru, hadi Kilaini Shule ya Msingi, wapate umeme. Niliahidiwa kuwa nitapata kupitia *REA* lakini hadi leo ni miaka inakaribia miwili sijaona kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anawaeleza nini watu wa Lukinda Katoma? Je, atawapa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake wa kuniwezesha na mimi niweze kushika kalamu na kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuweza kuandaa hotuba hii iliyoko mbele yetu iliyojaa matumaini. Mwenyezi Mungu awajaalieni muweze kutekeleza sio yabakie kwenye vitabu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza sana Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri iliyosaidia yale mapungufu ya Serikali iweze kujirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na kwa umuhimu sana, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Wenyeviti na Watendaji wote kwa jinsi wanavyoliendesha Bunge kwa kiwango kikubwa. Mwenyezi Mungu awasaidie. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa baada ya miaka mingi kisiwa cha Pemba kimeweza kukamilisha ile ndoto ya kupatra umeme wa uhakika na kuweza kujiletea maendeleo wananchi wa Kisiwa hicho. Lakini cha kusikitisha tena sana, ni kwamba umeme huo ni ghali sana kiasi kwamba wananchi wengi watabakia kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wachimbaji wadogo wadogo pamoja na kupitisha sheria hivi karibuni, lakini bado inaonekana kuna malalamiko makubwa ya wachimbaji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wa Mgusu Geita mpaka leo bado hawajaijua hatma yao, na wote ni wananchi wa Tanzania. Waende wakale wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria tumeipitisha kuhusu kukataza kusafirisha madini ya vito ambayo hayajasafishwa.  Je, Serikali imejiandaa vipi kuhusu hali hiyo ambayo wengi wanaofanya kazi hiyo ni wachimbaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, isije ikatokea kama mwaka 2006 tukakataza kutumia mkaa wakati hatujajiandaa na nishati mbadala, tukakamata watu na baadaye sasa makaa yamerudi kama hayajakatazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwawekee mazingira mazuri wachimbaji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe maelezo kuhusu kule Mkoani Mbeya ambapo hivi karibuni tumeona ndani ya Vyombo vya Habari jinsi Wachina wanavyofanya kazi zao za kuchimba madini bila hata kupata ridhaa za wananchi na Serikali za Mitaa. Je, kweli nchi hii iko salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, na kwa umuhimu mkubwa naipongeza Serikali kwa kuwapa adhabu kali wale waliochakachua mafuta Moshi na kuharibu gari za Rais (Msafara wake).

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wale ambao wametutia aibu katika nchi za jirani na wao wapate adhabu kali. Nakushukuru sana.  Ahsante.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana kwa kukubali kuupatia mji mdogo wa Ndala Umeme.  Asanteni na hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizarani kuna pesa shilingi bilioni nne za kuwakopesha wachimbaji wadogo. Je, ni shs. zilishakopeshwa?  Ni namna gani Wizara imewawezesha wachimbaji wadogo kupata mitaji ili wapate vifaa (zana) na kufuata soko

lenye bei nzuri? Nashauri pawe na dawati la kuweka bei elekezi kwa madini ili wachimbaji wasipunjwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandaji wa mara kwa mara wa bei ya umeme unatokana na sababu gani? Haiwezekani ikawekwa *formula* ya kudumu ili panapowekwa bei iwe ya muda mrefu? *STAMICO* ni Shirika ambalo likipewa mtaji na uwezo mkubwa litasaidida sana kuwa mhimili wa Sekta ya Madini nchini. Je, ni kiasi gani cha fedha zimetengwa maalum hasa mwaka 2010/2011?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Nyakato chenye lengo la kuziba pengo la Kampuni ya *DOWANS* ambayo ilianza mwaka 2007 imefikia wapi? Hata hivyo nawatakia heri nyote ili mshinde Mavuvuzela yaliyowakabili majimboni kwenu. *Inshallah*.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja ya Wizara. Awali ya yote napenda kuishukuru Wizara kwa kufungua Ofisi ya Madini Mjini Kigoma. Ufunguzi wa Ofisi hii ambao una takribani miaka mitatu sasa umewezesha kurahisisha watafiti na wachimbaji wadogo wadogo wa madini Mkoani Kigoma kupata ushauri na huduma muhimu katika Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Wizara wakati wa kujibu hoja itoe maelezo ya kina ni kwa muda gani Kampuni inayofanya utafiti wa madini eneo la Kaparaguru itaendelea kuwepo eneo lile? Utafiti huo unaofanyika katikati ya Vijiji vya Lubalisi na Rukoma Jimbo la Kigoma Kusini umeanza tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990. Matokeo ya utafiti huo hayawekwi bayana, wanachokiona wakazi wa eneo linalozunguka eneo la utafiti ni usombaji wa udongo mwingi ambao umekuwa unapelekwa nje ya nchi. Napenda Wizara inieleze: Je, hapo watafiti hao toka Australia wamekuja kutafiti madini au kuhamisha udongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuleta Kampuni toka Australia ambayo inakuja kutafiti Nishati ya Mafuta ndani ya Ziwa Tanganyika eneo la Jimbo la Kigoma Kusini. Ni matarajio yangu na ya wakazi wa eneo husika kuwa mafuta yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa Umeme eneo la Igamba Mto Malagarasi (Kigoma Kusini) ambao ungefanywa na Kampuni ya *MCC* umesitishwa kwa muda. Hii ni kutokana na hoja ya uhifadhi wa Vyura/Konokono ambao hawapatikani pengine popote duniani. Mheshimiwa Rais alipokuwa Kigoma hivi karibuni alitoa maelezo ya kina ya kutia moyo kuwa mradi huo haukufutwa ila umesitishwa ukisubiri kupatikana sehemu nyingine katika mto huo huo na kwamba mradi utaendelezwa muda sio mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali itoe maelezo ni lini utafiti wa sehemu nyingine na hatima ya maeneo yalivyokusudiwa na *MCC* yapate Umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuwa anajumuisha aeleze Umeme wa Igamba (Malagarasi) utazalishwa lini ili pia vijiji vya Kigoma Kusini vifaidike?

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na waandaaji wote katika Wizara hii. Ninawapongeza pia kwa hotuba nzuri. Pamoja na pongezi hizo ninayo yafuatayo ya kuchangia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shukrani, natoa shukrani zangu nikiamini kuwa mradi wa kusambaza umeme katika Jimbo la Kwimba kwa kuanza na ujenzi wa kupozea umeme Mabuki (unaofanywa na Tanesco) mradi unaofadhiliwa na *AFDB* haujafutwa. Ninasema hivyo nikiwa na mashaka kwa kuwa ufafanuzi wa *Electricity V,* hauko wazi. Ni taarifa iliyotajwa kwa ujasiri uliochanganyikana na uoga wa kuongopa. Ni taarifa fupi na ya jumla sana. Ninashukuru kwa kuwa bado hatujasahaulika na hatujatangaziwa kuwa mradi wa *Electricity V* umefutwa. Ninashukuru kwa kuwa tumewekwa na kutelekezwa mahali pa kuishi kwa matumaini japo kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu tu ni kupatiwa mara kwa mara taarifa ya maendeleo. Wananchi wa Hungumalwa hadi Shiuma wamekaa kwa muda mrefu wakisubiri umeme. Naomba wasikatishwe tamaa. Wananchi wa Tarafa za Nyamilama na Mwamashimba watafarijika sana kupata taarifa leo kuhusu maendeleo ya ujenzi wa mradi wa ujenzi wa kupozea umeme Mabuki ikielezea hatua zilizofikiwa hasa kwa kuamini kuwa ujenzi huo utafuatiwa na usambazaji ambao ndio utakohitaji ufadhili wa nje. Tafadhali sana ninaiomba taarifa hiyo japo kwa sentensi katika majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara hii hususani Kurugenzi ya Nishati Mbadala, Kurugenzi ambayo imekuwa nyepesi kupokea na kuelewa matatizo ya Kwimba. Kupitia Kurugenzi hii, tumefanikiwa kupata:-

(i) Umeme wa nguvu ya jua *(Solar).* Umeme huu umewekwa katika Shule za Sekondari za Mhande, Bupamwa, Mwamashimba, Kikubiji, Mwakilyambiti na katika Zahanati za Milyungu, Bugembe na Kituo cha Afya cha Mwamashimba.

(ii) Miradi ya *Biogas* kwa Shule za Sekondari za Mwamashimba, Nyamilama na Ngudu.

Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wote, wadau wa huduma ya Vituo hivyo ninatanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu wa Kurugenzi ya Nishati Mbadala kwa wepesi wake wa kuyapokea maombi na kuyaelewa. Ni imani na matumaini yangu kuwa ataendelea kutusikiliza. Hotuba ni nzuri, ninaunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kukupongeza kwa hotuba yako nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara

yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Nishati, kwa kuwa huduma ya umeme ni muhimu sana kwa maendeleo na Uchumi wa nchi yetu: Je, Serikali haioni kwamba gharama za umeme zikipunguzwa watapata wateja wengi kuliko hali ilivyo sasa kwamba gharama ni kubwa sana, wananchi wanashindwa kuvuta umeme katika majumba yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vijiji vya Nghambi, Chunyu, Msagali, Iyoma, Kisokwe, Idilo na Lupeta Wilayani Mpwapwa vitapata umeme wa mradi mkubwa wa *MCC* na Vijiji vya Mzase, Berege, Chitemo, Nhinila, na Mima watapata umeme wa mradi mkubwa wa *REA:* Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya umeme Vijiji vya Mbori, Makutupa, Bunila, Tambi, Mwenzele, Mlembule na kwa kuwa vijiji vya Manghangu, Kimagai na Godegode watapata umeme wa *REA:* Je, vijiji vya Mugoma, Mzogole na Kisisi watapata lini huduma ya umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upandaji holela wa bei ya mafuta ya dizeli, *petrol* na mafuta inaongeza gharama za nauli na usafirishaji kwa jumla: Je, Serikali inasema nini kuhusu upandaji holela wa mafuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu kumshukuru Rais – Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Wizara kwa kuanza kwa mradi wa Majenereta mawili Wilayani Kasulu. Hatua ya ziara ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete kuja Kasulu tarehe 15 Juni, 2010 na kuweka Jiwe la Msingi na kuangalia eneo la ujenzi wa mradi wa umeme ni mafanikio makubwa kwetu sisi wananchi wa Kasulu. Nawapa Wizara hongera sana na sasa *TANESCO*. Ombi kwa Wizara na *TANESCO* ni kuharakisha utekelezaji wa mradi huu. Tarehe za Novemba 2010 kama muda wa kuwashwa umeme, basi uzingatiwe sana, maana kiu ya wananchi pale ni kubwa sana kuliko maelezo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakala wa Nishati Vijijni, *REA*. Ninapenda pia kwa niaba ya wananchi wa Kasulu kushukuru sana juhudi zilizofanyika na *REA* kwa *facilitation* ya fedha kwa ajili ya *distribution* ya umeme Kasulu. Aidha, ninaomba sana vijiji (viunga) vya Mji wa Kasulu kama Kigondo, Kidyama, Ngansha na Nyantare viwe sehemu ya usambazaji umeme katika Mji wa Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi sasa vimeunganika kwa asilimia 90 na Mji wa Kasulu. *TANESCO* ilitizame jambo hili ili liende sambamba na kazi ambayo tayari imeanza pale Kasulu/Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Solar Packages – REA, REA* imepanga (mchakato umefika mbali) wa kujenga *Solar Packages* katika vijiji vya Kwaga (Shule ya

Sekondari Kabagwe), Nkundutsi (Shule ya Sekondari Nkundutsi) na Titye, Shule ya Sekondari Titye. Malengo pia ni kufanya vituo hivyo kuwa Vituo vya kusambaza nishati ya jua vijijini na hatua kwa hatua kuondoa koroboi na chemli vijijini ili kuboresha maisha na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa *REA* ni mzuri na sisi wananchi wa Kasulu, tunamshukuru sana *CEO* wa *REA* na Timu yake ya Ufundi kwa mara ya kwanza *(after 50 years)* kuelekeza macho na utashi wao katika Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu. Tunaomba sana mchakato huu ukamilishwe haraka pengine utekelezaji wake uwe sasa *(immediate)* kabla ya Agosti, 2010. Wanavijiji katika maeneo hayo matatu wanasubiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Malagarasi wa Umeme chini ya *MCC Project,* pamoja na yote yaliyotokea juu ya mradi huu na mambo ya hifadhi ya mazingira ninaomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *study* ya Malagarasi chini ya Igamba III iharakishwe ili nia ya kupeleka umeme Uvinza, Kigoma na Kasulu na Vijiji vyake ikamilike haraka. Hatua ya *MCC Team* kuafiki *fresh study* tumeifurahia na tunasubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara yako isimamie mchakato huu kwa karibu na taarifa za mara kwa mara kwa Wabunge zitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi Kwa kuwa Halmasharui ya Wilaya ya Kasulu imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuendeleza miradi hiyo, ninaomba sana *REA* ishirikiane na sisi Halmashauri ya Kasulu 2010/2011 kutekeleza miradi muhimu ya Mwoga *Min-hydro,* Kheri *Mission* Manyovu na Kabanga *Mission Min-hyro*. *Preliminary Studies* zimefanyika tayari, ongezeni nguvu ya kiufundi, tutekeleze miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Wizara, *TANESCO, REA* na Serikali kwa ujumla kwa miradi iliyopo na inayoendelea katika Mkoa wa Kigoma.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwa namna ya pekee, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri iliyofanyika ya kupeleka umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo maeneo ya Ndanda, Nyangao na Masasi, pia kuanza ujenzi wa kuziunganisha Wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi na eneo la Msimbati kwenye Gridi ya Umeme wa *Mnazi Bay*. Pongezi nyingine kwa Wizara ni kwa kupitisha sera mpya ya madini pamoja na kutunga sheria mpya ya madini ya mwaka 2010 ambayo imeonyesha kuwajali wachimbaji wadogo wadogo na kulenga kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri mengi yaliyofanywa na Wizara, ningependa kupata ufafanuzi kuhusu tatizo linalojitokeza hivi sasa Mkoani Mtwara la

kukatika ovyo umeme pamoja na mgao usioeleweka na kupelekea tatizo kubwa la kutopatikana maji kwenye mfumo wa mabomba. Je, tatizo hili linatokana na nini hasa? Je, ni kweli kwamba hizi ni hujuma za *TANESCO* kwa *ARTUMAS*? Je, ni kwa nini tatizo hili litokee katika kipindi ambacho *TANESCO* inakabidhi uendeshaji kwa Kampuni nyingine? Je, tatizo hili litakwisha lini? Naomba Serikali itambue kwamba wananchi wa Mtwara wanapata madhara ya kuharibikiwa vifaa vyao vya umeme vyenye thamani na hivyo kuongeza umasikini. Pia kutokana na matatizo ya mgao yanayoendelea, wananchi wameanza kutilia mashaka mradi wa kupeleka umeme Wilayani Newala na Tandahimba kama kweli utakuwa endelevu. Naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri awatoe mashaka haya wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuishauri Serikali mambo yafuatayo:-

- Wizara ya Nishati na Madini ishirikiane kwa karibu zaidi na Wizara ya mazingira ili kutumia taka ngumu kwa ajili ya kupata nishati mbadala vijijini.

- Kwa kuwa mahitaji ya matumizi ya kompyuta ni makubwa kwa sasa hadi vijijini, ni vyema sasa Serikali ihamasishe wawekezaji pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya matumizi ya umeme wa *Solar* vijijini hasa mashuleni na katika vituo vya Afya ambapo umeme huu unaweza kutumika kwa taa na matumizi mengine mengi.

- Kwa kuwa sheria mpya ya madini imeshasainiwa na Mheshimiwa Rais, basi Wizara iharakishe kutunga kanuni ikiwashirikisha wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa makambako – Songea KV 132 ukurasa wa 18 (sec. 30). Huyu Mkandarasi hasa atapatikana lini kwa uhakika ili tujue utekelezaji utaanza lini?

Mradi wa *MCC* – Malagarasi ukurasa wa 20 (sec. 36) Igamba III kwenye Mto Malagarasi iko juu au chini ya Igamba II?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wachimbaji wadogo katika ukurasa wa 35 (Sec. 65): Wilaya ya Ludewa ina aina za madini zaidi ya 15. Je, Wilaya ya Ludewa inaweza kuhusisha utengaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo ili kukwepa fujo zinazoanza kujitokeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa madini ya Urani, katika ukurasa wa 40 (Sec. 76). Wilaya ya Ludewa ina madini mengi ya Urani hususani katika Bonde la Mto Ruhuhu. Kwa nini utafiti wa Urani Ludewa haufanywi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa Ofisi za madini, katika ukurasa wa 47 (Sec. 82). Kwa nini hadi leo Ofisi ya Afisa Madini Ludewa haijajengwa licha ya ahadi za kila mwaka na kutengewa fedha katika bajeti mara kwa mara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne (IV) ya CCM hususani Wizara za Nishati na Madini na Viwanda na masoko, kwa kuanza rasmi miradi ya chumvi (Liganga) na Makaa ya Mawe (Ketawaka/Mchuchuma) iliyoshindikana kwa takribani karne moja iliyopita. Hongera CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni kuhakikisha fidia kwa wananchi waathirika wa Mundindi, Shaurimoyo na Amani inatolewa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mradi wa kasi mpya wa kuzalisha Chuma ghafi umeanza tangu tarehe 10 Mei, 2010 kwa ujenzi wa Miundombinu ya barabara na uchorongaji pamoja na kuchukua sampuli za Chuma na Makaa ya Mawe kwa uzalishaji wa majaribio kabla ya kuanza ujenzi wa Kiwanda na Uchimbaji wa Chuma na Makaa.

Changamoto hapa ni kuhakikisha fidia kwa wananchi waathirika wa Mundindi, Amani, Shaurimoyo na Mkomang'ombe inatolewa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kuipongeza Serikali kwa mkataba mzuri wa mradi wa chuma ghafi ambapo fedha imetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wana Ludewa *(Community Empowerment)* kushiriki katika mradi kwa kuwawezesha wananchi kuibua miradi inayoendana na mradi huu. Changamoto hapa, naomba mchakato huu wa uwezeshaji *(empowerment)* uanze mara moja ili uende sambamba na mradi.

Naishukuru Serikali kwa ruzuku iliyotolewa katika mradi mdogo wa umeme Mawengi ambao tayari unazalishwa kwa *KW 150* na umeanza kutumika. Changamoto, naomba Serikali itusaidie kukamilisha *KW 150* zilizosalia kipindi hiki cha miaka mitano ili wananchi wote wa Kata ya Mawengi wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mradi wa umeme *MW 400* Mchuchuma kufikia hatua ya kuwapata wawekezaji sita na kuwataka wawasilishe mapendekezo ya mradi ambapo mshindi atapatikana ifikapo Septemba, 2010. Changamoto, kwa uhakika mradi utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuwawezesha vikundi takribani 11 vya Uvuvi wa maeneo ya Mwambao wa Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Ludewa kupata zana za kisasa za uvuvi maboti na injini, ili kuwawezesha kuvuka kilindini. Uwezeshaji huu hauendi sambamba na kuboresha teknolojia ya kukausha samaki. Changamoto, tuwasaidie wavuvi teknolojia mbadala wa kukausha samaki badala ya kuni na kuharibu mazingira ya miteremko ya milima *livingstone*.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii. Naunga mkono hoja hii asilimia 99.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kuanza kazi ya kuweka umeme Mji wa Namanyere – Nkasi. Naomba Mkandarasi anayetandika nyaya toka Sumbawanga kuja Namanyere aanze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba naomba aanze kusambaza nguzo mji wa Namanyere ili kuwapa matumaini kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uchunguzi wa madini na vito ufanywe Nkasi yote, tafadhali sana Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. Naunga mkono.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara kwa kazi nzuri na yenye kutukuka. Ukweli ni kwamba jitihada kubwa inafanywa, tatizo ni ufinyu wa Bajeti. Ninaomba Serikali iongeze bajeti ya Nishati na Madini ili kukidhi mahitaji ya Nishati na uendelezaji wa Sekta ya Madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana *REA* kwa jinsi wanavyojitahidi sana kushughulikia suala la nishati hasa vijijini kwao. Ningependa tu kufahamu hatua za ubia zilizobakia katika kuanza mradi wa umeme maji katika Kata ya Mahaje Kijiji cha Mahaje Jimbo la Peramiho Lingatuta. Tungependa pia kufahamu vijana walioteuliwa kupitia mradi huo kwa ajili ya mafunzo, Semina maalum ya mradi huo wataanza lini? Kwani sasa ni kero inayoendana na hamu ya utekelezaji. Pamoja na wao kuwatuliza kwa maana ya kusubiri mapitio ya bajeti itakuwa vyema sana wakipata ufafanuzi wa matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme Makambako Songea ni wa utekelezaji wa ilani, sina uhakika mradi huo sasa utekelezaji wake utaanza lini. Pamoja na hayo yote kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho tunashukuru sana kwani saa umeme Peramiho umewaka, ukweli ni ukombozi mkubwa sana kwa Jimbo la Peramiho kwani sasa mawazo ya kuanzisha viwanda vya usindikaji yamejengwa na hasa Kiwanda cha Sukari Peramiho. Ninamaliza kwa kusema nawatakia utekelezaji mwema wa shughuli zote za kuwezesha upatikanaji wa nishati vijijini.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, **n**aona kama wataalam wa Wizara ya Nishati na Madini wanachanganya mambo kweli. Naomba Waziri aangalie vijiji/maeneo yatakayopatiwa umeme Mbozi, ukurasa wa tatu (jedwali) kauli ya Waziri Bungeni tarehe 2 Julai, 2010. Naomba aangalie jedwali Na.3 ukurasa wa 81 vijiji vitakavyopatiwa umeme Mbozi tofauti kabisa. Aidha, vijiji havipo Mbozi!

Mheshimiwa kulikoni naomba mfanye masahihisho katika hotuba yako ya bajeti leo.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitamke kuwa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maeneo mawili tu. La kwanza ni wachimbaji wadogo wadogo wa Malakite kule Nditi. Wachimbaji hawa wana mgogoro na mchimbaji mkubwa wa *Nikel* ambaye amemilikishwa eneo ambalo wachimbaji hawa wamekuwepo. Waziri Karamagi amewahi kulishughulikia jambo hili na Naibu Waziri –

Mheshimiwa Malima aliahidi kulishughulikia jambo hili kwa kutembelea sehemu ya tukio. Naamini bado atafanya ziara hiyo ndani ya uhai wa Serikali hii na nia ni kuwapatia eneo maalum wachimbaji hawa ili waendelee kujipatia maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni tatizo la umeme Nachingwea. Umeme wa Nachingwea unatokea Masasi ambako ndiko kuna mashine za kufua umeme. Pamoja na upatikanaji usiotosheleza pia Mheshimiwa Waziri aliahidi kushusha umeme katika vijiji vyote ambavyo umeme umepita kuelekea Ruangwa. Aliahidi kuweka *transformers* ili vijiji hivi vya njiani vipate umeme. Naamini bado Mheshimiwa Waziri atatekeleza ahadi yake hii kwa wananchi wa Matangini, Ikulu, Rupota na Marambo pamoja na Rufonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuwatakia Waheshimiwa Mawaziri Ngeleja na Malima, utekelezaji mwema na mafanikio katika shughuli za Kampeni katika Majimbo yenu.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuona matatizo sugu ya umeme Mjini Sumbawanga na Namanyere Mkoani Rukwa. Nampongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa W. Ngeleja, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam Malima na Wizara yote ya Nishati na Madini, kwa kuzindua ujenzi wa Kituo cha Umeme Mjini Sumbawanga, kitakachotoa umeme kwa Sumbawanga na Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la Serikali ni kufikisha umeme Vijijini, pamoja na mazuri ambayo yanaendelea Mkoani Rukwa kuhusu umeme, naomba Serikali iendelee kupanga namna Mkoa wa Rukwa utakavyopata umeme wa *Grid* ya Taifa utakaowawezesha wana Rukwa kufungua viwanda vijijini na miradi ya Kilimo na Umwagiliaji itakayotumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

1. Ni kwa nini Serikali inaonekana kutaka kutumia umeme wa Zambia kwa Mkoa wa Rukwa?

Je, mvua ikipungua huko Zambia, Rukwa *Hydro-power* madhara yake tumekwisha yaona tusifanye makosa hayo.

2. Kwa kuwa mpango wa Serikali ni kuunganisha umeme utokanao na *gas* katika *Grid* ya Taifa, kwa nini Serikali isibaki na msimamo wa kuipa Rukwa umeme wa *Grid* kama ilivyotamkwa wazi na Mheshimiwa Waziri W. Ngeleja wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa Kituo cha kutoa umeme Mjini Sumbawanga tarehe 19 Juni, 2010. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri Mheshimiwa William Ngeleja, Sengerema na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam K. Malima, Mbunge wa Mkuranga, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi mipya ya kupeleka umeme vijijini, katika mikoa na wilaya (10+) katika jedwali – Mkoa wa Tanga nimeona Wilaya ya Handeni katika Vijiji vya Chamka, Kibaoni, Msasa Magamba, Kwedikwazu na *Komnyanganyi Secondary School.* Napongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali, Wilaya ya Kilindi umeme umewaka miezi kama miwili iliyopita Makao Makuu – Songe. Tunapongeza Serikali sasa nimeona katika Kijiji (Kata) za Kisangasa – Mgera na Kata ya Kiburashi? Wamefunga *Transfoma.* Ninachojua huu umeme utasambazwa na mradi huu wa *REA* sasa katika jedwali Kilindi haimo. Mradi wake unapatikana wapi na lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kata ya Msanja Makao Makuu ya Kata Mswaki sisi wenyeji tunahitaji tupatiwe japo ka-*transfoma* kadogo tuweze kuvuta umeme majumbani. Tunalala giza! Katika Bajeti yenu mtatusaidiaje? Bahati nzuri hata Mheshimiwa Adam Malima, ninaongea naye. Tunaomba mshughulikie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kila la kheri, namwomba Mwenyezi Mungu asimamie Uchaguzi huu Mkuu wa mwaka huu Oktoba, 2010.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napongeza hotuba ya Wizara hii ni nzuri na imesheheni mambo mbalimbali ya kuleta Maendeleo katika nchi yetu. Msisitizo wangu ni kuomba sasa iwe ya vitendo zaidi kuliko nadaharia. Zimekuwepo ahadi nyingi sana kwenye hotuba, lakini vitendo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri William Ngeleja, Naibu wake Waziri Mheshimiwa Adam Malima, kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika Wizara hii .

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nampongeza sana Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara hii, *TANESCO* na Taasisi mbalimbali za Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuendeleza nchi hii kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Wizara hii kiuchumi ni kubwa sana ninawatakia kila la kheri katika kupambana na changamoto zilizopo mbele yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilio changu katika kuchangia hoja hii. Nimepitia orodha ya watakaopata umeme Vijijini *(REA).* Katika Mkoa wa Tanga ni Vijiji vya Wilaya ya Handeni tu ndio vinapatiwa umeme. Napenda kufahamu ni sababu zipi za msingi zilizofanya vijiji vyangu vya Wilaya ya Korogwe katika Kata za Kwamsisi, Kwakombo. Kijiji cha Kwakombo na Kwamsisi visipate umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kwamdolwa – Vijiji vya Kwameta, Gwangara, Daraja visipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kilole – Vijiji vya Bagamoyo visipate. Kata ya Mtonga – Kusambaza nguzo. Kata ya Ngombezi – Kusambaza umeme hadi Mgambo. Kama itawezekana katika Bajeti hii nikapatiwa msaada wa Vijiji vya Kata mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kwamdolwa. Kijiji cha Kwameta – Kijiji hiki ni zaidi ya miaka kumi (10) sasa vimeomba kuwekewa umeme. Wananchi zaidi ya 150 wanaweka *wire* ndani ya nyumba zao lakini hadi sasa ni ahadi tu! Nimeomba sana Kijiji hiki kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kwamsisi/Kwakombo. Kijiji hiki kina umeme nusu na sehemu nyingine haina kabisa. Wananchi wa eneo hili wametishia kuninyima kura kama kuna kuwa na upendeleo wa kuweka umeme kwa eneo moja na kuacha lingine kwenye Kijiji kimoja ni vizuri umeme kutoka Kijiji hiki ukamilishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mtonga/Mwambani. Umeme wa Kijiji hiki hiki eneo hili ni kubwa na nguzo bado hazijasambazwa. Kimsingi ninapenda kusisitiza kwamba mradi ukianza usichukue nusu nusu, ni busara kuanza mradi na kuumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa umeme katika Shule ya Sekondari za Kata. Ninaomba kupendekeza na kutoa ushauri wa Wizara kuja na mpango kamambe kwa kushirikiana na Halmashauri zetu kuziwekea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia tungeanza na Shule ambazo zipo karibu na umeme kama vile *Ngombezi Secondary School, Kwamdolwa Secondary School, Joel Nkaya Bendera Secondary School (Kwakombo)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, amewasilisha hoja yake vizuri, kwa ufasaha na taarifa za utekelezaji ni za kina. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mfupi, na unahusu Umeme Vijijini. Moja ya maamuzi ya busara na ya msingi ya Serikali ni kuunda chombo mahsusi cha kutoa msukumo wa kusambaza umeme vijijini. Miaka mitano ijayo, tutakapoorodhesha mafanikio ya chombo hicho, Wakala wa Umeme Vijijini, naamini tutashangazwa na kasi ya kusambaza Umeme Vijijini ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Wakala *(REA)* unachangamoto kubwa lakini palipo na changamoto maendeleo huwa ya kasi zaidi. Menejimenti ya *REA* ya sasa chini ya Dr. Lutengano Mwakahesya, ambaye nimebahatika kufanya naye kazi tukiwa pamoja katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini miaka ya 1990, ijione ina bahati isiyo ya kawaida ya kuwa menejimenti anzilishi nzuri. Vivyo hivyo kwa Bodi anzilishi ya *REA.* Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekee jimboni kwangu Rungwe Mashariki. Naanza kwa jambo la wataalam tu, kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini, *TANESCO*

na *REA,* hasa Waziri mwenyewe ambaye nimemsumbua sana nikifuatilia uunganishaji wa umeme kutoka Kandete kwenda Luteba na kutoka Mwakaleli kwenda Matamba. Namshukuru katika kauli aliyotoa Bungeni wiki iliyopita amethibitisha kwamba Mkandarasi tayari amepatikana, mikataba amesaini na hivi karibuni ataanza kazi. Nimemsumbua sana Dr. Lutengano Mwakahesya, amenivumilia, ametembelea Luteba na Matamba na maeneo mengine yenye uwezekano wa kuunganishwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa laini ya *KV33* ipo, uunganishaji wa umeme kwenye Vijiji vingi inawezekana na kwa gharama nafuu. Umbali katika laini hiyo kwenda sehemu yoyote ya jimbo si mkubwa. Natoa rai na ombi kwa *REA,* kutusaidia kwa kupeleka umeme maeneo yafuatayo:-

(i) Kutoka Lwangwa kwenda Lukasi;
(ii) Kutoka Kiwanda cha Kyejo gasi kwenda Mpata;
(iii) Kutoka Lugombo kwenda Ndala;
(iv) Kutoka Mwakaleli kwenda Lusanje; na
(v) Tunatoa maombi ya *transfoma* kwa maeneo yafuatayo:-
  (a) Lupata Kijijini (Shule ya Msingi);
  (b) Bujesi (Kwa Mbamba) kwa ajili ya Kijiji cha Nsasu na Sekondari ya Mzalendo;
  (c) Busekele;
  (d) Kisegese (Kuunganisha Shule ya Sekondari ya Kisegese);
  (e) Lusanje (kuunganisha Sekondari ya Kyejo);
(vi) Kuunganisha Mbigili na Lwangwa kupitia Lupaso;

Kama nilivyokwisha eleza hapo awali, umbali wa maeneo yote haya toka laini ya *KV33* ya Gridi ya Taifa si mkubwa. Hivyo basi tunaweza kuwapatia wananchi wengi umeme kwa shughuli za kiuchumi, elimu na nyumbani, kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii vile vile kumpongeza Ndugu Mhando, kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika letu muhimu sana la *TANESCO.* Amewahi kuwa Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Mbeya. Amefanya kazi kubwa nchini. Naamini kufikia ngazi hiyo ni kutokana na misingi ya kazi nzuri aliyoifanya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaifahamu sana Rungwe, na Rungwe Mashariki. Naamini imani aliyopewa na Taifa, atairudisha kwa kuimarisha *TANESCO.* Nampongeza vile vile Meneja wa *TANESCO* Tukuyu, Mama Lydia na Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kama nilivyoanza kwa kumpongeza tena Waziri Ngeleja na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Malima, Katibu Mkuu, Ndugu David Jairo, namfahamu, nimefanya kazi naye, ni mchapa kazi, mwadilifu, msikivu amekulia katika Wizara hiyo. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100%.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa hotuba yake nzuri. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri kwani ameonesha kuwa na uwezo mkubwa katika kumsaidia Waziri katika majukumu yake. pongezi pia ziwafikie Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii ya Nishati na Madini kwa utendaji wao kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Juni, 2010 Wizara kupitia swali langu iliahidi kuwa Nanyumbu itapatiwa umeme wa gesi kutoka *Mnazi Bay*. Ahadi hii ya Serikali kwa wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu. Nami kwa niaba yao naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa ahadi hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunasubiri ahadi hii ya Serikali, bado Makao Makuu ya Wilaya (Nanyumbu) yanakabiliwa na tatizo la umeme hasa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya *(DC)* pamoja na makazi yake, Ofisi za Halmashauri ya Wilaya pamoja na makazi ya watumishi wake. Ningependa Wizara katika majumuisho yake itoe maelezo kuhusu hoja hii. aidha wananchi wa Nanyumbu wanapenda kujua ni lini mradi wa kupeleka umeme wa uhakika utaanza kutekelezwa. Majibu pia yatolewe wakati mtoa hoja atakapohitimisha hoja ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara na Mashirika yake hasa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na Shirika la Kusambaza Umeme Vijijini *(REA)* kwa kazi nzuri na yasifia kwa mnayofanya hapa Tanzania. Kwa kweli kama Wizara zote zingekuwa zinafanya kazi kama nyie nchi yetu ingekuwa mbele sana kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Wizara yake kwa kupeleka *transforma* ya umeme Kijiji cha Singa kilikuwa kilio cha miaka mingi sana nashukuru kwa kupeleka *transforma* kubwa Kijiji cha Nkungi kwa matumizi ya Hospitali na wakazi wote wa eneo hilo, nashukuru kwa kuanza kupeleka nguzo za kutosha Tumuli Singa na Nkungi. Nashukuru mwaka huu wa fedha kwa kupeleka umeme Kijiji cha Msingi na hatimaye uende Lumanga, Mkalama na Ibaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi umeme umefika Nkungi na Mradi ulikuwa kutoa umeme Mtinko kupitia Nkungi, Ikunda mpaka Iambi na hatiamaye Nduguti, naomba hiyo ahadi ya Serikali iendelee kutekelezwa sasa hivi Wilaya ya Mkalama imeanzishwa na Makao Makuu ni Nduguti hapo sina wasiwasi kwa sababu Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Tanzania alishatamka kwa kauli yake kwamba umeme uende haraka sana kwenye Makao Mkuu ya Wilaya 18 mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ataleta makampuni ya kutafuta maeneo ya kutoa umeme wa upepo Iramba Mashariki. Napenda kukuhakikishia kuwa maeneo ni mengi sana yakiwepo Kikonda, Kinampanda, Singa, Nkungi, Kinyangiri, Ishenga, Mwanga, Kidarafa, Mwangeza, Ilolo, Endasiku, Nyuhaa, Mkade, Mpambala, Matongo, Mkalama, Gumanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliniahidi kupeleka umeme kwenye shule za sekondari za Igugumo ambayo ni kilomita mbili tu kutoka *line* ya umeme na Halmashauri ya Wilaya tayari imechangia Sh. 20 million, Tumuli robo kilomita toka wenye *line* ya umeme. Je, Serikali itakuwa tayari kukamilisha kazi hiyo sasa, na kwa kuwa umeme unatoka Kinampanda kwenda Msingi na Gumanga najua eneo la kwanza litakalofungwa umeme, ni Chuo cha Maendeleo Msingi. Naomba umeme uingie Zahanati ya Msingi, Shule ya Sekondari, JORMA pia uingie kwenye nyumba za Ibada (Makanisani na Misikitini), maana nao wameisha ombi na Gumanga uingie maeneo kama niliyoyataja hapo juu pia uingie Shule ya Sekondari Gumanga na Kituo cha Kilimo Gumanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kasi hiyo hiyo ya kupeleka umeme Nduguti, Gumanga, Msingi pia umeme uende Kinyangiri ambako tayari Shirika lilishapima njia ya kupitisha pia ni lazima uingie Shule ya Sekondari Kinyangiri. Umeme wa kwenda Nduguti ukifika Mwando uende Nkalakala, Kinyambuli Nkinto na Matongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%. Napenda nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walio chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ya utekelezaji wa Ilani ya CCM 2005. Pia kwa kuandaa hotuba hii yenye kuleta matumaini kwa Watanzania. Pamoja na pongezi hizi nina maoni yafuatayo:-

1. Umeme Vijijini. Serikali iharakishe utekelezaji wa programu ya usambazaji wa umeme vijijini uende kwa kasi zaidi na usimamizi wa karibu zaidi.

2. Uwekaji umeme pembezoni mwa mkoa wa Dar es Salaam. Kumekuwa na kusuasua kwa usambazaji wa umeme katika maeneo yaliyoko pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam kama maeneo ya Chanika kuelekea Msongola mpaka Chamazi hali ambayo imerudisha nyuma uchumi wa wananchi wa maeneo hayo. Je, Serikali inatoa kauli gani au itachukua hatua gani za haraka ili kuhakikisha eneo hilo linapitiwa na huduma ya umeme?

3. Hongereni sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mliyofanya kwa kipindi cha miaka mitano (5). Mungu awarudishe wote. Amina.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na wenzake kwa hotuba nzuri na nawatakia mafanikio katika utekelezaji wa mipango yao kwa mwaka 2010/2011.

Hata hivyo naomba kutoa maombi na ushauri ujao. Kwa kuwa umeme wa gridi umefika Wilaya ya Njombe na kwamba chini ya mpango wa kufikisha umeme Lupembe kwa msaada wa *Sweedish Aid* umeme huo ulikuwa kushushwa katika Vijiji unamopita waya wake Vijiji vya Ikando na Wanginyi havikushushiwa umeme,. Tunaomba vishushiwe umeme kama vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isambaze umeme wa gridi katika vijiji vyenye shule za sekondari zilizo katika vijiji husika (Ikuna, Sovu, Mtimbwe, Kipagamo, Mkilima, Maguvani, Itipingi, Kichiwa na Manyunyu (hizi ni sekondari) na katika vijiji vikubwa. Ieneze umeme katika vitongoji vyote vya Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Isambaze umeme katika Vijiji vya Kata ya Igongolo (Ikando, Ibumila, Maduma, Kichiwa, Tagamenda, Itepingi, Igengolo na Kivitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuleta maombi haya kwa maandishi kwa Waziri lakini sijapata majibu yoyote. Tafadhali naomba ushughulikie.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri inayoendelea kufanyika chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini. *Keep it up.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu nimekuwa nikiomba umeme ufike Tarafa ya Ndagalu, Jimbo la Magu. *Option* za kupeleka umeme huko ni (i) Kutokea Magu Mjini (ii) Kutokea Kasoli, Wilaya ya Bariadi na (iii) Kutokea Tallo Sekondari, Jimbo la Sumve. *Option ya \9iii\0* ndiyo iliyoonekana ina gharama nafuu zaidi. Je, ni lini sasa Wizara itanza kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri sana anazozifanya katika Wizara yake. Pia nampongeza Mheshimiwa Adamu Malima kwa kujibu maswali vizuri humu ndani ya Bunge letu. Nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Jairo na timu ya watendaji wenzake wote. Wanafanya kazi nzuri sana pamoja na ukweli kwamba Bajeti ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba nilete kilio changu cha siku nyingi kuhusu Umeme Vijijini katika Jimbo la Uchaguzi Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2006 Serikali iliahidi kupeleka umeme katika vijiji vya Rwabwere, Kamagambo, Nyakagoyagoye hadi Nyakaiga. Hadi leo hii ninapoandika hakuna dalili zozote za kupeleka umeme katika vijiji hivi. Bajeti ya mwaka huu fedha hizo sizioni. Je, Serikali imewadanganya wananchi wa vijiji hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha zitengwe katika Bajeti ya mwaka huu 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Vijiji vya Ndama, Nyabwegira, Runyaga, Kituntu na Rwambaizi bado Serikali haijatimiza ahadi yake. nguzo zimefika Kijiji cha Nyabwegira na sehemu za Kakilo Kijiji cha Runyaga zingine zimesimikwa na nyingine zimelala chini. Maana yake ni nini hasa? Kwa nini umeme haupelekwi vijiji hivi?

Mheshiniwa Spika, ahadi nyingine Jimboni Karagwe ni la Vijiji vya Bisheshe, Nyakayanja, Nyaishozi na Ihembe. Akijibu swali katika Bunge la Kumi na Tisa, hapa Bungeni, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alisema tayari Mkandarasi amepatikana na angeanza kazi Mei, 2010. Leo hii ni Julai, 2010 sijaona chochote kinachofanyika. Nasikia Mkandarasi yupo Bukoba Vijijini ni kwa nini asije Karagwe? Naomba afike haraka Karagwe na kuanza kazi kabla ya Bunge hili kuvunjwa. Sababu za kumtaka aje kabla ya Bunge kuvunjwa ziko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Serikali yangu kusikia kilio cha wana Rukwa kuhusu ufumbuzi wa kutupatia umeme wa uhakika kwa kuleta mpango wa Jenerata nne kubwa ambazo Mheshimiwa Rais aliziwekea jiwe la msingi mwezi uliopita. Kwa msingi huu, sina sababu ya kutounga Muswada na hoja hii ya Waziri wangu.

Mhehimiwa Spika, naomba sasa niulize maswali yafuatayo:-

Kwa kuwa usafiri wa Generata kwa kutumia magari makubwa umeleta utata wa ukubwa wa mashine hizo kulingana na uwezo wa barabara zetu na hadi kufanya Idara ya Mizani na Wasafirishaji waingie katika utata. Mfano ni ule wa *TANESCO* na *Usangu Transportors* ambao walishindwa kwa muda mrefu kusafirisha mzigo wao huo.

Kwa kuwa barabara na baadhi ya madaraja ya kwenda Sumbawanga siyo imara. Je tahadahri gani imeandaliwa kufikishwa mzigo huo wa jenerators hizi Sumbawanga kwa muda muafaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze hivi kule Mpanda kuna dhahabu ya kutosha? Mbona wawekezaji wengi wakiwemo Warusi wanaelekea wakija na kuamua kuondoka na kuacha mashimo baada ya muda kwa kusema kuwa hakuna dhahabu ya kutosha. Ukweli uko wapi? Mheshimiwa Waziri, tunakuomba ufuatilie ombi letu wana Rukwa na hasa Sumbawanga wa kutumia maporomoko ya Kalambo kwa kuzalisha umeme. Nini uchunguzi wa Wizara kuhusu uwezekano huo. Pia mkaa wa mawe wa Namwele ambao unaonekana una “ash content” kidogo na kuweza kuwa suluhisho ka baadaye kwa nishati mbadala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nampongeza Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa *TANESCO* Ndugu Mhando, kwa jinsi alivyokuja na ari mpya zaidi ya kuliamsha shirika hili ambalo tatizo lake ni ukwasi. Tumsaidie afanye kazi yake vizuri bila kukwamisha baadhi ya mapendekezo yake juu ya gharama ili afanye mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. kheri niwatakie Waziri, Naibu kwa Uchaguzi Mkuu ujao wa Oktoba mwaka huu 2010.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nchi yetu ina *gas* nyingi sana na takwimu zinaonesha uwezo wa kuiuza nje. Serikali ina mpango gani wa utekelezaji wa mradi huu. Serikali ili ipate gawio la kuridhisha inabidi nayo iwekeze mtaji kama wanavyofanya Botswana.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Swali kwa muda mrefu sasa nimekuwa nikiwaomba Wizara kupeleka umeme kwenye Mji wa Mbamba Bay bila majibu. Kwa kuwa sasa Mbamba Bay ni Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Ziwa Nyasa na kwa kuwa tayari Wilaya ya Mbinga imetoa *generator* ambayo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya hiyo na ambayo *TANESCO* waliitumia awali kufua umeme kabla ya Serikali kununua mpya, na kwa kuwa sera ya nchi kuhusu umeme ni kuwa kila penye Makao Makuu ya Wilaya papatiwe umeme na kwa kuwa kazi ya pale Mbambabay kwa *TANESCO* ni kusambaza nyaya za umeme tu ili kuwasha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini na kwa uharaka upi Mji wa Mbamba Bay utapatiwa huduma hiyo?

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kama timu nzuri ya kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwanza biashara ya Mafuta. Pamoja na juhudi ya Serikali ya kupambana na tatizo sugu la uchakachuaji wa mafuta, lakini inaelekea wenye vituo hivyo wamejenga kiburi kikubwa kwani tatizo bado ni kubwa. Natoa pongezi kwa Serikali kwa kuchukua hatua kali kwa kutoa faini na kuwafungia biashara wahalifu wanaobainika na matatizo hayo. Hata hivyo nashauri kuwepo pia na adhabu ya kulipa fidia kwa hasara inayopatikana baada ya uharibifu wa vyombo mbali mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia kuendelea kuchunguza kwa kina utitiri wa vituo vya mafuta katika barabara kati ya Chalinze na Kibaha. Vinatia mashaka makubwa. Kwa hesabu za haraka haraka kuna vituo visivyopungua thelathini katika maeneo hayo. Hivi Serikali haioni kwamba ni lazima kuna udanganyifu fulani unaoendelea katika maeneo hayo, kama si ukwepaji wa ushuru au ni uhalifu wa uchakachuaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuiomba Serikali kuziagiza Halmashauri za Wilaya na Miji, kupiga marufuku ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya makazi kwani kuruhusu hali hiyo ni hatari kubwa kwa maisha ya binadamu na mali za watu, inapotokea ajali ya moto katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti na uchimbaji wa madini. Pamoja na jitihada kubwa ya Serikali ya kukaribisha uwekezaji wa madini mbali mbali nchini, bado tuelewe hapa nchini tuna aina nyingi za madini ambayo bado hayajafanyiwe *exploration* ya kutosha hasa katika maeneo ya safu za Milima ya *Livingstone* ambako inasadikika kuna *Copper* na *Uranium* nyingi. Hivi sasa kuna watafiti wengi ambao hawana leseni halali za *exploration* kutoka nchi jirani wanaotembelea maeneo ya Milima ya *Livingstone,* utafiti ambao hatujui matokeo yake ni nini. Hata hivyo kuna haja ya Wizara hii kushirikiana na Wizara za Miundombinu na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhakikisha barabara zinachimbwa katika Ukanda huo wa Ziwa Nyasa la sivyo utafiti wala uchimbaji hauwezi kuwa wa mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza pia suala la Wizara hii kushirikisha *NEMC,* Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, Maji na Umwagiliaji na kadhalika kabla ya kutoa vibali vya utafutaji au uchimbaji wa Madini. Suala la kurudishia mazingira ya asili katika maeneo yaliyoharibiwa na wanaotafuta madini. Mikoa pia ishirikishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba wachimbaji wadogo wadogo hasa wanawake wachimbaji wa Mkoa wa Mbeya waendelezwe kimtaji kwa kuwasaidia kwa njia rahisi za kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Nawatakia afya na kazi njema.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii yoyote ile. Lakini cha kusikitisha kwa miaka 50 toka tumepata uhuru bado hata asilimia 15 ya Watanzania hawajapata umeme! Hii ni aibu sana tunaomba Serikali ione umuhimu wa nishati hii ili Maisha Bora kwa kila Mtanzania yapatikane. Nchi zote zilizoendelea zimefika hapo kutokana na viwanda na viwanda hivyo vinaendeshwa kwa umeme. Hivyo tunaona ni jinsi gani tumeshimndwa kufanya mapinduzi ya viwanda wakati tuna malighafi nyingi sana ambazo zingeweza kuchakatwa hapa hapa nchini.

Kwa kuwa umeme unasaidia sana sekta za huduma kama elimu na afya, inasikitisha sana kuona bado sekta hizi hazijapata umeme na hivyo kurudisha nyumba sekta hizi huku wagonjwa wakikosa huduma muhimu na hata kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo Serikali ingefanya ni kuwa na vyanzo mbadala vya umeme kama vile upepo na *solar* ambapo kwa kijiografia Tanzania ina mwanga wa jua katika kipindi chote cha mwaka. Nchi nyingi zilizoendelea zilianza na umeme wa makaa ya mawe. Tanzania tumejaliwa makaa haya lakini tumeshindwa kuyatumia na kwenda katika *hydro power* ambapo vyanzo vya maji vinategemea zaidi mvua.

Kuhusu nishati ya mafuta. Nishati hii ni ya muhimu kwani ndio huendesha mitambo, magari, ndege na vyombo vingi vya usafiri. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba wafanyabiashara wasio waaminifu wameamua kuchanganya mafuta ya taa na

dizeli ambayo kwa kiasi kikubwa imeharibu sana vyombo vya usafiri. Tunashukuru Waziri kwa kutoa kauli kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madini. Tanzania tumebahatika kuwa na madini ya aina mbali mbali kama almasi, dhahabu na vito mbali mbali ikiwemo *Tanzanite,* madini ambayo duniani kote yanapatikana hapa Tanzania tu. Jambo la kusikitisha ni kuwa madini haya yanapatikana nchi za Kenya na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyaswa na kushindwa kufanya kazi zao huku makampuni makubwa yakiendelea kuwanyanyasa kama ilivyotokea huko Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kumekuwa na matukio mabaya ya mahusiano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Hali hii siyo nzuri na ikiachwa iendelee hali inaweza kuwa mbaya zaidi.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mheshimiwa waziri kuniahidi mara kadhaa kuhusu kuja Mpanda kusikiliza kero za wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda na uhakika wa mgogoro wao ambao umekuwepo kwa takriban miaka kumi (10) sasa zimeshindikana na hakuna ufumbuzi wa tatizo hilo. Nitapenda kupitia Bunge hili kupata suluhisho la mgogoro huu ambao nyaraka zake zote niliwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri. Naiomba Wizara itoe kauli itakayowapa faraja wachimbaji hawa wa Mpanda ili kuthibitisha kwamba kwa muda wote kama mwakilishi wao nimekuwa nikilifuatilia kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mji wa Mpanda unakua kwa kasi, pia mahitaji ya umeme ni makubwa, nichukue nafasi hii kuishukuru Wizara na watendaji wake pia *TANESCO* kwa jitahada wanazofanya za kukarabati mashine zilizochoka ili kuondoa kero ya umeme. Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa kuwa mitambo iliyopo Mpanda ni chakavu na gharama za uendeshaji ni kubwa ili kupunguza mzigo huo wa gharama ni lazima *TANESCO* iongeze wateja ambao tayari wapo tatizo ni kujenga *Service Line* kwenye maeneo ya makazi, Majengo, Kazima, Nsemlwa, Shanwe, Misunkumilo na Ilembo. Nichukue nafasi hii kuiomba Serikali isaidie *TANESCO* kukamilisha miradi hii kwa nia ya kuongeza wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *Grid* katika Mkoa wa Rukwa bado ni tatizo ambalo hatujui ufumbuzi wake. Aidha itachukua muda mrefu sana kwa Mji wa Mpanda kuunganishwa katika *grid* ya Taifa kwa Mpango wa sasa ama kupata umeme toka Kaskazini (Geita) au Kusini (Mbeya). Niiombe Serikali sasa kuangalia upya mpango wa kuunganisha Mji wa Mpanda kupitia umeme wa *grid* ambao tayari umeishafikishwa Kaliua (Mkoa wa Tabora) kwa maana ni karibu zaidi kuliko njia hizo mbili za awali nilizozitaja kupitia Geita au Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika katika hotuba ya Waziri ameeleza mpango wa utafiti wa mafuta katika Ziwa Tanganyika – Kaskazini na Kusini niiombe Wizara kujenga utamaduni huu wa kutoa taarifa kwa umma kila mara kuondoa hofu kwa wananchi ambao wanaona shughuli zikiendelea katika maeneo yao. Kwa mfano utafiti kuendelea kule Mgambo (Kapalagulu) kwa zaidi ya miaka 15 sasa ni nini kinaendelea na wanatafuta nini hasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningependa kujua kama Serikali ina mpango wowote wa kufanya utafiti wa kina katika mwambao wa Ziwa Tanganyika Wilayani Mpanda juu ya madini ya shaba na kama tunaweza kunufaika kama Taifa kwa kuwepo kwa madini ya shaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uchimbaji wa shaba unahitaji utaalamu na mitambo na uwekezaji. Je, Serikali ina mpango gani katika uchimbaji wa shaba kupitia shirika lake la *STAMICO* au *NDC,* niishawishi sasa Serikali kuona kama upo uwezekano wa kuangalia na kujua wingi wa rasilimali hii ya shaba katika mwambao wa Ziwa Tanganyika kwa Mikoa ya Kigoma na Rukwa. Nakushukuru sana.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanyakazi kwenye Wizara ya Nishati na Madini, wanafanya kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nitoe pongezi zangu kwa juhudi za umeme Wilaya ya Mpanda wananchi wa Mpanda wanasema asante sana kwa umeme sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pongezi kwa Wilaya ya Sumbawanga Mjini pamoja na Wilaya ya Nkasi kwa matumaini ya umeme kwa mwaka huu wa 2010 wa fedha mambo yanatakiwa mazuri sana. Wilaya ya Mpanda kuna madini mengi ambayo wachimbaji wadogo wadogo ni wengi lakini mafunzo na ujuzi hawana. Kwa hiyo, tunaomba mafunzo au semina. Pia kusimamia taratibu za hifadhi na udhibiti wa mazingira kwenye machimbo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kutatua matatizo ya umeme lakini naomba matatizo ya wachimbaji wadogo wa Mugusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali ya wachimbaji Magosi tarehe 29/3/2009 na kufa. Baada ya ajali ile Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 2/4/2009 aliagiza kufunga machimbo kwa siku 90 na muda huo ulikamilika lakini mpaka leo wachimbaji hao hawajaruhusiwa kuchimba dhahabu tena, cha kusikitisha wachimbaji hao wakiuliza wanatishwa mpaka wakaamua kwa nguvu kuvamia machimbo mpaka ikapelekea Polisi kutumia mabomu ya machozi dhidi ya wananchi wale.

Je, ni hatua gani Serikali kuhusiana na suala hili ukizingatia wananchi wale wanategemea machimbo kwa maisha yao ya kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya migodi ambayo shughuli zao huambatana na kemikali ambazo huharibu vyanzo vya maji na kupelekea mazao kutokustawi vizuri. Je, Serikali inawakikishaje wananchi wa sehemu husika kwa mfano wananchi wa Nyakabale?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya usambazji umeme vijijini. Ukizingatia kauli mbiu ya Kilimo Kwanza ni lazima kuanzishwa viwanda vidogo na vya Kati vya kusindika mazao vijijini. Ni lazima umeme ukapelekwa vijijini na uwe na nguvu ya kutosha kuendesha mashine mbali mbali kwa sababu hata vile vijiji vilivyobahatika kupata umeme ni mdogo sana. Mwanga wake hata wa kibatari una nafuu. Hivyo basi umeme huo uwe ni wa uhakika isije ikawa ni siasa tu.

Je, Serikali inafikia hatua gani kununua mitambo ya *IPTL?* Hii ilipendekezwa na Kamati ya Madini ya Bunge ya Nishati na Madini ili kumpunguzia mtumiaji gharama kutokana na *(Capacity Charges)* ambazo huongeza bei kwenye *bill* za umeme kutoka *TANESCO* kwenda kwa mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mafuta imekuwa ikipanda kila kukicha kwa wafanyabiashara wanaouza mafuta kwa kisingizio cha dola kupanda bei. Lakini Serikali ilikuwa na mkakati wa kuiwezesha *TPDC* waagize mafuta kwa wingi na wao wasambaze kwa wafanyabiashara na hii ingesaidia ku-*control* bei. Je, mkakati huo umefikia wapi? Na kama *TPDC* wakiagiza mafuta na *TIPPER* imebinafishwa wataweka wapi mafuta hayo. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu madini kuongezewa thamani nchini. Tumekuwa tikiliongelea suala hili hapa Bungeni tangu 2005 ni lazima wawekezaji wanaokuja kuchimba madini wajenge viwanda vya kuongezea thamani hapa hapa. Serikali kwa sasa hivi inapoteza fedha nyingi sana.

Je, Serikali ni nani anayejua mchanga huo unaopelekwa nje ni madini kiasi gani yamepatikana na ni ya aina gain?

Je, utekelezaji wa sheria ya kulazimisha madini yaongezewe thamani hapa nchini utatekelezwa lini *(time frame).* Naomba majibu ya uhakika siyo ya kufurahisha Watanzania kwa nia ya kupata kura tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kupongeza msemaji mkuu wa upinzani kwa hotuba yake iliyofanyiwa utafiti wa kina ni mategemeo yangu Serikali itayatumia maoni hayo kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwailisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kijana wetu William Ngeleja na Naibu Waziri wake kijana mwenzie Mheshimiwa Adam Kigoma Malima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, sio muda muafaka isipokuwa naomba nisemee haya:-

Suala la kuondoa kodi kwenye vifaa vya kubadilisha magari yanayotumia *petrol/diesel* kutumia gesi. Je, vifaa hivyo vimesamehewa kodi? Na huo mradi mbona hauhamasishwi sana wakati kuna tatizo la nishati ya mafuta? Uelewa kwa watumiaji na uwezo wa huo wawekezaji wa kubadilisha ukoje? Mmefikia vipi kuhusu *132 KV* Makambako – Songea?

Suala la uchakachuaji wa mafuta ni nyeti kama ulivyosema jana, ipo haja ya kuangalia pia huo utaratibu mzima wa kodi hizo za mafuta ili ikiwezekana watu hao wasiokuwa na uwezo wawekewe utaratibu maalum wa kuwasaidia ambao hauna athari kubwa kwa wananchi.

Naipongeza *TANESCO bila* kumsahau Mkurugenzi Mtendaji Mkuu, Mhandisi Mhando, kwa kuteuliwa kuliongoza Shirika hili. Naamini atafanya vizuri. Pia utaongeza mtandao wa umeme pale Mbinga, katika Mkoa wa Ruvuma.

Nawashukuru kwa misaada mbali mbali mliyonisaidia katika eneo langu la uwakilishi katika Mkoa wa Ruvuma.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli natoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Shirika letu la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kwa kazi kubwa wanayofanya chini ya uongozi wa uadilifu na uwajibikaji mzuri wa Mhandisi Mhando. Nimeridhishwa sana na uchapaji kazi wa Shririka na hata mahusiano ya kikazi baina ya Shirika na ofisi yangu (Ofisi ya Mbunge katika Jimbo la Kigamboni). Tunalipelekea taarifa linashughulikia mara moja na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* hivi sasa katika Jimbo la Kigamboni wanapeleka umeme eneo la Kata ya Kisarawe II, Kata ya Somangila na Kata ya Kimbiji jambo ambalo limefurahiwa na wapiga kura wangu na vilevile itachochea maendeleo katika Kata hizo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya watalii kutembelea katika fukwe za bahari kwenye ukanda huo bila ya kusahau kutosheleza mahitaji ya umeme kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda mbalimbali ambavyo vilikwama kutokana na kukosekana umeme. Aidha, naiomba *TANESCO* kuendelea na zoezi la kupeleka umeme eneo la Kilungule, Charambe Saku, Chamazi, Kibada hadi kwenye mradi wa nyumba za 300 za *NSSF* pamoja na Kata ya Vijibweni, Jimbo la Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia *EWURA* hasa kwa kuainisha bei halali ya maji kwa ndoo/lita kwa Taifa zima. Naishauri *EWURA* kuangalia uwekezekano wa kuweka kituo/ofisi katika ngazi ya Wilaya kusimamia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa bei hizo. Aidha, *EWURA* mnastahili kupewa pongezi kwa kushinda vita vya kuchakachua mafuta. Hongera za pekee kwa kaka yangu Afisa Mtendaji Mkuu wa *EWURA* Ndugu Haruna Masebu. Fanyeni ukaguzi pia katika eneo la Kigamboni hasa *refinery* ziliopo katika Kata ya Vijibweni, Tungi Kigamboni.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Katibu Mkuu Ndugu David Kitundu Jairo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Bajeti ya mwaka huu 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Bajeti ya mwaka huu ninao mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme vijijini, mara kadhaa nimeikumbusha Wizara katika mfululizo wa Bajeti mbalimbali vipi kuhusu miradi ya umeme vijijini kwa vijiji vya Kitukutu Kata ya Ulemo, Kitusha, Maluga, Ng'anguli (Kata ya Kinampanda), Kibaya (Ndago Sekondari), Zinziligi, Songambele (Kata ya Ndago), Vijiji vya Simbalungwale, Mkulu, Motomoto, Kizaga (Kata ya Ulemo) kadhalika vijiji vya Kibigiri, Mgongo (Kituo cha Afya), Kizonzo, Mseko na Malendi (Kata ya Shelui). Vijiji hivi vyote vimepitiwa na njia ya umeme uliopozwa kwa nini hadi sasa vijiji hivi havipatiwi umeme? Naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya kina kwa nini muda mrefu Wizara imekuwa ikiahidi kufikisha umeme katika vijiji hivi lakini ahadi zimekuwa hewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kuingiza umeme majumbani upo ghali sana, kwa kuwa Serikali imeazimia kubadili matumizi ya nishati kutoka nishati ya kuni kuingia nishati ya umeme hivyo ni muhimu Serikali kuona umuhimu katika kuwapunguzia gharama wananchi kuingiza umeme. Gharama za nguzo na nyaya sio suala sahihi kumbebesha mtumiaji kwani kufanya hivyo ni kumwibia mteja kwani nguzo na nyaya ni mali ya *TANESCO*.

Kuhusu tatizo la kijiji cha Maluga kuhusu wachimbaji wadogo wadogo wanaohitaji eneo hilo kuliendeleza kwa nini Wizara inaendelea kumpatia leseni mtu asiye tayari kuliendeleza eneo hilo? Naomba Waziri wakati anatoa majibu anipe maelezo juu ya mmiliki wa eneo hilo kwani upo utata mkubwa wananchi kumfahamu mwekezaji aliyepewa leseni kuliendeleza eneo hilo. Machimbo ya Sekenke (Ngonkilangi) eneo hilo limeuzwa kinyemela na hivyo kulazimisha wakazi waliokuwa wamekaa eneo hilo kutakiwa kuondoka kwa nini wakati eneo hilo linauzwa wamiliki hawa kuwashirikisha wakazi wa eneo hilo? Kitendo cha kuuzwa eneo hilo kinyemela kimeleta shaka, naomba maelezo kuhusu hali hiyo machimboni Sekenke kwani wananchi wanahangaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EWURA*, chakachua ikomeshwe kwa kufungia baadhi ya vituo hasa vile vinavyoota kama uyoga, vile vilivyopo baina ya Kibaha na Chalinze. Mafuta ya taa yauzwe na Serikali. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa A. Malima, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kazi kubwa ya kuhakikisha Watanzania wananufaika na nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekubali kushiriki katika kuzalisha umeme, nami ni mmoja ya walioshiriki ziara nchini Malaysia kuona na kujifunza jinsi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inavyoshiriki katika uzalishaji umeme. Katika ziara hiyo, TPDC, Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ilishiriki na kuonesha nia ya ya kuingia mkataba na Serikali na kuanza mara moja kazi ya kuzalisha umeme. Je, makubaliano baina ya Serikali, *TPDC* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi tunaambiwa kuwa umeme wa jua ni rahisi katika matumizi, kama ni kweli kwa nini Serikali haijaweka umeme wa jua katika shule zetu za sekondari badala ya kung'ang'ania kupata umeme ghali wa *TANESCO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme unaotumiwa na Watanzania, ni ghali kutokana na madeni makubwa iliyobebeshwa *TANESCO*, kwa mfano malipo kwa *IPTL*, Richmond na kadhalika. Kwa nini Serikali haichukui madeni hayo kwa *TANESCO* ili umeme uwe rahisi na wananchi walio wengi wamudu kutumia umeme? Nguzo za umeme ni za *TANESCO*, mita za umeme ni za *TANESCO*, kwa nini mwananchi abebeshwe mzigo wa kulipia nguzo, mita katika kuweka umeme kwenye majumba yao? Kama kuna ulazima wa kubeba bei ya nguzo na mita, kwa nini mwananchi asilipe kidogo kidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya mafuta yanayochakachua mafuta, yanawasababishia hasara kubwa Watanzania walio maskini, wanaodunduliza pesa kupata magari. Nashauri Sheria/Kanuni za adhabu zirejewe upya ili adhabu kali za kufungwa kwa kituo au kufungwa mmiliki wa kituo ziwepo ili wachakachuaji waogope. Faini ya shilingi milioni kumi ni kidogo sana kwa matajiri hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TBA warejeshe nyumba za *STAMICO* walizochukua wakati Serikali ilipotaka kubinafsisha *STAMICO*. Nawapongeza viongozi wa *STAMICO* pamoja na wafanyakazi kwa kuifufu *STAMICO*.

Mheshimiwa William Ngeleja, hongera kwa hotuba nzuri ya Bajeti. Nakuombea kwa Mungu mambo yaende vizuri katika Bajeti yako leo. Pamoja na pongezi hizo naomba kujua hatma ya barua niliyokuletea ya Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Chamwino. Ombi lake la *TANESCO* kumwekea umeme nyumbani kwake Chamwino Ikulu (kama barua yake inavyojieleza). Tafadhali sana Mheshimiwa William Ngeleja mdogo wangu naomba majibu ya barua hiyo laa sivyo sipati kura za Chamwino. Hupendi nirudi Bungeni ndugu yangu? Naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake mzuri kwa kuyatambua madini ya *Tanzanite* kuwa madini maalum na pekee duniani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha madini haya yanalindwa na kupewa heshima kuliko madini yote ya vito duniani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ule mnada wa madini uliokuwa ukifanyika Arusha na kuleta wageni wengi kutoka

sehemu mbalimbali duniani na kuingizia Taifa fedha nyingi, je, Serikali iko tayari kurudisha mnada wa madini Arusha? Naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa Bajeti 2008/2009 Wizara ilitangaza Tarafa za Idodi *(Ruaha National Park),* Tarafa ya Pawaga na baadhi ya vijiji vya Tarafa ya Ismani vitapewa umeme wa *MCC* kwa bahati mbaya Bajeti ya *MCC* haikutosha ndipo katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 Waziri, Ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja baada ya kushauriana na wataalam wake walikubali kufanya mabadiliko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *MCC* ubaki na vijiji vifuatavyo; Igingilanyi, Kisinga, Ilambilole, Mkungugu, Ndolela, Ismani Tarafani, *Ismani Mission,* Kihorogota hadi Nyang'oro. Nashukuru hatua za awali zimefanyika za tathimini na upimaji. Nitashukuru kupata ratiba ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *REA* umeme kuelekea *Ruaha National Park* utatekelezwa na *REA* na Mheshimiwa Rais pia aliahidi, ingawa Mheshimiwa William Ngeleja alikwishakubali na kukubaliana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *DVD* yenye hotuba zote za Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri zipo ninazo. Uamuzi huo ulikuwa ni kupeleka umeme wa *REA* katika Tarafa za Idodi na Pawaga katika vijiji vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idodi ni katika vijiji vya Nyawahana/Mlowe (Malinzanga) Sekondari Malinzanga, Idodi, Mapogoro, *Kitanewa Mission* na Tungamelenga. Nashukuru sana *REA* wameshapima na sasa wanasema wanaanza kuchukua hatua za kupeleka nguzo. Naomba kazi hizo zifanyike haraka kwani zile alama zimeanza kuliwa na mchwa. Naunga mkono hatua ya kuanza mradi huu kuanzia kijiji cha Nyamihuu badala ya Tagamenda, kwani itapunguza gharama toka mabilioni hadi kiasi cha milioni mia nne tu nilivyoambiwa. Mungu akubariki Mheshimiwa Ngeleja, *TANESCO* na *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiit, eneo la Pawaga, umeme kwenda Tarafa hii inayozalisha mpunga mwingi katika Mikoa ya Iringa na Njombe, umeahidiwa na Mheshimiwa Waziri wakiwepo *REA* na mimi kwamba sasa utatekelezwa na *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni kuwa pamoja na kwamba hatua za awali ni kuchukua umeme Tagamenda, nashauri sasa *REA/TANESCO* ichukue umeme toka Mlowa (Malinzanga) ivushe Pawaga kuanzia kijiji cha Luganga, Magozi, Ilolo mpya, Sekeondari ya William Lukuvi, Mkombilenga, Sekondari ya Pawaga, Mboliboli, Kituo cha Afya cha KKKT – Mboliboli, Itunundu, Kimendi, Mbuyuni. Njia hii ni fupi kwa asilimia zaidi ya 50 ukilinganisha na ile ya Tagamenda – Kiwere – Luganga – Pawaga. Kwa hiyo, Kituo cha Mlowa (Malinzanga) kiimarishwe ili kisambaze umeme katika Tarafa ya Pawaga kupitia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiit, kwa niaba yangu na wananchi wa Iringa hususani Jimbo la Ismani nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri, *TANESCO, REA* na Wizara kwa nia njema na uungwana. Nawaomba tu Mungu awabariki wote ili mkamilishe ahadi hizo. Mheshimiwa Waziri ni mdogo wangu nampenda sana, Naibu Waziri ni mjomba wangu kabisa. Sisi na wapenda maendeleo wote tunawaunga mkono sana. Kazi ni ngumu lakini mnajitahidi. Viongozi wa *TANESCO* na *REA* ni rafiki zangu. Hongereni sana watendaji wa Wizara wakiongozwa na ndugu yangu David Jairo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri uniandikie tu mimi kunipa maandishi yanayothibitisha nia yake njema kwa Ismani *(MCC),* Idodi na Pawaga *(REA)* sihitaji mpate taabu ya kunijibu humu Bungeni bali nipeni barua tu Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM itashinda kwa jitihada zenu. Mbarikiwe sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Majibu kwa barua tu msisumbuke hapa Bungeni.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Bunge la Tanzania kwa kupitisha Sheria ya Umeme ya mwaka 2008. Lakini katika Sheria hii, kipengele S.41(7) kinakinzana na maana nzima ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina upungufu mkubwa wa nishati hii. Kipengele hiki kinazuia uzalishaji wa umeme *(Independent Power Producers - IPPs*) kwa miaka mitano. Naishauri Serikali ilete haraka marekebisho ya sheria hii ili kuondoa kipengele hicho ambacho kinaipelekea nchi kutojinasua katika tatizo lake sugu la kukatika katika umeme *(black outs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa *MCC.* Mradi huu umekuwa kama mchezo wa kuigiza kwani wananchi kama wa Jimbo la Nyang'hwale Serikali kupitia Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa nyakati tofauti na mara nyingi wamekuwa wakitoa tarehe za kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vya Kharumwa, Nyijundu, Nyanibele hadi Nyang'hwale hadi sasa hivi hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika kujibu hoja, Mheshimiwa Waziri atie msisitizo juu ya uhakika wa tarehe ya kutekeleza mradi huu sasa.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimwa Waziri kwa hotuba nzuri. Nitagusa masuala machache tu kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uamuzi wa Serikali wa kusitisha usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi nje ya nchi. Huu ni uamuzi mkubwa na muhimu sana ambao utatoa ajira zaidi kwa Watanzania katika viwanda vingi vitavyoanzishwa nchini vya kukata na kusanifu madini ya *Tanzanite.* Mapendekezo ya Kamati ya Nishati na Madini yaliyoridhiwa na Bunge yalitaka usafirishaji wa madini ghafi yote ya vito (si *Tanzanite*

pekee) usitishwe. Tuna madini ya vito zaidi ya kumi Tanzania na zaidi ya asilimia 95 yanasafirishwa nje ya nchi yakiwa ghafi, hivyo kwa bei ndogo sana! Swali langu kwa Waziri ni nini kinatuzuia kusitisha usafirishaji nje ya nchi wa madini ghafi ya vito yote? Ukurasa wa 38 wa hotuba ya Waziri unasema bado hatuna uwezo wa kuyaongeza thamani madini hayo nchini tutapata wapi uwezo kama hatuanzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile pamoja na kusitisha usafirishaji wa *Tanzanite* ghafi, bado tunaruhusu *Tanzanite* ghafi yenye michongo ya asili isafirishwe. Shida iko wapi kubakiza *Tanzanite* ghafi yenye michongo ya asili hapa hapa nchini ili wenye mahitaji waje kwenye soko lenyewe, waje nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili suala la malipo ya wafanyakazi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira, limekuwa fedheha kubwa sasa. Mwanzoni wafanyakazi karibu 500 na familia zao walikaa miezi 15 bila mishahara. Wakalipwa mwaka jana, lakini tangu walipwe huu ni mwezi wa tisa hawajalipwa mishahara. Kwa kuwa mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa Mgodi wa Kiwira, Serikali itoe kipaumbele kwa malipo hayo ya wafanyakazi,

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, suala la matumizi ya *X–ray Scanners* kwa wafanyakazi, *Tanzanite One,* napenda kusema ni aibu, ni fedheha kubwa kwa Taifa lililopata Uhuru miaka 49 iliyopita, kuruhusu mashine iliyotengenezwa kwa ajili ya kupimia mizigo, kutumika kupimia wananchi, si haki wala si halali. Ikiwa *Tanzanite One* hawawezi kuchimba madini bila kuwakaanga vijana wetu kwa mashine hizo basi waondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amezungumzia mambo 56 lakini niseme mawili tu. Jambo la kwanza ni kuhusu umeme vijijini. Tangu Sheria ile ya Umeme Vijijni imeundwa, sijaona matakeo yake. Tunahitaji umeme Ruangwa, Lindi na Liwale, umeme ni wa shida sana. Ni lini tutasaidiwa umeme katika maeneo hayo? Tulitegemea umeme utakuwepo Lindi Mkoani, baada ya kuwa na gesi Kilwa Songosongo na Mtwara lakini ni tofauti. Naomba tusaidiane umeme Mkoa wa Lindi. Vijana tunawaenzi na tunawathamini tusaidiwe umeme Lindi, Ruangwa, Nachingwea na Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu madini. Madini yaliyopo Mkoa wa Lindi ni mengi sana. Tunaomba Serikali mtusaidie, kuna madini kadhaa nchini angalau Lindi tu tusaidiwe wachimbaji wadogo kuna dhahabu Nachingwea kama ifuatavyo; Ruangwa – *green garnet, green tomaline,* dhahabu, unga wa kupaka kuta wa rangi mbalimbali, *gypsum,* Lindi Vijijini *gypsum* na gesi asilia – Kilwa. Wasaidieni wachimbaji wadogo wadogo.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Naomba kufahamu iwapo ahadi ya

umeme Malibwi, Mlola na Ngwelo mwaka 2010/2011 imezingatiwa katika Bajeti ya mwaka huu. Naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba nzuri na pia shukrani za pekee ziwaendee Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa ushirikiano mkubwa nilioupata kwa kipindi chote cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa inayonisumbua mimi pamoja na wananchi ni kutokuwa na umeme. Nashukuru jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali za kuleta umeme, lakini ahadi hii imechukua muda mrefu sana jambo ambalo linatupa wasiwasi. Naomba nipate maelezo ya kina na ufafanuzi ili wananchi wafahamu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa *MCC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila umeme hatuwezi kupiga hatua za kimaendeleo. Tukizungumzia viwanda vidogo haviwezekani bila ya kuwa na umeme. Shule zetu za sekondari pamoja na vituo vya afya na zahanati vyote vinahitaji umeme ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma. Uchimbaji wa madini unahitaji umeme. Hivyo basi naiomba Serikali ilishughulikie suala hili kwa haraka ili kuweza kuchochea maendeleo katika Jimbo la Busanda, Wilaya na Mkoa wa Geita kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya pili inawagusa wachimbaji wadogo wa madini ambao kwa hali ya kawaida wanafanya shughuli zao kwa taabu sana maana vifaa vyao vya uchimbaji ni duni sana kiasi kwamba wanakuwa katika hatari ya kupata ajali. Mfano halisi ni ile ajali iyotokea Sobora, Kata ya Kaseme ambapo watu walipoteza maisha. Wachimbaji hawa hawana mtaji hata wanapokwenda Benki hawakopesheki kwa kuwa Serikali imeamua kuwasaidia wachimbaji wadogo, naomba iangalie kuboresha yafuatayo:-

Jambo la kwanza, utengwe mfuko maalum kwa ajili ya kuwaelimisha wachimbaji wadogo juu ya teknolojia mpya ya namna ya kuchimba madini kwa urahisi na kwa utaalam na la pili, Wizara itenge mfuko maalum kwa ajili ya kuwakopesha wananchi hawa ili wanunue vifaa vya kisasa vya kuchimba madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mfuko maalum kwa wachimbaji wadogo bado napata wasiwasi namna ya kupata fedha hizi. Hivyo naiomba Wizara iweke utaratibu rahisi na mzuri wa namna ya kuwafikia moja kwa moja wananchi hawa maana katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo. Utaratibu uliotumika wa kutangaza zabuni, mimi pamoja na wananchi wa kule chini ilikuwa vigumu kupata taarifa. Cha pili kuhusu kuandika *proposal,* wananchi wengi hawawezi hivyo walikwama kutuma maombi yao. Matokeo yake wale wanaofaidi si wale walengwa halisi wa mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa Sheria mpya ya Madini ya mwaka 2010 ambayo imeweka bayana namna ya wachimbaji wadogo watakavyowezeshwa. Kwa sheria hii sisi tumefurahi sana na kuipongeza hatua hii.

Ninachoomba ni kwamba Wizara iandae mipango mahususi namna ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikitekeleza mipango yake kwa kuzingatia mambo niliyotaja hapo juu ni matumaini makubwa tutaweza kukuza uchumi wa wananchi, tutachangia Pato la Taifa na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangulize pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake. Pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya Mwenyezi Mungu awazidishie afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni Bagamoyo tunashukuru sana kwa kupata umeme kwa laini mpya inayoenda sambamba na barabara ya Bagamoyo – Dar es Salaam. Mradi huu umewezesha vijiji vingi vilivyopitiwa na laini hiyo kupata umeme. Changamoto za vijiji vya Bagamoyo katika Jimbo la Bagamoyo ni kukosa huduma ya umeme. *REA* haijaliona Jimbo la Bagamoyo. Vijiji vinavyokuwa kama vile kijiji cha Pande na Buma havina huduma ya umeme pamoja na kilio cha muda mrefu.

Pili shule zetu za sekondari za Kata Sanzale, Vigwaza na Dunda ziko jirani sana na gridi, lakini gharama za uunganishwaji ziko juu sana kiasi cha kusababisha kukosa umeme katika shule hizo. Shule zimetakiwa kulipa gharama za ununuzi wa transfoma. Maombi yangu ni kuwa gharama hizi zisibebeshwe shule zetu. Uwepo wa transfoma utawezesha uunganishaji wateja wengine zaidi ya shule. Serikali/*TANESCO* ilipie gharama za miundombinu ili shule zetu zipate umeme na kusogeza mbele vita yetu ya kumuelimisha mtoto wa Tanzania. Hili lifanywe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam kwa hotuba nzuri. Je, ni lini mradi wa *MCC line* ya Matui, Nguzero na Dosidosi utaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kuunganishiwa umeme bado ni za juu sana na wananchi wengi wanashindwa kumudu pia gharama za nguzo zinazotakiwa anazotozwa mlaji ni juu na siyo haki gharama hizi kutozwa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa *Prospecting Mining Licence* zitolewe kwa uangalifu mkubwa. Kijiji cha Kijungu Wilayani Kiteto, ardhi yake yote imepimwa kwa kampuni moja kwa ajili ya *Prospecting Mining Licence* bila ya wananchi kutoa ridhaa yao. Naomba hii *mining prospecting licence* iwe *revoked.*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Wizara ina uwezo pamoja na viongozi wake tena vijana wa kisasa suala la uchakachuaji mafuta ni aibu ya Wizara na Tanzania. Wizara inawadekeza watu hawa wanatuletea aibu mpaka Ikulu. Hawa ni wahujumu uchumi. Sheria ya Uhujumu Uchumi ipo itumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabalozi sasa wanafikiria kuanzisha visima vyao na kuagiza mafuta peke yao. Toa tamko kali Waziri leo la kuondoa hii aibu ya ofisi yako.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha Bajeti nzuri na naunga mkono. Sambamba na kuunga mkono naomba kupatiwa ufafanuzi ni lini umeme wa maeneo haya utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kutoka Lamadi hadi Kalemela, Nyamikoma na Nyashumo mradi huu unaanza lini? Pili, umeme kutoka Lamadi kwenda Mkula hadi *Ngasamo Ginnery* utaanza lini kutekelezwa? Na tatu umeme kutoka Nyashimo, Shigala hadi Igalukilo nao utaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho aainishe ni lini miradi hii itaanza kutekelezwa kwani imechukua muda mrefu sana bila ya ahadi za mara kwa mara za Serikali hapa Bungeni na hata kwa wananchi. Na yote, ningefurahi kusikia kuwa nguzo za umeme zinaanza kuwekwa *site* kuanzia wiki ijayo. Naunga mkono hoja.

**MHE. MCH. DR. GERTRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa hotuba yao nzuri inayokidhi mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie vipengele vichache ili kukazia na kushauri Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchakachuaji wa mafuta ni aibu, ni suala linalohitaji ufumbuzi wa kudumu, ahsante kwa kulishughulikia. Vituo vilivyofungwa visifunguliwe kabisa ili iwe fundisho, pia kodi ya mafuta ya taa iongezwe bila huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa nia ya kuboresha *Arusha Gemstone Centre* kwa kuwapatia *machine* zaidi na wakufunzi zaidi. Hiyo itatusaidia kupata faida kwa wingi na ongezeko la thamani ya madini yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mitaji, inaweza kusaidia wachimbaji wadogo wadogo kuinuka kiuchumi, lizingatiwe. Mheshimiwa Mwenyekiti, nafarijika kuona umeme unaendelea kusambazwa. Tunaridhika sana na juhudi zenu. Mwisho ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wachakachuaji wa mafuta ni wahujumu uchumi. Hatua kali inapaswa kuchukuliwa dhidi ya watu hawa kwani bila ya hatua kali hali hii itakuwa ni tatizo la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni moja katika mahitaji muhimu na ya lazima kwa maendeleo ya Watanzania. Serikali ina mikakati gani itakayohakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika mijini na vijijni na kwa bei nafuu ili watu wote au wengi waweze kuutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe elimu kuhusu upunguzaji wa matumizi ya kuni na mkaa ili kupunguza uharibifu wa mazingira na badala yake watumie majiko sanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wapewe elimu na wahamasishwe kuhusu matumizi ya gesi.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupitisha Muswada wa Sheria ya Madini kuwa madini ya vito yachimbwe na wazalendo. Wachimbaji wadogo wadogo na wafanyabiashara ya madini wamefarijika kwa kiasi kikubwa na kwamba jambo hili litaongeza ajira kwa vijana wa Kitanzania na kwa kuwa kuna taarifa iliyoandikwa na Jarida la *Business Day* la mwezi Mei, 2010 likielezea bayana kuwa Sheria Mpya ya Madini iliyopitishwa haitawagusa Kampuni ya *Tanzanite One* juu ya umiliki wa migodi yao iliyoko Mererani Wilaya ya Simanjiro. Je, Serikali inasemaje juu ya taarifa kama hizo?

**MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri na pia kwa kufanya kazi kwa bidii, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni mawili, la kwanza ni kuhusu uchakachuaji wa mafuta kwa kweli wafanyabiashara wamekuwa sio waaminifu, hawa ni wezi na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni wizi wa mafuta kiujanja kwa kuweka upepo badala ya mafuta, kwa mfano gari ina uwezo wa lita 83, wakiweka mafuta ule mshale unaenda mpaka lita 97 huu ni wizi, hii imenikuta mara kadhaa na vituo hivyo vipo vingi vinavyofanya wizi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuiomba Serikali kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kutenga maeneo rasmi kwa ajili yao. Naipongeza Serikali kwa kutenga maeneo sehemu mbalimbali nchini, Wilayani Same na Mkoani Kigoma maeneo zaidi yatengwe kwa ajili yao kama nilivyosema awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono haja.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondokana na tatizo la kuchakachua, hivi sasa hali ya bei ilivyo na kodi zake ni kuwa Petroli *(MSP)*shilingi 1,538 – 1,654 na kodi shilingi 539. Dizeli *(GO)*shilingi 1,530 – 1,645 na kodi shilingi 514 na mafuta ya taa *(IK)* shilingi 1,066 – 1,146 na kodi ni shilingi 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri aunguze kodi kwenye petroli na dizeli kwa shilingi 150. Kodi itashuka kwa petroli shilingi 389 na dizeli shilingi 364. Pia apandishe kodi ya mafuta ya taa shilingi 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza bei mpya kwa mafuta ya petroli *(MSP)* shilingi 1,388, dizeli *(GO)* shilingi 1,380 na mafuta ya taa *(IK)* shilingi 1,366. Naomba Wizara iwawezeshe *TPDC* ili gesi itumike vijijini kama nishati mbadala ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vijiji vifuatavyo katika Wilaya ya Pangani vipate umeme ambavyo ni Kijiji cha Mkalamo, Kijiji cha Masaika, Kijiji cha Mivumoni, Kijiji cha Kigurusimba na Kijiji cha Choba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nakutakieni kila la kheri na mafanikio. Ahsante.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umeme Makete. Katika mwaka wa fedha 2009 *TANESCO*, zilitengwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ifuatayo ya umeme:-

(i) Kupeleka umeme Kata ya Mfumbi.

(ii) Kupeleka umeme Kata ya Kitulo.

(iii) Kupeleka umeme katika Sekondari ya Matamba na Kijiji cha Kinyika. Hadi leo miradi hii haijatekelezwa. Aidha, nguzo zimeletwa kuanzia mwaka jana Kata ya Kitulo na Mfumbi, lakini ni muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo toka Serikalini kwamba ni lini miradi hii itatekelezwa na sababu zilizokwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya *MCC,* Makete. Miradi ya umeme inayofadhiliwa na *MCC* inachelewa sana. Serikali ifafanue ili wananchi waweze kuelewa sababu za kuchelewa miradi hii. Serikali ni vyema ikatoa ratiba ya utekelezaji wa miradi hii iwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Umeme Vijijini (*REA)*. Wilaya ya Makete ina vijiji 98, Kata 17 lakini hakuna mradi hata mmoja unaofadhiliwa na *REA*. Serikali ieleze vigezo ambavyo *REA* inatumia ku-*short list* miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanya Wilaya nzima kukosa mradi hata mmoja wa umeme vijijini. Napendekeza Serikali au Wizara itoe mkakati wa upelekaji umeme

vijijini unaoonesha kila Kata na Vijiji mpango wa kupeleka umeme ili kila Mkoa, Wilaya wajue na kurahisisha kusubiri bila malalamiko.

Mradi wa umeme, Rumakalya. Katika hotuba ya Waziri, mradi huu mkubwa *(MW 222),* aidha katika mpango mkakati wa Taifa inaonesha mradi huu unatazamiwa kuanza kutoa umeme 2017, lakini hakuna maandalizi yoyote yanayoendelea. Serikali itoe maelezo kuhusu hatua zilizokwishafikiwa kwa sasa.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Mallima pamoja na timu ya wataalam wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Jairo kwa kazi nzuri inayofanyika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba madini ya *Tanzanite* yanapatikana Mkoa wa Manyara lakini biashara yote kwa maana ya usanifu na hata uuzaji inafanywa katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupongeza uamuzi wa Serikali wa kupiga marufuku uuzaji wa *Tanzanite* ambayo haijasafishwa na kuongezewa thamani. Hii itasaidia kukuza uchumi, lakini pia kuongeza ajira kwa vijana hususan wa Mkoa wa Arusha na Mikoa jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara isaidie kutoa elimu ya muda mfupi na mrefu kwa vijana wanaojihusisha na shughuli hizi ili wapate utaalam wa kutosha na kufanya kazi ya ubora na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kukubali kuanzisha rasmi *Gemstone Shows* Mjini Arusha ili kukutanisha wenye vito hivyo na wanunuzi wa Kimataifa. Utaratibu huu utasaidia sana kuboresha shughuli hii ya uongezaji thamani kwani shughuli hii itafanyika kutokana na uhitaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada za Serikali na Wizara katika maeneo ya nishati mbadala na utunzaji wa mazingira. Aidha, napendekeza tume na kikosi kazi ambayo itahusisha wenzetu wa mazingira na wataalam dhidi ya Kamishna Msaidizi wa Nishati Mbadala ili kuwa na uratibu na ku-*share* taarifa kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia kuwapongeza sana Mawaziri pamoja na wataalam wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. LAWRENCE K. MASHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote wakiongozwa na Ndugu David Jairo, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamu maendeleo ya miradi ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Nyamagana kama ambavyo ilitangazwa katika bajeti ya Wizara miaka mitatu iliyopita. Kata zilizoahidiwa umeme ni Kata ya Mkolani, Igoma, Butimba na maeneo ya Buhongwa pamoja na kwamba baadhi ya kazi zilianza bado hazijakamilika. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii na kazi nzuri sana ambazo kwa kipindi hiki cha miaka mitano kazi zilizofanywa na Wizara hii zinaonekana ingawa Wizara ilikuwa na kazi kubwa ya kutatua matatizo mbalimbali yaliyokuwa yanaikabili nchi yetu kupitia Wizara hii hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya kazi kubwa sana ambayo katika historia ya nchi yetu toka tupate uhuru Mikoa ya Kusini ilikuwa na tatizo kubwa sana la umeme lakini kupitia uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi mahiri wa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara hii ya Nishati na Madini Mikoa ya Mtwara na Lindi tumeweza kupata umeme wa gesi wa Mnazi Bay kupitia Kampuni ya *ARTUMAS,* umeme ambao mikoa hii inatarajia kupata hadi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme kufika vijijini ni haki kwa wananchi wote lakini ili kutekeleza suala hili ni lazima Sheria yetu iliyopitishwa 2008, kifungu cha 41 kifungu kidogo cha 7 kiondolewe na kifanyiwe marekebisho ili kuwe na ushindani wa kibiashara kwani kipengele hiki kinatoa uwezo mkubwa kwa *EWURA* kwa kutoa kibali au kutotoa, hivyo tukiendelea kukitumia kifungu hiki suala la usambazaji umeme vijijini litakuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii ililetwa na Bunge na kupitishwa na Bunge. Naomba sana Serikali ifanye haraka kuleta marekebisho hayo katika Bunge hili ili marekebisho yakifanikiwa wananchi wa Mikoa hii wapate matunda ambayo Mikoa mingine wameyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukumbuke kuwa Mikoa ya Kusini inahitaji maendeleo kwa kasi zaidi ili nasi tuweze kuifikia Mikoa ambayo iko mbele kimaendeleo. Tunatambua sana umeme ni sehemu ya kuharakisha maendeleo kwa kasi. Hivyo, Wizara ione umuhimu wa kuweka utaratibu ambao utakuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ombi langu la kurekebisha kifungu cha 41(7). Tunashukuru pia kwa jitihada iliyofanywa na Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kupata mwekezaji ambaye atafanya utafiti wa kuchimba mafuta katika Bahari kule Mtwara.

Hii tunatambua kuwa ajira zitaongezeka lakini pia mafuta yakipatikana Serikali itanufaika kwa kiwango kikubwa na bei ya mafuta inaweza kushuka. Hivyo, naiomba Serikali kutoa ushirikiano kwa kampuni hii ili kuharakisha na kuleta ufanisi katika utafiti huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa hii ya Lindi na Mtwara kuna maeneo mengi ambayo yana madini mbalimbali ambayo hadi sasa kuna wachimbaji wadogo wadogo tu, jambo ambalo Serikali haijatilia sana mkazo juu ya uchimbaji madini katika Mikoa hii. Tunaomba sasa Serikali iwe na mpango madhubuti wa kufanya utafiti wa kina ili kuwe na mpango mzuri wa uchimbaji madini haya kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii muhimu, napongeza kwa mambo machache ambayo yanaendelea kufunga umeme sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi naomba nipate ufafanuzi kuhusu Wilaya nyingi ambazo zina madini kwa nini ndio zinakuwa maskini ukizingatia kuanzia miundombinu yote barabara, umeme, shule na zahanati. Kwa kuwa tuna wawekezaji ambao wanaweza kututengenezea miundombinu yetu au mikataba yetu mibovu inatufanya tuwe maskini? Wawekezaji wana viwanja vyao vya kusafirisha madini, hawatumii barabara zetu, wana zahanati zao kama ni mikataba yetu mibovu, je, wakati sasa umefika wa mikataba yetu kufaidisha wananchi wetu ambao Mungu amewapa mali hizo za madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Geita, Kahama, Shinyanga, Nyalugusu, Nyakagwe, Ngusu , Bukoli na sehemu nyingi sana. Hapa Tanzania tulikwenda Mtwara panapozalisha gesi, ni aibu kubwa umeme unapita kwenye majumba yao, hivi Wizara haioni kuwa ni ubaguzi wa kimakosa kwa Mungu aliyewaumba kuwa na sehemu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo Chunya. Kuna mchimbaji wa madini ambaye ni Mchina, anachimba kwenye mto pamoja na hayo wananchi wanatumia maji hayo. Je, Wizara ina mikakati gani kwa wananchi hao na inasemekana yale maji yana sumu. Naomba ufafanuzi faida kwa wananchi wa Chama cha Mapinduzi, mtakosa kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya wachimbaji wakichimba shimo wanaliacha wazi. Wananchi wetu kwa ajili ya umaskini walio nao wanaingia tena wanafunikwa na wanakufa humo humo na wanaingia kwa kujificha, wanakufa wengi na mashimo mengine wakikuta dhahabu wanauawa wanaacha hivyo hivyo, Wizara ina mikakati gani kuwanusuru wananchi na mmomonyoko na kuhakikisha hawatuachii mashimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa mkaa wa mawe pamoja na chuma Liganga, tumeingia Bunge hili tulitembelea tukaona, tukashauri kuanza mara moja, mpaka sasa hivi sijui Wizara ina mikakati gani kuanza mara moja? Je, kuna maandalizi gani ili kujua sasa wananchi watapata ajira na watafaidika na mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu LUKU Bukoba ni kero, kuna kituo kimoja tu, wananchi wanapata shida kubwa Jumamosi, Jumapili hawana pa kununua umeme, kiko *TANESCO* tu. Je, Wizara inawasaidiaje wananchi hao? Tunaomba msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa wawekezaji, wanavyonyanyasa wafanyakazi wanaowaajiri, tulitembelea Mererani, Arusha, machimbo ya *Tanzanite* wanateseka sana wanawadhalilisha wanawake, wanawavua nguo, tena si mwanamke kwa mwanamke ni wanaume, je, Wizara inajua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kuwa matatizo katika machimbo ya Wilaya ya Mpwapwa, Mkatanini. Kuna matatizo ya wachimbaji wadogo pamoja na wanaovamia machimbo hayo, inasemekana kuna wanaochimba kwa kukiuka Sheria ya Madini, wananchi wengi wanalalamika hawatumaini kifungu cha madini Na.14 cha Sheria ya Madini, Sura 123 wengi wao wachimbaji haramu hawafuati sheria hizo, wananchi wanalalamika. Je, hao waliundwa na nani ambao wana jeuri?

Je, Wizara inajua yote yanayotendeka huko Mpwapwa Mkatanini? Je, kama inajua ilimchukulia hatua gani? Ukitaka kuthibitisha ninayo mambo mengi sana ya unyanyaswaji yanayotendekea huko ambayo sio mazuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafu sehemu zote za machimbo wanatoa vinyesi ovyo, ndio maana magonjwa yanashamiri sana. Shida wanazozipata niliona Arusha na Nyalugusu. Viongozi walioko sehemu hizo walitakiwa kuwawawekea mikakati ya uchimbaji wa choo na kuchimba mbali na wanakoishi ili kupunguza magonjwa, bila hivyo hali ni mbaya sana sehemu zote za migodi.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini sambamba na pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wake. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba katika eneo moja tu la *TPDC*.

Kwanza, kutokana na Shirika hili la Serikali la *TPDC* na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi yetu inabidi shirika hili lisaidiwe sana na Serikali ili liweze kujiendesha kwa faida. Naiomba Serikali ilipatie fedha iliyoahidi *TPDC* ya kujiendesha. Nakusudia Shirika lipatiwe fedha za *Retention* katika mwaka huu wa fedha 2010/2011 na iendelee kupatiwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kutokana na uhaba wa ofisi kwa shirika hili la *TPDC* naiomba Serikali iwapatie sehemu zaidi katika jengo la Benjamin Mkapa (*NSSF*) kwa kuwa jengo hilo lilianzishwa na *TPDC* wenyewe kinyume na hivyo ni kuwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, matumizi ya gesi. Kutokana na kwamba nchi yetu inazalisha gesi kwa wingi na Shirika hili la *TPDC* ndio wanaoshughulika na mafuta

pamoja na gesi. Naishauri Serikali iweze kuhamasisha gesi itumike katika magari hasa katika mradi ambao utaanzishwa katika Jiji la Dar es Salaam wa magari yaendayo kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tutumie *diesel* au *petrol* ambayo tunanunua nje ya nchi tuiache gesi ambayo tunayo kwa wingi hapa Tanzania? Hatuoni kwamba tunakosa mapato ya Serikali kwa kukosa kuuza gesi yetu ambayo tunayo kwa wingi hapa petu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali gesi yetu itumike kwa manufaa ya nchi yetu na siyo kuneemesha nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Shirika la *TPDC* na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuipatia nchi yetu pato kubwa. Kwa hiyo, nasisitiza wasaidiwe kama mashirika mengine. Ahsante.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaunga mkono bajeti hii ningependa kupata msimamo wa Serikali kuhusu hatma ya Buhemba *Mines*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Buhemba umehujumiwa sana. Wananchi wa Musoma Vijijini wamekuwa wakihoji Serikali ni lini watafaidika na mgodi huo. Meremeta ilipoletwa niliitahadharisha Serikali kwamba hao wawekezaji walikuwa bomu. Yametokea. Mgodi huo sasa umeporwa kila kitu, Serikali inaangalia tu. Hivi kweli wananchi wa Musoma watakaa kimya kuona mali zao zinaporwa hivi hivi huku Serikali iko kimya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kwa mara nimekuwa nikimwomba Waziri Mkuu au Waziri wa Nishati na Madini afike pale Buhemba atamke wazi wazi hatma ya Buhemba bila mafanikio. Je, Serikali inawaambiaje wapiga kura wangu kuhusu mkasa wa uwekezaji wa Buhemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wanataka kujua kama mashimo hayo yaliyoachwa wazi na Meremeta yatafunikwa lini? Shule, zahanati, barabara, vyanzo vya maji na mazingira yaliyoharibiwa ni vielelezo kamili kwamba Serikali imewaonea wananchi wa eneo hilo. Je, isingekuwa vyema kwa Serikali kuwapa wananchi wangu *compensation* kwa uharibifu na wizi huo? Ni lini Waziri Mkuu au Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atatembelea mgodi huo na kuwaambia wananchi wangu ni nini wafanye kuhusu ufisadi uliofanywa na unazidi kufanywa Buhemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasubiri maelezo ya Serikali.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napenda kuuliza lini miradi mikubwa ya Mchuchuma na Liganga itaanza na wawekezaji wakubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ukiachia wawekezaji wadogo lini wawekezaji wakubwa wataanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini mradi wa Gridi wa Makambako – Songea – Ludewa utaanza rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kuhusu miradi mitatu ya *REA* kwa Wilaya ya Kongwa 2010/2011. Miradi hiyo ni:-

(i) Kibaigwa – Mgamai – Njoge (Km 18);
(ii) Songambele – Matongoro – Mageseni – Makawa (Km 20); na

(iii) Kibaigwa – Ndurugumi – Laikala (Km 10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana sana naomba ndugu yangu Mheshimiwa Waziri anisaidie.

**MHE. BENSON M, MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kwa nguvu zangu zote kwa sababu zifuatazo:-

(a) Nina imani kubwa na utendaji kazi wa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja, na Naibu Waziri Adam Kighoma Malima, wamekuwa ni mfano wa viongozi vijana wachapakazi na wafuatiliaji wazuri kwa kile wanachoahidi, hivyo ni budi kuiunga mkono hotuba yao ya bajeti.

(b) Watendaji wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara wanajitahidi sana kutekeleza sera ya Taifa ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nielekeze mchango wangu wa maandishi katika maeneo yafuatayo; kwanza, Miradi ya *MCC* – natoa pongezi nyingi kwa kufikiriwa kupewa miradi ya kupeleka umeme katika maeneo yafuatayo kwa mpango na ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation*:-

(a) Umeme – Iyela I – (Jiji la Mbeya);

(b) *Bible School* – Itende – (Jiji la Mbeya);

(c ) Isyesye – (Jiji la Mbeya); na

(d) Ituha II – Tembeta - (Jiji la Mbeya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kusikia tenda ya miradi hii kutekelezwa inafunguliwa leo saa 8 mchana. Hata hivyo, kuchelewa kuanza kwa miradi hii kumeleta kero mno katika Jimbo langu la Mbeya Mjini. Kumekuwa na malalamiko kuwa

imechukua muda mrefu hasa baada ya kuambiwa ingekamilika mwezi Aprili mwaka huu. Nashauri mkandarasi atakayeshinda zabuni aanze kutekeleza mara moja ili kupunguza kelele za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mradi wa Usambazaji Umeme. Ni muda mrefu sasa takriban miaka 10, maeneo ya bonde la Uyole, hasa Kata ya Iduda na Kata ya Iganjo, maeneo haya yameomba kupatiwa umeme miaka tisa sasa, kinachohitajika pale ni transfoma na nguzo ili wananchi wanufaike na huduma hii muhimu. Naamini kuwa safari hii miradi hii itakamilika kikamilifu. Naomba Waziri anihakikishie kuwa maeneo haya kupitia *TANESCO,* Mbeya watapatiwa umeme kwa *TANESCO* Mbeya kupewa bajeti ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Umeme wa Makaa wa Mawe Kiwira. Taifa linatakiwa kufanya uamuzi wa uhakika sasa. Tuna mitambo pale Kiwira mali ya Taifa, tuna rasilimali watu na utaalam wa kutosha wa kufua umeme kutumia makaa ya mawe. Nashauri mambo yafuatayo yafanyike Kiwira:-

(a) Mitambo ianze kufua umeme, Taifa liwekeze katika kuhakikisha Kiwira inatoa zaidi ya megawati 400 – 500 ili kuondoa kabisa tatizo la umeme. Hili ni eneo muhimu kwa sasa, Serikali tujifunze kwa wenzetu wa Afrika Kusini ambao zaidi ya asilimia 80 za umeme hufuliwa kwa kutumia makaa ya mawe;

(b) Rasilimali watu waliopo Kiwira *Coal Mine* walipwe haki zao na waandaliwe kuchukua nafasi yao kikamilifu; na

(c ) Umeme ardhi – *Thermo – Electricity* Songwe. Zipo dalili nzuri sana za kupata umeme kutokana na joto la ardhini pale Songwe – Mbeya, tafiti zinaonesha kuwa nchi zingine kama Kenya zimeanza kutumia nishati hii kwa mafanikio makubwa sana. Tufanye maamuzi sasa ili kutatua tatizo la uhaba wa nishati hii. Eneo hili linafikika kwa urahisi na ni karibu na Uwanja wa Ndege wa Songwe. Katika jambo hili naomba Mawaziri wawe *aggressive* katika kuhakikisha nishati hii inatumika kwa maslahi yetu kama nchi na kama Taifa. Wataalam wetu waende kule Kenya, wakajifunze namna ya kuutumia umeme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa utendaji wao wa kuendeleza sekta hii muhimu katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza, usambazaji wa Umeme Vijijini. Kwa kuwa utafiti wa uzalishaji umeme kwa njia ya maporomoko madogo ya maji umekwishafanyika Wilayani Ileje na kwa kuwa usambazaji wa umeme katika Wilaya ya Ileje umesimama kwa kipindi kirefu,

napenda kufahamishwa *TANESCO* na *REA* wana mipango gani ya kuendeleza usambazaji umeme katika Wilaya yetu ya Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha tena Wizara kwamba Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira upo Wilayani Ileje. Kwa mantiki hiyo ningependa kufahamishwa Wilaya ya Ileje itanufaika vipi na mradi wa kufua umeme katika mgodi huo. Mpaka sasa hakuna manufaa dhahiri yanayopatikana kutokana na rasilimali hiyo muhimu ya makaa iliyopo katika Wilaya yetu. Wananchi waliobahatika kuajiriwa na mgodi huo bado wana matatizo ya malipo ya mishahara yao. Halmashauri ya Wilaya ya Ileje haijaweza kufaidika kupata malipo stahili kutoka mgodi huo. Naomba Wizara ishughulikie maeneo haya ili Wilaya yetu iweze kupata haki yake na kuongeza kasi ya maendeleo kutokana na rasilimali hiyo ya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nishati mbadala. Naipongeza Wizara kwa mipango ya uendelezaji wa nishati jadidifu na mbadala. Kutokana na sera za kujenga shule za sekondari kila Kata na kujenga zahanati kila kijiji na vituo vya afya kila Kata, ingefaa mipango hiyo iwe endelevu na ihusishe Mikoa yote na Wilaya zote, hasa zile ambazo hazijafikiwa na mtandao wa *TANESCO* na *REA* hadi sasa. Suala la uwezo kiuchumi kwa wananchi katika maeneo husika lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuwatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri katika mchakato wa uchaguzi mkuu mwaka huu. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, William Nganga Ngeleja kwa hotuba yake nzuri na kwa kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kilosa lina matatizo ya umeme katika maeneo kadhaa. Naomba *TANESCO* na *REA* watuangalie kwa huruma angalau katika maeneo yenye shule za sekondari na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuwa katika fedha za *MCC*, Kilosa imo. Naomba mradi wa umeme kutoka Dumila hadi Berega Hospitali utekelezwe kikamilifu. Naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni msingi mkubwa wa maendeleo katika karne hii, kwani jamii wanahitaji zaidi katika shughuli zao za maisha ya kila siku. Hivyo basi, ni msingi mkubwa wa maisha hakuna budi sasa nishati hii kusambazwa sehemu zote, mijini na vijijini tena uwe umeme wa uhakika na kuondokana na umeme wa kukatika kwani hutuletea hasara kubwa na uharibifu wa vyombo tunavyotumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kujenga *submarine cable* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja, mradi huu uwe mradi endelevu na kufanyiwa ukarabati mara kwa mara ili kuondokana na tatizo lililojitokeza Unguja kwa kukatika umeme uliochukua

muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati na kuiweka Unguja katika giza zito kwa muda mrefu.

Kuhusu uchakachuaji na bei za mafuta, ni tatizo zito sana ambalo linaleta hasara kubwa sana kwa Taifa letu, kwani bei za mafuta haziendi sambamba na wakati ndio maana kumekuwako na upandaji wa bidhaa hizo ovyo ovyo, uchakachuaji baina ya *petrol* na mafuta ya taa. Jambo hili lazima likemewe na hatua zichukuliwe kukomesha lisitokee tena katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya na mazingira ya binadamu ni bora kuliko kitu chochote katika dunia hii. Migodi mingi huchafua mazingira tena kwa asilimia kubwa bila kujali kama mazingira hayo wanaishi binadamu, ipo haja sasa mazingira yaliyochafuliwa kujengwa upya na wachimba madini wahusika na yale yaliyotokea *North* Mara yasijitokeze tena kwani ni athari kwa wakazi na jamii yote kwa ujumla. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waiziri, Katibu Mkuu, Makamishna na watendaji kwa kuandaa hotuba iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hotuba hii ya 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutembelea Bukombe tarehe 30/06/2010 kutoa majibu yanayohusu lini umeme utawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijitahidi ili ahadi ya kuwaka umeme Bukombe ikamilike 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba Serikali ianze kuweka mpango wa kupeleka umeme maeneo ya Uyovu maarufu kama Runzewe. Hili ni eneo muhimu sana pia liko karibu na Mgodi wa Tulawaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la madini, naomba Serikali iwasaidie mkopo wachimbaji wadogo wadogo wa Katente, Chama cha Wachimba Madini ambao wameleta maombi yao Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia maeneo wachimbaji wa Bukombe. Hata hivyo, ni vizuri Serikali itatue mgogoro uliopo kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa wa Mgodi wa Tulawaka, Serikali isipotatua mgogoro huu ambao umeanza kufuka moshi baadaye yatakuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeza Wizara kwa juhudi kubwa wanazofanya hasa kwa kufuatilia kero za wananchi na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa hitimisho awahakikishie wanachama wa Katente kama watapata mkopo wakitimiza

vigezo. Ni vizuri alihakikishie Bunge hili uwakaji wa umeme Bukombe. Naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutangaza kwamba naunga mkono bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri William M. Ngeleja kwa kazi nzuri sana ya kuleta umeme toka Kenya, Namanga. Mpaka Namanga Tanzania na Makao Makuu ya Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mbunge wa Longido nimetangaza kwenye bajeti ya mwaka 2008/2009 na 2009/2010 kwamba umeme usipofika Longido mwaka huu sitachukua fomu ya kugombea Ubunge kwenye Jimbo la Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hatua nzuri ya kuleta umeme Jimboni kwani umeme umekwishawaka Namanga na kazi kubwa inafanyika kupeleka umeme Longido. Napenda kutoa pongezi kwa ajili ya kuniruhusu kugombea kwani kama siyo juhudi za Wizara hii nisingechukua fomu ya kugombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umeme toka Longido hautaweza kusambazwa Wilaya nzima kutokana na jiografia ya Wilaya. Napenda kukumbusha barua yangu niliyomwandikia kuhusu umeme toka Torokia/Rongai Rombo ambayo ni kilometa kumi tu kufikia Mji mdogo wa Kamwanga, Irkaswa, Lerangwa, Carmolok na Elerai. Pamoja na umeme kutoka Sanya Juu Siha kuunganisha na Vijiji nilivyovitaja vya Jimbo la Siha ziunganishwe na Kijiji cha Tingatinga ambao ni jirani sana na Siha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimueleze Mheshimiwa Waziri, malalamiko ya wananchi wa Jimbo la Longido ni kwamba Majimbo mengine yanayopakana nayo wana umeme lakini umeme haufiki katika Jimbo lao. Naomba sasa Serikali iunganishe umeme toka Rombo ambayo ni karibu sana na umeme toka Sanya Juu kwenda Tingatinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado natoa shukrani kwa niaba ya wananchi wa Wilaya yangu kwa shughuli nzuri sana inayoendelea Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Mungu awabariki watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naomba ufafanuzi kwa masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanzaq ni Mradi wa gesi Mnazi Bay. Tungependa kupata ukweli wa fedha za *ORET* ambazo zingesaidia kupunguza bei ya kuunganisha

umeme wa mradi huu. Je, ni kweli *EWURA* imesua sua hadi *deadline* tuliyowekewa ya Mei, 2010 ikapita?

Je, Serikali ina mpango gani wa kupata fedha nje ya ile *ORET* ambayo ingewanufaisha sana wakazi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara? Je, kuna mpango gani wa kupeleka umeme huo hadi Tunduru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu nishati mbadala. Kutokana na mibono, tumefikia wapi? Kuna mashamba mangapi ya mibono? Kwa nini wawekezaji wa kilimo cha mibono wanazungushwa sana kupata ardhi ya kilimo hiki, katika baadhi ya Mikoa na Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, gesi ya kupikia majumbani. Je, wanaopenda kuunganishwa na gasi ya kupikia hasa katika Jiji la Dar es Salaam afanye nini ili apate huduma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kusiwe na sheria ya kulazimisha ujenzi wa nyumba mpya hasa Dar es Salaam na Mikoa inakopatikana gesi ili nyumba ziwekewe miundombinu ya kupitisha gesi ya kupikia? Kama hilo haliwezekani, je, mtu binafsi anayetaka kujijengea miundombinu hiyo atapata wapi ushauri na kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono tena hoja hii.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera hongera sana kwa kutekeleza ahadi ya Serikali, Kigoma Mjini tumepata umeme!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TANESCO* Kigoma waache kunyanyasa watu. Wapeleke umeme Buhanda Businde, Kagera, Burega, Bigabiro *Mission,* Mahembe, Kibirizi na Mji Mpya Katonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchakachuaji wa mafuta ya *diesel* na *petrol* hapa nchini limekuwa kubwa na hata kuota mizizi kutokana na Serikali kutochukua hatua za haraka pale taarifa zinapotolewa juu ya uhujumu unaofanywa na wafanyabiashara. Karibu miaka minne sasa wananchi na Wabunge wameilalamikia Serikali kuhusu magari yao kuharibika kutokana na mafuta machafu, lakini Serikali haikuwahi kutoa tamko hapa Bungeni wala kuweka adhabu kali ya kudhibiti tabia hiyo hadi magari ya Rais yalipopatwa na shuluba ndipo Serikali imeamka! Huu ni udhaifu mkubwa kwa Taifa na ndiyo maana tunasema biashara hii ya uchakachuaji inafanywa na mtandao wa viongozi wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faini iliyowekwa sasa bado ni ndogo kutoa fundisho kwa watakaohusika. Ikiwa mfanyabiashara atachanganya mafuta na kupata

faida ya milioni 10 kwa siku akikamatwa analipa faini ya milioni tano wakati huo huo ameshaleta hasara ya mabilioni kwa kuharibu *engine* za magari, hiyo ni adhabu kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aeleze Bunge ni kwa utaratibu gani Serikali imetoa kibali cha kuchimba madini kwenye mito huko Chunya, Mbeya kwa Kampuni ya Kichina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sheria ipi inaruhusu uchimbaji wa madini kwenye vianzo vya maji? Huu ni mradi wa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu hata uongozi wa Mkoa wa Mbeya haukuwa na ufahamu wa uwepo wa wawekezaji hao wa China. Kwa muda wote wamekaa pale wakichimba madini huku wanaharibu vyanzo vya maji, hakuna pato lolote ambalo Mkoa umefaidika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tathmini ya mazingira iliyofanyika kabla ya uwekezaji kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wananchi kuibua hili tatizo na waandishi wa habari kufika kule ndiyo Mkuu wa Wilaya amesitisha zoezi kuendelea. Barua ya kusitisha uchimbaji huo haieleweki, nini kitafuata baada ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lielezwe nani atawajibika kurudisha hali ya mazingira yaliyoharibiwa vibaya. Tuelewe kama Taifa tumenufaikaje na uchimbaji huo wa madini. Adhabu gani inatolewa kwa wawekezaji hawa waliokiuka taratibu za nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapotoa bei elekezi kwa mafuta hapa nchini mfano *petrol, diezel* na mafuta ya taa, nani anafuatilia kuona kama wafanyabiashara wanatekeleza bei zilizotajwa. Wafanyabiashara wanataka *Super Profit*, nia yao ni faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali imetangaza bei elekezi za mafuta. Wafanyabiashara wengine wanauza bei zao ziko juu na Serikali inajua hilo kwani na magari ya Serikali yanajaza mafuta huko, kwa nini hatua dhidi yao haichukuliwi? Mfano, zipo *Shell* au Vituo vya mafuta wanauza *Diesel* Sh.1,720 – 1,780.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za umeme ni kubwa sana kwa wananchi wa kawaida kuweza kumudu. Gharama zinapanda kila leo maeneo mbalimbali hapa nchini. Mazingira yetu yanazidi kuharibiwa, misitu yetu inapotea kutokana na matumizi makubwa ya mkaa hapa nchini. Hata wananchi wa mjini ambao ndio wenye uwezo zaidi ya asilimia themanini, bado wanategemea mkaa kama nishati hawawezi kumudu gharama za umeme. Je, vipi kwenye miji midogo, au vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia gharama za kuunganisha umeme majumbani pia ni kubwa sana. Vipato vya wananchi wa Tanzania, Serikali inavijua lakini kila leo gharama

zinaongezwa. Kweli kwa mwendo huu ni Watanzania wangapi wataweza kuwasha umeme kwenye nyumba zao?

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na watendaji wao wote kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa kuiwezesha *TANESCO* kufikisha umeme katika Vijiji vya Kondoa na sehemu ya Mamoyo katika (Kata ya Mabwerebwere), Kijiji cha Rivungu (Kata ya Kilangali) na Changarawe, Masanze Sekondari. Baada ya kupeleka umeme katika vijiji hivi mwisho wa mwaka 2009, usambazaji umeme katika vijiji vingine vilivyofanyiwa *Survey* na kupangwa kutekelezwa, utekelezaji umesimama kabisa kwa sababu zisizoeleweka. Vijiji hivyo ni Zombo, Ulaya Kibaoni na Ulaya Mbuyuni, Kisanga, (Msolwa Sekondari na Msange (Kata ya Kisanga). Dhana nzima inayostahili kupelekwa umeme huko ni kufanikisha utekelezaji wa Kilimo Kwanza, hususan kwa kukoboa na kusaga mahindi na mpunga ambao hulimwa mra mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijji vingine vinavyohitaji kipaumbele ambavyo *survey* ilifanyika ni Kijiji cha Kidogobasi (Kata ya Ruhembe) na Msowero (Kata ya Kidodi). Vijiji hivi viko jirani na vijiji ambavyo vina umeme tayari jirani na Kituo cha umeme cha Kidatu, katika eneo la mashamba ya wakulima wa miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha hoja hii atoe tamko ni kwa sababu zipi usambazaji umeme katika vijiji tajwa umesimama na ni lini miradi hii itaendelea. Naunga mkono hoja.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuwapongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani pamoja na Mashirika yake yote, kwa kazi nzuri ya matayarisho ya bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa shughuli zilizoko chini ya Wizara hii hazihitaji kusisitizwa. Aidha, haipendezi kuona kwamba Taifa letu bado halijaweza kuzitumia fursa mbalimbali tulizonazo za vyanzo vya nishati na madini. Nchi yetu ingeweza/inaweza kuzalisha umeme wa kutosha kwa matumizi yetu na ziada ya kuuza nje. Mpaka sasa hatujaweza hata kutosheleza mahitaji yetu ya umeme hapa Tanzania. Ni lazima tubadilike kwa kuhakikisha kwamba tunawekeza ipasavyo katika kuendeleza vyanzo mbalimbali vya uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria mpya ya Umeme *(Electricity Act, 2008,)* ianze kutumika haraka ili sekta binafsi iweze kuruhusiwa kushiriki rasmi katika uzalishaji wa umeme. Aidha, kuna haja ya kimkakati ya kubadilisha muundo wa *TANESCO* ili kutenganisha majukumu yake ya uzalishaji *(generation),* usafirishaji *(transmission)* na *(distribution)* usambazaji. Mabadiliko haya ya muundo wa *TANESCO* yataongeza tija na ufanisi wa utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini. Mji wa Tabora unazungukwa na Kata kumi na mbili (12) za Vijijini ambazo hazina umeme pamoja na kuwa karibu sana na Mji ambao una umeme wa kutosha kuweza kuzifikia Kata hizi za pembezoni. Kata zinazohusika ni Tumbi, Malolo, Kalunde, Itekemia, Misha, Kabila, Kakola, Ntakuja, Ikomwa, Igosha, Ndevelwa na Honjanda.

Aidha, baadhi ya Kata hizi tayari zinapitiwa na umeme wenye msongo mkubwa toka Tabora – Sikonge, Tabora – Isikizya (Uyui) na toka Tabora – Urambo. Naiomba Wizara iziingize Kata hizi katika mpango wa kuzipatia umeme wa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kuunganisha umeme, nazo ni kubwa kiasi cha wananchi wengi na hasa wa Vijijini kushindwa kuzimudu. Naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza gharama za kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi asilia. Nchi yetu ina hazina kubwa ya gesi asilia ambayo mpaka sasa haijaweza kutumika ipasavyo kwa manufaa ya uchumi wetu. Kwa nini mpaka sasa matumizi ya gesi asilia kwa kuendesha magari na majumbani hayajaanza? Ni lini Serikali itaiwezesha *TPDC* kukamilisha miradi hii mapema iwezekanavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soda Ash ya Lake Natron. Soda Ash iliyoko Lake Natron, ni miongoni mwa rasilimali muhimu sana za nchi hii lakini mpaka sasa nchi yetu inaagiza magadi toka nchi ya jirani na kuacha magadi yaliyopo hapa Tanzania. Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa tathmini ya athari za mazingira ikiwa mradi huu wa magadi ya Lake Natron utaanza kufanya kazi? Tufanye haraka kuanza kuyatumia magadi haya ili tuokoe fedha za kigeni na tuongeze mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya magadi nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakachuaji wa mafuta ya petroli. Tatizo la uchakachuaji wa mafuta, ni kubwa na linaathiri vibaya uchumi wetu. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo imeanza kuzichukua katika kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi ninaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza tofauti kubwa ya bei za mafuta ya taa na dizeli. Hii ndiyo njia rahisi ya kupambana na tatizo hili la uchakachuaji wa mafuta. Aidha, ili kufanikisha zoezi hili, Serikali haina budi kuangalia/kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili kufidia upungufu utakaoletwa na kupunguza kodi katika bidhaa ya dizeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia mchango wangu kwa kusisitiza ombi langu la kupatiwa umeme katika angalau baadhi ya Kata za Vijijini za Mji wa Tabora na hususan zile ambazo tayari ziko kwenye njia kuu za kusafirisha umeme kama vile Itetemia, Malolo, Tumbi, Misha, Kazima na Itonjanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini, kwa kutembelea Jimbo langu la Mtwara Vijijini na kuwapa matumaini wananchi wa Mtwara Vijijini ya upatikanaji wa umeme wa uhakika kwenye Jimbo hili, hasa ukizingatia kuwa gesi ambayo inazalisha umeme kwenye Mkoa wa Mtwara na Lindi inatoka katika Jimbo la Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wakati anahitimisha hoja yake, awaambie wananchi wa Miji ya Nanyamba, Misimbati na Vijiji vyake, ni lini vitakuwa vimepata umeme (umeme utakuwa umewashwa majumbani)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D . J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana rafiki yangu na ndugu yangu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo imetolewa asubuhi hii. Kipekee napenda pia kumpongeza jirani na rafiki yangu, Mheshimiwa Adam Malima, MNEC, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa msaada mkubwa anaompa Waziri mwenye dhamana na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua fursa hii, kuishukuru Wizara chini ya uongozi wa Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kukumbuka kuviingiza baadhi ya Vijiji vya Siha katika mpango wa kupeleka umeme Vijijini. Inatoka chini ya sakafu ya moyo wangu kusema kwamba ahsante kwa Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imetimiza ahadi yake ya kuvipelekea umeme Vijiji vya Donya Moruak, Ngumbaru, Olmelili, Olkolili, Kandashi, Lekrimuni, Mawailiano, Wiri na Magadini. Mungu awabariki na awape maisha marefu. Ahsante, ahsante, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukumbusha kuwa Kijiji cha Embokoi kilidondoka katika orodha hiyo hapo juu. Najua mradi umevitaja hivyo vijiji *"and two other villages"*, nataka niamini kimoja katika hivyo vijiji ni kile cha Embokoi ambacho ni sehemu ya Vijiji vya Donyomoruak na Ngumbaro kabla ya Vijiji hivyo kugawanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba kukumbushia ombi la muda mrefu la kumalizia mradi wa muda mrefu uendao katika Vijiji vya Mese, Samaki, Maini, Nshere – Hehe, Kitongoji cha Kyaboo katika Kijiji cha Mowo Njamu na umeme wa *high tension* uendao Tarafa ya Siha Magharibi *(West Kilimanjaro)* – Ngarenairobi na Ndumeti kwa maana ya Kata ambazo bado haujaanza ingawa umeahidiwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kukumbushia ombi la muda la kufungua Ofisi ya *TANESCO* Wilaya ya Siha. Kwa sasa tuna kituo kidogo kinachotoa huduma katika Mji Mdogo wa Sanya Juu ambacho hakikidhi mahitaji halisi ya Wilaya.

Jitihada za hali ya juu zinafanyika kuona kuwa *NMB* na *CRDB* wanafungua benki Sanya Juu ili kurahisisha ulipaji wa ankara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumshukuru Mheshimiwa William Ngeleja (Mb) na Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima (Mb), kwa kutukumbuka kule Siha. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu ili washinde kwa kishindo katika Majimbo yao ya uchaguzi. Naamini dua na sala zangu/zetu zitakwenda kukubalika mbele ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Ndugu D. Jairo na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuinua pato la Taifa kupitia madini kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, ninawatanguliza kwenye maombi Mheshimiwa William Ngeleja Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii na Mheshimiwa Adamu Kighoma Malima, Naibu Waziri ili wapiga kura wao wawapigie kura za kishindo, warudi madarakani tena kwa nguvu zaidi, kasi zaidi na ari zaidi katika kutekeleza bajeti waliyoiandaa. Ninaimani Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano anatambua uwezo wao ulivyo mkubwa na hekima zao pia katika kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza kaka yangu David Jairo kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu kwenye Wizara hii nyeti na muhimu sana kwa uchumi wa Taifa. Ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu afya, nguvu na ufanisi mkubwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kupitia Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha umeme, ninaipongeza sana Serikali kwa juhudi zake za kupeleka umeme Vijijini kupitia mradi wa *REA*. Kwa kuwa Serikali ilikwishaahidi kupeleka umeme Sepuka, Wilaya ya Singida, Jimbo la Singida Magharibi pamoja na umeme wa kutoka Manyoni kwenda Muhalala, Kilimatinde, Chikuyu hadi Kintinku, zimetengwa kiasi gani na utekelezaji wake ukoje kwani wananchi wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu. Ndio maana hapa Bungeni nimeuliza maswali mara nyingi pamoja na Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, kaka yangu na Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi ambalo ni jipya. Ninasubiri maelezo yenye matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa chumvi Sekenke na Majiri, Manyoni Mashariki. Ninawapongeza sana wanawake, kwa juhudi zao za kuondokana na umaskini kwa kuendesha mradi wa kutengeneza chumvi maeneo ya Nkonkilangi, Tarafa ya Shelui na Kata ya Ntwike na huko Majiri, Tarafa ya Kilimatinde. Kero, chumvi hii huwa haina madini joto, akina mama hawa hawana vitendea kazi na chumvi yao haina soko la

uhakika. Naomba Serikali kuangalia namna ya kusaidia kero nilizoziorodhesha hapo juu ili juhudi za akina mama hawa zizae matunda kwa maslahi ya familia zao na Taifa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya wachimbaji wadogo wadogo wa Sambaru na Londoni. Ni imani yangu Serikali inafahamu kero kubwa iliyojitokeza ya wachimbaji wadogo wadogo wa Vijiji vya Sambaru na Londoni. Ninapenda kuitahadharisha Serikali kuwa kero hii ni kubwa na inatia huruma kwa wachimbaaji ambao wanadai malipo kwa wamiliki wa migodi ya vijiji hivyo hapo juu wa awali baada ya migodi hiyo kununuliwa na wawekezaji wakubwa kisha wawekezaji hao kutoa fidia kwa wamiliki wa awali ambao hawakuwalipa wadau wao yaani wachimbaji wadogo wadogo. Ninaishauri Serikali ili kumaliza kero hii, bora iundwe Kamati Ndogo kufuatilia na kusimamia tatizo hili ili haki itendeke kwani hata wachimbaji wadogo wadogo wako wenye haki hata wanaodanganya pia wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wadogo kuwezeshwa. Vilevile yapo machimbo ambayo bado yanamilikiwa na wachimbaji wadogo wadogo mfano machimbo ya Sekenke, Kibigiri na kadhalika Mkoani Singida. Kwa kuwa ni lengo la Serikali kuwainua Watanzania wote basi ninaishauri Serikali kuwapa mikopo wachimbaji hawa ili waweze kuwa na vitendea kazi vyenye uwezo kulingana na kazi yao. Hii itasaidia hata vijana wetu kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yanayotokana na madini kwa binadamu na wanyama. Kuna taarifa ambazo sio rasmi kuwa ziko athari zinazowapata wananchi kiafya wanaoishi karibu na machimbo au maeneo ambayo kuna madini mfano madini ya *uranium*. Ninaomba utafiti ufanyike ili kuwepo tahadhari ya kuzuia madhara ambayo yanadhaniwa kuwepo hapo baadaye au sasa hasa madini ya *uranium* Wilayani Singida na Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa upepo. Wananchi wa Mkoa wa Singida walifurahi sana waliposikia kuwa kuna upepo unaoweza kuzalisha umeme huko Kititimo, Manispaa ya Singida. Hii itasaidia kusambaza umeme hadi Vijijini kwa urahisi sana vilevile vijana wetu wengi watapata ajira. Ninapenda kujua ni wawekezaji gani wamepata tenda ya mradi wa umeme huu wa upepo na pia vijana na wananchi wangapi wanatarajiwa kupata ajira katika mradi huu mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii kwa moyo mkunjufu nikitegemea majibu au maelezo juu ya hoja mbalimbali kupitia mchango wangu. Pia ninaomba Serikali kuongeza kasi ya kufunga Luku kwenye makazi ya watu ili kuondokana na kero ya kudai *bill* za umeme.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake iliyotayarishwa kwa umahiri mkubwa yenye kuelezea mambo mbalimbali ikiwemo mipango mikakati ya utekelezaji wa mipango mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sitampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamishna wa Madini na Nishati, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii na taasisi zake, kwa kazi nzuri wanayofanya katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa letu na hivyo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni siri iliyowazi kuwa upatikanaji wa nishati, hususan umeme, ni chachu kubwa ya maendeleo ya nchi. Serikali, kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO),* imeandaa mpango kabambe wa usambazaji wa umeme nchini utakaotekelezwa hadi mwaka 2033. Pia kupitia Wakala wa Kusambaza Umeme Vijijini *(REA),* imeandaa mpango mkakati wa kusambaza umeme vijijini ikiwa ni pamoja na umeme mbadala kutokana na vyanzo mbalimblali kama umeme jua, jotoardhi na upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yote miwili, kwa bahati mbaya kabisa pamoja na kilio cha muda mrefu, Jimbo la Mbozi Magharibi (Wilaya Mpya ya Momba), halijajumuishwa katika mpango wowote na hivyo kuashiria kuwa hakutakuwa na mpango wowote wa kufikisha umeme huko kabla ya mwaka 2033. Wananchi hawa, kutokana na hilo wanakosa haki ya msingi ya kupata maendeleo sambamba na wananchi wa sehemu nyingine za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati wa mkutano wa bajeti, niliuliza swali kuhusu mpango wa kupeleka umeme Jimboni kwangu kwa kutumia vyanzo mbadala. Nikajibiwa kuwa suala hili lilikuwa linahitaji utafiti kwani ilikuwa inahitajika kufahamu kiasi cha nishati ya jua inayoweza kupatikana na pia nguvu na mwelekeo wa upepo katika eneo hili.

Naomba kuelewa ni hatua gani zimechukuliwa hadi sasa na ikitiliwa maanani kuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini hapo tarehe 30/10/2009 akiwa ameongozana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitembelea Tarafa moja kati ya nne za Jimbo hili (Wilaya Mpya). Naomba kwa heshima na taadhima nikumbushe kuwa katika Jimbo hili lenye Tarafa nne, Kata 14, Vijiji 85 na Vitongoji 318, kuna umeme katika Kijiji kimoja na Mji Mdogo wa Tunduma tu, ambako nako umeme huo hauwafikii wakazi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la wananchi wangu ni kwamba umeme wa gridi usambazwe zaidi hususani Tarafa mpya ya Tunduma ambayo ni eneo maalum kibiashara kutokana na kuwepo kwenye barabara kuu ya Kaskazini mpakani na nchi ya Zambia. Aidha, kutokana na Jimbo hili kupewa hadhi ya Wilaya, wafikiriwe kupewa umeme kwa Tarafa tatu za Kamsamba, Msangano na Ndalambo kutokana na chanzo chochote kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madini, napenda kuomba Wizara hii ijikite katika utafiti wa kina, kwani eneo hili lina *'potential'* ya madini na vito vya thamani mbalimbali ambavyo, kutokana na hapo awali kutokuwepo miundombinu mizuri ya barabara, havijafanyiwa kazi. Tunaloliona ni watu mbalimbali kufika na kuondoka na madini na vito hivyo kwa madai kuwa wanaenda kuyafanyia upembuzi wa kikemikali

kwa miaka nenda rudi. Kuna uhakika wa uwepo wa *sapphires*, *tormalines, garsets, amethyst, rhodolites* na hata dhahabu mbali na aina maalum kabisa ya mwamba wa marumaru ambao kwa miaka kadhaa ulifanyiwa upimaji bila hata mrabaha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya mwisho ya 1970 na ya mwanzo ya 1980 kulikuwa na utafiti wa mafuta *(petroleum)* kandokando ya Ziwa Rukwa lakini mpaka sasa nini kilipatikana haijaelezwa. Naomba maelezo, kwani wananchi wa Jimbo langu, Kata za Kamsamba na Ivuna pamoja na jirani zetu wa Jimbo la Songwe, Chunya na wa Kwela, Sumbawanga bado hawaelewi ni kitu gani kilitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa wanazozifanya za kuhakikisha kuwa kero zote zilizokuwapo kabla ya kupewa nyadhifa hizo zinaondolewa. Wizara hii kwa miaka mingi ilikuwa midomoni mwa wananchi lakini kutokana na uongozi bora uliokuwapo, sasa Wizara hii haipo tena midomoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Serikali kwa kuwezesha Miji ya Kibiti, Bungu na Mchukwi kupata umeme toka Ikwiriri. Tangu uanze kuwashwa wiki tatu zilizopita, wananchi wamefurahi na *TANESCO* Ikwiriri wameshaanza kuunganisha umeme huo kwa wateja katika Mji wa Kibiti. Naiomba Serikali iongeze kasi ya kuwaunganishia umeme wateja wote walioomba ili waweze kufaidika na nishati hiyo. Aidha, naiomba Serikali isiishie kuwaunganishia umeme wale waliokuwa umbali wa mita 50 toka kwenye njia kubwa bali izidi kupeleka umeme hadi kwa watu walio walau mita 500 ili nao wapate umeme huo. Kwa upande wa Miji ya Bungu na Mchukwi, naiomba Serikali ianze mchakato wa kuunganisha umeme kwa wateja walioomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kujua ni hatua gani sasa zimechukuliwa ili kuwasha umeme kwenye Daraja la Mkapa (Mto Rufiji). Majibu ya Serikali kama yalivyoainishwa katika Kitabu cha Hotuba, ukurasa wa 20, yanaelezea upatikanaji wa Mkandarasi ambaye kwa sasa anaandaa michoro ili kazi hiyo ianze katika mwaka 2010/2011. Ninachotaka kujua ni Mkandarasi yupi aliyepewa dhamana hiyo? Michoro hiyo itakamilika lini na lini ataanza kazi ya kuvusha nyaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa wahanga waliokatiwa mazao yao katika awamu ya pili ili kupisha nguzo za umeme katika Mji wa Bungu, hadi sasa wananchi 24 hawajalipwa fidia zao. Naiomba Serikali ieleze ni lini wananchi hao watapewa fidia hiyo ili kuondoa kero hii kubwa iliyodumu kwa miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira. Najua wazi azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mgodi huu wanapewa *STAMICO* kwa niaba yake, lakini tatizo la Serikali ni kutoa ahadi ambayo utekelezaji wake unachukua muda mrefu na kusababisha Taifa kupata hasara kubwa. Hadi sasa *STAMICO* wako tayari kuanza kazi lakini bado Serikali haijakamilisha hatua zote za kuuchukua mgodi huo toka kwa waliounua. Ni vema kwa Serikali kuharakisha umiliki wake wa mgodi huo ili kuhakikisha kuwa mgodi huo unafanya kazi na hivyo kulipunguzia Taifa hasara ya kuwalipa wafanyakazi wa mgodi huo ambao hawafanyi kazi yoyote lakini bado wanaendelea kulipwa na Serikali. Naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa William M. Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri sana. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwapongeza, Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri, Bwana D. Jairo, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo na watendaji wote wa Wizara, kwa kumsaidia Waziri kwa dhati na uadilifu hadi kumwesha kutoa hoja nzuri sana. Hongereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme wa Mgwashi, Jimbo la Bumbuli ambao utekelezaji wake ulisimamishwa ili nguvu yote ipelekwe Kilindi. Sasa hakuna mvua, naomba ile kazi iendelezwe maana imesimama kwa miezi nane (8) sasa.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ngeleja, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima pamoja na wataalamu wa Wizara, kwa hotuba iliojaa matumaini kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo, sasa napenda kutoa mchango wangu katika Wizara. Watanzania wako wakulima, wafugaji, wavuvi na wako wachimbaji wadogo wadogo. Kwa pamoja, nia ya kazi hizi ni kuwapa uwezo wa kuishi na familia zao. Napata wasiwasi mkubwa juu ya wachimbaji wadogo wadogo huko Mgusu Geita. Wachimbaji hawa walifungiwa kwa muda na nadhani mpaka leo eneo hilo hawajaruhusiwa. Je, ni msaada gani wa Serikali inayotoa kwa watu hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuweza kuikoa Zanzibar kutoka katika himaya ya kuwa kiza. Tendo hili limevifanya visiwa vya Unguja na Pemba sasa kuwa na umeme. Nasema ahsante sana Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali kwa suala hili, kuna msiba badala ya furaha katika visiwa vyetu hivyo. Msiba wetu ni ughali wa umeme wenyewe. Malipo ni makubwa kwa bili za umeme wa majumbani. Pia watu kushindwa kuvuta umeme katika maeneo yao. Tunaiomba Serikali iitazame hali ya maisha ya watu

wengi ambao ni maskini. Mheshimiwa Waziri, tafadhali waonee huruma Watanzania wenzako, umeme ni ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kutoa kauli kuhusiana na tatizo la uchanganyaji wa mafuta ya petroli nchini. Suala hili limeitia Taifa hasara kubwa. Naipongeza *EWURA* kwa jitihada zake za kufuatilia tatizo hili na kugundua udhaifu wa wafanyabiashara wa mafuta hapa nchini na kuweza kutoa hukumu. Hongera Mheshimiwa Ngeleja, hongera Mheshimiwa Malima, hongera wataalamu, hongera *EWURA*. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote wa Wizara na Taasisi na Mashirika yote yaliyopo chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maoni, ushauri na napenda kupata maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mradi wa bomba la Mafuta Dar es Salaam – Mwanza. Njia moja ya kurahisisha usafirishaji wa mafuta kwa gharama nafuu na kwa usalama na kulinda ubora wa mafuta, ni kutekeleza mradi wa usafirishaji wa mafuta kwa njia ya bomba. Kwa kuwa mradi huo ulikuwepo lakini haukutekelezwa, hadi sasa Wizara inasema nini juu ya mpango wa utekelezaji wa mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mradi wa matumizi ya gesi kwa kuendeshea magari. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* lilibuni mradi huo na kufanya majaribio kwa kushirikiana na *Dar es Salaam Institute of Technology*. Watanzania wengi wamekuwa na shauku ya kuona mradi huo unaanza. Wizara itoe maelezo juu ya mkakati wa utekelezaji wa mradi huo ikiwa ni pamoja na usambazaji wa gesi majumbani kwa kuanzia na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mfumo wa *EWURA/TANESCO* kubebesha wananchi kulipia gharama za nguzo na usambazaji umeme. Hivi sasa *TANESCO* inawataka wateja wanaohitaji umeme kulipia gharama zote ikiwa ni pamoja na gharama za nguzo kufuatana na viwango vya Mamlaka ya *EWURA*. Mpango huu sio sahihi kwa sababu kimsingi nguzo ni mali ya *TANESCO* na siyo ya mteja. Tunakaribisha migogoro itakapomlazimu mteja kudai haki ya umiliki wa nguzo alizolipia na kuruhusu wateja wengine kuwekewa umeme kutokana na mkondo uliogharamiwa na mteja mmoja. Ni vema Wizara ikatoa ufafanuzi mzuri juu ya mawazo hayo ya wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, matumizi ya LUKU. Kutokana na mfumo wa sasa wa wasomaji mita kuelemewa na kazi na mara nyingi kuweka hesabu zisizo sahihi kwa wateja, umuhimu wa kutumia LUKU unaongezeka. *TANESCO* itoe mwongozo na utaratibu wa kuweka LUKU kwa watumiaji umeme. Mradi wa LUKU utekelezwe kwa haraka na kwa mpangilio mzuri ili kuwezesha upatikanaji wa LUKU kwa urahisi hasa ukizingatia wateja wa Vijijini watakaokuwa mbali na vituo vya mauzo ya LUKU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumiaji wa LUKU katika Wilaya ya Muheza kwa muda mrefu wamekuwa wakilazimika kwenda kununua LUKU Tanga, zaidi ya kilomita 30. *TANESCO* inasema nini juu ya hali kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kusimama kwa muda mrefu utekelezaji wa miradi ifuatayo Wilaya ya Muheza. Mradi wa Umeme wa Songa Batini. Mradi huu unasimamiwa na *TANESCO* Wilaya ya Korogwe na Mradi wa Umeme wa Bwembwera. Mradi huu unasimamiwa na *TANESCO*, Wilaya ya Korogwe. Maelezo ya watendaji yanaonesha kuwepo kwa upungufu wa nguzo kama ndio chanzo cha miradi hiyo kutoendelezwa. Ni vema *TANESCO* ikaeleza hasa tatizo ni nini na litatatuliwa lini ili wananchi wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ujenzi wa *canopy* kwa Vituo vya Mafuta. Kanuni mpya zinataka vituo vyote vya mafuta kujenga *canopy*. Licha ya kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa kununi hiyo bado vituo vingi havijakamilisha kazi hiyo kutokana na gharama kuwa kubwa. Tunaomba muda huo uongezwe ili kutoa nafasi ya kukamilishwa kwa kanuni hiyo. Wawekezaji binafsi katika sekta hii ya usambazaji wa mafuta wanatumia mitaji yao kujenga vituo vya mafuta badala ya makampuni ya mafuta kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Sheria mpya ya Madini. Dhamira kuu ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutaka kupitiwa kwa Sheria ya Madini na kuiboresha, ilikuwa ni kuona Tanzania inapata pato kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa katika miradi ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kwa Sheria mpya ya Madini kuwezesha wawekezaji waliokuwa na mikataba ya madini kabla ya Sheria mpya kurekebisha viwango vyao katika mikataba ya zamani ili kuwezesha nchi kupata kipato zaidi, kunaendelea kuidhoofisha Tanzania. Wizara lazima iendeleze jitihada za kuwezesha wawekezaji wa zamani ambao ni wengi na wakubwa kuliko wapya watakaokuja upya kuridhia mabadiliko ya Sheria mpya yenye manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanapata umeme na wanafaidi madini yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Watanzania wengi waishio Vijijini wako kizani. Ahadi ya Serikali ni kuwapatia wananchi wa vijijini umeme wa uhakika. Hadi leo zaidi ya Wilaya 10 hazina umeme. Serikali haina budi kuongeza juhudi katika suala hili maana umeme ni maendeleo, bila umeme hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine ni bei au gharama za kuingiza umeme majumbani. Nina ushahidi kuwa gharama za kuingiza umeme nyumbani si chini

ya shilingi milioni moja. Je, itawezekanaje kwa Mtanzania wa Kijijini kumudu kutumia umeme huo hata hapo utakapopelekwa Vijijini kama bei ni kubwa kiasi hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Meremeta. Bunge hili Tukufu limekuwa mara zote linahoji umiliki wa Mgodi wa Meremeta lakini Serikali imeshindwa kutoa maelezo sahihi kwa wananchi. Hata kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka hapa Bungeni kuwa masuala ya Meremeta yanauhusiana na ulinzi na usalama wa nchi lakini bado Watanzania wanataka maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kudhibiti bei ya mafuta zimefanywa na *EWURA* kwa kiasi kikubwa. Lakini Dar es Salaam kwa mfano, bei ya mafuta inatofautina kwa vituo mbalimbali, kwa nini kuwe na tofauti hiyo wakati Dar es Salaam ni moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme Pemba. Naishukuru Serikali ya Muungano na Shirika la *TANESCO* kwa kufanikisha kupeleka umeme Pemba, Kisiwa ambacho kilikuwa gizani kwa miongo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali za sasa kufanya madini yawanufaishe Watanzania wachimbaji wadogo wadogo bado azma hiyo haijafikiwa. Kwa kweli wachimbaji wadogo bado hawana hakika ya ajira hii ambayo inadhibitiwa na wawekezaji wakubwa. Naomba Wizara yako iendelee kuwaandalia mazingira mazuri hawa wachimbaji wadogo ili na wao wafaidi rasilimali za nchi yao.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, *Rural Energy Agency (REA),* ni Kitengo ambacho kama tutakipa uwezo, kinaweza kuleta mapinduzi ya haraka katika dhana nzima ya *rural electrification*. Tanzania ina vyanzo vidogo vidogo vingi ambavyo vinaweza kuzalisha umeme wa tangu Kw50 – Mg1 na zaidi. Pamoja kwamba *REA* inachangiwa kila mwezi kwa watumiaji kukatwa asilimia 3%, kama Sheria ilivyopitishwa, kiasi hiki hakitoshi, kama tunataka matokeo ya haraka katika kuvipatia umeme vijiji vyetu zaidi ya 14,000 nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* imekuwepo tangu uhuru na baada ya miaka yote hiyo, ni asilimia 10% tu ya watu ndiyo wenye kuwa na nishati hiyo ya umeme majumbani. Tangu uhuru hadi leo ni takriban miaka 50 na tumeweza kusambaza kwa asilimia 10% tu. Nchi kama Ghana ambayo imetofautiana na Tanzania kwa miaka minne tu tangu kupata uhuru (Ghana ilipata uhuru mwaka 1957), lakini leo hii watu wake 75% wamepatiwa umeme. Hii inatokana na mipango mikubwa waliyokuwa nayo mara baada ya uhuru *(The Akosambo Dam).* Kwetu sisi mradi kama huo ungefanana na ule wa

Stigler's Gorge, ambao tangu uhuru umebaki katika vitabu tu. Kwa mwendo huu hatutafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba *REA* chini ya *Director General*, Dr. Mwakahesya ipewe support kubwa na Serikali kwa sababu kwanza, Kilimo Kwanza kinategemea umeme ili tuweze kuchochea *Agro-processing industries* kule kule kwenye maeneo ya uzalishaji. Pili, viwanda ni sekta mama katika ukuaji wa uchumi, lakini huwezi kuwa na viwanda bila umeme na tatu ni vizuri basi Wizara hizi tatu, Kilimo, Viwanda Biashara na Masoko na Nishati na Madini wakakaa pamoja ili kupanga vipaumbele vya *electrification* Vijijini, ili kujiandaa na Soko la Pamoja katika nchi za Afrika Mashariki ambalo limezinduliwa rasmi tarehe 1/7/2010. *REA* itathmini vyanzo mbalimbali kila Wilaya ambavyo vitaleta kwa vijiji vyetu nishati hii muhimu. *TANESCO* ibaki kuwa inashughulikia miradi mikubwa kama Stigler's Gorge, Mchuchuma, Kiwira na kadhalika. Katika Wilaya yangu ya Kilombero, kuna maporomoko mengi madogo madogo ambayo yanaweza kuwa chanzo cha umeme. Kwa mfano Mto Sanje, Mto Lumemo, Mto Ruipa, Mto Mngeta, Mto Chita, Mto Udagaji, Mto Kihansi na Mto Mpanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kupeleka umeme Malinyi Wilaya ya Ulanga. Kwanza naishukuru Serikali kwa mradi huu mpya wa kupeleka umeme Wilaya ya Ulanga. Kwa vile chanzo cha umeme ni Wilaya yangu, ni matumaini yangu vijiji vifuatavyo vitakuwa katika programu hii kutoka *Kihansi Hydro Power Plant.* Vijiji hivyo ni Chisano, Ngwai, Kalengakero, Mpanga, Utengule na Ngalimira. Hapa ningetoa angalizo, hasa umeme utakapofika Mpanga. Naomba umeme huu upitie Kijiji cha Utengule badala ya kutoka Mpanga kwenda Ngalimira moja kwa moja na kuvuka Mto kwenda Biro hadi Malinyi. Naomba umeme ukifika Mpanga upitie Shule yetu ya Sekondari na baadaye Kijiji cha Utengule na kisha uvuke Mto Mnyera kwenda Ngalimira hadi Biro mpaka Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, umeme kuelekea barabara ya Mlimba – Ifakara. Sehemu ya Mlimba kwenda Ifakara imepita kwenye Bonde la Mto Kilombero ambalo kwa sasa limefunguka kiuwekezaji. Ipo miradi mikubwa ambayo imefunguliwa kama *Kilombero Plantions Limited* (5815ha) – Mngeta; JKT Chita (3000ha) – Chita; *Syngen Fuels and Agro-Products* (12,000ha) – Merera na *Ruipa Suga Cane Project* (13,000ha) – Ruipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo ni muhimu katika Kilimo Kwanza na ni vizuri kama nilivyoeleza mara nyingi kuwa pale Kihansi kwenye *Switchyard* pana kila kifaa kinachofaa *technically* kuunganisha umeme kwenda Vijiji vya Udagaji, Chita, Chita JKT, Ikule, Mkangawalo, Mngeta, Mduombe mpaka Njage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kuishukuru Serikali kwa kutoa msaada kupitia *REA* kwa *Sisters* wa *Convent* ya Mbinga kwa kuwatafutia mafundi wa kufunga mtambo wao vizuri na baadaye kuwezesha kujenga miundombinu ya kusambaza umeme katika Vijiji vya Mbinga, Namwawala, Mofu na hata Mchombe. Tayari wananchi wameshapelekwa Wilaya ya Ludewa (Iringa) kujifunza jinsi ya kuendesha miradi hii

midogo ya *hydropower*. Kituo cha Masista cha Mbinga chini ya Sister Seki, kina uwezo wa kutoa umeme wa Kw850.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaam wote wa Wizara waliohusika katika maandalizi ya bajeti na kuiwasilisha hapa Bungeni. Hata hivyo, nina maeneo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, usambazaji wa umeme Vijijini. Moja ya maeneo yatakayofaidika na usambazaji wa umeme vijijini ni pamoja na Wilaya ya Mbozi, Jimbo la Mashariki. Hata hivyo, moja ya miradi ambayo ilianza zamani lakini haikuendelezwa ni ule wa Vwawa – Hasamba.

Bahati mbaya sana mradi huo ambao niliahidiwa utakuwepo siuoni. Rejea taarifa ya Mheshimiwa Waziri (Uk.3) aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 2/7/2010. Nataka kujua mradi huu umeachwa kwa makosa au kimetokea kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika taarifa hiyo (Kauli ya Serikali) kama ilivyotolewa na Waziri kuwa Vijiji vilivyotajwa ambavyo ni 'Saganda na Mlimanjiwa' ambavyo havipo Jimboni kwangu nataka kujua vijiji hivyo ni vya Wilaya gani? Kama ni vya Jimbo langu basi naomba yatafutwe majina sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kauli hiyo ya Serikali, Waziri anasema miradi hiyo itakamilika katika kipindi cha miezi kumi na mbili (12). Nataka kujua miezi hiyo inahesabika kuanzia lini? Maana wananchi wa Mbozi ambako miradi hiyo ipo waliambiwa na Mkurugenzi Mkuu wa *REA*, Dr. Mwakahesya, kwamba umeme utawaka katika maeneo yao ifikapo Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ahadi ya Rais ya kupeleka umeme Itaka, Nambinzo. Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembelea Wilaya ya Mbozi mnamo Mwezi Oktoba, 2009. Katika hotuba yake aliyoitoa kwa wananchi wa Halungu na Waitake, mwezi Novemba 2008, alisema wananchi hao watapatiwa umeme. Katika hotuba ya bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma mbele ya Bunge lako, sijasikia Waziri akisema chochote. Aidha, nilipofuatilia *REA* ahadi hiyo ya Rais, niliambiwa kwa maandishi kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010 – 2011. Naomba Waziri awaeleze wana Mbozi ahadi ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa lini au imepuuzwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Makaa ya Mawe, Isansa, Magamba. Kwa zaidi ya miaka mitano (5) sasa tangu shughuli za uchimbaji makaa ya mawe yaanze kuchimbwa katika Kijiji cha Magamba, Kata ya Isansa. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana, hadi leo si wananchi wa maeneo hayo au uongozi wa Wilaya wanaoelewa kwa hakika juu ya kinachoendelea. Naomba kujua kwa niaba ya wananchi, nini hali halisi *(status)* ya mradi huo wa makaa ya mawe Magamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo pia maneno kwa baadhi ya viongozi na wananchi wa Wilaya ya Chunya wanaosema kwamba mradi huo upo upande wa Chunya lakini

Mbozi tunaamini upo Wilaya ya Mbozi maana ndipo uchimbaji/utafiti ulipoanzia. Naomba Serikali Kuu iingilie kati suala hilo ili lisije likazua sitofahamu kwa pande hizo mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, usambazaji wa umeme kwa Vijiji vinavyopitiwa na *National Grid*. Umeme uliwaka Mbozi kwa mara ya kwanza mwaka 1994 kupitia gridi ya Taifa. Kuna vijiji kadha ambavyo vimepatiwa na gridi hiyo kama vile Nanyala, Senjele, Luwanga na kadhalika, hadi leo vijiji hivyo havijapatiwa umeme, pamoja na kwamba upo mpango wa kuvipatia Vijiji hivyo umeme. Sasa nataka kujua mpango huo utatekelezwa mwaka huu wa fedha au vipi? Ni vema ikaeleweka kwamba wananchi hawa ndio wanaotunza miundombinu ya gridi hiyo ya umeme ya Taifa. Nawasilisha, ahsante sana.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Malima kwa kazi nzuri. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, Mheshimiwa Jairo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kutoa masikitiko yangu kuhusu tatizo la kutopatikana umeme Sepuka ingawa ni tatizo la nenda rudi na ahadi ya muda mrefu tena kwa maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mazungumzo ya jana tarehe 8/7/2010 kati yangu na Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Mkurugenzi Mkuu wa *REA,* Dr. Mwakahesya na Ndugu Msote, yamenipa matumaini na kunirejeshea amani. Matazamio yangu ni kuwa ahadi niliyopewa jana tarehe 8/7/2010 na Mheshimiwa Waziri, uongozi wa *REA* wakiwepo itatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uchakachuaji wa mafuta, ni tatizo kubwa na sasa limeanza kuiabisha nchi yetu kwani limevuka mpaka hadi Rwanda. Magari zaidi 20 yaliyorudishwa nchini baada ya kubainika kuchakachua mafuta pamoja na jitihada inayofanywa na Serikali bado haijazaa matunda. Ushauri wangu ni kuoanisha bei ya diseli na mafuta ya taa na ndege hata kama ni lazima kushusha bei ya diseli badala ya kupandisha mafuta ya taa. Bado adhabu kwa wanaochanganya mafuta ni ndogo ukilinganisha na madhara yanayopatikana kiuchumi na kijamii. Ipo haja ya Serikali kuwa wakali zaidi kwa kuchukua hatua thabiti. Huruma imezidi, watu wanaitumia vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Vijijini, gharama za kuunganisha umeme ni kubwa sana kwani wananchi wa Vijijini uwezo wao ni mdogo. Kuna haja ya kupunguza gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuiomba Serikali ieleze ni lini hasa umeme kupitia mradi wa Songas wa Somanga Fungu utawaka kwa mara ya kwanza. Kauli nyingi zimetolewa na Serikali na kauli ya mwisho ni hii ya leo ya Mheshimiwa Waziri kwamba *'testing'* ya umeme huo itafanyika wiki hii. Kauli hizi zote kama zingetekelezwa toka wakati huo, umeme ungekuwa tayari umeshaanzawaka katika Wilaya za Kilwa na Lindi. Kinachoendelea hadi sasa ni kauli zisizoisha. Naiomba Serikali itaje siku kamili ambayo *'testing'* itafanywa pale Somanga Fungu. Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Adamu K.A. Malima, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wametembelea miradi mingi nchini lakini tunataka kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam K.A. Malima, pamoja na maafisa toka *TANESCO* na Wizara, kwa kutembelea mradi wa Somanga Fungu na kufanya mazungumzo na Wabunge wa Rufiji na Kibiti. Wilaya yetu imepata imani kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunausifu mpango wa Songas yaani umeme wa Somanga Funga. Mpango huu, utatupatia umeme katika vijiji vya Mohoro, Nyamwage, Kindwitwi na Mji wa Utete. Vijiji hivi vyote pamoja na Mji wa Utete, nyaya zimeshawekwa mitaani na watu wameshaanza kulipia uunganishaji wa umeme huo. Kwa vile Serikali imeahidi kuleta umeme katika Mji wa Utete ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji, utawaka mwezi Juni, 2010, tunaomba sana umeme huo uwashwe mara moja, mradi huu sasa ni siasa katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali kuwapatia umeme Vijiji vya Chumbi, Utunge na Kijiji cha Mloka *(Selous Tourist Village).* Aidha, tunaomba kuipongeza Serikali kwa kuwasha umeme katika Mji Mdogo wa Kibiti, Bungu na Hospitali ya Mchukiwi katika Wilaya ya Rufiji, ahsante sana *TANESCO* kwa kazi nzuri. Naomba bei ya kuunganishiwa umeme katika vijiji vyetu, ipunguzwe yaani iwe *'affordable".* Tafadhali tuwasaidie wananchi vijijini kwa kupunguza gharama ya kuunganishwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Vijiji vya Mkongo, Kilimani, Ngorongo na Nyaminywili, zitiwe katika Mpango wa Umeme Vijijini yaani *Rural Electrification Authority*. Tunaomba sana, vijiji hivi ni muhimu sana, tusaidieni nasi tupate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilete marekebisho Bungeni ya Sheria ili makosa ya uchakachuaji wa mafuta yawe katika jinai ya kuhujumu uchumi na waliokosa wafungwe jela na kusiwe na faini hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kwa kuwa hoja hii inagusa sana maisha ya watu ya kila siku, baadhi yao ndio kazi yao na familia zao. Pia napenda kumshukuru na kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Malima, kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuwaletea wananchi wa Tanzania mwanga na madini pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kusema kuwa tupunguze kutumia mkaa na tutumie nishati mbadala, nafikiri nishati ya kwanza ingekuwa ni umeme, lakini umeme haujafika maeneo mengi hapa nchini, sio Vijijini tu hata Mijini pia, hili ni tatizo kubwa sana. Kama mtu utamwambia apikie gesi, ni wangapi watatumia gesi kwa kupikia na matumizi mengine kama pasi, taa, jokofu na vifaa vingi vya ndani? Ni bora Wizara hii ijitahidi kuwapatia wananchi wengi zaidi umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia gharama za umeme bado ni kubwa hata wananchi wengi kushindwa kuingiza umeme ndani ya nyumba zao. Naiomba Serikali kuangalia hili kwani ni tatizo, hasa ukizingatia Mtanzania wa kawaida anaishi chini ya dola moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao mkubwa wa umeme, ni tatizo kubwa kwa maendeleo ya wananchi, hasa wale wanaotumia umeme kwa uwajibikaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iliangalie kwa umakini suala la umeme katika Mji wa Mwanza. Kwa kuwa kuna mpango wa kuongeza *generator*, hivyo basi ni bora ikafanya hivyo mapema kwani katika maeneo ya Nyasaka na maeneo mengi ya Nyakato hayapati maji tatizo ni umeme mdogo ambao hauwezi kusukuma maji. Hii ni hatari sana. Kwani kuna shule nyingi za *boarding* katika eneo hili na halina maji ya uhakika, tatizo ni umeme. Hebu Wizara hii imalize tatizo hili la umeme kwa haraka ili kuondoa tatizo kubwa la maji na kuepukana na watu kutumia maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kilio cha wachimbaji wadogo wadogo wa madini wakiwamo wachimbaji wa Mgusu, huko Geita, ambao waliokwishapata kibali cha kumilikishwa eneo hilo toka kwa Kamishna wa Madini. Wakati wa kutokea maafa, mgodi huo ulifungwa, lakini fununu ni kwamba pale katika mgodi uliofungwa kuna Askari na baadhi ya Askari hao kwa usiri hupokea kitu kidogo kwa baadhi ya wananchi na kuwaruhusu kuchimba kinyemela. Je, Wizara inalijua hilo? Ni lini basi mgodi huo utaanza kufanya kazi? Kwa kuwa watu hawa hiyo ndio kazi yao basi Serikali ingetoa tamko la kuruhusu watu hawa wakaweza kumudu maisha yao. Ahsante.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji umeme Vijijini. Naomba niseme kwamba, naishukuru Serikali kwa kusambaza umeme toka Ngara Mjini mpaka Mji Mdogo wa *Kabanga Border*. Lakini naomba Serikali itenge pesa ili Vijiji vilivyopo njiani kati ya Muhweza na Kabanga vipate umeme. Vijiji hivyo ni pamoja na Murugalama, Ntungamo, Kibumbwe na Kumwuzuza. Vijiji hivi vipo njiani na umeme umepita juu ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwenda Mji Mdogo wa Rulenge. Umeme umesambazwa kutoka Ngara Mjini kwenda Kabanga lakini toka njiapanda ya kwenda Rulenge – Kabanga kwa sasa hivi hakuna nguzo na waya toka hapa njiapanda kwenda Rulenge. Wananchi wa Rulenge wanaomba umeme usambazwe toka njiapanda ya Kabanga - Rulenge kwenda Rulenge ili wananchi wa Rulenge waweze kupata maendeleo. Mji wa Rulenge unakua kwa haraka sana. Mji wa Rulenge upo karibu na Kabanga Nikeli. Kwa hiyo, watu wengi wamejiandaa kwa mgodi wa Kabanga Nikeli kwa kujenga nyumba nyingi Rulenge lakini hakuna umeme. Wananchi wa Rulenge wanaomba kusambaziwa umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maporomoko ya Rusumo. Rusumo kuna maporomoko ya maji ambayo yanaweza kuzalisha *megawatt 60*. Wananchi wa Ngara wanaomba mradi huu uanze ili tupate umeme wa kuanzisha mradi wa Kabanga Nikeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza kwa kusema naunga mkono hoja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wetu vijana hawa wanaojitahidi sana kwa kushirikiana na watendaji wengine hapo Wizarani, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri tuliyoyasoma kwenye kitabu cha hotuba, ninaomba nichangie katika mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Wilayani Hai kuna maeneo unakopita umeme mkubwa *(high tension)* lakini umeme mdogo wa kusambazwa kwa wananchi haujashushwa hivyo wananchi wanaishia kuona nyaya tu. Tunaomba tuangalie maeneo yote ili tuongeze pato la *TANESCO* na wananchi wafaidike pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kutoka Kituo kidogo cha Kikuletwa, ni nini kinachoendelea hivi sasa kwani ni siku nyingi tangu *tender* ya kuendeleza Kituo hicho kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule umeme unaozalishwa na Kiwanda cha *TPC*, ni lini utaingizwa kwenye Gridi ya *TANESCO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa hatua zilizochukuliwa hadi hivi sasa kuhusu madini ya vito, lakini bado tunahitaji kuangalia zaidi na kudhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara zingine wanao wajibu mkubwa sana wa kuhakikisha tunapata nishati mbadala ili kuokoa mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunahitaji hatua madhubuti na sheria kali sana katika kudhibiti biashara ya mafuta yaani uchakachuaji kwani ni hasara sana na aibu kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli Shirika letu la *TPDC* siyo wao watakaoagiza mafuta kwa *bulk*? Tunahitaji majibu ya uhakika na uzalendo wetu tuupe nafasi/kipaumbele. Naunga Mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, sasa namwita Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Naibu Waziri yeye atatumia dakika 15 kama walivyokubaliana na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja na yeye atakuja kutumia dakika 25.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu na ardhi, mwingi wa rehema kwa kuniruhusu mimi mja wake dhalili niweze kusimama hapa mbele ya nyumba hii tukufu, mbele ya Watanzania wenzangu na kusema haya ninayoyasema kwa makusudi ya kuchangia katika maendeleo ya nchi yangu na ya Watanzania wenzangu. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru wazazi wangu, mama yangu mzazi, marehemu mzee wangu kwa hiki nilichokuwa nacho, naomba nimshukuru mke wangu Naima Mwapwani, barafu yuko pale juu, watoto wangu na ndugu zangu. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamana hii na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa mwongozo wake na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa uongozi wa kila siku katika kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, tunafanya kazi kwa ushirikiano sana kwa uongozi wake, naomba nimtakie kila la kheri yeye na Blandina ushindi wa kishindo huko Sengerema. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru viongozi wenzangu wa CCM, Mwenyekiti wangu wa Wilaya alikuwepo kule juu amejaa tele, ananiona anafanana na Mbunge wake na Katibu wangu wa Wilaya na viongozi wenzangu, Madiwani wangu, viongozi wa chama kule juu na wananchi wa Mkuranga kwa kazi ya ushirikiano uliofanywa katika miaka hii mitano ambayo imetuwezesha kuitoa Wilaya pale ilivyokuwa miaka mitano tulivyoikuta na ilipokuwa leo na naomba niwahakikishie wananchi wa Mkuranga kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda hao wanaopita wana kazi yao na ni sehemu ya kuboresha mchakato wa uchaguzi, lakini Wazaramo wanasema *zilongwa mbali na zitendwa mbali* yaani kusema mbali na kufanya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nichangie katika maeneo yafuatayo kwa ujumla na yeye tumekubaliana, na kama ilivyo adha ilivyokuwa kawaida atawatambua wachangiaji wote waliochangia katika hoja hii ya Nishati na Madini. Lakini yapo mambo ambayo yamezungumzwa ambayo tunaomba tuyaseme kwa ujumla wake tu na katika mambo hayo moja ni hili suala la *Single Point Mooring (SPM)* hili la kupakua na kupeleka mafuta kwenye sehemu za hifadhi na baadaye kuzisafirisha kwenda nje ama kuzihifadhi Tanzania lakini kwa lengo la kuboresha ule mfumo wa manunuzi ya jumla ambayo tumekubaliana kimsingi tangu tulipokuja na fikra hii, kwamba hii itasaidia katika kupunguza gharama za mafuta lakini

pia katika kupunguza msongamano ulioko pale kwenye Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilizungumzwa katika mikutano ya pamoja ya Wizara zetu mbili, sisi na Wizara ya Nishati na Maji ya Zambia mwaka jana mwezi Aprili na tulikubaliana na Zambia walisema kwamba wangeweza kuchangia lakini baadaye ikaonekana kwamba Mamlaka ya Bandari *(TPA)* ilikuja na fikra kwamba wao wangetoa hizo fedha na kuanzisha *feasibility study* na kadhalika. Kwa hiyo, naomba niseme kwa wale waliochangia katika hili suala la *SPM* ni kwamba ni suala ambalo linafanyiwa kazi na nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba muda sasa umefika ili ifike kwenye kikomo chake kwa sababu haliwezi likawa kila siku linazungumzwa tu. Tumekubaliana na Waziri wa Nishati na Madini kwamba tutoe tamko kuwa tunakubali kwamba hili jambo limefika wakati wa kulifikisha hitimisho baina ya sisi na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu kama wasimamizi wakuu wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali lingine ambalo limezungumzwa sana ni suala la miradi ya umeme vijijini na utekelezaji wake na mwisho nadhani hapa Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni amelizungumza. Hili suala la miradi ya umeme vijijini lina sura nyingi na limezungumzwa katika sura nyingi na namna ya kulipatia ufumbuzi kwa namna nyingi. Kuna wengine wamezungumza kwa namna ya kuboresha mapato ya Wakala wa Nishati Vijijini, wengine wamezungumza namna ya kuboresha mfumo wa kuchangia ili Mfuko wa Nishati Vijijini upate nguvu zaidi labda kwa kutazama vyanzo vingine, wengine wamezungumzia namna ya kuboresha mawasiliano baina ya *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijijini ili kupata ufanisi wa utekelezaji. Lakini pia limezungumzwa suala la *TPDC* na Wakala wa Nishati Vijijini kutafuta namna ya kuwasiliana ili pawe na matumizi ya gesi katika vyanzo hivi vidogo vidogo kama Wakala wa Nishati Vijijini waingie humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kimsingi Wakala wa Nishati Vijijini ana upana mkubwa wa kazi zake na mara nyingi tunapomzungumzia Wakala wa Nishati Vijijini tunamwangalia katika ule mtazamo wa umeme. Lakini kazi yake ni kubwa sana katika *terms of reference* alizopewa kisheria. Niseme tu kwamba katika moja ya mambo ambayo tunarajia ayatazame ni masuala haya ya *off grid solutions* haya mambo ya kupatia umeme au nishati pale ambapo *grid* haifiki, lakini huenda pakawa na ufanisi mzuri zaidi wa kiuchumi kama mkiweza kuufikisha umeme kwa njia nyingine nje ya utaratibu wa kutarajia *grid. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko nchi nyingi ambazo si kila sehemu ya umeme iliyopo pale nchini inatoka kwenye *grid,* zingine ni gridi ndogo *(mini grids),* kama huu mfumo ambao utatumika kwa ajili ya mikoa ya Lindi na Mtwara na labda mpaka kule Mangaka na Tunduru kwa akina Mheshimiwa Dunstan Mkapa na Mheshimiwa Mtutura Mtutura. Ukifanikiwa kupata umeme wa kutosha kutokana na chanzo cha gesi pale unazungumzia uwezo wa kuwa na *off grid solutions, main grid* lakini ukiwa na gridi yako ndogo pale na ikakidhi mahitaji ya viwanda na maendeleo yote ambayo yanakuja. Sasa hayo ni mambo ambayo tunatarajia kwamba Wakala wa Nishati Vijijini watafanya utafiti wao wa kutosha ili pale ambapo vyanzo vinavyohitajika vya megawati 3, 4, 5 huenda ikawa ni bora zaidi au gharama nafuu zaidi kiuchumi kuboresha mfumo huo kuliko

kurejea nyuma na kusema uvute nyaya labda kilomita 100, 120 na kadhalika ambazo gharama zake kusema kweli ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme kwamba pamoja na hili tunafikiria namna ya kuboresha ushirikiano na uratibu baina ya *TPDC,* Wakala wa Nishati na kadhalika lakini pia suala la gharama la kuunganisha umeme na upana wa usambazaji limezungumzwa sana na ni jambo ambalo tumewapatia *TANESCO* wanalifanyia kazi na tunatarajia kwamba uwekezaji unaotumika katika hizi gharama za umeme zitasaidia kama tukipata ufanisi wa uwekezaji tutaweza kufikia hatua ya kupunguza kidogo gharama za kuunganisha umeme, lakini pia kusambaza umeme zaidi kwa wingi wa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili suala la umeme wa Mtwara ambalo lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara na Lindi, lakini pia limezungumzwa na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. Nadhani hili suala la kwamba *EWURA* imelalamikiwa kama ya kamungu mtu fulani hasa kutokana na hili suala la *tarriff methodology.*

Mimi nadhani tukubaliane tu kwamba *EWURA* inafanya kazi kwa taratibu zake za kisheria ambazo zimejiwekea. Lakini hapo hapo tena watu wa Pwani wanasema busara inashinda taratibu, kwamba labda kuna wakati mwingine ambapo kuliko kuleta hasara ya mabilioni ni vizuri kutumia busara ili kuweza kupata ufanisi katika utekelezaji wa jambo ambalo lina maslahi kwa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la kuleta marekebisho kwenye Sheria ya Umeme namba 41(6), (7), (8), mpaka (9). Limezungumzwa hapa na tumeshalitafakari na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na amekubali na tunatarajia kwamba huenda baada ya taratibu na Serikali huenda likaja katika marekebisho ya *Miscellanous Amendments* ili kuweza kuondoa hivi vikwazo ambavyo vinaleta matatizo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la uchakachuaji. Hili kwa kutambua uzito Serikali imetoa tamko au kauli jana ambayo imesomwa na Mheshimiwa William Ngeleja nadhani kuna masuala mawili, kuna suala la adhabu na kuna suala la kodi. Kodi imewekwa maalum pale kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania wenye kipato kidogo. Mimi nadhani tunaafikiana kimsingi kwenye Wizara kwamba tatizo lililokuwepo ni tatizo la adhabu ambalo linabidi liangaliwe upya na huenda kama walivyoshauri Wabunge walio wengi kuihamisha hii adhabu kwenda kwenye Sheria ya Wahujumu Uchumi ili ziweze kupatikana adhabu nzito zaidi kuliko hizi zinazopatikana sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza masuala ya makusanyo ya maduhuli, suala la kwamba Wakala wa Ukaguzi wa Madini uongezewe nguvu kwa kufanywa mamlaka, suala la Wakala wa Jiolojia ipewe fedha zaidi ili kuwezesha uwekezaji mkubwa zaidi ndani ya mitambo na mchango mkubwa kwa sekta ya madini. Haya yote yamepokelewa na tayari Wizara yangu imeanza kuyafanyia kazi na hata mwaka huu mkiangalia Wakala wa Jiolojia ameongezewa fedha nyingi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili suala la kukamilisha sheria ya *STAMICO* lakini pia na mauzo ya nyumba za *STAMICO* ili *STAMICO* ipate kuimarisha mizani yake, hili ni jambo ambalo lilipendekezwa ndani ya Wizara yetu kwa muda mrefu sasa na tunafurahi kwamba linapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wamezungumzia suala la kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, limezungumzia kwa ajili ya maeneo mbalimbali na Kamishna wa Madini ameanza kulifanyia kazi, mchakato wa kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo yaliyotajwa umekwishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengaji wa maeneo unafanywa kwa kuangalia vigezo vingi lakini moja ambalo pia tunaomba wachimbaji wadogo watusaidie sana ni suala la kuzingatia sheria katika kazi zote hizi. Wachimbaji wadogo mkakati uliokuwepo sasa hivi ni kwamba tutengeneze mikakati ya makusudi ili waweze kukopesheka, sasa hivi wakienda kwenye mabenki na kadhalika bado ni gumu kidogo. Kwa hiyo, tunatarajia huu mfuko wa wachimbaji wadogo ambao umeanza kwa fedha ndogo lakini utatarajia kuboreka baadaye utaongeza nguvu ya wachimbaji wadogo na kuongeza uwezo wao wa kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo limezungumzwa la *scan machine* hili ambalo nadhani limezungumzwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Dorah Mushi amelichangia. Mimi sidhani kama Serikali au Wizara ya Nishati na Madini kwa namna yoyote ile inajaribu kumkandamiza Mtanzania au kujaribu kuungana na mtu fulani, sidhani. *(Makofi)*

Nadhani tulikwenda kule mimi na Waheshimiwa Wabunge na wengine wote na tumerudi na taarifa tukasema kwamba tupate kuthibitisha kitaalamu kama hili jambo kweli lipo au hapana na wakati huo jambo lililokuwepo ni kwamba zile mashine zilikuwa zinasababisha kwamba ule uwezo wa kiume wa wale mabwana waliokuwa wanafanya kazi pale wakifika nyumbani usiku unakuwa umepungua. Kisayansi kilichokuwepo pale ni kwamba je, hizi mashine kweli zinasababisha hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiit, sasa kama yapo madhara mengine tukasema pia wanasayansi watubainishie. Tumepata taarifa ambazo zimeletwa na watu mbalimbali waliochangia. Sasa tunatarajia kwamba Kamati ya Bunge imelifanyia kazi, mtalileta Serikalini na sisi tutaangalia ripoti za hao wengine na katika kufanya maamuzi kama haya ni lazima kuangalia maeneo yote ili usimwonee mtu mmoja dhidi ya mwingine na mimi nadhani tutafikia sehemu ambayo tutapata muafaka ambao utakuwa una manufaa na maslahi kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili suala la wachimbaji wadogo ambao limezungumzwa hapa kwamba wamenyang'anywa maeneo. Nadhani tatizo hapa lilikuwepo si kweli kuwa wachimbaji wadogo wananyanga'anywa maeneo na kupewa wachimbaji wakubwa kwani leseni za uchimbaji madini hutolewa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Madini ambazo huzingatia masuala mbalimbali kwa jinsi taratibu za maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nalo tunasema kwamba kama kuna maeneo yoyote ambayo tunadhani wachimbaji wadogo wameonewa kwa namna yoyote ile katika utoaji wa leseni, ni vema tukapata maelezo haya ili tukayafanyie kazi kwa sababu kama tunavyosema amezungumza pale Mheshimiwa Victor Mwambalaswa kwamba yanahitajika kuzingatia hali fulani mle ndani ya kitengo cha Kamisheni ya Madini basi na Kamishna wa Madini amesikia na sisi wajibu wetu ni kusikiliza na kwenda kufanya ile kazi ambayo inaleta maboresho katika kazi zetu lakini pia kwa maslahi ya Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yako mengi na mimi naamini kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atakuja kuongeza katika kuchangia haya pamoja na kutambua wachingiaji wengine. Naomba nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu huenda hii ndiyo ikawa nafasi ya mwisho ya kupata nafasi kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika miaka hii mitano niliyokuwa Bungeni nafasi hii nimepata kukaa na Waheshimiwa Wabunge na kufanya kazi na ninyi naamini imeniongeza katika uwezo na busara na kadhalika na naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa na ninyi humu Bungeni na ninaamini kwamba licha ya mavuvuzela yaliyotanda huko kote wengi wetu tutarudi ili kuendelea na kazi ya kujenga maendeleo ya Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kama ambavyo Bunge lako Tukufu linavyoendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha hatimaye kufikia hatua hii ya kufanya majumuisho ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha huu wa 2010/2011. Niseme kwa dhati na kwa kurudia kama nilivyosema asubuhi na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri natoa majumuisho haya mbele ya familia zetu na kwa mara nyingine tena napenda kutambua uwepo wa Mama Blandina Ngeleja akiwa anashuhudia tukio hili. Lakini pia tunakushukuru wewe Mwenyekiti binafsi kwa jinsi unavyotuendeshea mjadala huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kabla sijawatambua waliochangia idadi ya wachangiaji mpaka sasa hivi. Kwa wale waliochangia kwa kuongea ni wachangiaji 24 na waliochangia kwa maandishi mpaka sasa hivi wako 93. Kwa hiyo, tunapata jumla ya wachangiaji kwa hesabu za haraka haraka kama 117. Hawa ni kwale ambao wamechangia wakati mjadala huu unaendelea. Lakini tunatambua kwamba tangu tuanze mkutano huu wachangiaji katika Wizara mbalimbali wamekuwa wakipata fursa za kuchangia hoja zinazohusu Wizara ya Nishati na Madini naomba niwaahidi kwamba tutaendelea kuzitolea ufafanuzi kama ulivyo utaratibu wa kawaida katika Bunge lako Tukufu kwa maandishi, kwa kina na kwa maelezo sahihi kwa wote ambao wamechangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka na kwa sababu natambua nafasi ya kutambua waliochangia haijumuishwi katika muda huo napenda niwatambue kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuongea wa kwanza alikuwa Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, akafuata Mheshimiwa Mhandisi Habib Mohammed Mnyaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani lakini pia ndiye Waziri Kivuli, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Omari Kwaangw' Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na hatimaye amemalizia Mheshimiwa Adam Kighoma Malima kwa kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali. *(Makofi)*

Lakini waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi alikuwa Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mussa Zungu, Mheshimiwa Kepteni Mstaafu John Komba, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Dr. Bilinith Mahenge, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Lawrence Masha, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Mheshimiwa Omar Mzee na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mohammed Misanga, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Bernadeta

Mushashu, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Mathius Chikawe.

Wengine ni Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Rished Abdalah, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi na Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wanaendelea kuwasilisha nakazia kwamba tutaendelea kuwatambua kwa michango waliyowasilisha. Kama tulivyoshuhudia kwa mchangiaji wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa William Shellukindo kwa niaba ya Kamati ya Nishati na Madini. La kwanza ni kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa michango yao nafahamu hatutapa muda wa kutosha kumpitia kila mmoja lakini nikielezea masuala ya msingi kwa ujumla hoja ambazo zimeelezewa na wachangiaji wengi zikiwa ni msingi wa hoja mbalimbali ambazo kimsingi Waheshimiwa wawakilishi wa wananchi wamekuwa wakiziongelea kwa muda mrefu. Kwa ujumla tunapokea ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla lakini natambau mchango wa Kamati ya Nishati na Madini chini ya Mheshimiwa William Shellukindo kwa ushauri ambao wametupa na hasa namna ya kuboresha uwezekano wa kupata fedha zaidi kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa haraka zaidi katika miradi ya umeme, kwa hilo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukubali kupokea changamoto ambazo Kamati ya Mheshimiwa Shellukindo imezileta kwetu na tunatambua kwa jinsi ambavyo tumekuwa tukifanya nayo kazi kwa karibu na tunaamini kwamba tutaendelea vizuri na hatimaye haya ambayo tunapendekeza kupitia taratibu za kawaida yatafanyiwa kazi na kutufikisha kule ambako tunakusudia. Kwa uchache tu ulikuwepo ushauri ambao ulitolea. Ushauri kuhusu Serikali kubuni vyanzo vingine vya fedha ili kuwezesha Wakala wa Nishati wa Vijiji kupeleka umeme vijijini. Kama nilivyosema tumechukua vifaa kwa ajili ya shughuli za umeme zipewe ruzuku. Haya ni mambo ambayo yanahitaji utaratibu wake na tuombe kwamba Bunge hili Tukufu litatusaidia sana kuwezesha haya mambo. Tukikubaliana namna ya kuyashughulikia, tunaamini kwamba tunaweza tukafikia pale ambapo tunakusudia. Lakini pia wameshauri kwamba *REA* na Shirika la *TPDC* washirikiane kwenye miradi ya umeme inayotumia gesi. Hiki ndicho kinachoendelea kila mahali ambapo kuna mradi unahusu gesi na mafuta, *TPDC* ni mbia. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Kamati kwa kuendelea kutushauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *financial recovery plan* itekelezwe. Ni kazi inayoendelea kwa sasa hivi. Serikali ifanyie marekebisho Sheria ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ili itoe huduma kwa wengine. Hili tuendelee kusaidiana pamoja na

naamini kwamba Bunge lako Tukufu hili na viongozi katika Kamati mbalimbali na naamini Kamati ya Miundombinu wanasikia na tunaamini kwamba mbele ya safari katika mazungumzo ya pamoja tunakubaliana namna ambavyo mapato yanayopatikana katika maeneo kadhaa na vyanzo mbalimbali vya Serikali vinaweza kusaidia kutumika katika kuboresha mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini au kwa ujumla katika Sekta ya Nishati ili tuendelee kufanikisha mambo mengi. Hoja au maoni yaliyotolewa na Kamati ya Nishati na Madini yalikuwa katika sekta hizo mbili. Lakini lilikuwepo lingine kuhusu makusanyo ya maduhuli. Kulikuwa na hoja kwamba makusanyo ya maduhuli bado hayatoshelezi na eneo hili litiliwe mkazo. Kama nilivyosema tunachukua ushauri na tunaendelea kulifanyia kazi. Lakini pia tumeshauriwa kwamba Wakala wa Ukaguzi wa Madini igeuzwe kuwa Mamlaka ili kuipa uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi na nafahamu hii hoja ni mwendelezo wa hoja iliyojitokeza wakati tunajadili Sheria mpya ya Madini. Tunawashukuru na tutaendelea kulifanyia kazi pengine mbele ya safari Wakala huu pengine unaweza ukageuzwa kuwa Mamlaka ya Madini badala ya kuanza na mchakato mpya kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshauriwa pia kwamba Wakala wa Jiolojia Tanzania *(GST)* ipatiwe fedha zaidi ili kuwezesha kufanya kazi ya ugunduzi zaidi wa mashapo na pia kuwasaidia wachimbaji wadogo. Kwa kweli hili liko katika mipango ya Serikali tumekuwa tukisema siku zote na tunaamini kwamba tutafikia huko. Kadri siku zinavyokwenda tunazidi kuongeza Bajeti ya Wakala wa Jiolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali ikamilishe Sheria ya *STAMICO,* tunakubali na hii ni kazi ambayo inaendelea kwa sababu tulishaanza kulifanyia kazi. Mapato ya mauzo ya nyumba za *STAMICO* zilizouzwa na *TBA* ipewe *STAMICO* ili kuiimarisha. Ni kazi iliyoanza kufanyika na Kamati inafahamu, tunawashukuru sana. Migodi ya Kiwira na Barrick uimarishwe na Serikali itafute fedha zaidi za kuimarisha miradi hiyo. Serikali imeielekeza *STAMICO* kuanza mchakato wa kutafuta mbia mpya kwenye Mgodi wa Barrick, ni kazi inayoendelea sasa hivi. Tupo kwenye hatua za mwisho hatua za awali ni kuhakikisha mradi unafanyiwa upembuzi yakinifu na kuwezesha kupata fedha na kuanza uchimbaji. Baada ya Mgodi wa Kiwira kurudishwa Serikali *STAMICO* iendelee na juhudi za kutafuta mbia wa kuendelea mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusema kuhusu suala la Kiwira kwa sababu nafahamu limechangiwa na wachangiaji wengi nafahamu mchango uliofanywa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na wachangiaji wengine. Mgodi wa Kiwira kwa sasa hivi tunaendelea kukamilisha taratibu zile za kuurudisha Serikalini lakini pia tunaendelea kukamilisha taratibu zingine zilizokuwa zinazunguka mgodi huo nayo tunaendelea kuyafanyia kazi. Kikubwa tunavyoongea hivi leo wahasibu wa Wizara ya Nishati na Madini wako mgodini Kiwira wakiendelea kuwalipa wafanyakazi wa Kiwira kwa malimbikizo yaliyobaki kuanza mwezi wa pili mpaka hapa tulipo. Kwa hiyo, kuanzia mwezi wa 12 mpaka hapa tulipo ni zoezi ambalo linaendelea vizuri, tunawashukuru sana wafanyakazi wa mgodi wa Kiwara.

Mheshimiwa Mwenyekiit, lakini kwa sababu pia limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi katika Bajeti hii imefanya nini? Serikali ilichofanya ni kuwaingiza wafanyakazi wote wa Mgodi wa Kiwira katika Bajeti tuliyonayo. Kwa hiyo, kuipitisha Bajeti hii leo pia ni moja ya manufaa ya wafanyakazi wa Kiwira. Kwa hiyo, wakati tunapomaliza wafanyakazi wa Kiwira watajua kwamba mshahara wao wa kila mwezi sasa si suala la kudaiana kama malimbikizo bali ni sehemu ya kulipwa kama wafanyakazi wengine katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Nilidhani hili tulieleze ili na wenzetu twende kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kusema hayo aliyefuatia kuchangia kwa kuzunguzia alikuwa Mheshimiwa Habib Mnyaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Alikuwa na hoja nyingi lakini napenda kuzifafanua kama ifuatavyo; hoja ya kwanza ilikuwa ni kiasi gani kililipwa mishahara ya Kiwira ambacho nimesema tumekamilisha zoezi la ulipaji wa malimbikizo ya mishahara yote mpaka tunavyoongea leo hii na kiasi kilichotumia mpaka sasa ni shilingi bilioni 2.44. Lakini pia katika hoja aliyoitoa Mheshimiwa Mnyaa alionesha kwamba kuna tofuati ya fedha ambazo zililipwa na akataka ufafanuzi. Kuna fedha zililipwa Kiwira na kuna fedha zilikuwa zimelipwa kwenye Wakala wa Madini *(TMAA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kiwira nimesema mpaka leo tunavyoongea ni shilingi bilioni 2.4 lakini kwa Wakala wa Madini tumelipa shilingi bilioni moja na tulilipa hiyo kwa ajili kuimarisha kazi ya ukaguzi. Ukisoma hotuba yangu inaelezea kwamba ukaguzi wa migodi mikubwa yote imeshakamilika na taarifa imeshawasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Matarajio yetu kwa kazi iliyofanywa itatuwezesha sasa kubaini na kujiridhisha kwamba migodi hii mikubwa iliyopo pengine ni siku za hivi karibuni itaanza kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa habari njema ni kwamba ukiondoa taarifa tuliyotoa mwaka jana kwamba Mgodi wa Geita ulikuwa umeshaanza kulipa kodi. Mgodi wa *Gorden Pride* ulioko Nzega kwa Mheshimiwa Lucas Selelii nao umeshaanza kulipa kodi ya mapato mwaka huu kutokana na kazi inayofanywa na Wakala wa Madini. Sasa hizi taarifa zingine ambazo zinafanyiwa kazi na *TRA* kwa kushirikiana na Wakala huu tunaamini kwamba utaleta matokeo mazuri, ni jambo la kusubiri kidogo tuone nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja zilizotolewa kwamba Serikali itoe sababu na maana ya kufanya uhamisho ikiwa hata hiyo fedha iliyoidhinishwa na Bunge haikufikiwa. Kulikuwa na fedha kiasi cha shilingi bilioni 27 hivi. Kuendesha nchi ni kama kuendesha familia. Yapo mambo unaweza kuyapanga yasifanikiwe. Tunachokisema hapa ni kwamba kuhamisha fedha kwanza wananchi kupitia Bunge hili wafahamu kwamba si jambo haramu kama limefata utaratibu na likakubalika. Kwa hiyo, tunataka kujenga uelewa kwa wananchi wanaofatilia mjadala huu wasidhani kwamba kufanya *reallocation* ni jambo haramu. Ni jambo haramu kama halikufuata utaratibu, lakini kama limefuata utaratibu ni jambo halali. Kwa hiyo, hili jambo limekuwa likifanyiwa utaratibu lakini kwa sababu kuna vyombo vingine vinakuwa vinapitia na vinajiridhisha kama jambo hili ni halali nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu

kwamba uhamisho wa fedha uliofanywa pamoja na malengo ya makusanyo na kutolewa fedha kutotimia kama ilivyokusudia bado fedha hizi zilitumika kwa matumizi halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ilikuwa ni mafuta ya mitambo ya *IPTL* kwa kipindi ambacho tulikuwa na matatizo ya umeme, mishahara ya Kiwira kama nilivyosema na kulikuwa na gharama za kuendeshea kesi Mahakamani. Tunafahamu tuna kesi ya *IPTL* iko Mahakamani muda mrefu na pale Serikali ina nafasi yake ya kulipa gharama za kesi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimesema suala la shilingi bilioni moja kwa ajili ya suala la ukaguzi wa fedha. Kwa hiyo, ni mambo yanakwenda vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Habib Mnyaa, Waziri Kivuli katika Wizara yetu hii asiwe na hofu. *Reallocation* ilifanyika kihalali na tunaamini mwisho wa siku utabaini kwamba twende pamoja ili tuharakishe kutoa fedha za watu wa Kiwira na maeneo mengine. Lakini pia kulikuwa na hoja ilijitokeza kwa nini fedha hazitoki kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu Bajeti yetu, tunaongea Bajeti ya ujumla katika kufahamu kwamba uwezo wa kifedha wa Serikali vyanzo vyake vinapatikana vipi. Kwa hiyo, si jambo la kushangaza sana tunatumia kwa kadri tunavyopata. Ndiyo maana kunakuwa na hoja ya kupanga vipaumbele kwa kuzingatia uwezo wetu wa makusanyo ya vyanzo vya fedha ili kutekeleza miradi tuliyonayo na mipango tuliyojipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Habib Mnyaa alishangazwa kidogo kwa jinsi fedha inavyotoka taratibu kutoka Hazina akaona hofu kwamba kazi ya kufikisha miradi ya umeme katika Makao Makuu ya Wilaya na tunamshukuru kwa kutambua hilo kwa sababu ndiyo sera ya Chama cha Mapinduzi na akasema katika ukurasa wa 51 na 52, lakini nimkumbushe Mheshimiwa Mnyaa ukurasa wa 51 na 52 wa hotuba yangu atabaini kwamba tunavyoongea leo Wilaya zilizobaki ni tisa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zote hizo ambazo zimebaki ambazo ni Namtumbo mkoani Ruvuma, Wilaya Nkasi mkoani Rukwa, Wilaya ya Ngorongoro katika mji wake wa Loliondo ndani ya Mkoa wa Arusha, Longido mkoani Arusha, Bukombe na Kishapu mkoani Shinyanga na kwa sasa Bukombe iko Mkoa wa Geita na Kishapu inakuwa Simiyu, Kibondo mkoa wa Kigoma na Nanyumbu katika mkoa wa Mtwara, zote hizo zitapitishiwa umeme ndani ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu Bajeti hii tunayopitisha ndiyo Bajeti ya mwisho katika Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, hata tunavyoongea hivi kwa sababu Bajeti hiyo itaisha tarehe 30 Juni mwaka kesho sisi makusudi yetu na malengo yetu ni kuhakikisha kuwa Wilaya zote zitakuwa zimekwishapatiwa umeme na niseme tu kuwa maandalizi pia ya kuzifikishia Makao Makuu ya Wilaya mpya zilizotangazwa hivi karibuni yamekwishaanza ili kwamba tukibaini katika Makao Makuu ya Wilaya ambayo imetengwa lakini haijatangazwa

tutafikisha maeneo hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnyaa hili ni suala la uandishi siyo tatizo kubwa sana nadhani siyo hoja kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo ya dharula ya megawati 160 kasi yake inakwenda vizuri, tulipata changamoto mwaka jana kwa sababu tuliona kwamba jinsi mchakato ulivyokuwa umeenda ulikuwa na kasoro. Tukasema ni bora kuchelewa kwa kujihami kutopata madhara mbele ya safari tukaamua kurudia ule mchakato, ule mchakato umekwisha na umekamilika na tunaamini zoezi lote zima la mwezi huu wa saba litakamilika ili wakandarasi watakaokuwa wameshinda walete hiyo mitambo na *timeline* yetu tuliojiwekea ni ya muda wa mwaka mmoja.

Kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hili ni jambo ambalo linazungumzika, tumeshaanza kulifanyia kazi, tulikuwa na hofu na mradi wa Kinyerezi kulikuwa na takwimu za megawati 300 na megawati 240 ukweli ni kwamba baada ya stadi zilizofanyika ni megawati 240, Mheshimiwa Mnyaa aliuliza ni miujiza gani Waziri atafanya ya kujenga mtambo wa Kinyerezi wa megawati 240 na kukamilika mwaka 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnyaa aliuliza kuwa kabla ya kuwepo mtambo mwingine wa kusafisha gesi bila ya kupanua miundombinu ya usafirishaji, jibu lake ni hakuna miujiza inayofanyika, ni mipango iliyopo na mipango iliyopo ni kwamba sasa hivi kuna mradi mkubwa unaofanywa na wawekezaji binafsi ikiwamo kampuni ya *SONGAS* na makampuni mengine kama *Pan Africa Energy* ambayo sasa wanakaribisha taratibu na *EWURA* kufanya mradi wa upanuzi wa miundombinu na kusafisha gesi kwa kiwango cha mara mbili ya uwezo wa sasa uliopo, uwezo huo utatufikisha kuongeza uwezo zaidi ya mara mbili ya uwezo tunaozalisha sasa hivi kwa kutumia mipango ya kuzalisha gesi asili kwa hiyo, mipango hii inaenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachofahamu ni kuwa taarifa hizi huwa tunaziandaa bila kuwasiliana kwa sababu wakati mwingine ni kufanyiana *timing* lakini kama tungefanya mawasiliano na Mheshimiwa Habib Mnyaa ungeelewa kuwa ule mradi unaendelea kwa hiyo, hili jambo linafanyiwa kazi.

Kuna suala la Waziri alielezee Bunge kuna ndoa gani kati ya *SONGAS* na Wizara ya Nishati na Madini kiasi kwamba hawairuhusu *TPDC* kukopa. Jibu ni kuwa hakuna ndoa yoyote, hapa tunachofanya ni kwamba kila ulipo mradi wa gesi kama nilivyosema *TPDC* ni mshiriki kwa mfano kwenye *SONGAS.* Miradi ya *SONGAS* hii tunayoisema *TPDC* ni mmojawapo ya wabia kwa hiyo, ni jambo ambalo tunakwenda pamoja lakini ni suala la kuelewa tu nikushukuru sana Mheshimiwa Mnyaa kwa kuungana na Waheshimiwa wengi kama Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir na Waheshimiwa wengi waliochangia hapa kwa kuonyesha msisitizo wa mabadailiko ya Sheria la umeme tuliopitisha mwaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupendekeza kile kifungu cha 41 kirekebishwe ili kuwezesha sasa utekelezaji wa miradi ya watu binafsi au makampuni binafsi kwa nia ya kusaidi kasi ya usambazaji wa umeme katika nchi hii. Hilo tumelizingatia na tunalifanyia kazi. Suala la kuagiza mafuta kwa pamoja ulisema kuwa kuna kampuni inaitwa *Live Take*

pengine imepewa ni kampuni ya kizalendo, hakuna kitu kama hicho, utaratibu ulipo ni kwamba tutaendelea kulifanya zoezi kila baada ya miezi mitatu *tender* itakapotangazwa anayeshinda anaagiza mafuta kwa miezi mitatu baada ya hapo inatangazwa tena *tender* nyingine analetwa mtu mwingine. Kwa hiyo, suala la kampuni ya *Live Take* au kampuni yoyote ile ambayo inasemekana imepata kwa utaratibu usiokuwa wa wazi hapana.

Kuhusu *TPDC* kuwezesha miradi mbalimbali ya usambazaji gesi katika jiji la Dar es Salaam ni miradi ambayo inaendelea na *TPDC* anawasiliana na anaendelea kuzungumza na makampuni mbalimbali ambayo yanaonyesha nia ya kushiriki katika mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la bei ya umeme kwa Zanzibar kwanza niseme tu kwamba ile tozo ya 3% tunasema Zanzibar haitozwi. Kwa hiyo, ni suala tu la kuweka kumbukumbu sahihi. Lakini kuhusu tofauti ya bei ya ongezeko lililofanyika mwaka 2007 na Mamlaka ya juu ya Serikali jambo hili inalifanyia kazi, tunafahamu kuwa jambo hili siyo kwamba linatusumbua, tunafahamu kuwa litaisha vizuri.

Kuhusu utekelezaji wa *sub marine cable* ambao ratiba inaonyesha mwaka 2010 mpaka 2012 ni kipindi kirefu sana na Mheshimiwa Mnyaa alijiridhisha kwamba inavyoelekea teknolojia ya sasa inawezekana kufanya jambo hili kurahisisha kwa muda mfupi zaidi lakini maelezo ni kwamba kazi hiyo ilitangazwa kwa kutumia utaratibu wa Kimataifa wa *tender* za wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahisi na kuamini kwamba endapo ingekuwepo kampuni yenye teknolojia ambayo ingewezesha kutekeleza mradi kwa kasi zaidi na hata kama Mheshimiwa Mnyaa haifahamu lazima ingekuwa imefuatilia na kuomba na pengine ingekuwa mmoja wa washindi katika hili, lakini kwa utaratibu uliofanyika tunaamini kwamba kampuni iliyopata na ratiba inavyoonyesha ni ratiba ambayo imezingatia utalaamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANSALT* tumehamisha kutoka Uingereza Jiji la London lakini sasa ni kampuni ambayo inafanya kazi hapa Tanzania kwa hiyo, kazi zilizokusudiwa zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme ya ujumla ya umeme vijijini. Waheshimiwa Wabunge wamesema sana hapa ninafahamu kilio chako Mheshimiwa Lawrence Masha mjini pale, ninafahamu kilio cha Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Mohammed Misanga, Mheshimiwa Wilson Masilingi na wapo Waheshimiwa wengi hapa wamesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ninafahamu kuwa ulikuwa unaongea kwa uchungu. Lakini ukweli ni kwamba juzi wakati tunatoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ile ya mikoa 16 takribani tumewekeza shilingi bilioni 103, kimsingi siyo shilingi bilioni 98. Shilingi bilioni 98 zile zinaonekana katika miradi ile ya mikoa 16 lakini hujaweka miradi ya mkoa wa Bagamoyo, hujaweka mradi wa Kishapu pale ambayo sasa inakupa gharama ya shilingi bilioni 103 ndiyo tuliyotumia sasa hivi miradi

hii miongoni mwake ilikuwa imekuwa imekaa bila ya kutekelezwa kwa zaidi ya miaka kumi tukasema tuanze na hiyo, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mlitaka niwahakikishie.

Mheshimiwa Hassan Kigwalilo amesema kwa uchungu sana kuhusu Liwale, tunafahamu kuwa hili tatizo la dharula ni uharibifu wa mashine kwa sababu Liwale haijaunganishwa na gridi ya Taifa lakini wataalamu wameshafikisha *spare parts* na vipuri vinafanyiwa kazi, mashine hizo zitapona lakini bado mpango wetu wa kuhamisha mashine za Ikwiriri na kwa sababu mpango wetu wa kupitisha Daraja la Mkapa kufikia mwishoni mwa mwaka huu utakuwa umekwisha kamilika mpango wetu bado uko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuletea mashine kwa nia ya kuwasaidia, kwa nia ya kuwawezesha Watanzania hawa. Tunafahamu adha unayoipata na hasa katika kipindi hiki lakini naomba niseme kama walivyosema Waheshimiwa wengine hapa wako watu wanatumia fursa ya mwaka huu kupotosha umma na mimi naomba nitumie nafasi hii kuwaambia kama alivyosema Mheshimiwa mmoja hapa haiwezekani kwamba mgombea mtarajiwa kwa kutumia fursa hii akataka kujinadi kuwa angekuwa yeye angeyawezesha. Angeyawezesha kwa utaratibu upi? Miradi hii inafanywa na Serikali na Serikali ni yetu wote, tunashukuru Mheshimiwa Hassan Kigwalilo na tunaomba wananchi wa Liwale wafahamu hawa watu wanaosema kuwa wanatumia fursa hii siyo kwako tu, wako katika majimbo mengi hizo ni fitina tu za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengi wanasema hizo ni kama mvua za wakati wa kiangazi hazidumu sana. Lakini sisi kama wadau wa nchi hii wote tunastahili kuwaambia ukweli na tunaamini ya kwamba sifa mojawapo ya kiongozi ni kuwa mkweli katika hili kwa kuwa tunatumikia maslahi ya watu kwa hiyo, Mheshimiwa Kigwalilo naomba tu wananchi wa Liwale wafahamu kuwa ni *propaganda* hizo za kwamba wangekuwa wao wangeboresha mradi ule kuliko wewe unavyofuatalia Wizarani na Serikalini siyo kweli na kama kigezo ndiyo hicho sitaki kuingia kwenye mambo ya kampeni lakini hawamtendei haki Mwenyezi Mungu kwa hiyo, wapigakura wawahukumu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Buhemba, Mheshimiwa Nimrod Mkono tunalifuatilia, tumepata ushauri wako, tunalifanyia kazi na ni jambo ambalo tumekuwa tukilifanyia kazi na tumeendelea kulifanyia kazi na tunaamini kuwa tutafikia pazuri.

Mheshimiwa Naibu Waziri kaongelea masuala ya mashine za *X-ray* kaliongelea vizuri lakini tuseme ukweli kabisa kuwa pengine jambo hili Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeke tukuballiane tu kuwa tuko kwenye Kamati moja ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo tulilichukulia kwa utaratibu kabisa tu na kwenda kufanya tathimini ikaundwa *team* ya wataalamu, jana niliulizwa swali hapa kuhusu mradi wa umeme Dar es Salaam kwamba unakwendaje, kulikuwa na hisia tukifikia mahali tusipoamini maendeleo ya teknolojia dunia hii, sayansi inapofanyika kwa maana ya utaalamu unaofanyika na kutupa matokeo tutapata matatizo kidogo katika

maamuzi na safari yetu ya maendeleo. Kwa hiyo, mimi namuomba Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka pamoja na hisia zilizopo hapa na Waheshimiwa wengine ambao wanaamini kwamba *X-ray* hizo bado zina madhara kwa wananchi, tuipe nafasi fursa ya wanasayansi na wataalamu wetu kutuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili Tukufu limekuwa likisisitiza kuamini taarifa za wataalamu, leo tukifika mahali ambako Serikali inaweza kufanya ni kusema tuongeze muda kidogo wa wataalamu wengine kuunda *team* nyingine ya wataalamu kama hao waliokuwepo tunamashaka nao. Lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini sitaki kuingia kuwa nafasi Kamati ya Nishati ya Madini ikoje katika hili, lakini inatosha tu kusema kuwa Mheshimiwa Christopher Ole–Sendeka unafahamu vizuri na hili suala limefanywa kitaalamu na halikufanywa kisiasa na ni sayansi ndiyo imethibitisha hivyo lakini kama tunataka kufanya maamuzi ambayo yako kinyume na masuala ya sayansi ni hiyari yetu, lakini naamini kabisa kuwa mustakabali wa nchi hii hauwezi kwenda kwa *style* hiyo kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka tunaheshimu sana kauli yako na mchango wako ulioutoa lakini tukubaliane pia kuwa utaalamu hapa unachukua nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo hapa sisi hatuwezi kuendesha kwa hisia yako mambo yanayoweza kuthibitishwa kitaalamu, kwa hiyo, mimi nakuomba Mheshimiwa Ole-Sendeka uamini kuwa Serikali ina nia ya dhati na katika hili hakuna anayependelewa. Mheshimiwa Ole–Sendeka zipo hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa kama ingekuwa hivyo pengine yako mambo mbalimbali ambayo sasa hivi tungekuwa tunaongea kinyume chake lakini wote tumeshuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchakachuaji. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kabisa tunarekebisha sheria kwa maana ya kuziboresha, tunachukua hatua mbalimbali hili la kutumia vinasaba ndiyo liliwasaidia Waganda wakafika hapo walipo leo wamedhibiti hilo si kwa sababu siyo suala la rangi tu, ni suala la kubaini hali halisi ya mafuta kwa hiyo, tunachowaomba Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie, mtukubalie kwamba hata hili tunalolifanya limesaidia nchi nyingine hili la kuanza na vinasaba. Ninachotaka kusema ni kuwa Serikali haitaki kuchukua hatua za mkato za kuwaumiza wananchi kwa sababu kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaonekana kwamba ni kama vile tuna *compromise* kuwa tumeshindwa kufanya kazi, tunataka tuchukue fursa mbalimbali ambazo zipo za kuwezesha kutekeleza jambo hilo na tunaamini kuwa kwa zoezi ambalo tutaanza mwishoni mwa mwezi huu au mwanzoni mwa mwezi kwa kutumia vipimo hivi tunaamini kuwa litatusogeza mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hilo halitukwamishi wala halitucheleweshi sisi kubadili sheria hizi na kuziongezea makali kwa ajili ya kuwadhibiti hawa maharamia ambao wamekuwa wakifanya biashara hii. Sheria ya umeme narudia pia kusema kuwa tumekubali na tumeshakubaliana na Seriklai tunaifanyia kazi na tunapenda tuifanyie kazi kwa haraka kwa namna ambayo isiwe kikwazo mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu ni jinsi gani wananchi walivyoumia na baada ya kusema hayo nitumie fursa hii kurudia kuwa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba tumekusikia na Waheshimiwa wengine miradi ya *MCC tender* zimefunguliwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo wale wanaotumia nafasi hii kusema kuwa wangekuwa wao wangewahisha siyo kweli ni ghiriba za kisiasa, nimesema kuwa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula wa Bukombe pamoja na maeneo mengine ya Dar es Salaam, tumesema sasa hivi tumeshamaliza kasoro ambazo zilikuwepo na tunaamini kuwa kati ya sasa na mwezi wa tisa mwishoni, tutakuwa tumekamilisha zoezi hilo na mkandarasi atakuwa amepatikana kwa ajili kuanza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema mradi wa Makambako - Songea kikwazo kilichokuwepo kimeshakamilishwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi. Kinachofanyika sasa ni kukamilisha taratibu zinazohitajika kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ule nao tumesema unaanza mwaka huu, nirudie kuwaambia Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kuwa kuhusu uzalishaji wa umeme tumeseme kuwa ndani ya mwaka huu wa fedha tutakamilisha miradi mbalimbali ya uzalishaji ambayo itatutoa hapa tulipo na kutusogeza mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa kwa hatua inayofuata.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini

Kifungu 1001 - *Administration and General* ...............Sh. 3,037,912,600

**MWENYEKITI:** Namuona Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Christopherv Ole- Sendeka, Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Habib Mnyaa, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, nihamie huku sasa.

Wengine ni Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Fatma Mikidadi pia nimekuruka Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa

Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge namuona pia yupo Mheshimiwa Bujiku Sakila na mama yangu Mheshimiwa Tatu Ntimizi. Haya naanza na Mheshimiwa John Cheyo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba kutumia dakika moja tu kutoa masikitiko yangu kwamba jana tarehe nane mabaraza yote ya madiwani yamevunjwa lakini madiwani wote hawana *cheque* zao, kwa hiyo, Serikali ingefanya hima ili wawatendee haki inayostahili. *(Makofi)*

Swali langu ni dogo tu katika ukurasa *schedule* ya miradi ya mikoa, mkoa wa Shinyanga mmetupangia shilingi bilioni tisa kwa ajili ya miradi mbalimbali Bariadi, Shinyanga, Kahama na Meatu sasa toka mwaka jana nilikuwa nakuomba kwamba Mheshimiwa Rais alifungua Bwawa la Nkoma na maji yale yamekaa tu kwa sababu hatuna pampu, siyo hiyo tu, tuna kituo cha afya ambacho kimejengwa na *World Vision,* naishukuru Serikali angalau tumeweza kupeleka *ambulance* sasa katika shilingi bilioni hizi tisa hatuwezi kuchukua hela kidogo kuhakikisha kuwa tunapeleka umeme kwa ajili ya bwawa hili na kwa ajili ya kituo cha afya.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kuwa tulichukue, tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge na tuwashirikishe *TANESCO* na Mfuko wa Nishati Vijijini tuone namna ambavyo tutafanikisha hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Amour Arfi tafadhali. Samahani kuna majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi tafadhali. Chomeka kadi kisha washa.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa swali la kwanza ambalo aliliulisza Mheshimiwa John Cheyo nilifikiri halikuhusu sana Bajeti ya Mheshimiwa William Ngeleja. Kwa hiyo, nilitaka kutoa ufafanuzi kuwa Bajeti ya *gratuity* ya madiwani nimeishaipitisha na madiwani wote nchini watalipwa ndani ya mwezi huu. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa pamoja na majumuisho ya mambo ya msingi ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaona na kuwasilisha hakuwagusa kabisa wachimbaji wadogo wadogo. Ni kwa kiasi gani inavyoonyesha wachimbaji wadogo wadogo wanavyopuuzwa, wanavyodharauliwa na hasa pale Mheshimiwa Waziri alipotoa ahadi katika Bunge lako Tukufu kwamba angekuja kuzungumza na wachimbaji wadogo wadogo wa Mpanda na mpaka sasa tunamaliza muda hakufanya hivyo na mgogoro ule ambao umedumu kwa zaidi ya mika nane haujapata ufumbuzi ni dhahiri kabisa kwamba wachimbaj wadogo wadogo katika nchi hii hawana nafasi? Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Amour Arfi pamoja na kwamba ni kwa umri ni baba yangu mzazi lakini pia ni rafiki

yangu wa karibu sana. Sikuwahi kukusudia kumuahidi jambo ambalo sikuwa na mpango wa kulitekeleza. Lakini naomba wananchi wa Mpanda watanielewa, nimekuwa nikiongea naye Mheshimiwa Said Amour Arfi tulikusudia kufika huko, lakini mialiko imekuwa mingi sana, nchi nzima na kwa majaliwa ya Mwenyezi Mungu ninaendelea kuwa na nafasi hii mpaka pengine mwezi wa kumi mwishoni ahadi yangu bado iko pale pale, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi tuliowaahidi kwamba tutafika maeneo hayo, juzi tulikuwa kwa Mheshimiwa Hawa Ghasia, tunamwaliko Bagamoyo kwa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa na maeneo mengi. Lakini niseme tu kwamba wakati Naibu Waziri anatoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja aliliongelea suala la wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo tunawathamini sana, Serikalini tumekuwa tukisema siku zote hapa tumeshaanza utaratibu wa kuwatengea maeneo yao maalum na kwenye hotuba yetu kwamba tuna mfuko wa shilingi bilioni moja ambao sasa tumeshaanza kuutumia. Vipo vikundi vingi na hata leo asubuhi miongoni mwa wageni wa Waziri tuliowatambulisha walikuwa ni wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuwahakikishia wachimbaji wadogo ni kwamba Serikali inawathamini sana, lakini kwa hilo ambalo hatujalitekeleza sasa bado tuna kipindi cha kuyatekeleza, kama nilivyosema kwa sababu nafasi hizi bado tunaendelea kuwa nazo. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia pamoja na kutambua kazi nzuri iliyofanywa na Waziri pamoja na wasaidizi wake katika Jimbo langu na Taifa zima, nilielezea suala la *x-ray body scan* kwa wafanyakazi wa kampuni ya *Tanzanite One*, nikaeleza kwamba si kwa vile sitambui uwezo wa watalaam waliopo kwenye *Tanzania Atomic Energy Commission,* hapana! Nimesema watu hawa ndiyo waliokuwa watuhumiwa wa kutoa leseni na miongoni mwa wengine waliotuhumiwa ni Menejimenti ya *Tanzanite One*. Katika Kamati zote mbili zilizokuwa zimefanya kazi hiyo, ile ya Pendo Nyanda na ile nyingine ya Daktari kutoka *KCMC* zote zilikuwa na watu kutoka *Tanzanite One* ambao ni Menejimenti akiwepo Meneja wa *Plant* ya *Tanzanite One*. Nikaeleza mgongano wa maslahi uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu kwa sababu hoja yenyewe ilikuwa inatarajiwa iletwe na Kamati ndogo ya Nishati iliyokuwa imeundwa kwa maana ya kupokea ripoti zile. Lakini kwa bahati mbaya sana hii imechomekwa kwenye taarifa ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taabu ninayopata ni kwamba Serikali itakuwa tayari kuzingatia ushauri utakaokuwa umeletwa na Kamati ndogo iliyokuwa imeundwa ya Nishati na Madini kwa kuzingatia ushauri wa watalaam badala ya kuchukua tu hicho kipengele kimoja kinachosema hakuna madhara na madhara yenyewe yanayozungumzwa ni ya muda mfupi, hakuna aliyefanya utafiti wa madhara ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndiyo jambo ambalo nilikuwa nataka maelezo pamoja na mgongano wa maslahi uliopo kwa wale ambao wameandaa ripoti hizo kwamba wewe ni mtuhumiwa wakati huo huo wewe mwenyewe ndiyo unaenda kujichunguza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri hata Naibu anaweza kukusaidia majibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni kweli nafahamu tunakwenda vizuri na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, tuliongea kabla kidogo. Lakini niseme tu ni kwamba Wizara ilishamwandikia Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ajili ya kuona kwa sababu ilikuwa kweli kuna mchakato fulani. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba bado suala hili litaisha kwa namna ambayo ni bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti pengine kwa sasa nimwombe Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kwa sababu alikuwa anasema pengine anashika *break* kidogo, pengine sasa kwa hili tunaweza kwenda pamoja kwa sababu tayari tumeshamwandikia Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini na Kamati kwa kushirikiana na Serikali tutaona ni kitu gani tufanye kwa maslahi ya pande zote mbili. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA MWENYEKITI**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nahitaji Mwongozo wako kwamba katika taarifa yetu, kwa sababu suala hili tumelielezea, kwa bahati mbaya asubuhi taarifa yote hatukuisoma lakini iliingia katika *Hansard*. Kuna kifungu ambacho tumesema kuhusu suala la malalamiko ya wafanyakazi wa Mererani na taarifa imeshakabidhiwa kwa Spika, kwa hiyo hatukuweza kuendelea zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwa taarifa yako, nadhani itasaidia pia pamoja na majibu ya Waziri.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo tu. Wakati nachangia nilizungumza juu ya kampuni moja kupewa miradi mingi na muda wa kumaliza, nilitoa angalizo kwamba kwenye kitabu cha Waziri, miradi ya Mkoa wa Manyara inatekelezwa kwa miezi kumi na mbili kwenye kauli yake, lakini kwenye kitabu nimeona kwamba ni miezi sita. Nilitaka kujua ipi ni sahihi sasa katika kutekeleza miradi ya vijiji ambavyo vipo Babati Mjini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Omari Kwaangw'. Tulipotoa ile kauli ya Serikali na ukiisoma ile sentensi inayoelezea kipindi ambacho miradi hii itatekelezwa, tulisema miradi yote kwa pamoja itatekelezwa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili. Katika ratiba hiyo ipo miradi ambayo itatekelezwa kwa miezi mitano, miezi sita, miezi saba, miezi nane lakini kwa ujumla hakuna mradi ambao utazidi miezi kumi na mbili. Kwa hivyo, Mheshimiwa Omari Kwaangw' inawezekana kabisa mradi wako ukatekelezwa chini ya kipindi hicho kama inavyoonesha kwenye ratiba. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate ufafanuzi. Kabla ya ufafanuzi ningependa kumshukuru sana mdogo wangu Mheshimiwa William Ngeleja kwa sababu Bajeti ya mwaka juzi na

mwaka jana nilisema kwamba umeme usipofika Longido sitagombea tena na nilikwishaaga wananchi na umeme sasa umefika Longido nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwandikia Waziri barua siku moja na nimeeleza kwenye maandishi kwamba kuna umeme unaotoka Rongai ni kilomita 10 tu ufike Kamwanga, niliomba umeme uvutwe kutoka Rongai kilomita 10 ufike Jimboni kwangu na umeme kutoka Siha ambako kuna vijiji vingi pale ambavyo vimeandikwa katika *list* yako, ikaacha vijiji vya Longido ambavyo vinapakana pale.

Naomba ufafanuzi kama umeme unaweza kuvutwa kutoka hivyo vijiji vya Rombo na Siha ili umeme ufike Longido, kwa sababu ya kijiografia umeme wa Longido hauwezi ukafika huku kwa sababu ni mbali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichosema Mheshimiwa Mbunge, Wizara yetu ina barua ambayo alituwasilishia mwaka jana tumeifanyia kazi, kilichojitokeza ni kwamba kwa sababu sasa hivi tulitaka kwanza tumalize malimbikizo ya deni la miradi ya muda mrefu. Lakini mradi wake tunaufanyia kazi kupitia wakala wetu wa Nishati Vijijini pamoja na *TANESCO* na tunaamini kwa miezi michache ijayo tutampa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji, tutakuwa tumefikia wapi katika mradi huo. Lakini ni mradi ambao upo katika taratibu zetu za utekelezaji.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilimpongeza Waziri na Serikali kwa kutekeleza ahadi ya Serikali kuleta umeme katika Mji wa Kigoma. Nakupongeza sana Waziri na ninakutakia kila lenye heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina jambo dogo tu, kwa sababu umeme pale Kigoma ni mwingi sana, kuna maeneo ya Buhanda, Businde, Kagera, Kibirizi, Bushabani, *Bigabiro Mission* na Mahembe, naomba nayo yapatiwe umeme, kwa sababu umeme ule upo lakini kuna urasimu mkubwa sana *TANESCO* Kigoma. Waziri naomba ulitolee tamko hili, maana wale watu wako wa *TANESCO* wanaangusha *speed* yako. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa na wananchi wa Kigoma kwa ujumla kwa uvumilivu waliouonesha wakati wakiwa na matatizo makubwa sana ya umeme. Kilichotokea Mkoani Kigoma katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, ni kitu cha kuigwa katika sehemu zingine za nchi yetu, naamini Waheshimiwa Wabunge pia mtaendelea kutumia mfano wa Kigoma ili kuwa na imani kwa yale ambayo Serikali inasema. Wananchi wa Kigoma wamepata taabu kwa muda mrefu lakini kama anavyosema Mbunge sasa kuna umeme wa ziada. Wanaziada zaidi ya mara mbili ya mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo Mbunge ameyaombea umeme tayari tumeshayachukua na tutaendelea kuyafanyia kazi. Tunaahidi kwamba maeneo mengi tu ya Kigoma kwa sababu ya ziada hiyo yatapata umeme. Lakini jambo lingine ni

kuhusu watendaji. Jana nilijibu swali hapa, kwa wale ambao wanachelewesha umeme, nilikuwa namjibu Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Kahama, kama wapo wafanyakazi ambao wanaleta matatizo tupate taarifa hata kama ni za siri na kwa hili ambalo Mheshimiwa Peter Serukamba kwanza nalikemea kwa dhati kabisa lakini pia naomba wananchi wazidi kutuwasilishia majina ya watendaji hao. Hatuna muda nao, nchi hii ina watu wengi tunahitaji kwenda kwa kasi kwa ajili ya kufika hatua ya mbele zaidi. Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua kuwadhibiti hawa wachache wakorofi. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi kwanza nimemshukuru sana Waziri kwa mpango mzuri wa Serikali wa kupeleka umeme katika vijiji vya Ng'ambi, Chunyu, Msagali, Yoma, Kisokwe na Idoro pamoja na Kimadai, Godegode, Berege Chitemo na Mima. Ombi langu ni kwamba Kijiji cha Tambi katika Kata ya Matomondo kiko karibu sana na Kijiji cha Mseta katika Jimbo la Kongwa ni kama kilomita tatu na pale Kijiji cha Tambi kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, je, Serikali inasemaje kuwasaidia wananchi wa Tambi ili waweze kupata umeme ambao utasaidia na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali hapa Bungeni ni mahali ambapo Serikali inaweza kuwa inaendelea kuchukua hoja na mapendekezo ya utekelezaji wa miradi mingi. Hili la Mheshimiwa George Lubeleje katika maeneo ambayo anayasema ni mojawapo ya fursa ya sisi kulichukua kwenda kulifanyia kazi. Kwa hiyo, tunamuahidi Mheshimiwa Lubeleje kuwa tunalichukua na tutalifanyia kazi. Tutafanya kwanza tathmini kuona ni kiasi gani kinahitajika, mambo ya kitalaamu na baadaye tutampa taarifa ya maendeleo. Tuwaombe tu wananchi wa Mpwapwa wazidi kumtumia yeye au mwakilishi wao ili azidi kufuatilia mradi huo kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu hapa Bungeni leo asubuhi nilitoa malalamiko ya wananchi wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini kwamba wameachwa ama wamesahauliwa kwa muda mrefu wakati wakiwa na umeme katika eneo lao hawaunganishiwi umeme na nilitaja vijiji 32. lakini katika mpango wa Wilaya na Mkoa una vijiji 10 vya Dalai, Tandala, Churuku, Mapango, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mwailanje, Mwaikisabe na Isusumya, viliorodheshwa kuwa vitaunganishiwa umeme mwaka huu. Lakini katika orodha ya Waziri ile iliyotolewa kwenye kauli yake wiki iliyopita na katika kitabu cha hotuba yake vijiji hivi havionekani kabisa. Nataka kujua kwamba hivi vijiji vimeorodheshwa katika kitabu kipi kwa sababu vipo kwenye mpango na ningependa nipate maelezo na kama hana maelezo hapa naomba aniandikie kwa maandishi kwamba hivi vijiji vitatekelezwa kupitia pesa zipi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Paschal Degera. Ni bahati mbaya kwamba mwaka huu hatukurudia orodha ya miradi ya *MCC* kwa sababu mwaka jana kwenye kitabu chetu cha Bajeti mtaona kwenye viambatanisho tulikuwa tumeorodhesha miradi yote ambayo itatekelezwa kwa

utaratibu wa *MCC* lakini pia miradi itakayotekelezwa kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 103 Mheshimiwa Paschal Degera atagundua kwamba vijiji vya Hamai, Dalai, Pai, kupitia Mnenia vyote hivi vipo katika mpango wa *MCC*. Ninamuahidi Mheshimiwa Degera kwamba kwa sababu bado tupo hapa kama taarifa iliyopo kwenye kitabu kile na ataona haitoshelezi tutamwandikia barua ya kumthibitishia na tunafanya hivyo kwa kutambua mazingira ya sasa kwamba miradi hii ipo lakini kikubwa kwa sababu Wanakondoa wanasikia sasa kwamba *tender* za miradi hiyo zimefunguliwa leo. Kwa hivyo, kufikia mwisho wa mwezi huu mzabuni atakayekuwa ameshindwa kutekeleza miradi hiyo atakuwa ameshajulikana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, nalazimika kutumia Kifungu cha 104(1) kwamba iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu. Mwenyekiti anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kuihoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitisha mafungu yaliyobakia.

Kwa hiyo, natumia mamlaka hiyo kuzidisha muda usiozidi dakika 30 baada ya muda wa Bunge wa kawaida uliopangwa tutakapofikia. Baada ya hapo Mheshimiwa Degera tulitengua vifungu vya Kanuni kwa hiyo unapata nafasi moja tu ya kumhoji Waziri na hutapata nyingine, kama hukuridhika nafikiri ulishatoa maelezo kwamba akuletee kwa maandishi, na kwa kuwa watu wapo wengi sana nasikitika sana kwamba sitakupa hiyo fursa ya kuendelea kuhoji hapa. Waheshimiwa tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nasikitika ulininyima nafasi ambayo ilikuwa haki yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge mhoji Waziri, umezuia Kifungu kwa ajili ya kumhoji Waziri, nafasi yako ni dakika kumi sikuwa nazo dakika kumi za kukupa ndiyo maana nilikuruka, naomba umwuulize Waziri. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi kwanza nimeanza kumpongeza Waziri na Wizara yake nzima kwa jinsi ambavyo wamekubali sasa kupeleka umeme katika vijiji vya Ndala, Puge na vyote ambavyo vinapitiwa na Gridi ya Taifa. Serikali mara zote inasisitiza juu ya uhifadhi wa mazingira na mara nyingi wanasema tusitumie mkaa au kukata miti ovyo. Juzi hapa Waziri alisema kwamba nishati mbadala ni pamoja na umeme lakini kila kukicha, ukiamka bei ya umeme inapanda, sijui ni *TANESCO* au Wizara lakini mara kwa mara bei ya umeme inapandishwa. Hivi uhifadhi wa mazingira unaweza kufanyika iwapo bei ya umeme ipo juu, watumiaji wa umeme ambao ni watu wa kawaida watashindwa kutumia umeme kwa sababu ni aghali sana na kufanya mazingira yaweze kuharibika. Waziri

haoni haja sasa iwekewe *formula* maalum ambayo bei ya umeme itakuwa ni nafuu na kukidhi mahitaji ya wananchi wa kawaida?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumepata mchango wa Mheshimiwa Lucas Selelii. Niseme tu kwamba masuala ya udhibiti na upangaji wa bei hapa Tanzania halipo huria, kuna mamlaka ya udhibiti wa masuala ya Nishati na Maji *(EWURA)* wanashughulikia hili suala. Lakini sura ya pili ya suala hili ni kwamba kweli gharama tunazoziona sasa zipo juu lakini kwa gharama za uzalishaji umeme sasa hivi bei hizi bado haziko juu sana. Nafahamu si tamu sana kuielezea lakini pia ukizilinganisha na nchi zingine za jirani kwa mfano ukanda wa nchi za Afrika Mashariki, sisi ni miongoni mwa nchi ambao tuna bei ya chini sana. Kwa hivyo ni suala tu la kuelewa uhalisia wake lakini si kusema kwamba labda Serikali inaridhika na hii hali ambayo inanung'unikiwa na wananchi na sisi tunafanya juhudi ili kuhakikisha kwamba bei hazipandi. Kwa hiyo, hoja hiyo tunaizingatia. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilipochangia nilimpongeza sana Waziri kwa kupeleka *transfoma* Singa na vile vile kupeleka *transfoma* Nkungi, pia kupeleka *transfoma* mpya baada ya ile ya Tumuli kuungua. Lakini katika michango yangu yote ya kuandika na kuzungumza niligusia juu ya kupeleka umeme Shule ya Sekondari Iguguno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye michango yangu yote ya kuandika na kuzungumza niligusia juu ya kupeleka umeme shule ya sekondari Iguguno ambayo iko chini ya kilomita mbili na shule ya Sekondari ya Tumuli ambayo iko mita 500 na nilichangia vile vile kusema kwamba Halmashauri imeona umuhimu wa kupeleka huo umeme, imechangia shilingi milioni 20, sasa ningeomba kauli ya Waziri, pamoja na kupeleka umeme naeneo hayo ya vijiji hivyo, haoni kwamba ni muhimu asaidie kupeleka umeme kwenye hizi sekondari mbili ya Iguguno na Tumuli ambapo tayari Halmashauri ya Wilaya imeshachangia fedha?

**WAZIRI WA NISHATI NAMADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kauli ya Serikali ni kwamba tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuwezesha jambo hili kufanikiwa na yapo maeneo mengi aliyoyaombea lakini tutaanza na hayo ambayo ameyasisitiza Mheshimiwa Mbunge, tutashirikiana na wakala wetu wa nishati vijijini pamoja na *TANESCO*. Muongozo wetu utakuwa kwanza tupate tathmini ya gharama halisi na tuone kilichopo tunaweza kuanza na kipi kati ya hayo ambayo ameyaomba. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na pia katika mchango wangu kwenye Mkutano wa Bunge kama hili mwaka jana, nilielezea juu ya uwepo wa umeme katika vijiji viwili tu kati ya vijiji 85 katika Jimbo la Mbozi Magharibi ambayo sasa hivi ni Wilaya mpya ya Momba, suala ambalo hadi hivi sasa ni hivyo hivyo halijabadilika na nikawa nimeomba kwamba kuwepo na uwezekano wa kupeleka umeme wa nguvu mbadala ikiwemo nguvu ya upepo. Jibu nililolipata kwa wakati ule niliambiwa huenda upepo wa sehemu ile ulikuwa unavuma hovyo hovyo kwa hiyo, ilikuwa inahitaji kufanya utafiti kwanza na bahati nzuri baada ya hapo Mheshimiwa Waziri alifika pamoja na Mheshimiwa Rais kwenye ziara

yake akajionea hali halisi, napenda kujua hii leo katika ile hali ya utafiti wamefikia hatua gani.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tangu tufike pale eneo lile na tangu tunuahidi Mheshimiwa Mbunge, tumekuwa tukifanya utafiti huo wa kujiridhisha , lakini ambacho naweza kusema kwa sasa hivi, hatujafikia mahali pazuri sana kwa sababu bado hatujapata matokeo ambayo yanaweza kutupa muongozo wa kufanya kile tulichokusudia. Lakini tunampa matumaini sana Mbunge, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame kwa sababu sasa Jimbo lile limeshakuwa Wilaya na moja wapo ya masharti ya Wilaya ya Makao Makuu yake lazima yawe na umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa hili linaharakisha kasi hata kama hatutatumia hiyo njia tuliyoikusudia mwanzoni, tutatumia njia zingine kuhakikisha kwamba tunafikishia Makao Makuu ya Wilaya hiyo umeme ambao naamini utakapofika hapo utaanza safari ya kuelekea maeneo mengine ambako wananchi wanahitaji. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kunipa majibu mazuri angalau kwa asilimia 50 hasa lile la uhamisho ule wa shilingi bilioni 27 na matumizi yake alivyoyafafanua vizuri, nashukuru na hili nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Lakini nina mashaka kidogo kwa Bajeti kutokana na mabadilikoyaliyotokea ambayo amewasilisha Waziri hivi asubuhi kwamba jumla ya fedha iliyoombwa ni shilingi bilioni 249.9 na alifafanua vizuri kutokana na Bajeti ya Wizara ya Fedha zikatolewa zile za *MCC* ni sawa, lakini katika vitabu tulivyopewa, fungu la 58 la muhtasari pamoja na *volume four* na *volume two* Bajeti ilikuwa ni shilingi bilioni 270.95.

Katika hivi vitabu, bila shaka yapo makosa ni kama yale niliyohoji ya shilingi bilioni tatu na akasema katika wakati huu wa uchaguzi ni hatari kwa sababu tunaweza tukafikiria vingine, lakini ndio imeonekana kuna matatizo na kwa sababu ipo katika kipengele cha *emergency power* kuna shilingi bilioni 26 na shilingi bilioni 20 zinazokwenda kwa majenereta ya *emergency* lakini jumla kile kifungu ni shilingi bilioni 49. Sasa hapo ndipo naweza nikagundua kwamba, palikuwa na makosa ile shilingi bilioni tatu, lakini sasa tofauti ya shilingi bilioni 270.9 na Bajeti iliyoombwa ya shilingi bilioni 45 kuna *difference* ya shilingi bilioni 21. Sasa vitabu vyote vitaonekana hesabu zile zinakwenda katika zile shilingi bilioni 270. Je, sasa ina maana vifungu vyote sasa hivi vitabadilika? Shilingi milioni 21 itatoka wapi katika vile vifungu? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, muda wako umekwisha, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika ambacho amekielezea Mheshimiwa Mnyaa, lakini nashukuru kwamba ameielewa ile ya tofauti aliyokuwa ameisema kwamba aliona kama kuna tofauti ya shilingi bilioni tatu kwa sababu tumesema sisi Bajeti tuliyonayo pale ni shilingi bilioni 49, sasa kwa hili ni kwamba tofauti anayoielezea, kwanza tuseme mchakato wa maandalizi ya Bajeti hizi, kumekuwa na mabadiliko kadhaa wakati zinaandaliwa hasa mpaka kufikia mwisho tukaja hapa. Inawezekana Mheshimiwa Mnyaa alikuwa na taarifa ambayo ilikuwa ni kabla ya

marekebisho ambapo shilingi bilioni 21 zilipunguzwa ambazo zilikuwa ni fedha za kigeni.

Sasa katika hili nadhani hatuwezi kulimaliza kwa utaratibu huu wa hapa kwa hapa, lakini Mheshimiwa Mnyaa yeye na sisi tukikaa kueleweshana na kufuatilia hasa kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati, ule mtiririko ambavyo tulikuwa na makadirio mwanzoni yakawa ya kiasi fulani, baadaye yakarekebishwa, nadhani ni jambo ambalo tunaweza kuelewana kwa sababu ni suala la takwimu kwa kweli. Tunahitaji kukaa vizuri kuishughulikia tukaeleweshana hadi tulipofikia. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nasikitishwa kwa sababu masuala yangu yote niliyoandika sikupata jibu hata moja. Labda kwa tatizo nilianza kuwapongeza kupeleka umeme vijiji vya Karagwe na vijiji vya Bukoba Vijijini. Mimi tatizo ni dogo tu ambalo anifafanulie. Bukoka Mjini watu wamejitahidi kuweka umeme wa LUKU, lakini na umeme huo wana kituo kimoja ambacho kinafunguliwa siku ya Ijumaa pekee yake. Siku ya Jumapili na Jumamosi hawapati umeme kabisa, unawashauri nini hawa watu wa *TANESCO* ili wawawekee angalau kituo kingine cha dharula waweze kupata umeme?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimuombe Mheshimiwa Savelina Mwijage usikate tamaa wala usisikitike kwa sababu ni kweli kama nilivyosema hoja za wachangiaji 117 iko kazi kweli na mmoja kwa kifupi anachangia hoja tatu ama nne, lakini la ujumla ni kwamba hili ni la kiutendaji, *TANESCO* wanachofanya sasa hivi, wamekuja na utaratibu nadhani tumekuwa tukifuatilia hata kwenye vyombo vya habari wa kuuza hii huduma ya umeme sasa kupitia kwa mfano kama upo *Vodacom M-Pesa,* uko kampuni ya *Zain* wanaita *Zap* na kampuni zingine ambazo zina mtandao wa namna hiyo.

Mojawapo ni kumhakikishia na kumuondolea mtumiaji ama mteja adha aliyokuwa anaipata kwa sababu ya kwenda kituoni kununua hiyo huduma. Kwa sababu yote haya yanafanywa kwa pamoja na yanasambaa nchini. Juzi tulikuwa na Mheshimiwa Dr. Balozi Getrude Mongela kule Ukerewe, tukaelezea mpango huu na ambao tayari sasa hivi *TANESCO* wameshawaanzishia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Savelina Mwijage tukuombe tu waambie wananchi tunazingatia hilo, tunasogeza hizo huduma kwa utaratibu wa teknolojia ya kisasa zaidi ili kuwapunguzia hiyo adha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi pamoja na mambo mengine niliyochangia ni kuhusu huu mradi wa umeme vijijini ambao kwa bahati mbaya haukugusa mkoa wa Tabora katika Kata za nje ya Tabora Mjini. Naomba ufafanuzi Kata zangu 12 za nje ya Mji wa Tabora zitapataje umeme ikiwa hazikuguswa na mradi wa kupeleka umeme vijijini. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Kaboyonga kama kaka yangu nilipata fursa ya kuteta nae nje kabla ya kuja humu ndani na nikamhakikishia kwamba na hilo huwa ni jambo la kimila kwamba

nimhakikishie tu kwamba *TANESCO* maeneo yake yako ndani ya *TANESCO,* hayako kwenye eneo ambalo linahudumiwa na wakala wa nishati vijijini, tumekubaliana kwa sababu *TANESCO* imepitia katika mawimbi magumu kidogo, sasa *TANESCO* inaanza kusimama, tutazingatia, tutafuatilia, tuna *commitment* ya kweli kuhakikisha kwamba tunaongeza usambazaji wa umeme kupitia mtandao wa Kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amesema. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maneno na kwa maandishi nilileta kilio juu ya Wanakagera juu ya umeme vijijini, nafurahia kwamba angalau Bukoba Vijijini katika vijiji vya Ibwela, Kafunjo, Izimbia Katoro na Karagwe katika eneo la Bisheshe, Nyaishozi na Ihyembe watapatiwa umeme kwa hiyo, Kagera ni kubwa sana, huu ni mwanzo mzuri, tunaomba na wengine muendelee kuwapatia. Mheshimiwa Waziri nilikuja ofisini kwako nikaleta ombi la umeme katika Kata ya Katoma, Kijiji cha Rukindo kwamba pale kinachohitajika ni *stuff station* ukaniambia niende nilete *estimates*, nikazileta, zilikuwa chini ya shilingi milioni 100 na ukaniahidi kwamba kwa Bajeti ile kama itashindikana utaangalia dalili. Unasemaje kwenye hii Bajeti ya mwaka huu? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli. Uzuri ni kwamba mafungu ya utekelezaji wa miradi hasa ya vijijini hayategemei sana, kinachoonekana kwenye Bajeti kwa sababu wakala wetu wa Nishati Vijijini, unakusanya fedha kwa kila mwezi, labda niseme tu kwamba kwa mfano kwa wastani ni kiasi kisichopungua shilingi bilioni moja kinapatikana kutoka *TANESCO* ambacho kinakwenda kule kwenye wakala wetu. Kwa hivyo, miradi mingi itatekelezwa ndio maana nikawa nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa *AG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Mwanasheria Mkuu Mheshimiwa Jaji Frederick Werema umefuatilia sana maombi ya umeme katika maeneo unakotoka nyumbani, haya tunayafuatilia kwa karibu, ninafahamu Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala anafuatilia sana eneo lake, tunafahamu wapo Waheshimiwa wengi hapa, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Gosbert Blandes ilinitisha kwenye wakati anachangia kwenye Wizara ya Mhehsimiwa Waziri Mkuu lakini ukweli ni kwamba ni miradi inayoendelea kutekelezwa na hawa niliowataja ni kama kiwakilishi lakini miradi mingi tunaendelea kuitekeleza kupitia wakala wetu wa nishati vijijini. *(Makofi)*

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nasikitika sana kwa chenga zake za dana dana anazozipiga maana kila siku wakubwa hawa wanakuja mtambo ule wa Somangafungu wanasema kwamba *test* itafanyika kesho, mara kesho kutwa na leo tena imerudiwa tena kesho, kesho kutwa. Je, mtambo huu ratiba yake ikoje ili niweze kuwaambia mavuvuzela? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ili wananchi wajue ili sio mavuvuzela, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyosema Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda mara ya mwisho tulikwenda nae, mimi nadhani kama mwanzo wa mwezi wa tano hivi na wakati ule kituo cha Somangafungu ule ukarabati wa kitaalamu pamoja na mashine na kila kitu ulishamalizika na matarajio yalikuwa kwamba umeme ungewashwa mwisho wa mwezi wa tano. Lakini baadaye ikabainika kwamba palikuwa na tatizo la kitaalamu kidogo katika kuangalia zile *gas detectors,* yaani kama gesi ikianza kuvuja kwenye mitambo, ni mashine gani itakuashiria kwamba kuna tatizo pale la kuweza kudhibiti labda moto au kadhalika kwa dharura kubwa namna hiyo.

Sasa kwa sababu lile jambo lilikuwa halikuwepo ikabidi kwa dharura kabla ya kuwasha lile, lazima vijimitambo vile vipatikane, ndio maana Mheshimiwa Waziri wakati anasema, alisema jambo hilo linaweza likamalizika wiki ijayo kwa sababu mitambo hiyo imepatikana *SONGAS* na watu wale wa mitambo wanakusanyika ili kuidhibiti na kwa hakika wiki ijayo wakishamaliza kufunga vile vijimitambo watawasha gesi na kubaini kwamba hakuna uvujaji na kadhalika ili kwa upande ule sasa wa Kilwa huku mpaka Malendegu huku Utete kwa Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na kadhalika umeme huo uwashwe, lakini kwa upande huu wa Kibiti ambako tunatumia mashine tu za kawaida na za zamani tayari umeme umeshawashwa. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilimpelekea Waziri kilio kikubwa sana cha wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale wa vijiji vya Karumwa, Ikangara Kitongo, Nyarubere, Nyijundu, Nyaruguguna, Nyang'hwale kuhusu utekelezaji wa mradi huo wa umeme chini ya mpango wa *MCC*. Lakini nashukuru leo umetamka hapa kwamba *tender* zimefunguliwa leo. Sasa tatizo langu hapa nilisema kwenye maandishi ni ile Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 ambayo inazuia wale *independent power producers* kutoa leseni kwa muda wa miaka mitano wakati hali halisi ya umeme nchini inajulikana. Kwa hiyo, nikasema yaletwe mabadiliko ya sheria hiyo ili kifungu hicho kifanyiwe marekebisho, kifungu cha 41(7) ili kuweze kuwaruhusu hawa *independent power producers* waweze kupata leseni kutatua tatizo ambalo najua sasa hivi tutaanza kukatakata umeme miezi hii ya nane, wa tisa, wa kumi kuna kukata umeme kwingi sana. Nilitaka majibu yako Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo anayoyasema Mheshimiwa James Musalika yapo katika utaratibu ule ule tulioelezea hapa kwamba vile vipengele wakati vinaletwa hapa kwenye sheria mwezi Aprili, 2008 na mazingira yaliyopo sasa hivi, tumegundua kwamba yanakwaza na Waheshimiwa Wabunge mmechangia sana inakwaza maendeleo na uzalishaji wa umeme kwa sekta binafsi, watu binafsi *(independent power producers).* Kwa hiyo, kama tulivyosema tumeshazungumza na Mwanasheria Mkuu na kwa vile kile kipengele cha 41(7), (8), (9) nadhani na cha (6) pia tumeshakubaliana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwamba itakuja wiki ijayo ili Bunge hili liridhie kwamba vifanyiwe mabadiliko ili viweze kuruhusu uzalishaji wa sekta binafsi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Hoja yangu ni kwamba naishukuru sana Serikali hasa Wizara hii kwa kutuwezesha

kuwa na imani kwamba tutapata umeme katika Mji wa Utete, lakini inasikitisha sana kwa sababu Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima mwenyewe amefika na akaahidi na akasema Juni, tu umeme utawaka. Naomba uwaambie wana Utete lini watapa umeme? Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa Somangafungu ni ule ule ambao unamhusu pia Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda kwa sababu pale kwenye kituo cha Somangafungu ukishaanza uzalishaji pale wa gesi, *line* moja inaenda Kusini mpaka Kilwa na *line* moja inakwenda Kaskazini inakuja Malendego, inakwenda Muhoro, ikitoka Muhoro inakuja mpaka Utete na nyingine inakata kulia inakwenda mpaka Kibiti na Bungu. Kwa hiyo, taratibu ni ile ile tu kwamba kwanza kwa Utete kuna matatizo mawili, kwanza kuna ile kwamba ile mitambo yenyewe kama nilivyosema kwenye jibu langu la awali kwamba kulikuwa na masuala ya *gas lickage detectors*. *(Makofi)*

Lakini kuna lingine la kwamba kuna matatizo ya fidia pale Malendegu kuja mpaka maeneo kidogo huku kama unakuja Muholo ambayo Halmashauri ya Rufiji na Halmashauri ya Kilwa hazijamaliza ku-*resolve* lile tatizo. Kwa hiyo, hata tukimaliza tatizo la uzalishaji wa gesi utakuja mpaka Somanga hapa Kaskazini na Kusini utakwenda Kilwa. Pale Malendego bado pana tatizo la Halmashauri, sasa mimi nadhani ni vizuri kwamba mimi na Profesa na viongozi wengine wote tujaribu kufanya hili ili liishe kwa kushirikiana kwa pamoja na wananchi walipwe fidia na wamalize kuvusha nyaya pale juu. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Langu fupi tu. Nilimuandikia Waziri nikazungumza hapa mwisho kwamba yeye mwenyewe amekuja na Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi wa kumi kule Mbozi na kwenye mkutano wa hadhara pale Kata ya Halungu au Kijiji cha Halungu, Mheshimiwa Rais aliahidi umeme kwa wananchi wa Itaka, Halungu yenyewe na Nambinzo na vijiji vyake vyote. Lakini Mheshimiwa Waziri pamoja na kumuomba sana hakusema lolote. Naomba sasa atoe kauli anawaambia nini wananchi wa Mbozi na hasa Kata ya Halungu na Kata ya Itaka ambako Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba atawapelekea umeme maana kwenye Bajeti ya safari hii mimi sijaona kitu chochote. Nini kauli ya Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Godfrey Zambi tulikuwa nae Jimboni kwake, ahadi ikatolewa na Serikali na mchana tumefanya mawasiliano naye kupitia wataalam wetu. Kwa kweli niseme tu kwamba hili lilikuwa ni kosa la kiufundi kutoonyesha hii miradi kwa sababu miradi ya Vwawa na Hasanga, itatekelezwa na imo. Kwa hiyo, nakuthibitishia na nimthibitishie Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba hiyo tunayo na tutatekeleza na hata hili ombi jipya ambalo liliahidiwa kwa sababu Vwawa na Hasanga tumekuwa nalo kwa muda mrefu, miaka yote Mheshimiwa Zambi amekuwa akifuatilia. Lakini hili la Itaka lilijitokeza tulivyokuwa kule kwenye ziara na Mheshimiwa Rais. Namhakikishia kwamba ahadi ile maelekezo ya Mheshimiwa Rais yanakuwa ni mojawapo ya mpango wa utekelezaji. Kwa hivi hili nalo tutatekeleza. Nimwombe Mheshimuwa Zambi

tukishamaliza kikao hiki tumweleze ratiba ya utekelezaji kwa sababu tayari tumeshaongea na watalaam kwa maana ya kuitekeleza. Halina ubishi katika yale ambayo tumekusudia kuyafanya. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na wakati nachangia kwa maandishi kuhusiana na suala zima la kuongezeka kwa ankara za umeme zinatoka *TANESCO* kwenda *ZECO* kwamba ni kero kubwa kwa Wazanzibar kuhusiana na kupanda kwa bei ya umeme kila kukicha, wananchi walipeleka kilio chao katika chombo chao ambacho kinawakilisha Baraza la Wawakilishi ambapo yalifikishwa malalamiko hayo katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi na Kamati iliamua kwa makusudi kupeleka taarifa kwa Waziri kwamba itakwenda kumwona Waziri ili kujua kiini na undani wa masuala hayo ili kuondosha kero hiyo na jinsi gani ya kuweza kuitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kamati ilirudi ndani ya chombo cha Baraza la Wawakilishi kwa masikitiko makubwa ikisema kwamba Waziri alikataa kuonana na Kamati hiyo na nilitaka kupata sababu ni kwa nini Waziri alikataa kuonana na Kamati hiyo ambapo ilileta picha ndani ya chombo cha Baraza la Wawakilishi kwamba Waziri anakidharau chombo hicho cha Baraza la Wawakilishi? Naomba jibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke kumbukumbu sahihi. Kwanza nikiri kwamba nilipata ombi la wenzetu kutoka Zanzibar kuja kuonana Kiwizara siyo binafsi kama Waziri. Lakini bahati mbaya kwa wakati huo imekuja ilikuwa ni taarifa ya muda mfupi.

Mimi nilikuwa jimboni, lakini nikasema wataalam na Mheshimiwa Naibu Waziri wapo Dar es Salaam wapo maeneo ya karibu wangeweza kukutana. Lakini nadhani ni bahati mbaya kwamba ni suala la mawasiliano tu kwamba kwa sababu nilikuwa nje, nilikuwa jimboni na pengine dhamira ya ujumbe ule ilikuwa ni kumwona Waziri mwenye dhamana. Naelewa pengine katika hali halisi ya kibinadamu ndiyo hicho ambacho kilijitokeza. Lakini hata kidogo haikukusudiwa kwamba sisi tulikataa, kwa sababu mahusiano tuliyonayo ni mazuri sana, tumekuwa tukiwasiliana hata sisi Mawaziri wenye Wizara ambazo zinafanya shughuli za pamoja kwa mfano Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kule na sisi tunawasiliana vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ilikuwa ni kwa sababu ya mwingiliano wa ratiba, hapakuwa na jambo lingine na nitumie nafasi hii kuwaomba sana wenzetu wasiwe na hisia hizo. Hatukukusudia, ni kwa sababu mimi nilikuwa nje nilikuwa jimboni. Vinginevyo tuko tayari kuendelea kushirikiana kwa sababu tumekuwa tukishirikiana kwa uzuri sana kuhusu masuala ya bei. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilishakata tamaa. Mheshimiwa Waziri hujaniambia chochote kuhusiana na Kijiji cha Chazimba ambacho kiko jirani na kwako. Lakini suala langu hapa ni kuhusiana na hawa wanafunzi *I mean* wafanyakazi 700 waliopunguzwa na huu mgodi wa *Williamson Diamonds.* Hili

ni suala zito sana na ni la muda mrefu. Nilitaka Mheshimiwa Waziri aniambie kama *at least* kwa sababu naamini Watanzania hawa walioathirika na kuangalia na kutegemea, unaweza ukaanza kulifanyia mchakato upya hili suala? Ama ndiyo imekula kwao hawa wananchi maskini? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, misamiati hii najua inafahamika. Lakini nataka nianze kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wale ambao anawasema ni wafanyakazi ambao walikuwa na malalamiko yao 700 wale kwa vyovyote vile haiwezi kuwa imekula kwao katika mazingira haya. Lakini niseme tu kwamba mpaka tunavyoingia hapa mimi sikuwa na taarifa hizo na nimekuwepo pale Wizarani leo ni mwaka wa nne, sijapata taarifa zozote. Kwa sababu Mheshimiwa Mbunge alisema ana taarifa, ana kumbukumbu na akasema atatuwasilishia ili tuzione na tuzifanyie kazi. Kwa sababu mengi yalishafanyika na hata Kamati yetu inafahamu wako watu ambao wakati mwingine kwa hisia tu mbalimbali ama ushauri fulani, wanaanzisha jambo lakini likishafanyiwa utafiti, uchunguzi unaonekana kwamba kumbe jambo lilishaisha. Kwa hiyo, hata hili sina jibu la haraka sana. Lakini Mheshimiwa Halima Mdee tutazisoma kwanza hizi nyaraka tuone na tutafuatilia huko lilikotokea, kwa nini haikuwa mwaka jana, mwaka juzi, mwaka juzi ule, ni sasa? Kwa hiyo, tutaangalia halafu baadaye tutajua cha kufanya.

Kuhusu Chazimba, haya ni maeneo ambayo yako ndani ya Shirika la *TANESCO,* mchango tumeusoma vizuri Mheshimiwa Halima Mdee, tunakushukuru kwa chagizo. Nafahamu kwa nini unataka Serikali itamke jambo kusema kuhusu Chazimba sasa kwa sababu ya mazingira Fulani, lakini ndani ya *TANESCO*. Hoja tumeisikia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekusikiliza Waziri ulipozungumzia kuhusu umeme kutoka Makambako kwenda Songea na Ludewa. Juma lililopita tulikubaliana kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na wenzetu wa *VETA* Makao Makuu kwamba ujenzi wa Chuo cha Ufundi *VETA* pale Shaurimoyo karibu na Liganga pale utaanza mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wametutaka sisi Halmashauri tuthibitishe kwamba tutakuwa na umeme watakapokamilisha ujenzi ule katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Oktoba mwaka huu. Tukaahidi tutawasiliana na Wizara hii tujue kama tutakuwa na umeme ifikapo wakati huo. Naomba nipate uthibitisho je, umeme utakuwa umepatikana katika muda wa mwaka mmoja na miezi kama mitatu hivi kuanzia sasa ufike pale Liganga ukielekea kwenye vijiji vingine ambavyo vinakwenda mpaka Ludewa Mjini. Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hoja hiyo tumeizingatia, tunaifuatilia. Mheshimiwa Profesa Mwalyosi tutashirikiana naye kwanza tufanye tathmini kama utaratibu ulivyo. Tujue umbali uliopo na gharama halisi inayotakiwa na kwa kushirikiana na Halmashauri nadhani tunaweza kufanikisha. Mwaka mmoja na kitu ni muda mzuri kuweza kujipanga vizuri kwa ajili ya utekelezaji na

niunganishe na lile ambalo Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ulisema kuhusu ujenzi wa ofisi yako tunaendelea. Ule mradi ni wa miaka mitano, tunaanzia ngazi ya Kanda na sasa tunakuja. Kwa hiyo, usikate tamaa kuhusu ile ofisi ambayo tulikuahidi Mheshimiwa Profesa Mwalyosi. Nakumbuka ulichangia katika hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge watu walionyanyuka kwa ajili ya kuzuia hili Fungu bado watu wapo zaidi ya kumi, lakini na muda nao sasa umetulazimisha twende tena kwenye Kanuni. Kanuni ya 104(2) inasema; "Iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufika muda ulioongezwa chini ya fasili ya (1) ya Kanuni hii na Kamati bado haijamaliza kufikiria mafungu yote yanayohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote yanayoendelea na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia, kama yapo."

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………..Sh. 3,037,912,600
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*………………Sh. 1,405,332,800
Kifungu 1003 – *Policy and Planning*………..…………..Sh. 756,927,900
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………..…………….Sh. 288,543,000
Kifungu 1005 – *Legal Services* ……………………………Sh. 242,723,000
Kifungu 1006 - *Information, Edu. & Comm.*..............……Sh. 295,263,500
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit* ……Sh. 279,928,400
Kifungu 1008 – *Environment Management*.......……….Sh. 213,775,900
Kifungu 1009 – *Management Information System*…………………..........................…..Sh. 200,785,300
Kifungu 2001 – *Minerals* ………………………………..Sh. 16,224,959,500
Kifungu 2002 - *Madini Institute*……………………………..Sh.15,000,000
Kifungu 2003 – *Research and Laboratory Services*………………Sh. 0
Kifungu 2004 – *Tanzania Diamond Sorting Agency (TANSORT)* …...................................................................…Sh. 668,432,000
Kifungu 2005 – *Eastern Zone*……………..……………..Sh. 733,467,500
Kifungu 2006 – *Western Zone*…………………..……….Sh. 432,929,000
Kifungu 2007 – *Lake Zone*………………………………..Sh. 643,701,000
Kifungu 2008 – *Northern Zone*…………...……………..Sh. 483,961,800
Kifungu 2009 – *Southern Zone*……………………………Sh. 481,582,000
Kifungu 2010 – *Central Western Zone*………………….Sh. 540,788,600
Kifungu 2011 – *Central Zone*…...………………………..Sh. 456,382,800
Kifungu 2012 - *Southern Western Zone*…….…………Sh. 455,484,000
Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum*……………..Sh. 36,735,320,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini**

Kifungu 1001 – *Administration and General* …………Sh. 146,788,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* …………………….Sh. 992,000,000
Kifungu 1008 – *Environment Management Unit* ……Sh. 180,000,000
Kifungu 2001 – *Minerals*………………………………..Sh. 15,580,080,000
Kifungu 2002 – *Madini Institute* …………………………Sh. 650,000,000
Kifungu 2003 – *Research and Laboratory Services*……….......…Sh. 0
Kifungu 3001 – *Energy and Petroleum*……………..Sh. 166,452,527,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*
*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako tukufu limekaa kama Kamatu ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi naliomba Bunge lako tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana. Nakupongezeni nyote wawili, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako kwa muda mliochukua kujibu. Maswali yalikuwa mengi, lakini bila shaka wale ambao hoja zao nyingine mtazijibu kwa maandishi wataweza kuridhika na yale ambayo mtakuwa mmewasaidia katika majibu yenu ya maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli zimekamilika kwenye *Order Paper* na muda pia umemalizika, sasa nachukua fursa hii kuahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 12 Julai, 2010 saa tatu barabara asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Julai, 2010 saa tatu asubuhi)*